**13 JUNI, 2024**

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI NA TANO**

**Kikao cha Arobaini na Saba – Tarehe 13 Juni, 2024**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa tuketi. Katibu.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, *ndc* – KATIBU WA BUNGE:**

**TAARIFA YA SPIKA**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, leo asubuhi tumepokea taarifa kwamba Mheshimiwa Dkt. Shogo Richard Mlozi ambae tulimchagua kuwa Mbunge wa Bunge la Afrika Mashariki, hatunaye tena. Hii ni taarifa ya awali, tutakapopata taarifa za ziada tutawataarifu. Mwenyezi Mungu ailaze roho yake mahali pema peponi.

Waheshimiwa Wabunge, tusimame ili tuweze kumpa heshima hiyo kwa dakika moja.

*(Hapa Wabunge walisimama kwa dakika moja kumkumbuka Marehemu Mhe. Dkt. Shogo Richard Mlozi)*

**SPIKA:** Mwenyezi Mungu ailaze roho ya Marehemu Dkt. Shogo Richard Mlozi mahali pema peponi, amina.

Katibu.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI,** *ndc* **– KATIBU WA BUNGE:**

**KIAPO CHA UAMINIFU**

1. Mhe. Khamis Yussuf Mussa

*(Mbunge Aliyetajwa hapo Juu Aliapa Kiapo cha Uaminifu)*

**SPIKA:** Katibu.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI,** ***ndc*** **– KATIBU WA BUNGE:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na: -

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:**

Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2023 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:**

Muhtasari wa Tamko la Sera ya Fedha *(Monetary Policy Statement)* kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

**SPIKA:** Ahsante sana. Katibu.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI,** ***ndc*** **– KATIBU WA BUNGE:**

**MASWALI KWA WAZIRI MKUU**

**SPIKA:** Maswali kwa Waziri Mkuu, Waheshimiwa Wabunge sasa nimuite Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa ajili ya kujibu maswali kutoka kwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tutaanza na Mheshimiwa Prof. Patrick Alois Ndakidemi, Mbunge wa Moshi Vijijini.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kumuuliza Waziri Mkuu swali langu. Kwenye mipango ya kuboresha uchumi wa nchi yetu na kuongeza Pato la Taifa letu, Serikali yetu imekuwa na mikakati ya kuboresha sera katika maeneo mbalimbali ili kuvutia wawekezaji wa ndani na wa nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sekta ambazo zimevutia sana wawekezaji ni sekta za viwanda na biashara, madini, utalii na kilimo. Je, Serikali ina mikakati gani ya kuboresha au kurekebisha sera hizi ili zitoe upendeleo maalum kwa wawekezaji wa ndani, wazawa, ili waweze kushiriki kikamilifu kwenye kujenga uchumi endelevu wa nchi yetu? Nashukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabla sijaanza kujibu swali la Mheshimiwa Profesa, naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Khamis - Mbunge wa Kwahani, maarufu kama Mheshimiwa Pele, kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi na leo umeapa. Mimi nataka nikukaribishe kwenye Bunge letu, sisi Wabunge wote wa Bunge hili tutakupa ushirikiano wa hali ya juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nianze kujibu swali la Mheshimiwa Prof. Ndakidemi, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwanza nikubaliane naye kwamba Serikali yetu imefanikiwa kuhamasisha wawekezaji na wawekezaji wengi wamejitokeza. Kwenye maeneo aliyoyataja Mheshimiwa Mbunge, ni kweli tumewekeza kwa kiasi kikubwa na tumeanza kuona faida yake, kwenye madini, kilimo, mifugo, uvuvi na sekta nyingine.

Mheshimiwa Spika, Serikali yetu inayo sera na sheria ambazo zinawapa fursa Watanzania kuingia kwenye uwekezaji na kupata mapato yanayosaidia kuchangia kwenye Pato letu la Taifa. Tuna chombo cha uwekezaji nchini, *TIC,* ambacho kinapokea wawekezaji na kuratibu shughuli zao na kuwapeleka kwenye maeneo wanayohitaji kuwekeza.

Mheshimiwa Spika, pia tunayo Kamati ya Kitaifa ambayo Waziri Mkuu ndiyo Mwenyekiti wa Kamati ya Uwekezaji kitaifa ambayo pia inasimamia utekelezaji wa sera hii. Moja kati ya mkakati wa kuwawezesha Watanzania kuingia kwenye uwekezaji na kupata tija ni pale ambapo hii taasisi yetu ya *TIC*, tumetunga sheria inayoiongoza *TIC* kutengeneza mazingira yanayowezesha Mtanzania kupata fursa kuwekeza pale ambako kuna kampuni kutoka nje na kuzitaka ziingie ubia na Watanzania kama wawekezaji wenza.

Mheshimiwa Spika, hii inatoa nafasi kwa Watanzania kuwekeza na kupata uzoefu wa uwekezaji na kupata faida na kuchangia kwenye pato letu. Kama vile haitoshi, kupitia vikao vyetu vya Kamati ya Uwekezaji vya kitaifa, iko sheria ambayo tumeisimamia na inatoa nafasi kwa Mtanzania kupata fursa ya kuwekeza na kujijengea uchumi yeye mwenyewe na pia hata kitaifa tunanufaika nayo. Hii ni pale ambapo Mtanzania amewekeza na anahitaji kupata cheti cha vivutio ambako anapata unafuu katika maeneo mbalimbali ikiwemo kodi, Mtanzania anaweza kuwekeza mtaji wa chini ukilinganisha na mtu kutoka nje.

Mheshimiwa Spika, watu wa nje wanatakiwa kuwa na dola laki moja lakini pia Watanzania ni dola 59,000. Hizi ni sheria mbazo inampa unafuu Mtanzania kuingia kwenye uwekezaji na kupata cheti cha vivutio. Siyo cheti cha vivutio peke yake kuna kile cheti cha mwekezaji mahiri. Ili uweze kuwa mwekezaji mahiri, mtaji wa kuwekeza kuwa mwekezaji mahiri nao pia tumeweka unafuu kwa Mtanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna dola milioni 20 kwa Mtanzania lakini kwa watu wa nje ni dola milioni 50. Sasa utaona watu wa nje wana mtaji mkubwa zaidi kuliko Watanzania, hii yote ni kutoa nafasi kwa Watanzania kuingia kwenye uwekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo sera zetu zinatupeleka kutoa unafuu kwa Watanzania kuingia kwenye uwekezaji na tunaendelea kufanya maboresho ya uwekezaji huu ili pia Watanzania waweze kupata nafasi ya kuwekeza.

Mheshimiwa Spika, siyo hilo tu tuna hii sera yetu ambayo tumeitengenezea sheria ya *local content* kwa miradi mikubwa ambayo inatekelezwa kama vile miradi ya Bwawa la Mwalimu Nyerere, reli yetu, Daraja la Busisi hata ule ujenzi wa meli na miradi mikubwa ya kimkakati, miradi yote hii mikubwa tumeweka sheria inayowabana wawekezaji kutoka nje kutengeneza fursa za Watanzania kushiriki kwenye ujenzi na wao pia kupata fedha.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, utaona mradi kama reli, Watanzania wengi wameingia huko wakiwa mafundi, pia Watanzania wamekuwa wakipeleka vifaa mbalimbali na wengine wameshiriki masuala ya ujenzi wa aina fulani ya mahitaji kwenye mradi wenyewe, hii ni *local content* ambayo inawasaidia Watanzania kushiriki na baada ya mradi huu tunaweza kupata mafundi wetu ndani ya nchi wakajenga miradi ya aina hii.

Mheshimiwa Spika, hii ni sera ambayo inawapa Watanzania unafuu na uwezo wa kushiriki kwenye uwekezaji na kukua. Kwa hiyo, Serikali yetu itaendelea kuwajenga Watanzania na kuwajengea mazingira wezeshi yatakayowezesha wao kuwa wawekezaji mahiri wakiwa hapa ndani ya nchi, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Elibariki Immanuel Kingu, Mbunge wa Singida Magharibi.

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kumuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu swali.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, sekta ya kilimo katika Taifa letu ndiyo sekta inayopelekea mageuzi makubwa sana ya kiuchumi na kuajiri nguvu kazi kubwa sana ya Taifa letu kwa *almost* asilimia 70 ya ajira. *(Makofi)*

Je, Serikali yetu ya Awamu ya Sita ina mikakati gani kuhakikisha kwamba wanakuja na takwimu za kuwajua wakulima hususan wadogo wadogo, kwa majina yao nchi nzima ili waweze kupata *access* na *data* za kuwafikishia mikopo na tuweze kuwa na tathmini ya kuona mikopo tunayoitoa tumeitoa kwa nani, imeleta *impact* gani kwa masuala mazima ya uchumi wa Taifa, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Elibariki Kingu, Mbunge wa Singida Magharibi kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, nataka nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa sababu ninakumbuka nimefanya ziara kwenye eneo lake na moja kati ya maombi aliyokuwa ametoa kwa Serikali ilikuwa ni hili ambalo leo analileta kama swali la papo kwa papo la kuitaka ama kuiomba Serikali ijenge utaratibu wa kusajili wakulima ili waweze kutambulika, waweze kuingia kwenye fursa ambazo wanatakiwa wazipate. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba uko uhitaji wa usajili wa wakulima kwenye mazao yao ili waweze kutambulika. Uhitaji huu unaendelea sasa chini ya Wizara ya Kilimo. Tuna bodi za mazao, bodi hizi kwetu imekuwa rahisi kuziagiza kwa sababu bodi kama vile ya kahawa yenyewe ndiyo inashughulika na wakulima wote wa kahawa. Kwa hiyo, tumeagiza kupitia Wizara ya Kilimo, kusajili wakulima wote wa kahawa ambao wengi ni wadogo wadodo, tuweze kuwatambua kwa majina yao, maeneo walipo, kiwango cha kilimo kwa hekari na pia kuja kufuatilia uzalishaji wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia tunavyo vyama vya ushirika, vya msingi na vikuu, navyo pia Wizara ya Kilimo imeviagiza vihakikishe vinasajili wanachama wake wote wa ushirika ili kuweza kuwatambua kwenye maeneo ambayo nimeyaeleza mwanzo. Malengo ni kufahamu mahali walipo na pia kuweza kuwafikia na kuwasikiliza wakiwa na sauti moja ya pamoja na kuweza kuwahudumia.

Mheshimiwa Spika, pili, tunahitaji kufuatilia mwenendo wa zao lenyewe na kuhakikisha kwamba tunaliingiza kwenye masoko kwa urahisi na pia hata usimamizi wa masoko yenyewe na wao wanakuwa sehemu yao. Kwa hiyo, suala la usajili linaendelea na kupitia usajili huu tunakuja kuona sasa fursa hizo na tutaendela kufanya kazi ya kuelimisha wakulima waweze kujisajili kwenye mazao yao ili wapate faida zozote ambazo sasa hivi Serikali inaziratibu.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kazi ile inaendelea na tunachotaka kuona ni kwamba wakulima wote wanapata nafasi ya kutambulika na hasa wadogo wadogo, waweze kuwa na sauti inayosikika kwa pamoja na mahali ambapo wanajua, Serikali tuweze kujipanga, tunahitaji mbolea kiasi gani, tunawafikia wapi na kwa namna gani, hayo yote yatakuwa yamerahisishwa kupitia kusajili wakulima kwenye maeneo yao, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma, Mbunge wa Viti Maalum.

**MHE. HAWA M. CHAKOMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kumuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu swali.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Serikali imekuwa ikiwekeza kiasi kidogo cha asilimia moja ya bajeti ya sekta nzima ya elimu kila mwaka katika masuala ya ubunifu, sayansi na teknolojia.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha inawekeza zaidi katika kuongeza na kuimarisha ubunifu, sayansi na teknolojia ili kuimarisha sekta nzima ya elimu, ahsante?*(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo. Serikali yetu inao utaratibu kwa sasa wa kuwakusanya pamoja wabunifu kwenye masuala ya sayansi na teknolojia. Hata wiki mbili zilizopita nilikuwa Mkoani Tanga nikiwa Mgeni Rasmi kwenye Maonesho ya Kitaifa ya Ubunifu Sayansi na Teknolojia ambayo yameshirikisha wadau wote kutoka shule za msingi, sekondari, vyuo vikuu na hata wadau walioko nje ambao wanaweza kuwa wabunifu kuonesha kazi zao na ubunifu wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jukumu hili la Serikali linao uwekezaji. Sasa kinachofanyika chini ya Wizara ya Elimu ni kuhakikisha kwamba uwekezaji huu tunaupanua. Tunaongeza kama ni asilimia moja, tunaamini uwekezaji wetu kwenye eneo hili la ubunifu, tutauongeza kwa sababu tumeona kuna faida. Serikali imeanza kuwahudumia wabunifu ambao pia wanafanya kazi zao kwa kuanzia na utafiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tunaimarisha Kitengo cha Utafiti ambacho kinapelekea watu kutafiti kazi mbalimbali na baadaye kubuni jambo ambalo linaweza kuwaletea faida kwenye majukumu yao. Kwa hiyo tunayo maonesho ambayo yanatoa fursa na maonesho haya, Serikali inachangia kuwapunguzia gharama za kuleta maonesho yao. Mkakati wa Serikali uliopo sasa ni kuhamasisha ubunifu kwenye sayansi na *technology* kuanzia shule za msingi mpaka vyuo vikuu na wale ambao wako uraiani ambao pia ni wabunifu.

Mheshimiwa Spika, tunatoa nafasi hii ya utafiti na hiyo vilevile tumeichangia na tumeunda taasisi zinazosimamia utafiti. Pia, tunaendelea kuona kupitia vyanzo mbalimbali vya taasisi zinazosimamia masuala ya ubunifu kama vile Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, *SUA* na maeneo mengine nayo pia wanapata fungu la kuweza kuongeza kwenye utafiti.

Mheshimiwa Spika, lugha ya jumla ni kwamba Serikali inaendelea kuongeza bajeti ya Wizara ya Elimu ambako ndiyo wanasimamia masuala ya ubunifu, sayansi na teknolojia, ili kuwezesha Sekta hii iweze kukua. Malengo ya jumla, ni hawa wabunifu na kazi zao walizofanyia utafiti na kuzifanyia kazi ziendelee na kupanua wigo wa kazi hizo, tuziingize kwenye masoko, zianze kuwarejeshea mitaji yao waliyoipata na wapate faida kutokana na uwekezaji kwenye ubunifu wa *science* na *technology*.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Innocent Sebba Bilakwate, Mbunge wa Kyerwa.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kunipa nafasi ya kumuuliza swali Mheshimiwa Waziri Mkuu. Mheshimiwa Waziri Mkuu, Serikali ilitoa agizo mazao yote ya kimkakati kuuzwa kwa njia ya ushirika kupitia minada. Pamoja na agizo hilo, kuna maeneo mengine nchini bado hawajaanza kutekeleza agizo hilo na tayari tumeshuhudia kwa maeneo ambayo wanatekeleza, bei zimeanza kupanda. Je, nini kauli ya Serikali kwa maeneo mengine ambayo bado hayajaanza kutekeleza agizo hilo la kuuza mazao ya kimkakati kwa njia ya mnada? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Bilakwate, Mbunge wa Kyerwa, kama ifuatavyo. Ni kweli tunao ushirika lakini pia tunao wakulima ambao tumeamua kuwaweka pamoja na kuratibu pia mauzo ya mazao yao. Hii inasaidia sana katika kupata bei nzuri kwa sababu mfumo wa uuzaji ambao ni mnada, unaleta mafanikio makubwa sana.

Mheshimiwa Spika, natoa mfano, Mheshimiwa Mbunge anatoka Kyerwa na kule kuna wakulima wazuri sana wa kahawa pamoja na wilaya za jirani kama vile Karagwe, Muleba na Bukoba Vijijini, wanazalisha sana kahawa. Awali, pamoja na kwamba

tulikuwa na ushirika, bado bei ilikuwa inasuasua na ikawafanya wananchi wengi waende nchi ya jirani kwenda kutafuta masoko.

Mheshimiwa Spika, tulipoanza na utaratibu wa mnada, tukaanza kuona mabadiliko makubwa na kupata bei nzuri. Hata sasa bei ni nzuri na mwaka huu tunatarajia tunaweza tukapata bei nzuri. Sijafuatilia kuona mwenendo wa mnada ukoje lakini suala la mnada linawaleta wanunuzi pamoja na wakulima wanakaa upande wa pili. Wakulima wanasubiri ununuzi kwa njia ya mnada, wanataka bei gani. Kila mmoja anazungumza bei na kwa kuwa wana *order* za maeneo mbalimbali na wanatakiwa wapeleke zao hilo huko walipopata *order*, watakuwa wanashindana kupata bei nzuri.

Mheshimiwa Spika, ule ushindani unapelekea bei ya mazao yale kupanda na wakulima wananufaika zaidi. Sasa, kama kuna maeneo ambayo bado hayajaanza mfumo huo wa mnada pamoja na maelekezo ambayo tumeyatoa, Wizara ya Kilimo wamesikia, wafuatilie maeneo yote na hasa mikoa na wilaya ambako vyama vya ushirika vipo na ndiko minada inaendeshwa.

Mheshimiwa Spika, nawaagiza sasa Wakuu wa Mikoa wote nchini kufuatilia kwenye ngazi za wilaya ambako vyama vya ushirika vipo, kufuatilia kama; je, mazao yetu yanauzwa kwa njia ya mnada kama ambavyo Wizara ya Kilimo imeelekeza? Kama haiuzi, kwa nini wakati mnada ndiyo unapeleka fursa kuuza kwa bei nzuri? Hata hivyo, tunajua kuunda ushirika ni *process*, ni lazima tutoe elimu kwanza, wananchi wajue umuhimu wa kukaa pamoja, lakini pia elimu hii waendelee kuwaelimisha faida za mnada.

Mheshimiwa Spika, kuna maelekezo ya kuwa na ghala maalum la kukusanyia, ndiyo tunauza iwe kwa Mfumo wa Stakabadhi Ghalani. Kwa hiyo yote haya ni mambo muhimu. Kwa hiyo nataka kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali tunaendelea kujipanga kutoa elimu kwa wakulima, ya kuunda ushirika, kukaa pamoja na mazao yao yaweze kuuzwa kwa mnada

ili yaweze kuleta ushindani wa ununuzi na kusababisha kuwa na bei ya juu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tutaendelea na zoezi hili, tutapita kila eneo kuona aina ya mazao yanayofaa kwa mnada ili yaingie kwenye mnada kwa ajili ya kuuza, tupate bei nzuri.

Mheshimiwa Spika, haya ndiyo majibu ya swali hilo. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Sylvia Francis Sigula, Mbunge wa Viti Maalum.

**MHE. SYLVIA F. SIGULA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kumuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu swali. Mheshimiwa Waziri Mkuu, tunatambua kwamba vijana ndiyo nguvu kazi ya Taifa letu na kutokana na uhaba wa ajira, vijana wengi wameamua kujiajiri. Vijana wengine wamejiajiri kwenye Sekta ya Usafirishaji yaani bodaboda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Sekta hii imekuwa ikikumbwa na changamoto nyingi hasa za ajali ambazo zinasababisha ulemavu wa kudumu lakini pia wakati mwingine zinasababisha vifo kwa vijana wengi. Imekuwa ni sharti la lazima kwamba kila kijana anayeendesha pikipiki au bodaboda ni lazima awe na leseni na leseni hiyo Mheshimiwa Waziri Mkuu ni gharama.

Mheshimiwa Spika, sasa nataka kujua, Serikali haioni haja kuweka sharti la msingi wakati wa ukataji leseni, kwa gharama ileile leseni ile ijumlishe na bima ili vijana hawa watakapopata changamoto ya ajali, waweze kumudu gharama za matibabu na waweze kuzuia vifo kwa vijana wetu? Mheshimiwa Waziri Mkuu, nakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sylvia, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo. Kwanza nakiri kwamba Sekta hii ya usafirishaji wa bodaboda ni Sekta ambayo sasa tumeshuhudia ikiwezesha kupunguza ugumu wa usafiri kwa watu wetu. Pia, inatoa pato kwa hawa vijana wanaojishughulisha na uendeshaji wa bodaboda lakini pia hata Taifa linapata uchumi na utulivu kwa sababu kila mmoja anaonekana yuko kwenye shughuli ikiwemo na uendeshaji wa bodaboda.

Mheshimiwa Spika, suala la leseni ya bodaboda ni la kisheria kwa sababu Sheria inataka kila anayeendesha chombo cha moto, lazima awe na leseni. Gharama za leseni hizi, ziko kwenye madaraja kulingana na ukubwa wa chombo chenyewe. Mheshimiwa Mbunge anataka kuwa na sharti la lazima la kuambatisha gharama ileile ya leseni kuwa ni sehemu ya malipo ya bima ya afya.

Mheshimiwa Spika, suala la leseni lipo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani. Hiyo ni Sheria iko Wizara ya Mambo ya Ndani, inayogusa waendeshaji wa bodaboda au waendeshaji wa vyombo vya moto lakini suala la bima ya afya, iko Wizara ya Afya, nako kuna Sheria yake. Sasa, kuambatisha Sheria hizi pamoja, ni jambo ambalo tumelipitisha pia hata kwa wadau tulipokuwa tunajadili kuanzisha mfumo wa bima ya afya kwa Watanzania wote, ambayo sasa tumeianza na tunaanza kutekeleza hatua kwa hatua.

Mheshimiwa Spika, suala la kuambatisha kama sharti kwenye maeneo mbalimbali kupata bima ya afya, tumelijadili sana. Bado tunaendelea kuliangalia, kuna uzuri wake na matatizo yake. Leo kama ulivyosema Mheshimiwa Mbunge kwamba, gharama hii ni kubwa na kwa hiyo waendesha bodaboda hawana uwezo nayo, na leo tukiambatisha na bima ya afya ambayo pia na yenyewe ina viwango vyake, tunaweza kupata tatizo kidogo.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, sasa bado linazungumzwa na Wizara ya Afya na kwa hiyo nasema tu kwamba, kwa kuwa bima ya afya bado tunafanya maboresho, pamoja na kuwa tumeanza hiyo

Sheria, lakini tunafanya maboresho, suala la viambatishi kama sharti la msingi katika kupata bima ya afya, tuliliangalia pia kwamba; je, anayepata bima ya afya tuambatishe na nini? Kwa mfano, mtu anayepata *passport*, asipate *passport* tuweke sharti la bima ya afya.

Mheshimiwa Spika, tuliangalia pia na hiyo, anayejiunga na chuo kikuu, labda asiingie atakapokuwa anajiunga lazima ajiunge na bima ya afya. Tuliangalia yote lakini tukasema, wakati huu bado si muafaka kuambatisha, kazi kubwa ambayo tunaifanya sasa ni elimu. Kwa hiyo nataka kuahidi kwamba, utoaji wa bima ya afya kwa wananchi, bado tunaendelea na kutoa elimu, kwanza Watanzania wajue umuhimu wa bima ya afya.

Mheshimiwa Spika, pia, zile gharama zenyewe ziendelee, watu waone umuhimu wa kugharamia kwa gharama hizo ili kuwa sehemu ya bima ya afya ambayo ni ya Watanzania wote. Kwa hiyo tulisema tunaenda hatua kwa hatua ili kuweza kutengeneza Sheria na Kanuni zitakazopelekea kuambatisha gharama ya jambo unalolihitaji kuwa ni lazima liende pamoja na bima ya afya.

Mheshimiwa Spika, haiwezi kuwa kiwango kilekile cha leseni, lazima kutakuwa na ongezeko na ndiyo kwa sababu hatukuambatisha kwa sababu kama ulivyosema, leseni ni gharama kubwa. Sasa, ukiongeza na gharama ile, inaweza kuwa kubwa zaidi na watu wasipate leseni, kwa hiyo haya tumeyaangalia kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, ahadi yangu ni kwamba tunalichukua hili, tunaendelea nalo kwenye mijadala yetu kuona kama kuna umuhimu wa kuambatisha si tu kwa bodaboda lakini na maeneo mengine. Tutakuja kuleta Bungeni na mtajadili pia Waheshimiwa Wabunge, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava, Mbunge wa Korogwe Vijijini.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa nyakati tofauti tumeshuhudia kusimama ghafla kwa uzalishaji, uchakataji na usindikaji wa mazao kwa viwanda ambavyo vilikuwa ni viwanda vya Umma zamani lakini baadaye vikabinafsishwa nikitolea mfano wa viwanda vya chai.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwa na sababu na visingizio vingi, lakini hali ya kawaida inaonesha sababu kubwa ni uwekezaji na uendeshaji usioridhisha. Mheshimiwa Waziri Mkuu, nataka kujua, Serikali haioni sasa uko umuhimu wa kufanya tathmini ya kina kwa viwanda na mashamba yaliyobinafsishwa ili tuweze kuokoa uchumi na kuwasaidia wananchi wetu? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa *Advocate* Mnzava, Mbunge wa Korogwe, kama ifuatavyo. Ni kweli tuna mashamba makubwa na viwanda ambavyo zamani vilikuwa vinamilikiwa na Sekta ya Umma lakini tuliona tubinafsishe tupeleke Sekta Binafsi waweze kuviendeleza. Baadaye tulivyogundua kwamba wale wote ambao tumewapa mali hizi viwanda pamoja na mashamba makubwa, wako wengine sasa hivi hawatekelezi kama ambavyo tumekubaliana.

Mheshimiwa Spika, kazi ambayo inafanywa na Wizara ya Kilimo ni kufanya upembuzi kwa maana ya tathmini ya wale wote waliopewa mashamba haya na viwanda hivi ili waviendeleze kwa masharti tuliyokubaliana viendelee, wako wengine wameshindwa kabisa. Kwa hiyo tathmini hii inayofanywa na Wizara ya Kilimo, inapelekea kuja kufanya maamuzi ya wale wote ambao walipewa viwanda hivi na mashamba haya na hawajaendeleza mpaka leo.

Mheshimiwa Spika, mara kadhaa Wizara kupitia Kamati yake ya Ardhi na Kamati ya Kilimo, imepita maeneo mengi, imegundua tunayo migogoro kati ya wananchi na wawekezaji ambao wananchi wanaona kuna ardhi imeachwa kwa muda mrefu lakini

haitumiki na inaonekana ni ya mwekezaji. Alipewa wakati huo kulikuwa na uzalishaji, leo hazalishi pamoja na viwanda vilevile.

Mheshimiwa Spika, tathmini hii itatupelekea sasa kufanya maamuzi ya kurudisha maeneo haya ili tuweze kuyaendeleza kama Sekta ya Umma au tutoe kwa mwekezaji mwingine ambaye anahitaji kuwekeza ili aweze kuendeleza. Mimi natambua Mheshimiwa Mnzava kule kwake ana kiwanda cha chai eneo la Mponde. Nimeenda mara kadhaa kuuona uwekezaji ule wa Sekta Binafsi. Ambaye tulikuwa tumebinafsisha tukampa na ameshindwa kabisa, tumekirudisha na tumeipa Taasisi zetu za *PSSSF* na *NSSF*.

Mheshimiwa Spika, wanaendesha kile kiwanda angalau kwa hatua hizo kidogo kidogo lakini wananchi wanapata kulima chai yao, wanaipeleka kwenye kiwanda kile. Tumeona kukwama kwa maendeleo ya viwanda kule Njombe maeneo ya Kibena, nimefanya ziara pale, nimeenda pia eneo la Lupembe, *somewhere* Lupembe, Njombe, hakuna uwekezaji, mashamba yamekwama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hali hii iko maeneo mengi. Nimeenda pia hata Rungwe, pale Mjini Tukuyu kuna mashamba mengi ya chai yamekwama. Tumezungumza na wawekezaji na mgogoro wetu ni huo kwa nini hawatekelezi na kwa nini hawayatumii maeneo yale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nawaahidi Waheshimiwa Wabunge na tunamuahidi Mheshimiwa Mnzava kwamba hatua ambazo Serikali inazichukua za kufanya tathmini, zinapelekea kwenda kufanya maamuzi. Maamuzi yake tunanyang'anya kama mtu atakuwa ameshindwa kabisa kutekeleza maamuzi yetu na tutawapa wengine ambao wana uwezo wa kuendeleza mashamba haya.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Zahor Mohammed Haji, Mbunge wa Mwera.

**MHE. ZAHOR MOHAMMED HAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ili kuweza kumuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu swali langu. Mheshimiwa Waziri Mkuu, pamoja na jitihada za Serikali ambapo Wizara au Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira imejitahidi sana kuhusu kutoa maelezo na ufafanuzi kwenye changamoto zinazoitwa za Muungano.

Mheshimiwa Spika, pia, kumekuwa na jitihada za makusudi ambazo zinafanywa ili kuupotosha Umma na hasa kwa sababu asilimia kubwa kwa mujibu wa Taarifa ya Sensa 2022, vijana walio wengi wako chini ya umri wa miaka 60. Wiki moja au mbili zilizopita, Serikali iliahidi kwamba itaendelea kutoa taaluma pamoja na majalada mbalimbali. Hivi vitawafikia sana wanaopenda kusoma magazeti na kuangalia televisheni, lakini vijana walio wengi, wanatumia mitandao ya kijamii.

Mheshimiwa Spika, sasa swali langu Mheshimiwa Waziri Mkuu. Je, Serikali haioni sasa ipo haja ili kuepusha upotoshaji huu wa makusudi ambao unaleta chuki, fitina na migawanyo kwa vijana, Serikali haioni sasa ni muhimu kuwafikia vijana ili kuwaeleza changamoto hizi kinagaubaga zilivyopatiwa ufumbuzi kwa kutumia mitandao ya kijamii? Nakushukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zahor, Mbunge wa Mwera – Zanzibar, kama ifuatavyo. Ni kweli Tanzania ni matokeo ya muungano kati ya Tanganyika na Zanzibar na Muungano huu ambao unatuunganisha wa Bara na Visiwani, tunaendelea nao. Tunazo hoja za Muungano na tunayo mafanikio makubwa ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, mimi nikiwa ni sehemu ya Wajumbe wa Vikao vinavyopitia hoja za Muungano, ninaweza kusema kwamba

hatua tuliyoifikia sasa ni nzuri kwa sababu hoja nyingi zimepatiwa ufumbuzi. Ofisi ya Makamu wa Rais ambayo inashughulikia Muungano imefanya jitihada kubwa kwa pamoja na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais – Zanzibar, zimekuwa zikikaa pamoja na kuainisha zile hoja zote ambazo zinahitaji kutatuliwa ili kuufanya Muungano uweze kwenda vizuri. Vikao hivi vimekuwepo, ila vikao vya kitaifa ambavyo vinajumuisha baadhi ya Mawaziri na watendaji ndani ya Serikali zetu zote mbili kupitia hoja hizi na kuzifumbua kuweza kuzitatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kweli tuna vijana wengi wako chini ya umri wa Muungano, wako wanaoufahamu kupitia vyombo vya habari na wako ambao hawaufahamu, ambao hawajishughulishi na kusoma. Jukumu letu sisi Serikali ni kuendelea kutoa elimu kwa Watanzania wote ili waelewe Muungano ni nini na faida zake. Tutaendelea kutumia mifumo yote ya mawasiliano ili kuwafikishia ujumbe.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi tumegundua kwamba wengi wako kwenye mitandao ya kijamii. Niwaahidi kwamba tutatumia mitandao ya kijamii kuendelea kuelimisha umuhimu wa Muungano, hoja za Muungano na namna ambavyo tunazitatua hoja hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia kwa makubaliano ya kikao chetu cha mwisho tulichokutana Zanzibar tumeamua kwamba kila panapokuwa na semina, makongamano, warsha, moja kati ya ajenda ambayo ilitakiwa tuifikishe kwa washiriki wa maeneo haya, hata kwenye mikutano ya kisiasa basi tueleze faida za Muungano, tuwahakikishie kwamba hoja za Muungano zinatatuliwa na zinawezekana kutatuliwa na zikaisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Muungano unaendelea na nyakati zinabadilika, kuna mahitaji kadhaa yanaibuka. Kwa hiyo, Wizara zetu mbili, Wizara ya Muungano iliyoko Ofisi ya Makamu wa Rais na Kitengo cha Muungano kilichoko Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais – Zanzibar wataendelea kuratibu haya yote yanayoibuka kulingana na wakati kwa lengo la kuirodhesha pamoja na kupitia

vikao vyetu tuyapitie tuone namna ya kutatua. Malengo yetu ni kuhakikisha kwamba tunakuwa na Muungano imara wenye maslahi kwa Watanzania wote, lakini ambao pia utasaidia kutuunganisha na kuendelea kutuunganisha Watanzania ili tuweze kuishi kama ndugu kama ambavyo sasa tunaishi kama ndugu. Kwa mchanganyiko huu sasa tunaona watu tumeingiliana sana na tumeendelea pia kuwa wamoja na tutaendelea kuwa wamoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge, Waheshimiwa Wabunge tunaendelea. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, *ndc* – KATIBU WA BUNGE:**

## MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali ya kawaida ataingia hapa Mheshimiwa Naibu Spika kunipokea.

*Hapa Naibu Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alikalia Kiti*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali ya kawaida, Ofisi ya Rais, Mheshimiwa Edward Olelekaita Kisau.

Na. 606

### Kuboresha Miundombinu ya Minada – Kiteto

**MHE. EDWARD O. KISAU** auliza:-

Je, lini Serikali itatenga fedha kuboresha miundombinu ya Minada ya Kibaya, Dosidosi na Sunya?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Kiteto kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi ipo kwenye taratibu za kupata fedha za kujenga miradi ya kitaifa ikiwemo minada saba katika Halmashauri ya Kiteto, ikianza na Mnada wa Dosidosi ambapo upembuzi yakinifu na usanifu wa mnada huo umeshafanyika. Aidha, miundombinu ya Minada ya Kibaya na Sunya itaendelea kuboreshwa kwa awamu, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Olelekaita.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na ninaishukuru Serikali kwa majibu mazuri sana na wananchi wa Kiteto wamesikia, lakini pamoja na hayo nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Minada hii ya Sunya na Kibaya ni Minada mikongwe sana; je, kwa nini Serikali haioni haja kutoa fedha hizi ili miradi hii imalizike?

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri atakuwa tayari ili kwa siku za hivi karibuni tutembelee hii minada mitatu ya Dosidosi, Sunya na Kibaya?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba minada hii ya Kibaya na Sunya ni minada ya siku nyingi, mikongwe na ni chakavu. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, amefuatilia mara kadhaa, ni kwamba tayari Serikali imekwishafanyia upembuzi na inatafuta fedha kwa ajili ya kwenda kuijenga. Minada hii inagharimu takribani shilingi milioni 700 kila mmoja. Kwa hiyo, nimhakikishie kwamba tutaanza na Dosidosi na baada ya hapo utafuata Kibaya na Sunya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niko tayari kuambatana naye Mheshimiwa Mbunge. Tutakaa mimi na yeye ili tukubaliane, tuweke ratiba ili twende Kiteto tuikague minada hii ili tuweze kusukuma utekelezaji wake, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, swali sasa la Mheshimiwa Waitara.

Na. 607

**Kuongeza Posho kwa Wenyeviti wa Vijiji, Mitaa na Madiwani**

**MHE. MWITA M. WAITARA** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itaongeza posho kwa Wenyeviti wa Vijiji, Mitaa na Madiwani?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua kazi kubwa inayofanywa na Waheshimiwa Madiwani pamoja na Wenyeviti wa Mitaa na Vijiji katika kutoa huduma mbalimbali kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na halmashauri kuwa na uwezo mdogo wa mapato ya ndani kulipa Waheshimiwa Madiwani, Serikali katika mwaka wa fedha 2021/2022 ilianza kulipa posho kwa Waheshimiwa Madiwani katika halmashauri 168 kati ya 184 zilizopo kwa fedha kutoka Serikali Kuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, posho za Waheshimiwa Madiwani na Wenyeviti bado hazikidhi mahitaji kutokana na halmashauri nyingi kutokuwa na uwezo wa kulipa kupitia mapato ya ndani. Aidha, Serikali imeendelea kubuni vyanzo vya mapato ndani ya halmashauri ili hatimaye posho za Waheshimiwa Madiwani na

Wenyeviti wa Vijiji na Mitaa zilipwe kwa ufanisi zaidi, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waitara.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina maswali ya nyongeza.

Swali la kwanza, ni kwa nini Serikali sasa isitoe mwongozo kwenye halmashauri zile ambazo zinaweza kuwa na mapato ya ziada wakajipangia viwango vya kulipana posho kulingana na shughuli zao na mapato yao badala ya kuweka *flat rate* nchi nzima ilhali halmashauri zinatofautiana katika mapato yale makusanyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, nimekuwa nikiuliza swali hili mara kwa mara na Serikali inasema halmashauri wanapaswa kurejesha 20% kwenda kwenye vijiji ili kusaidia uendeshaji wa vijiji; je, Serikali ipo tayari kuleta takwimu humu Bungeni na kutuambia ni halmashauri gani ambayo imeshapeleka 20% kwenye vijiji kwa sababu utafiti haujafanyika?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali ilishatoa mwongozo kwamba katika malipo ya posho za Wenyeviti wa Vijiji na Mitaa, halmashauri hulipa kulingana na uwezo wa mapato ya halmashauri na ndiyo maana malipo ya Wenyeviti hawa yanatofautiana kulingana na uwezo wa halmashauri, kutoka halmashauri moja kwenda nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaendelea kusisitiza kwamba wakurugenzi wa halmashauri waendelee kuweka kipaumbele kwenye bajeti zao kuhakikisha kwamba wanalipa posho wenyeviti wa serikali za vijiji na mitaa wakati Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa kuboresha malipo kwa ajili ya Waheshimiwa Madiwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili kuhusiana na takwimu za halmashauri ambazo zimepelekewa 20%; Serikali ipo tayari na nikitoka hapa nitawasiliana na Mheshimiwa Mbunge ili niweze kumshirikisha kwenye taarifa hizo ambazo Serikali imewasilisha 20% katika vijiji vyetu, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Waheshimiwa tunaendelea Mheshimiwa Sangu, Mheshimiwa Waziri ana dharura, Mheshimiwa nenda sasa kwenye dharura yako, au swali ni lako vilevile?

Swali la kwako hili? Mheshimiwa Deus Sangu.

Na. 608

**Kujenga Madaraja Yaliyoharibika – Kwela**

**MHE. DEUS C. SANGU** aliuliza: -

Je, Serikali ina mkakati gani wa haraka wa kujenga madaraja yaliyoharibika katika Jimbo la Kwela?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imetenga fedha za dharura kwa ajili ya kurejesha mawasiliano katika maeneo yaliyokatika kutokana na mvua za *El-Nino* zilizonyesha kuanzia mwezi Oktoba, 2023 hadi mwaka huu 2024 ambapo Jimbo la Kwela limepata shilingi milioni 100 kwa ajili ya ujenzi wa Daraja la Kasekela katika Barabara ya Mfinga – Kasekela – Msila. Aidha, katika mwaka 2024/2025 Serikali imetenga shilingi milioni 167 ambapo Daraja la Mfinga katika Barabara ya Mfinga – Kasekela hadi Msila lililoharibiwa na mvua litajengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, usanifu wa Daraja la Ilembo katika Mto Nyinaluzi umekamilika na limekadiriwa kugharimu shilingi bilioni 1.35 ambapo ujenzi wake utaanza pindi fedha zitakapopatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea na usanifu wa daraja moja la Chitete katika Barabara ya Chitete – Chisungamile na madaraja matatu ya *Mnokola One*, *Mnokola Two* na *Mititi One* katika Barabara ya Mnokola – Mititi – Mombo ambapo baada ya usanifu kukamilika Serikali itatafuta fedha za kurejesha miundombinu iliyoharibiwa na mafuriko.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sangu.

**MHE. DEUS C. SANGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru, pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, barabara zinazounganisha Kata ya Lusaka na vijiji vyake, kwa maana ya Barabara ya Ndelema kwenda Mpembano mpaka Kamnyaja na kutoka Lusaka mpaka Kizumbi zina hali mbaya; je, Serikali ina mpango gani wa kwenda kujenga barabara hizi?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili; Barabara ya Liwelyamvula yenye urefu wa kilometa 15 kwenda mpaka Kapenta ina hali mbaya; na hii ni barabara ya kimkakati kwa ajili ya uchumi hasa kilimo cha mpunga wanaitegemea sana barabara hasa kipindi hiki cha mavuno; ninataka kupata kauli ya Serikali, je, wana mkakati gani wa kujenga barabara hii?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kumpongeza Mheshimiwa Mbunge, amekuwa akifuatilia kwa

ukaribu sana maendeleo ya miundombinu ya barabara katika Jimbo lake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali lake ya kwanza Barabara ya Ndelema – Kanyamzaya na Ndelema – Mbembano katika mwaka wa fedha 2022/2023 Serikali ilitenga shilingi milioni 93.139 ambapo ilichonga kilometa tisa na pia kilometa 2.5 ziliwekwa changarawe. Vilevile lilijengwa kalavati moja na mtaro wa meta 200 pia ulijengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2023/2024 Serikali imetenga shilingi milioni 22.26 kwa ajili ya kutengeneza Barabara ya Lusaka – Kizumbi kwa urefu wa kilometa nne.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha ujao wa 2024/2025 Serikali imetenga shilingi milioni 35.2 kwa ajili ya kuendelea kurekebisha barabara hii na hasa matengenezo ya kipande kile cha Ndelema – Kamnyazya. Kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inaendelea kutoa fedha kuhakikisha inarekebisha miundombinu ya barabara hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuhusu…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ndulane, Oh, *sorry*…

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** … swali lake la pili ambapo ameuliza kuhusu Barabara ya Liwelyamvula katika Kata ya Kapenta ambayo ina urefu wa kilometa 15.7, katika mwaka wa fedha 2024/2025 Serikali imetenga shilingi milioni 400 kwa ajili ya kuifungua na kuitengeneza barabara hii kwa urefu wa kilometa 5.8 ikiwa ni awamu ya kwanza. Marekebisho hayo yatafanywa katika Kijiji cha Kikwale kuelekea Liwelyamvula.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa Serikali inatambua umuhimu mkubwa sana wa barabara hii hasa katika kilimo cha mpunga. Serikali

itaendelea kutenga fedha kuhakikisha inaboresha miundombinu ili kutokukwamisha uchumi wa wananchi na hasa kwenye shughuli za kilimo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ndulane.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Naibu Spika, je, Serikali ina mkakati gani wa kujenga upya daraja liliopo katika eneo la Mashine ya Maji lililosambaratishwa na mvua za *El-Nino* ambalo linaunganisha Kata za Kibata na Kipatimu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua kwamba mvua za *El-Nino* zimeleta madhara makubwa sana katika miundombinu hasa ya barabara. Serikali tayari ipo kazini inaendelea kufanya tathmini ili kubaini yale maeneo ambayo miundombinu yake imeharibika sana na mvua ili sasa Serikali iweze kutafuta fedha na kuhakikisha kwamba inarejesha miundombinu hiyo hasa kwa wakati huu Serikali inachukua hatua za kidharura kwenye yale maeneo ambayo mawasiliano yamekatika ili kuhakikisha inarudisha mawasiliano. Kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa Serikali ipo kazini na itafanya jitihada ili kuhakikisha kwamba inakuja kujenga daraja hili. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Bonnah Kamoli.

Na. 609

**Hasara Kutokana na Kukatika kwa Umeme – Segerea**

**MHE. BONNAH L. KAMOLI** aliuliza:-

Je, Serikali inatoa kauli gani kwa wafanyabiashara wanaopata hasara kutokana na kukatika kwa umeme pasipo mpangilio Segerea?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli hapo awali Jimbo la Segerea lilikuwa na changamoto ya kukatika kwa umeme kutokana na kuzidiwa kwa Kituo cha Kupoza Umeme cha Gongolamboto ambapo kuna *transformer* ya *MVA50*. Kwa sasa hali imeimarika baada ya baadhi ya wateja kuhamishiwa kwenye njia ya umeme kutokea Kituo cha Kupoza Umeme cha Kipawa na kwa sasa wanapata umeme kutoka Kituo cha Kupoza Umeme cha Kipawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuendelea kuimarisha zaidi upatikanaji wa umeme Segerea, Serikali kupitia *TANESCO* inatekeleza miradi ya upanuzi wa Kituo cha Kupoza Umeme cha Gongolamboto ambapo kunawekwa *transformer* kubwa ya *MVA120* na ujenzi wa njia mpya ya kusafirisha umeme kutoka Kituo cha Kupoza Umeme cha Ubungo mpaka Tabata ili wateja wengine wapate umeme kutoka Ubungo ambapo kuna *transformer* kubwa ya *MVA120*. Miradi hii itasaidia upatikanaji wa umeme wa uhakika katika Jimbo la Segerea, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kamoli.

**MHE. BONNAH L. KAMOLI:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, pamoja na kwamba kwa sasa wameweza kuboresha na umeme upo kwa kila siku; je, Serikali ina mpango gani kwa wale watu ambao wameunguliwa vitu vyao wakati umeme unazimika na kukatika?

Swali la pili, je, Serikali ina mpango gani kwa watu ambao sasa hivi umeme unaporudi ghafla nyumba zao zinaungua?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na nishukuru kwa swali zuri la Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza tungependa kuwasihi wananchi kuweka vifaa vya kuzuia ama kupunguza nguvu ya umeme kwenye vifaa vyao vya umeme kwa sababu wote tunafahamu kwamba umeme ukikatika ukirudi kwa kasi unaweza kuwa na madhara. Kwa hiyo, tunaendelea kuwasisitiza kuchukua hatua kwa kuweka vifaa ambavyo vinazuia au vinapunguza nguvu ya umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa wale ambao wanapata madhara makubwa kama kuunguliwa nyumba na mengineyo kama inathibitika kwamba tatizo hilo ni kutokana na hitilifu ambazo zimesababishwa na sisi au *TANESCO* basi huwa tunachukua hatua kupitia *EWURA,* sisi na kupitia taratibu ambazo zimewekwa ili waweze kupata fidia, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kakoso.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwanza nitoe nafasi ya kuishukuru Serikali kwa kuleta miundombinu ya umeme wa *REA* kwenye maeneo yote ikiwemo Wilaya ya Tanganyika eneo la Mishamo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo lililopo Mishamo ni kwamba hakuna upelekaji wa umeme kwenye maeneo muhimu ya vijijini hasa kwenye eneo la kituo cha afya na eneo la soko Mishamo; je, ni lini watapeleka nguzo za umeme kwenye maeneo hayo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na nimshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa swali zuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni mkakati wa Serikali kuhakikisha umeme unaenda kwenye kila kijiji na miradi inaendelea kuhakikisha tunamalizia vijiji vichache ambavyo vimebakia. Kwa miradi ya kwenye vitongoji ambayo inabidi umeme uendelee kwenda kufika kwenye vitongoji tayari tumeanza na miradi ya vitongoji 15 na tutaendelea na miradi mingine inayokuja ikiwemo vitongoji 4,000 kwa mwaka wa fedha unaokuja. Pia tutaendelea mpaka kumaliza vitongoji 20,000 ambavyo tumeviweka kwenye mpango kulingana na upatikanaji wa fedha. Maeneo ya vituo vya afya pamoja na taasisi zingine katika eneo hili la Mishamo nalo litaendelea kupelekewa umeme kwa kadri ya upatikanaji wa fedha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kawawa.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninaishukuru sana Serikali kwa kutuletea umeme katika Wilaya yetu ya Namtumbo na wananchi walihamasika sana kuunganisha umeme pia kuweka viwanda vidogo. Hali hii imesababisha umeme kuwa mdogo, kiasi kwamba hauwezi kufikia viwango vya kuzalisha kwenye viwanda tulivyoviweka Namtumbo; je, Serikali inaweza sasa kutuongezea nguvu ya umeme kwa maana ya kuongeza *transfomer* katika maeneo yenye upungufu wa umeme?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na nimshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa swali zuri na vilevile nimpongeze kwa kazi nzuri anayoifanya pale Namtumbo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninatambua kuwa wananchi wa Wilaya ya Namtumbo ni wananchi wachapakazi sana na wanajihusisha sana na kilimo. Kwa hiyo, wameanzisha viwanda vidogo vingi sana kwa ajili ya kuongeza thamani katika mazao yao. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Mradi wa *REA* ulikuwa unalenga kupeleka vijijini, na kwenye kila kijiji ulikuwa una idadi ambayo kidogo iko ndogo kwenye umeme ule wa *three phase*. Nimhakikishie kwamba kwa sasa tunayo mikakati ya kuendelea

kuongeza nguvu za umeme kwenye vijiji na Wilaya ya Namtumbo na tutaiangalia kwa jicho la pekee.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Benaya Kapinga, kwa niaba Mheshimiwa Ntara.

Na. 610

**Kujenga Chuo cha *VETA* – Mbinga**

**MHE. DKT. THEA M. NTARA K.n.y. MHE. BENAYA L. KAPINGA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Chuo cha VETA Wilayani Mbinga?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa sasa inaendelea na utekelezaji wa azma ya kujenga Chuo cha Ufundi Stadi katika kila mkoa na wilaya nchini. Katika mwaka wa fedha 2022/2023, Serikali ilitenga kiasi cha shilingi bilioni 100 kwa ajili ya kujenga Vyuo vya Ufundi Stadi katika wilaya 64 ambazo zilikuwa hazijajengewa Vyuo vya Ufundi Stadi pamoja na Chuo cha Mkoa wa Songwe. Aidha, Wilaya ya Mbinga ni miongoni mwa wilaya 64 ambazo zinajengewa Vyuo vya Ufundi Stadi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa Serikali imeshapeleka kiasi cha shilingi 324,694,243 pamoja na vifaa vya ujenzi ikiwemo nondo na *cement* kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Chuo cha *VETA* cha Wilaya ya Mbinga ambapo ujenzi wa chuo hiki upo katika hatua ya ujenzi wa kuta za boma na ufungaji wa *lintel* pamoja na ukamilishaji wa misingi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ntara.

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru kwa majibu yake, sasa hivi ni miaka miwili tokea chuo hicho kinajengwa polepole. Je, ni lini sasa fedha zitapelekwa kwa haraka ili chuo hicho kikamilike? Swali hili ni la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, Serikali ina mpango gani sasa kuboresha masomo ya ufundi kila mkoa ili yaendane na matakwa ya jamii, kwa mfano, ususi au ufinyanzi? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara kama aifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la lini tutakamilisha ujenzi wa chuo hiki, malengo na Azma ya Serikali ya kuhakikisha kwamba, itakapofika mwezi wa kumi mwaka huu tuweze kukamilisha kwa sababu ujenzi huu tunajenga kwa awamu na ya kwanza tunajenga majengo tisa. Kwa hiyo, dhamira yetu tuweze kukamilisha haya majengo tisa na huduma za masomo ziweze kuanza, ili twende kwenye awamu ya pili ambayo ni majengo mengine tisa, ili hivi vyuo vya wilaya viweze kukamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lake la pili kuhusiana na suala la masomo; kama mnavyofahamu Waheshimiwa Wabunge tumefanya maboresho makubwa ya sera pamoja na mitaala kuanzia elimu ya awali, msingi, sekondari mpaka vyuo vikuu. Vilevile, ni azma ya Serikali kuhakikisha kwamba, mitaala yetu ya elimu ya *VETA* au Ufundi na yenyewe vilevile inakwenda kuboreshwa. Lengo kuu ni kuhakikisha kwamba, kozi zitakazokuwa zinatolewa kwenye vyuo hivi vilingane na shughuli za kiuchumi zinazofanyika kwenye maeneo husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimuondoe wasiwasi Mheshimiwa Dkt. Thea kwamba, masomo yakatayotolewa na kozi

zitakazofundishwa kwenye maeneo mengi ya vyuo hivi zita-*reflect* au zinategemea na shughuli za kiuchumi zinazopatikana katika maeneo hayo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kunti.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, Chuo cha *VETA* kimekamilika lakini changamoto kubwa tuliyonayo ni uwepo wa walimu pamoja na vifaa vya kufundishia. Je, ni lini sasa Serikali itatupatia vifaa vya kufundishia pamoja na walimu, ili chuo hiki kiweze kuwa na tija kwa jamii ya Wanachemba? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naomba kujibu swali dogo la Mheshimiwa Kunti kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli tulikuwa na ujenzi wa awamu ya kwanza wa vile vyuo 25 vya wilaya pamoja na vyuo vinne vya mikoa. Chemba ni miongoni mwa wilaya 25 ambazo zilijengewa vyuo hivyo na vilikamilika mwaka jana na kozi za muda mfupi zilianza kutolewa toka Novemba mwaka jana na mwaka huu tumeanza kozi za muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafahamu kwamba kuna changamoto ya vifaa vya kujifunzia na kufundishia pamoja na watumishi kwa namna moja au nyingine. Nimuondoe hofu Mheshimiwa Mbunge, upande wa watumishi tayari tumeshapata kibali cha kuajiri walimu zaidi ya 571 na mchakato umeanza tumeshaajiri zaidi ya walimu 300 na baadhi yao tumeshawapeleka pale Chemba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utaratibu wa vifaa katika bajeti yetu ya mwaka huu tuna bajeti ya ununuzi wa vifaa vya kujifunzia na kufundishia pamoja na bajeti yetu ya 2024/2025 tuna *token* vilevile ya vifaa. Nikuondoe hofu bajeti hiyo ipo na

tutahakikisha kwamba vifaa vinanunuliwa kwa ajili ya kuwapeleka ndugu zetu wa Chemba. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Chumi.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi, wananchi wa Halmahsauri ya Mji wa Mafinga hatuna Chuo cha *VETA* na tuliomba kujengewa shule maalum ya ufundi mnaita Shule ya Amali. Wananchi wa Mafinga wangependa kusikia je, tupo katika orodha ya kujengewa shule hiyo ya ufundi? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, nikijibu swali dogo la Mheshimiwa Chumi kama ifauatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Chumi amekuwa akifuatilia jambo hili kwa muda mrefu amekuja mpaka ofisini, siyo mara moja au mbili tukakutana na Naibu Katibu Mkuu Dkt. Rwezamula, akakupitisha kwenye orodha na katika orodha ile Mheshimiwa Chumi Wilaya na Jimbo la Mafinga limo mwenyewe uliona na ujenzi ule tunatarajia ifikapo Julai mwaka huu kwa maana ya mwaka ujao wa Fedha, tunatarajia kuanza ujenzi wa hizi Shule za Amali katika majimbo 100 ambayo yalikuwa hayana vyuo vya *VETA*. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Zuena Bushiri.

Na.611

**Ujenzi wa Barabara ya Holili (Rotima) Tarakea**

**MHE. ZUENA A. BUSHIRI** aliuliza: -

Je, lini Serikali itamaliza ujenzi wa Barabara ya Holili hadi Tarakea Wilayani Rombo? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS)* imekamilisha maandalizi ya Nyaraka za Zabuni kwa ajili ya kumpata Mkandarasi wa ujenzi kwa kiwango cha lami wa Barabara ya Tarakea – Holili yenye urefu wa kilometa 52.8, sehemu ya kilometa 10 kuanzia Kijiji cha Munga hadi Kijiji cha Kiwanda. Kwa sehemu iliyobaki Serikali itaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuendelea na ujenzi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Zuena.

**MHE. ZUENA A. BUSHIRI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara ya Rombo ina changamoto kubwa sana ya msongamano wa magari yakiwemo malori ya magari makubwa yanayobeba makaa ya mawe kupeleka Kenya, barabara hiyo ina kona nyingi sana. Je, nini mkakati wa haraka wa Serikali wa kukamilisha mradi huu ili kumaliza changamoto hii? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili, je, ni lini Serikali itatangaza hii zabuni, ili kumpata Mkandarasi na kufanya haraka katika ujenzi wa barabara hii? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza kwa pamoja ya Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na changamoto aliyoieleza ya kona nyingi na miinuko ndio maana Serikali imekuja na mpango wa kujenga barabara ya kutoka Holili hadi Tarakea ambayo wao wamezoea kuiita *Lower Road*. Tumeshakamilisha usanifu kwa barabara yote na tayari tumetangaza kuanza kuijenga kwa kiwango cha lami na tutaanza na kilometa 10.

Mheshimiwa Naibu Spika, lini zabuni zitatangazwa? Naomba kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge, kwa sababu bajeti tumeshapitishiwa, barabara hii tunategemea mwaka wa fedha unaokuja mapema kabisa zitawekwa ili zianze kujengwa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Aida.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi, Mheshimiwa Naibu Waziri watu wa Nkasi tungependa kufahamu mchakato wa Barabara ya Namanyele – Kipili *Port* umefikia wapi kwa kiwango cha lami?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, barabara aliyoitaja tayari tumeshafanya usanifu na kwa sasa Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuijenga hiyo barabara muhimu sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Londo.

**MHE. DENNIS L. LONDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa ikitangaza barabara mpya na kutenga fedha za ujenzi huku ikiacha viporo kwa kusema kwamba inaendelea kutafuta fedha. Je, haya maarifa ambayo wanayafanya ya kupata fedha za barabara mpya kwa nini wasiyatumie kumaliza barabara viporo kama ile ya kutoka Kilosa kwenda Mikumi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, nimuhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba, barabara zote ambazo tumeshaanza, tunaendelea kuzijenga na hatuachi ikiwa ni pamoja na Barabara yake ya Kilosa – Mikumi tulishaanza na nimuombe Mheshimiwa Mbunge kwamba, tutahakikisha tunaikamilisha na kizuri zaidi hiyo barabara kwa umuhimu wake ilikuwa ni *regional road,* sasa inapandishwa kuwa *Truck* barabara kuu.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Mheshimiwa Twaha Mpembenwe. *(Makofi)*

Na. 612

**Ujenzi wa Barabara ya Kibiti – Dimani – Mloka kwa Kiwango cha Lami**

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Barabara ya Kibiti – Dimani hadi Mloka kwa kiwango cha lami?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara ya Kibiti – Dimani – Mloka yenye urefu wa kilometa 100.18 imeingizwa kwenye Mpango wa mwaka wa fedha 2024/2025 kwa ajili ya kuifanyia upembuzi yakinifu na usanifu wa kina. Kazi hii ikikamilika Serikali itatafuta fedha kwa ajili ya kuijenga kwa kiwango cha lami.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Twaha.

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, pamoja na majibu ya Serikali mwaka 2021, 2022, 2023

nimeuliza swali hili majibu ni haya haya na mwaka 2024 nimeuliza swali hili na majibu yanajirudia hivi hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kujua Serikali ina mpango gani wa kujenga Barabara ya Kibiti – Dimani – Mloka ukizingatia barabra hii ipo ndani ya utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, je, Mheshimiwa Waziri upo tayari sasa kuongozana na mimi twende kwa wapigakura wangu kule Watu wa Kibiti, Dimani na Mloka, uende ukawathibitishie kauli ya Serikali? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, Naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge wa Kibiti kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, nikianza na swali la pili, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, nipo tayari na tutapanga twende katika Wilaya ama Jimbo lake tuweze kuwaeleza wananchi hawa Mpango wa Serikali kujenga hiyo barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, Mheshimiwa Mbunge anafahamu kwamba, hii barabara ni kweli ipo kwenye ilani na mwaka ujao tunategemea kuifanyia upembuzi yakinifu na usanifu wa kina. Pia ndiyo barabara inayotumika kwa sasa na wenzetu wa *TANESCO* kupitia Mradi wa Nyerere kupitisha vifaa vyote na wanaifanyia *maintenance*. Tuna uhakika baada ya hapa hiyo azma ya Serikali ya kuijenga kwa kiwango cha lami kwa maana tunaanza usanifu tutaikamilisha na kuijenga, ili pia wananchi waweze kufika kwa urahisi katika Bwawa la Mwalimu Nyerere.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Awack.

**MHE. DANIEL A. TLEMAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi. Je, Barabara ya Karatu – Mang'ola – Matala, Lalabo lini itajengwa kwa kiwango cha lami?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, hii ni barabara kuu ambayo ipo kwenye ilani, Serikali inaendelea kutafuta fedha kuijenga hiyo barabara kwa kiwango cha lami na Mpango wa Serikali ni kuhakikisha kwamba tunafika eneo la Mang'ola ambapo kuna kilimo kikubwa sana cha vitunguu.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Mheshimiwa Cecil Mwambe, kwa niaba Mheshimiwa Mafuwe.

Na. 613

**Mafao ya Wastaafu Waliopigana na Vita vya Kagera**

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE K.n.y. MHE. CECIL D. MWAMBE** aliuliza: -

Je, lini wanajeshi wastaafu waliopigana Vita ya Kagera watalipwa mafao yao?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Wanajeshi wote wastaafu waliopigana vita vya Kagera na waliostahili malipo ya viinua migongo na pensheni walikwishalipwa na wengine wanaendelea kulipwa kwa mujibu wa Sheria ya Pensheni na Viinua Mgongo ya Mwaka 1966, ikiwemo malipo ya ulemavu na kustaafu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imekuwa ikikabiliana na changamoto mbalimbali kuhusiana na Maveterani wa Vita ya Kagera. Miongoni mwa changamoto hizo ni madai ya kuingizwa katika Daftari la Pensheni kwa Maveterani wote licha ya baadhi yao kutokidhi vigezo kwa mujibu wa Sheria, na madai kuwa pensheni ni ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kukabiliana na changamoto hizo, Wizara inaandaa mapendekezo ya maboresho ya Sheria ya Pensheni na Viinua Mgongo ya mwaka 1966.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mafuwe.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, naomba kwa niaba ya Mheshimiwa…

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba utulivu ndani ya Bunge. Mheshimiwa Mafuwe.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, ningependa kufahamu ni lini sasa Serikali italeta sheria hii kwa sababu wanajeshi hawa wastaafu wanapata shida sana?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa Serikali imekubali wapo wanajeshi wastaafu ambao walipigana Vita ya Kagera wanadai Serikali. Je, Serikali haioni ni wakati sahihi sasa kuandaa orodha ya wale wote waliopigana vita, waliolipwa na ambao hawajalipwa, ili watu hawa waache kuhangaika huko mitaani kila mara kudai stahiki zao? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika swali langu la msingi nimeeleza kwamba, maveterani wote waliokuwa wanastahili walishalipwa, kwa hiyo, hakuna anayedai.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jibu la pili linaloendana na hilo ni kwamba, orodha ipo, tunayo orodha ya maveterani wote kwa sababu tunaitumia kwa shughuli mbalimbali. Pia hivi karibuni tuliwaomba waweze kwenda kuhakiki kama kweli wamo katika hiyo orodha na orodha ipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, ambalo lilikuwa la kwanza katika jinsi ulivyowasilisha, lini Serikali italeta sheria ya maboresho? Mchakato huu unaendelea tuna imani katika Bunge lako kwa Mwaka wa Fedha unaokuja sheria hii itakuwa imekamilishwa maboresho haya, ili yaweze kuletwa Bungeni baada ya kukamilisha mchakato ndani ya Serikali.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Matiko, Mheshimiwa Jesca jiandae.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, kumekuwepo na malalamiko ya wastaafu kucheleweshewa mafao yao kwa muda mrefu sana kutokana na sababu mbalimbali ikiwepo malimbikizo ya michango yao na sababu nyingine. Ninataka kujua Serikali imeshachukua hatua gani kwa waajiri ambao wanachelewesha mafao haya kwa wastaafu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mafao ya wastaafu kwa jinsi ambavyo Mheshimiwa Matiko ameliweka, naona ameliweka kwa Serikali kwa mapana yake. Kwa hiyo, wastaafu wanaohusiana na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, hususan na Jeshi la Ulinzi wa Wananchi wa Tanzania, malimbikizo hayapo kwa sababu wameendelea kulipwa, ndio maana nimesema tunafanya uhakiki endapo tutabaini kwamba yapo malimbikizo basi yatalipwa kulingana na taratibu zilizopo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jesca. Mheshimiwa Tarimba jiandae.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, ili tuweze kupata wanajeshi wastaafu tunategemea kuwapata kwenye programu tofauti tofauti tunazofanya ikiwemo wale tunaowa-*recruit* kwa mujibu wa sheria. Je, Serikali inatoa kauli gani kwa wale wanafunzi wote waliomaliza Kidato cha Sita kuripoti katika Kambi za JKT?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Mbunge kwa nia yake njema ya kuhakikisha kwamba, wahitimu wote wa Kidato cha Sita wanaweza kujiunga na Jeshi la Kujenga Taifa. Nimeshajibu swali hili mara nyingi na hata wakati nikiwasilisha Hotuba ya Bajeti mwaka huu tarehe 14 nilieleza pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango uliopo sasa hivi ni nia na dhamira ya Serikali kuhakikisha kwamba, vijana wote hawa wanaweza kuchukuliwa kwa sababu madhumuni ni kuhakikisha kwamba, wanajengewa uzalendo na pia wanaweza kujengewa umahiri na uhodari na kuwa walinzi wa Taifa letu kabla hawajajiunga huko watakapojiunga.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwa sasa tunafanya tathmini ambayo itatuwezesha kujua mahitaji ya kuweza kuwachukua vijana wote. Tathmini hii imekwishafika mbali na baada ya hapo, bila shaka hatuwezi kuwachukua wote kwa wakati mmoja. Kwa hiyo, mpango tutakaokuja nao ni kuona jinsi gani tunaweza tukaboresha miundombinu kwa sababu kikubwa kinachohitajika ni miudombinu ya kuweza kuwachukua vijana hawa kwa bajeti ili tuweze kuwachukua awamu kwa awamu na hatimaye kuwachukua vijana wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa mpango huu unaonesha utakuwa miaka mitano mpaka 10 lakini hatujaukamilisha. Tunaomba kwa sababu tuliahidi hapa Bungeni kuleta mpango huo, basi

tutaleta mpango huo na majibu hayo ili kuweza kuipata picha kamili kwamba tutakwenda namna gani.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tarimba.

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri amekiri kwamba, Serikali inayo orodha ya majina ya hawa wanajeshi wastaafu waliopigana vita na wanajeshi wengine, yamkini orodha hii wanayo Wizarani.

Je, Serikali haioni umuhimu wa kushusha majina haya ya wanajeshi katika ngazi ya wilaya kwa Mkuu wa Wilaya, ili angalau wanajeshi hawa waweze kujitambua kwamba wapo maana yake wanapata tabu ya kujua majina yao yapo wapi? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika uhakiki unaoendelea maveterani wote waliombwa kufika Wilayani. Kwa hiyo, tutaendelea na zoezi hili na kama kuna *veteran* ambaye anaona kwamba anashindwa kupata haki yake anaweza kuwasiliana na sisi wakati wowote kupitia Wizarani au Kambi yoyote iliyo karibu na eneo lake na atahudumiwa ipasavyo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Gwajima.

**MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Kawe lina askari wengi sana wa Jeshi la Wananchi waliostaafu ambao pia, ni wapiga kura wangu. Mheshimiwa Waziri ulikuja kuonananao wakakwambia shida zao. Wanakuomba, kama itakupendeza, je, unaweza tena kufanya kikao uonanenao wakwambie shida zao?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Ni kweli, ninakushukuru sana Mheshimiwa Gwajima kwa kuendelea kuwatetea wastaafu walioko katika jimbo lako pamoja na wastaafu wote nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeweka utaratibu ambao tutaona ni jinsi gani, siyo kuja tu kwenye Jimbo la Kawe, ya kuweza kupata mahitaji yote, ushauri wote na changamoto zote walizonazo wastaafu wetu. Kwa hiyo, utaratibu huo ukikamilika tutaanza kuutekeleza. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, maswali yamekwisha na muda wetu umekwisha.

Wageni waliopo Bungeni asubuhi hii, wapo wageni waliokaa Jukwaa la Spika; wageni wa Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo - Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kutoka Tume ya Mipango; Ndugu Lawrence Mafuru - Katibu Mtendaji Tume ya Mipango; Ndugu Frank Nyabundege - Mkurugenzi Mtendaji Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania; Profesa Joseph Semboja - Makamu Mwenyekiti Timu ya Dira ya Taifa 2050; Ndugu Samwel Kilua - Mkurugenzi Mkazi *Gatsby Africa;* Ndugu Emmil Muchwa - Mkurugenzi wa *Sera UK Tanzania Gree Growth Facility* na Ndugu Kemi Williams - Naibu Balozi/Mkurugenzi wa Maendeleo. *(Makofi)*

Pia yupo Ndugu Evan Tarimo - Mkurugenzi *Bankable;* Ndugu Majaliwa Marwa - Mwakilishi wa Mkazi *UNFPA* Tanzania; Ndugu Anjela Shayo - Mkurugenzi Mipango ya Kitaifa Tume ya Mipango; Profesa Felister Mombo - Mkufunzi Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine *(SUA);* Ndugu Loyal Lyanga - Meneja Miradi Kitaifa Tume ya Mipango na Ndugu Erick Kiraba - Mhariri Mkuu wa Mtandao wa Uwekezaji Tanzania. *(Makofi)*

Wageni wengine wa Mheshimiwa Profesa Kitila Alexander Mkumbo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji ni Maafisa kutoka Wizara ya Mipango na Uwekezaji na familia yake; Ndugu Giliad Teri - Mkurugenzi Mtendaji Kituo cha Uwekezaji

Tanzania *(TIC);* Ndugu Charles Itembe - Mkurugenzi Mkuu *EPZA;* Ndugu Lilian Mbassy - Mkurugenzi Mtendaji *TIB* na Ndugu Evarist Mgangaluma, Msaidizi wa Makamu wa Rais. *(Makofi)*

Pia yupo Ndugu Nehemia Mchechu - Msajili wa Hazina; Ndugu Prosista Prosper Laswai, Mke wa Mheshimiwa Waziri na Ndugu Abigail Kitila Mkumbo, mtoto wa Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Tunao wageni wa Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba - Waziri wa Fedha ambao ni Dkt. Natu Mwamba - Katibu Mkuu; Ndugu Jenifa Omolo - Naibu Katibu Mkuu Huduma za Hazina; Ndugu Amina Shaabani - Naibu Katibu Mkuu Usimamizi wa Fedha za Umma na Ndugu Elijah Mwandumbya - Naibu Katibu Mkuu Usimamizi wa Uchumi. *(Makofi)*

Yupo pia Mheshimiwa Peter Serukamba - Mkuu wa Mkoa wa Iringa; Ndugu Alphayo Kidata - Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania; Ndugu Mcha Hassan Mcha - Naibu Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania; Ndugu David Kafulila - Mkurugenzi Mtendaji *PPP Centre;* Dkt. Baghayo Saqware - Kamishna wa Bima *TIRA*; Ndugu Khadija Said - Naibu Kamishna wa Bima *TIRA* na Ndugu Meshack Anyingisye - Kamishna wa Bajeti. *(Makofi)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge; wapo wageni 12 wa Mheshimiwa Profesa Kitila Alexander Mkumbo - Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, hawa ni Watendaji wa Kata kutoka Jimbo la Ubungo, Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Wapo wageni 38 wa Mheshimiwa Omary Juma Kipanga - Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia. *(Makofi)*

Wapo wanafunzi wa Kada ya Ualimu kutoka Chuo cha Kiislamu Morogoro. *(Makofi)*

Wageni wanne wa Mheshimiwa Dkt. Stephen Kiruswa - Naibu Waziri Madini ambao ni wapiga kura wake kutoka Jimbo la Longido, Mkoa wa Arusha. *(Makofi)*

Tunao wageni 19 wa Mheshimiwa Khamis Yussuf Mussa kutoka Mkoa wa Mjini Zanzibar. *(Makofi)*

Wageni wa Mheshimiwa Stella Alex Ikupa ambaye ni rafiki yake kutoka Segerea, Mkoa wa Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Stanslaus Mabula, huyu ni mdogo wake kutoka Mwanza. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Festo Richard Sanga, ambaye ni rafiki yake kutoka Kyela, Mkoa wa Mbeya na wageni wawili wa Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, ambao ni Wahadhiri kutoka Chuo Kikuu cha *UDOM* na wageni wanne wa Mheshimiwa Vedastus Mathayo, ambao ni wapiga kura wake kutoka Musoma, Mkoa wa Mara. *(Makofi)*

Wageni watano wa Mheshimiwa Michael Constantino Mwakamo, wawekezaji wa *Modern Industrial Park* kutoka Kibaha, Mkoa wa Pwani. *(Makofi)*

Wageni saba wa Mheshimiwa George Mwenisongole, rafiki zake kutoka Jijini Dodoma na wageni tisa wa Mheshimiwa Ally Juma Makoa, rafiki zake kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; yupo Ndugu Lucy Mwanfupa kutoka Jijini Arusha. *(Makofi)*

Wapo pia wanafunzi 84 na walimu 11 wa Shule ya Msingi Mwenyeheri Anuarite kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Pia wapo wanafunzi 11 kutoka Chuo Kikuu cha Kikatoliki cha Afya na Sayansi Shirikishi *(CUHAS Bugando)* Jijini Mwanza na wapo pia wachezaji wanne wa mpira wa miguu kutoka timu mbalimbali nchini Tanzania. *(Makofi)*

Katibu wa Bunge anaomba kuwatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kuwa leo tarehe 13 Juni, kutakuwa na semina

kuhusu Uhuru wa Vyombo vya Habari na Mipaka yake katika Utoaji wa Habari za Bunge. Semina hii itafanyika katika Ukumbi wa Pius Msekwa mara baada ya kusitisha shughuli za Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, wote mnakaribishwa kuhudhuria semina hiyo.

Katibu.

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2023 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu Lipokee na Kujadili Taarifa ya Hali ya Uchumi kwa mwaka 2023 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2024/25. Pamoja na Hotuba hii, ninawasilisha Kitabu cha Taarifa ya Hali ya Uchumi kwa Mwaka 2023 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2024/25. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa zilizopo katika kitabu hicho ndiyo msingi wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2024/25 ambayo Mheshimiwa Waziri wa Fedha ataiwasilisha katika Bunge lako Tukufu, leo alasiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote ninamshukuru Mwenyenzi Mungu kwa kutuwezesha kuendelea kushiriki Mkutano wa 15 wa Bunge hili la 12 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tukiwa na afya njema, amani na utulivu. Aidha, ninamshukuru

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa kuendesha majadiliano ya Bunge hili la Bajeti kwa umahiri mkubwa tangu siku Mheshimiwa Waziri Mkuu alipowasilisha hotuba yake ya Bajeti na baadaye hotuba za bajeti za Mawaziri wenzangu hadi leo hii tunapoelekea kuhitimisha kwa hotuba yangu hii na baadaye, alasiri Hotuba ya Bajeti ya Serikali itakayosomwa na Waziri wa Fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, uniruhusu nitoe salamu zangu za pole sana kufuatia msiba ambao tumetangaziwa leo asubuhi wa Mheshimiwa Dkt. Shogo Mlozi aliyekuwa Mbunge wa Bunge la Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kumshukuru kwa dhati Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa jinsi anavyoendelea kuliongoza Taifa letu kwa weledi, umahiri na utulivu mkubwa. Katika kipindi chake cha miaka mitatu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ameonesha weledi na kuthibitisha uadilifu na uzalendo wa hali ya juu kwa nchi yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, zaidi ya yote amethibitisha kuwa kiongozi muungwana na mpenda haki. Kupitia falsafa yake ya uongozi ya *4R* amejenga maridhiano mapana ya kijamii na kisiasa na kuweka mazingira sawia ya kufanya siasa kwa vyama vyote nchini. Ametoa uhuru wa kutosha wa kutoa maoni bila woga wala vitisho huku akionesha ustahimilivu wa hali ya juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kiongozi wetu ameleta mageuzi makubwa katika kuweka mazingira bora ya uwekezaji na kufanya biashara. Ameimarisha Sekta za Kilimo, Mifugo, Uvuvi na Madini na kuwapa matumaini mapya mamilioni ya wakulima, wafugaji, wavuvi na wachimbaji wadogo wa madini. Hakika anaijenga upya nchi yetu na kupitia uongozi wake Serikali na nchi yetu iposalama.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, ninawashukuru Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa

Tanzania, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, kwa jinsi wanavyomsaidia Mheshimiwa Rais katika kusimamia shughuli za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawashukuru Dkt. Tausi Mbaga Kida, Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Mipango na Uwekezaji, Ndg. Lawrence Nyasebwa Mafuru, Katibu Mtendaji Tume ya Mipango na watumishi wote wa Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji na watumishi wa Tume ya Mipango kwa ushirikiano wao katika kuandaa hotuba na kitabu ambacho tumewasilisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza sana Mheshimiwa Stanslaus Haroon Nyongo, Mbunge wa Maswa Mashariki, kwa heshima aliyopata ya kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji. Ninamfahamu Mheshimiwa Nyongo katika kipindi cha uhai wa Bunge hili la 12 nikiwa nimefanyanaye kazi kwa karibu kwa iliyokuwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii ambapo yeye alikuwa Mwenyekiti wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni mtu makini, mtulivu, msikivu, mpana wa fikra na mwenye kuthamini sana mawazo na maoni ya wenzake. Ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kutuletea kiongozi huyu tusaidianenaye katika kuongoza ofisi yake hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naungana na Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na Mheshimiwa Spika kumpongeza sana Mheshimiwa Khamis Yussuf Mussa, Mbunge wa Kwahani, kwa ushindi mkubwa alioupata huko Kwahani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2023 na Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Mwaka 2024/25 zimeandaliwa kwa kuzingatia dhana ya ushirikishwaji mpana wa wadau katika hatua mbalimbali za maandalizi, ikiwemo

maoni ambayo Waheshimiwa Wabunge waliyatoa katika Bunge la Novemba, mwaka jana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba sasa nifanye mapitio ya Mwenendo na Mwelekeo wa Hali ya Uchumi nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwaka 2023, Pato halisi la Taifa lilifikia shilingi trilioni 148.3 kutoka shilingi trilioni 141.2 Mwaka 2022, sawa na ukuaji wa asilimia 5.1 ikilinganishwa na asimilia 4.7 Mwaka 2022. Ukuaji huo umechangiwa na jitihada mbalimbali zilizochukuliwa na Serikali, ikiwemo mikakati ya kukabiliana na athari za vita kati ya Ukraine na Urusi pamoja na uwekezaji wa kimkakati katika miundombinu ya nishati, maji, afya, elimu na usafirishaji. Kuongezeka kwa uzalishaji wa madini, hususan dhahabu na makaa ya mawe, na kuongezeka kwa mikopo kwa Sekta Binafsi iliyochachua shughuli za kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfumuko wa bei ulifikia asilimia 3.1 katika kipindi kilichoishia Mwezi Aprili 2024 ikilinganishwa na asilimia 4.3 katika kipindi kama hicho mwaka 2023. Aidha, mfumuko wa bei ulifikia wastani wa asilimia 3.8 mwaka 2023 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 4.3 Mwaka 2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha hadi Machi, samahani. Kwa mujibu wa Taarifa ya Dunia ya Maendeleo ya Watu ya Mwaka 2023, Tanzania imeendelea kupiga hatua kwa kuzingatia Fahirisi ya Maendeleo ya Watu *(Human Development Index)* ambapo ilifikia 0.532 Mwaka 2022, ikilinganishwa na 0.529 Mwaka 2021. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tathmini ya muda mrefu ya uchumi wa Tanzania inaonesha masuala makubwa matatu. Mosi, uchumi umekuwa stahimilivu na kukua katika hali endelevu, licha ya changamoto zilizoyumbisha uchumi wa dunia katika vipindi mbalimbali ikiwemo mabadiliko ya tabia nchi, Ugonjwa wa UVIKO – 19 na vita mbalimbali ambazo zinaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kuongezeka kwa mauzo ya bidhaa za Tanzania nje ya nchi mwaka hadi mwaka. Kwa mfano, thamani ya mauzo ya bidhaa za Tanzania nje ya nchi iliongezeka kutoka Dola za Kimarekani milioni 975 Mwaka 2000 hadi kufikia dola za Kimarekani bilioni 5.63 Mwaka 2022 na kufikia Dola za Kimarekani bilioni 8.20 mwaka 2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali hii ilisababisha kuongezeka kwa uwiano kati ya mauzo ya bidhaa nje ya nchi na pato la Taifa kutoka asilimia 9.6 mwaka 2000 hadi asilimia 20.9 mwaka 2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, aina ya bidhaa za Tanzania zinazouzwa nje ya nchi zimebadilika katika kipindi cha miongo miwili iliyopita. Kwa mfano, katika miaka ya 2000 asilimia 57 ya mauzo ya bidhaa zetu nje ya nchi ilihusisha mazao ya kilimo na yalienda katika masoko ya Ulaya, Marekani na Afrika kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, miaka 20 baadaye mauzo ya bidhaa za Tanzania nje ya nchi yametawaliwa zaidi na madini na bidhaa nyingine zinazouzwa katika masoko ya Asia na nchi za Afrika. Kwa mfano, asilimia 49 ya bidhaa zilizouzwa nje ya nchi Mwaka 2023 ilikuwa ni madini, ikifuatiwa na bidhaa za viwandani asilimia 17 na kilimo asilimia 12.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mwelekeo mzuri wa ukuaji wa uchumi wa Tanzania katika kipindi cha miongo miwili iliyopita, mambo matano ni bayana kuhusu uchumi wa Tanzania. Mosi ni ukuaji wa uchumi umekuwa ukihusisha zaidi sekta chache ambazo hazijaajiri watu wengi kutoka katika kaya maskini. Sekta hizi ni pamoja na sanaa kwa asilimia 17.7, fedha na bima asilimia 12.2, madini asilimia 11.3 na malazi na chakula asilimia 8.3. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ambazo zilitarajiwa kuajiri watu wengi zilikua kwa kasi kidogo. Sekta hizi ni pamoja na kilimo asilimia 4.2, viwanda asilimia 4.3 na biashara 4.2.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, ukuaji wa uchumi nchini umekuwa ukitegemea uwekezaji wa umma katika miundombinu na Sekta Binafsi haijaonekana kuchukua nafasi yake kikamilifu kama ilivyotarajiwa. Uwekezaji wa Sekta Binafsi ndio unaotarajiwa kuchochea zaidi ajira na uzalishaji viwandani.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, mauzo ya bidhaa ya nje ya nchi yameendelea kutawaliwa zaidi na bidhaa ambazo hazijaongezewa thamani. Kwa mfano, wakati uzalishaji wa viwandani ulitarajiwa kuchangia asilimia 24.4 ya mauzo ya bidhaa za Tanzania nje ya nchi ifikapo Mwaka 2025, mchango wa sekta hii kwa wastani wa miaka mitano ulikuwa asilimia 17.14. Nchi yetu bado inanunua zaidi kutoka nje kuliko tunavyouza na hivyo, bado tuna urari mkubwa katika biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, thamani ya mauzo ya bidhaa za Tanzania nje ya nchi kama nilivyosema kwa Mwaka 2023, ilikuwa Dola za Kimarekani bilioni 8.2 ukilinganisha na thamani ya manunuzi ambayo tuliyafanya yaliyofikia Dola za Kimarekani bilioni 13.7.

Mheshimiwa Naibu Spika, tano, uchumi umeendelea kukua kwa kasi zaidi katika maeneo ya mijini kuliko vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuhakikisha kuwa ukuaji wa uchumi unakuwa na athari chanya katika kuinua kiwango cha maisha ya watu wetu na kupunguza umaskini, mipango ya muda mfupi na mrefu ya Serikali ijayo itajikita zaidi katika kuhakikisha kuwa, ukuaji wa uchumi wetu unakuwa jumuishi, unapunguza umaskini, unazalisha ajira, unaleta ustawi na unachochea mauzo ya bidhaa zilizoongezwa thamani nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, malengo na shabaha za ukuaji wa uchumi wa jumla kwa mwaka ujao ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mosi. Kuongezeka kwa kasi ya ukuaji wa Pato la Taifa kufikia 5.4% mwaka 2024, kutoka ukuaji halisi wa 5.1% mwaka 2023.

(i) Kuendelea kudhibiti mfumuko wa bei na kuhakikisha kuwa unabaki kwenye wigo wa tarakimu moja ya wastani wa asilimia kati ya tatu na tano katika muda wa kati;

(ii) Mapato ya ndani kufikia 15.8% ya Pato la Taifa mwaka 2024/2025 ikilinganishwa na matarajio ya 15.4% mwaka 2023/2024;

(iii) Mapato ya kodi kufikia 12.9% ya Pato la Taifa mwaka 2024/2025 kutoka matarajio ya 12.6% mwaka 2023/2024; na

(iv) Kuwe na nakisi ya bajeti isiyozidi asilimia tatu ya Pato la Taifa na kuwa na akiba ya fedha za kigeni kwa kiwango cha kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi minne.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nifanye tathmini ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2023/2024. Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2023/2024 ni wa tatu katika utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2021/2022 – 2025/2026. Mpango huu ulilenga kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi na kuchochea maendeleo ya watu na mpango huu unavyovipaumbele vitano ambavyo ni kuchochea uchumi shirikishi na shindani, kuimarisha uwezo wa uzalishaji viwandani na utoaji huduma, kukuza uwekezaji na biashara na kuchochea maendeleo ya watu na mwisho kuendeleza rasilimali watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jumla ya programu na miradi 193 ikiwemo miradi ya kielelezo 17 inatekelezwa katika kufikia malengo na mpango tuliyojiwekea katika mpango wa maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nipitie baadhi ya mafanikio 10 yaliyopatikana kutokana na utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa miaka mitano pamoja na mpango uliyopita wa mwaka 2023/2024.

(i) Kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao ya kilimo kutoka tani milioni 30.5 mwaka 2021 hadi kufikia tani milioni 36.4 mwaka 2022/2023. Uzalishaji wa mazao ya nafaka umeongezeka kutoka tani milioni 9.04 mwaka 2021 hadi kufikia tani milioni 11.4 mwaka 2022/2023. Hali hii imeimarisha hali ya usalama wa chakula nchini, ambapo hali ya utoshelevu wa chakula imefikia 24% mwaka 2022/2023 ikilinganishwa na lengo la kufikia 130% ifikapo mwaka 2025/2026; *(Makofi)*

(ii) Kuongezeka kwa uzalishaji wa umeme kutoka *megawatt* 1,872.1 mwaka 2022/2023 hadi kufikia *megawatt* 2,138 mwezi Machi mwaka 2024. Hii ni kutokana na kuanza uzalishaji wa umeme katika miradi ya bwawa la Mwalimu Nyerere *megawatt* 235, Mradi wa Kinyerezi moja *megawatt* 160 na Mradi wa Rusumo *megawatt* 80. Aidha jumla ya vijiji 11,837 sawa sawa na 99.37% ya vijiji vyote Tanzania Bara vimeunganishwa na umeme kufikia Disemba 2023; *(Makofi)*

(iii) Kuongezeka kwa watumiaji wa mtandao wa *internet* kutoka 43% mwaka 2019/2020 hadi kufikia 58.1% mwaka 2023/2024. Kuongezeka kwa idadi ya watu waliofikiwa na masafa ya mawasiliano kutoka 45% mwaka 2019/2020 hadi 86% kwa mtandao wa *3G* na 79% kwa mtandao wa *4G* mwaka 2023/2024 na kuongezeka kwa maeneo yaliyofikiwa na masafa ya mawasiliano kufikia 70%. Aidha kumekuwa na ongezeko kwa idadi ya kaya zinazotumia mfumo wa anuani ya makazi na misimbo ya Posta kutoka kaya 450,980 mwaka 2019 sawa na 32% hadi kufikia kaya 11,126,234 mwaka 2023 sawa na 78% ya kaya zote Tanzania;

(iv) Kuendelea kuimarika kwa mazingira ya biashara na uwekezaji ambapo miradi ya uwekezaji iliyosajiliwa na Kituo cha Uwekezaji Tanzania iliongezeka kutoka miradi 207 kwa mwaka 2020 hadi kufikia miradi 526 kwa mwaka 2023 na kiwango cha mitaji kilichovutia kufikia Dola za Kimarekani bilioni 5.7 mwaka 2023. Aidha idadi ya ajira inayotokana na miradi ya uwekezaji imeongezeka kutoka ajira 17,385 mwaka 2020 hadi kufikia ajira 137,010 mwaka 2023;

(v) Kuongezeka kwa thamani ya mauzo ya bidhaa za Tanzania nje ya nchi kutoka Dola za Kimarekani bilioni 5.63 mwaka 2020 hadi kufikia Dola za Kimarekani bilioni 8.20 mwaka 2023. Aidha katika kuimarisha uwezo wa uzalishaji viwandani, kiwango cha mauzo ya bidhaa za viwandani kiliongezeka kwa 20.8% kutoka Dola za Kimarekani bilioni 1.1 mwaka 2021 na kufikia Dola za Kimarekani bilioni 1.3 mwaka 2023 na hadi kufikia Dola za Kimarekani bilioni 1.4 mwaka 2023;

(vi) Kiwango cha uandikishaji wanafunzi wa elimu ya msingi ilifikia 108.5% mwaka 2022 ikiwa ni zaidi ya lengo la kufikia 100% ifikapo mwaka 2025. Aidha kiwango cha uandikishaji wanafunzi wa sekondari kimeongezeka kutoka 47.4% mwaka 2021 hadi 48.2% mwaka 2022 ikiwa ni zaidi ya lengo la kufikia 48% mwaka 2025/2026;

(vii) Kupungua kwa vifo vinavyotokana na uzazi kutoka vifo 556 kwa vizazi hai 100,000 mwaka 2014/2015 hadi kufikia vifo 104 kwa kila vizazi hai 100,000 mwaka 2022;

(viii) Hali ya upatikanaji wa maji vijijini imeboreka kufikia 79.6% na mijini imefikia 91.5%;

(ix) Mapato ya utalii yameongezeka kutoka Dola za Kimarekani bilioni 2.6 mwaka 2019/2020 hadi kufikia Dola za Kimarekani bilioni 3.4 mwaka 2023/2024 sawa na

ongezeko la 23% ukilinganisha na jitihada za kufikia Dola za Kimarekani bilioni sita ifikapo mwaka 2025/2026; na

(x) Kama sehemu ya mafanikio ya utekelezaji wa Falsafa ya *4R* hususani ya mageuzi, utawala wa sheria umeendelea kuimarika na demokrasia nchini imeendelea kupanuka kunakothibitishwa na kushamiri kwa uhuru wa kutoa maoni bila hofu yakusumbuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nipitie malengo na vipaumbele vya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2024/2025. Vipaumbele vya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2024/2025 vimezingatia Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano ambao nimekwisha kuueleza, umezingatia pia Ilani ya CCM kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 na sera na mikakati mbalimbali ya kisekta. Aidha mpango umezingatia mipango mingine ya kikanda na kimataifa zikiwemo: Dira ya Maendeleo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya Mwaka 2050; Dira ya Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini Mwa Afrika *(SADC)* ya Mwaka 2050 na Ajenda 2063 ya Maendeleo ya Afrika na Maendeleo Endelevu ya Mwaka 2030.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhakikisha kuwa ukuaji wa uchumi wetu unakuwa jumuishi, unapunguza umaskini, unazalisha ajira nyingi, unaleta ustawi na unachochea mauzo ya bidhaa zilizoongezwa thamani nje ya nchi, ninaomba kusisitiza masuala 10 ambayo Serikali ya Awamu ya Sita ya Chama Cha Mapinduzi inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mwenyekiti wa CCM, itayapa msukumo wa kipekee katika mwaka ujao wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza, tutaendelea kuwekeza katika kukuza uzalishaji katika sekta za kilimo kwa kuhamasisha na kuwezesha matumizi ya mbegu bora, matumizi ya mbolea, kilimo cha umwagiliaji na matumizi ya zana za kisasa katika kilimo. Kama tunavyofahamu uchumi wa viwanda tunaojaribu kuujenga malighafi zake nyingi zinategemea kilimo. Aidha katika

kipindi cha muda mfupi na muda wa kati, Watanzania wengi wataendelea kuajiriwa na kujiajiri katika sekta ya kilimo. Hivyo hatuwezi kuzungumzia mapinduzi ya viwanda bila kuzungumzia mapinduzi ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, tutaendelea kuweka na kutekeleza mkakati wa kuchochea uwekezaji katika viwanda vyenye kulenga kuzalisha bidhaa zitakazoifanya nchi yetu ijitosheleze kwa mahitaji ya bidhaa muhimu na kukuza mauzo ya bidhaa zilizoongezwa thamani nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu, tutaendelea kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji ili kuchochea ukuaji wa sekta binafsi hususani tukilenga kuweka mazingira maalumu ya kukuza na kuimarisha biashara na uwekezaji mdogo na wakati *(small and medium enterprises)*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, tutaendelea kulinda na kusimamia matumizi endelevu ya rasilimali za Taifa zikiwemo: gesi, madini, misitu, bandari, maziwa na kadhalika. Mwelekeo wa kisera wa Serikali ya CCM ni kutumia rasilimali hizi kama msingi wa kujenga uchumi wa viwanda na kuweka mkazo katika kuongeza thamani mazao yatokanayo na rasilimali za Taifa. Serikali itahakikisha kuwa nchi yetu inapunguza na hatimaye kuzuia kabisa kusafirisha kama malighafi rasilimali zinazovunwa kutoka katika ardhi, misitu na maji ya Tanzania, bali kuweka mazingira ya kisera na kisheria yatakayohakikisha kuwa rasilimali hizi zinachakatwa na kuongezwa thamani nchini kabla ya kusafirishwa nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tano, tutaendelea kuzingatia nafasi ya madini katika kuendelea kukuza ujazo wa mauzo ya bidhaa zetu nje ya nchi na kwa kuzingatia umuhimu wa madini ya kimkakati (*strategic mineral resources)* katika kutimiza azma ya dunia ya kuzalisha nishati safi na salama kwa mazingira, tutaweka mazingira mahususi kwa lengo la kuvutia wawekezaji watakaokuwa tayari kujenga viwanda vya kuongeza thamani ya madini hapa nchini. Tunataka kuona tunasafirisha nje ya nchi betri

za magari na siyo madini yetu ya kimkakati. Tumesema wazi kwamba wakati dunia inaelekea mwaka 2050 ikizungumzia kuwa na *zero emission* tunataka kuona kwamba rasilimali hizi zinatusaidia na sisi ifikapo mwaka 2050 tunakuwa na *zero poverty*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la sita, kwa kuzingatia kuwa rasilimali watu ndiyo *engine* ya maendeleo na ndiyo rasilimali kubwa zaidi tuliyonayo kama Taifa na kwa kuzingatia kuwa idadi kubwa ya Watanzania 76% ni watoto na vijana chini ya umri wa miaka 35. Serikali itaendelea kuwekeza katika kuhakikisha kuwa nchi yetu ina rasilimali watu wa kutosha na wenye ubora unaokidhi mahitaji ya dunia ya leo na kesho. Hivyo basi elimu na mafunzo yataendelea kuwa kipaumbele mama katika mipango ya maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la saba, kwa kuzingatia nafasi na umuhimu wa miundombinu ya usafiri na usafirishaji pamoja na miundombinu ya kidijiti katika kuchochea maendeleo ya uchumi, Serikali itaendelea kuwekeza katika ujenzi na utunzaji wa miundombinu hii kwa kushirikiana na sekta binafsi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la nane, tutaendelea kuimarisha uzalishaji wa nishati kama nyenzo muhimu katika ujenzi wa uchumi wa viwanda pamoja na kutekeleza kikamilifu mkakati wa miaka 10 wa matumizi ya nishati safi ya kupikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tisa, tutaendelea kuimarisha upatikanaji wa huduma bora na za kutosheleza za jamii zikiwepo afya, maji na umeme hususani katika maeneo ya vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kumi, kwa kuzingatia kuwa sehemu kubwa ya wananchi wetu wanaishi vijijini na katika kuchochea ukuaji wa uchumi jumuishi na katika kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi katika maeneo ya vijijini, Serikali itaweka mkazo maalumu katika kuchochea maendeleo vijijini kwa kuchukua hatua tano zifuatazo: -

(i) Kuendelea kuwekeza katika ujenzi wa miundombinu ya barabara na mawasiliano vijijini kwa kuimarisha zaidi na kuiwezesha *TARURA*; *(Makofi)*

(ii) Katika kuongeza kasi na kiwango cha wananchi wa vijijini kutumia teknolojia ya habari katika shughuli za kiuchumi na kijamii, Serikali itaendelea kutekeleza Mradi wa Mawasiliano Vijijini *(Mobile Network Rural Coverage Project)* na tutaanzisha na kutekeleza Mpango Maalum wa Kuunganisha Vijiji Kidijiti *(Rural Broadband Programme)*; *(Makofi)*

(iii) Serikali itapitia upya Mfumo wa Uuzaji wa Mazao ya Kilimo, Mifugo, Uvuvi na Misitu kwa lengo la kurahisisha na kuwezesha mazingira ya kufanya biashara vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado wakulima wetu, wavuvi na wafugaji vijijini wanasumbuliwa sana katika kufanya biashara, hatuna namna ya kuondoa umaskini katika nchi hii zaidi ya kuwezesha wananchi wetu kufanya biashara ili wajipatie kipato. Kwa hivyo tunatoa wito kwa watumishi wetu wa umma waweke mazingira rahisi kwa wananchi vijijini kufanya biashara kutokana na mazao yao ya kilimo, mifugo, uvuvi na misitu. *(Makofi)*

(iv) Tutaweka mazingira maalumu katika kuvutia ujenzi wa viwanda vidogo vijijini kwa lengo la kufanya ongezeko la awali la thamani *(primary processing)* katika sekta za kimikakati ikiwemo kilimo, mifugo, uvuvi na misitu. Serikali itatumia sera za kifedha na kikodi ili kuvutia wawekezaji katika maeneo ya vijijini ili mazao ya kilimo, mifugo, uvuvi na misitu yatoke vijijini yakiwa yameanza kufanyiwa uchakataji wa awali *(semi processed)*. Viwanda vya vijijini vitabakisha thamani kubwa vijijini na kutoa nafasi ya ajira kwa vijana na wanawake ambao wengi wao sasa wana elimu ya sekondari. Katika hatua hii tutahitaji kulipanga upya Shirika la Viwanda Vidogovidogo *(SIDO)*; na *(Makofi)*

(v) Tutapitia upya Sera za Kifedha, sheria na kanuni zinazosimamia mikopo kwa lengo la kuzisukuma taasisi za kifedha, kuelekeza mikopo katika sekta za uzalishaji hususani kilimo, ufugaji, uvuvi na wachimbaji wadogo wa madini vijijini. Lengo ni kuwa na sera ya wazi kuhusu ugharamiaji wa sekta za uzalishaji hapa nchini. Kwa sasa kama unavyofahamu pamoja na kwamba wananchi wetu wengi wanajihusisha na kilimo, mifugo na uvuvi lakini mikopo mingi bado haiwafikii. Katika hatua ya muda mfupi Serikali kupitia Wizara ya Kilimo itaanzisha hati fungani ya usalama wa chakula *(food security bond)* kuanzia mwaka ujao wa fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia mpango huu ninaowasilisha hapa na mipango ambayo waheshimiwa Mawaziri wa Kisekta waliwasilisha kupitia hotuba zao za bajeti pamoja na michango ya Waheshimiwa Wabunge hakuna shaka kuwa sisi Wabunge na Watanzania kwa ujumla tunaijua nchi yetu vizuri, tunajua tulipo na tunajua tunapotaka kwenda na namna ya kufika huko. Hata hivyo, kuwa na mipango mizuri ni jambo moja na kuitekeleza mipango hiyo kikamilifu ni jambo lingine. Hivyo katika hatua inayofuata baada ya Bunge lako kupitisha mipango na Bajeti ya Serikali ni muhimu kujipanga katika kusimamia utekelezaji wake kikamilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imejipanga vizuri kuimarisha mfumo wa usimamizi na ufuatiliaji wa utekelezaji wa programu na miradi ambayo Bunge lako Tukufu limepitisha hapa. Mfumo huu umejengwa katika nguzo tatu ambazo ni:-

(i) Kuainisha vipaumbele bayana na kwa uwazi kwa kila sekta *(prioritization)*;

(ii) Nidhamu ya utekelezaji *(discipline of implementation);* na

(iii) uwajibikaji *(accountability)*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza mfumo huu kuanzia mwaka ujao wa fedha unaoanza tarehe 01/07/2024 Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ameelekeza Serikali kutekeleza hatua nne zifuatazo katika kuimarisha mfumo wa usimamizi wa miradi na programu za maendeleo:-

(i) Kila sekta inayotekeleza programu na miradi ya maendeleo itaweka bayana malengo na matokeo ya utekelezaji yanayopimika *(key performance indicators)* pamoja na kazi mbalimbali zitakazofanyika katika kufikia malengo hayo;

(ii) Taarifa ya utekelezaji itawasilishwa kwa Waziri wa sekta husika kwa kila wiki. Waziri husika atawasilisha taarifa ya utekelezaji kila mwezi kwa Tume ya Mipango; *(Makofi)*

(iii) Tume ya Mipango itatoa taarifa ya utekelezaji wa programu ya miradi ya maendeleo kwa umma na matokeo yaliyopatikana kila mwaka kupitia tukio la wazi; *(Makofi)*

(iv) Kwa kuzingatia Kifungu cha saba cha Sheria ya Tume ya Mipango 2023, Tume itakuwa na mamlaka ya kuitisha vikao vya viongozi wa juu wanaosimamia utekelezaji wa programu na miradi ya maendeleo kwa lengo la kuratibu uchambuzi wa changamoto za utekelezaji na kusukuma utekelezaji wa shughuli zinazokubalika, zilizokubalika ili kuondoa vikwazo vya utekelezaji, kuboresha utaratibu na kupata taarifa kwa muda muafaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo ni kuondokana na kupimana kwa kazi zilizofanyika lakini kuelekea kwenye kupimana kwa kuzingatia matokeo yaliyopatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2024/2025 niliyowasilisha ni sehemu ya utekelezaji wa

Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2021/2022 – 2025/2026 ambao umetokana na Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa ajili ya uchaguzi wa mwaka 2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, msingi wa Sera za CCM ni maendeleo ya watu. Tunapowekeza katika ujenzi wa miundombinu na barabara, reli, anga na kadhalika tunafanya hivyo kama nyenzo ya kuleta maendeleo ya watu. Tunapowekeza katika kuongeza idadi ya majengo ya shule kutatafsiriwa tu kama tendo la maendeleo ya watu kama hatimaye majengo hayo yanatumika kuongeza ujuzi na elimu kwa watu wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo hivyo kuongeza kwa mazao ya chakula na biashara ni tendo la maendeleo kama hatimaye watu wetu watapata chakula bora na kwamba mazao ya biashara hatimaye yatauzwa kwa bei nzuri na kuwapatia wakulima fedha zitakazotumika kununulia vitu vitakavyoboresha afya zao na kuwapa furaha zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango tuliyowasilisha na mipango yote inayowasilishwa katika Bunge hili ni kwa ajili ya maendeleo ya watu na ndiyo maana viashiria vya mafanikio vilivyowekwa katika Mpango wa Taifa wa Maendeleo vinazingatia kupima matokeo yanayozingatia maendeleo ya watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hayati Benjamini Mkapa, Rais wa tatu wa Tanzania aliwahi kutuasa, ninanukuu; "Kuzeeka peke yake ndiyo inaweza kutokea bila kupanga lakini maendeleo ya kweli yanatokana na mipango mizuri na nidhamu ya utekelezaji wa mipango hiyo." Akihutubia katika mkutano wa Halmashauri Kuu ya CCM Dodoma tarehe 25/08/2004 Rais Mkapa alisisitiza umuhimu wa mipango mizuri kwa kusema; "Kuongoza ni kupanda kwanza, mipango mizuri huleta maamuzi mazuri kimkakati na kiutendaji." *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Chama Cha Mapinduzi ni chama kiongozi na kuongoza ni kuonesha njia. Ni imani yangu kuwa

Mpango wa Maendeleo wa Taifa tuliowasilisha hapa ni mpango sahihi unaoakisi maono ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan na Ilani ya CCM. Sisi kama Serikali tumejipanga vizuri kutekeleza mpango huu. Ninapohitimisha, ninaomba kutumia fursa hii kuwashukuru wadau wote wa maendeleo wakiwemo Waheshimiwa Wabunge, Waheshimiwa Madiwani, Washirika wa Maendeleo, taasisi za elimu na tafiti, sekta binafsi, asasi za kiraia, taasisi za dini na wananchi wote kwa namna wanavyojitoa na kushiriki kikamilifu katika hatua mbalimbali za utekeleza wa programu na miradi ya maendeleo na kuimarisha uchumi wa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wadau hawa wamekuwa na mchango mkubwa katika utekelezaji wa shughuli mbalimbali za maendeleo. Kwa msingi huo niwaombe kuendelea kushirikiana na Serikali yetu inayoongozwa na Jemedari shupavu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nichukue nafasi hii kumshukuru sana mke wangu na rafiki yangu wa karibu Prosista Laswai na leo yupo hapa pamoja na watoto wetu Tandu, Kalvin na Nsumbu wamewakilishwa na mdogo wao Nsumbu kwa upendo wao na ushirikiano wanaonipa katika kutekeleza majukumu yangu ya kifamilia na kiofisi kama Mbunge wa Jimbo la Ubungo na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji. Ninawapenda sana kama wao wanavyonipenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa umuhimu mkubwa ninaomba niwashukuru wananchi wenzangu wa Jimbo la Ubungo kwa ushirikiano wanaonipatia tunapoendelea kutekeleza Ilani ya Chama Cha Mapinduzi katika jimbo letu ambalo linalenga kujiletea maendeleo ikichagizwa na kauli mbiu yetu; "Ubungo yetu fahari yetu."

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba yangu na kitabu ambacho tumewasilisha inapatikana pia katika tovuti ya Wizara yetu *www.planninginvestment.go.tz*.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo ninaomba sasa Bunge lako Tukufu lipokee na kujadili Taarifa ya Hali ya Uchumi ya mwaka 2023 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa mwaka 2024/2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono.

Waheshimiwa Wabunge, kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri, *scientific presentation*. Nichukue nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa mipango kabambe na niwahakikishie kuwa Bunge litashirikiana na Serikali *to walk the talk*.

Tuna mgeni wa Mbunge wetu mpya Mheshimiwa Hamis Yusuph ambaye amekuja kumsindikiza kwenye kiapo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge niwaombe leo jioni ifikapo saa tisa na nusu wabunge wote tuwe tayari kwenye viti vyetu kusubiri hotuba ya bajeti. Nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi jioni.

*(Saa 5.05 Asubuhi Bunge Lilisitishwa hadi Saa 10.00 Jioni)*

*(Saa 10.00 Jioni Bunge Lilirejea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tuketi.

Waheshimiwa Wabunge, Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ibara ya 62(1) inasema, kutakuwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambalo litakuwa na sehemu mbili yaani Rais na Wabunge. Siku ya leo Mheshimiwa Rais, anaungana na sisi kama sehemu ya Bunge atakuwa anatufuatilia kutoka Chamwino, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ahsanteni sana kwa makofi hayo, Mheshimiwa wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, tunakukaribisha sana Bungeni, kuungana pamoja na sisi. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, *ndc*- KATIBU WA BUNGE:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, baada ya Katibu wetu wa Bunge, kusema hayo nitumie sasa fursa hii kumuita Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Waziri wa Fedha, aje awasilishe Bajeti Kuu ya Serikali. *(Makofi/Vigelegele)*

*(Hapa Waziri wa Fedha (Mhe. Dkt. Mwigulu L. Nchemba) Aliingia Ukumbini kuwasilisha Bajeti Kuu ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, ulikuwa umeshaitwa kwa hiyo unaweza kuendelea, karibu.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, kwa moyo wa simanzi niruhusu nitoe pole kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Waheshimiwa Wabunge pamoja na Watanzania kwa ujumla kwa kuondokewa na

wapendwa Hayati Ali Hassan Mwinyi, aliyekuwa Rais wa Awamu ya Pili wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Hayati Edward Ngoyai Lowassa, aliyekuwa kuwa Mbunge wa Jimbo la Monduli na Waziri Mkuu Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, nitoe pole kwa kuondokewa na Waheshimiwa Francis Leonard Mtega, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Mbarali, na Mheshimiwa Ahmed Yahya Abdulwakil, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Kwahani, pamoja na Viongozi wengine wa Serikali waliofariki katika mwaka huu wa fedha. Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi.

Mheshimiwa Spika, pia niruhusu, pia nitumie fursa hii kutoa pole kwa wananchi wote waliothiriwa na majanga mbalimbali ikiwemo ajali, mafuriko yaliyotokea maeneo mbalimbali nchini kutokana na mvua za *El-Nino*. Majanga haya yamesababisha athari mbalimbali vikiwemo vifo na madhara mengine.

Mheshimiwa Spika, baada ya salamu hizo za utangulizi naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu, lipokee, lijadili na kukubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Bajeti hii inawasilishwa kwa mujibu wa Ibara ya 137 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 ikisomwa pamoja na Kifungu cha 23 (3) cha Sheria ya Bajeti, Sura Namba 439 ya Kifungu cha 124(4) cha Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari, mwaka 2023.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hotuba hii nawasilisha vitabu vinne vinavyoelezea kwa kina Makadirio ya Bajeti ya Serikali. Kitabu cha Kwanza, ni Makadirio ya Mapato, Kitabu cha Pili, ni Makadirio ya Matumizi ya Kawaida kwa Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala za Serikali na Kitabu cha Tatu, ni Makadirio ya Matumizi ya Kawaida kwa Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa na Kitabu cha Nne, ni Makadirio ya Matumizi ya Maendeleo kwa Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Aidha, Muswada wa Sheria ya Fedha

ya Mwaka 2024 pamoja na Muswada wa Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2024, kwa pamoja ni sehemu ya bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ninaomba niwasilishe Makadirio ya Serikali kwa mwaka 2024/2025. Bajeti ya Serikali ya mwaka 2024/2025 ni ya nne katika utekelezaji wa Mpango wa tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/2022 - 2025/2026) wenye dhima ya kujenga uchumi shindani na viwanda kwa maendeleo ya watu. Aidha, dhima kuu ya bajeti ya mwaka 2024/2025 kama ilivyokubaliwa na nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ni mageuzi endelevu ya kiuchumi kupitia uimarishaji wa Sera za Kibajeti na uwekezaji katika kuhimili na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kwa maendeleo ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na nyaraka na miongozo iliyozingatiwa katika uandaaji wa bajeti hii, shabaha za uchumi jumla ni kama ifuatavyo:-

(i) Kuongeza kasi ya ukuaji wa Pato la Taifa kufikia asilimia 5.4 kwa mwaka 2024 kutokana na ukuaji wa asilimia 5.1 kwa mwaka 2023;

(ii) Kuendelea kudhibiti kasi ya mfumuko wa bei na kuhakikisha kuwa unabaki kwenye wigo wa tarakimu moja ya wastani wa asilimia kati ya 3.0 - 5.0 katika muda wa kati;

(iii) Mapato ya ndani kufikia asilimia 15.8 ya Pato la Taifa mwaka 2024/2025 ikilinganishwa na matarajio ya asilimia 15.4 mwaka 2023/2024;

(iv) Mapato ya kodi kufikia asilimia 12.9 ya Pato la Taifa mwaka 2024/2025;

(v) Kuwa na nakisi ya bajeti (ikijumuisha misaada) isiyozidi asilimia 3.0 ya Pato la Taifa; na

(vi) Kuwa na akiba ya fedha za kigeni kwa kiwango cha kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi minne. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, misingi ya bajeti ni kama ifuatavyo:-

(i) Kuongezeka kwa ushiriki wa sekta binafsi kwenye shughuli za uwekezaji na biashara;

(ii) Kuendelea kuhimili athari za majanga ya asili na yasiyo ya asili ikiwemo ukame, vita, magonjwa ya mlipuko, mafuriko na mengineyo.

(iii) Kuimarika kwa uchumi wa dunia na utulivu wa bei katika masoko ya fedha na bidhaa;

(iv) Kuendelea kuimarika kwa upatikanaji na usalama wa chakula hapa nchini; na

(v) Uwepo wa amani, usalama, umoja na utulivu wa ndani na nchi jirani.

Mheshimimiwa Spika, Bajeti ya Serikali ya mwaka 2024/2025 imelenga kutekeleza vipaumbele vilivyozingatiwa kama vilivyoainishwa kwenye Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/2022 hadi 2025/2026 wenye dhima ya kujenga uchumi shindani na viwanda kwa maendeleo ya watu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Mpango wa Maendelo wa Taifa wa mwaka 2024/2025 maeneo ya vipaumbele yaliyoainishwa katika Mpango ni pamoja na:- Kuchochea uchumi shindani na shirikishi, kuimarisha uwezo wa uzalishaji viwandani na utoaji huduma na kukuza biashara na uwekezaji na kuchochea maendeleo ya watu na kuendeleza rasimali watu.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya maeneo mahususi yatakayopewa kipaumbele ni pamoja na haya yafuatayo:-

(i) Kukamilisha miradi ya kielelezo na ile ya kimkakati. *(Makofi)*

(ii) Kuimarisha sekta za uzalishaji.

(iii) Kuimarisha rasilimali watu hususani katika sekta za huduma za jamii.

(iv) Kuongeza matumizi ya TEHAMA.

(v) Kuboresha mazingira ya ufanyaji biashara na uwekezaji wa sekta binafsi. Maeneo mengine ambayo tumeyatilia muhimu ni kugharamia: mishahara ya watumishi wa umma; deni la Serikali; Uchaguzi wa Serikali za Mitaa kwa Mwaka 2024; maandalizi ya Uchaguzi Mkuu kwa Mwaka 2025 na maandalizi ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050. *(Makofi)*

Mheshmiwa Spika, miradi ya mahsusi katika maeneo ya kipaumbele ambayo Serikali itatekeleza kupitia bajeti ya mwaka 2024/2025 imeainishwa kwa kina na ilitolewa katika hotuba iliyowasilishwa leo asubuhi na Mheshimiwa Prof. Kitila Alexander Mkumbo, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji. Nimpongeze sana kwa hotuba nzuri aliyoitoa leo asubuhi ambayo imetupa mwanga wa bajeti tutakayoijadili ambayo ninaiwasilisha hivi sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mafaniko ya Serikali ya Awamu ya Sita, napenda kutumia fursa hii kumpongeza kwa dhati ya moyo wangu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania, kwa uongozi wake shupavu ambao umedhihirishwa wazi na majira ambayo nchi yetu imepitia. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshmiwa Spika, ikumbukwe kuwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, alipokea usukani wa kuongoza nchi hii ikiwa imepatwa na tukio la huzuni la kuondokewa na aliyekuwa Rais wa

Jamhuri ya Muuungano wa Tanzania, Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, tukio ambalo halikuwahi kutoa hapa nchini lakini Mama hakuyumba na hata sasa tunasonga mbele na nchi haijakwama kwa jambo lolote, nchi inasonga mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, alipokea nchi katika kipindi ambacho dunia nzima ilikuwa inapita katika msukosuko wa kiuchumi kufuatia UVIKO -19 na baadaye kidogo mzozo wa kisiasa kule Ulaya Mashariki, msukosuko wa kiuchumi ambao uliyumbisha hata chumi za Mataifa makubwa, sababu hizo zingetosha kabisa kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kusema miradi mikubwa iahirishwe, lakini bado Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, akasema ataendeleza miradi yote iliyoachwa na Awamu zilizopita na kuleta miradi mipya. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Spika, licha ya misukosuko hiyo Serikali ya Chama cha Mapinduzi, inayoongozwa kwa umahiri mkubwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, imefanya mambo makubwa ngoja niseme kwa uchache.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa sekta ya uchukuzi, kama nilivyosema Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, aliahidi utekelezaji wa miradi hiyo iliyoachwa na Awamu zilizopita kwamba, haitakwama na italetwa mipya ni dhahiri sasa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, hakusema tu bali ametekeleza kauli hiyo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, alipokea Mradi wa Reli ukiwa takribani asilimia 57 kwa *lot* ya pili na asilimia 83.55 kwa *lot* ya kwanza. Hadi hivi tunavyoongea sasa *lot* inayotoka Dar es Salaam hadi Dodoma, imeshakamilika imeshajaribiwa na sasa hata nauli ya kufika Dodoma imeshatangazwa. Hata nauli ya kufika Dodoma imeshatangazwa takribini shilingi 31,000. Hii inatuambia nini? Hii inatuambia Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ameweza pasipo mashaka kuongoza Tanzania. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Spika, kama alivyosema ataleta na miradi mipya itakumbukwa kuwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, aliahidi kuanzisha miradi mingine hilo hakuliahidi tu bali amelitekeleza kikamilifu. Kwa kuanzisha ujenzi wa reli *lot three,* ambayo inatokea Makutupora mpaka Tabora, *lot four,* ambayo inatokea Tabora - Isaka na *lot six,* ambayo inatokea Tabora kwenda Kigoma na Kigoma, na Kigoma Uvinza hadi Musongati ambazo hazikuwepo wakati anapokea usukani wa kuendesha nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea pia kuboresha miundombinu ya bandari ikiwemo kuongeza kina kufikia mita 15.5 na upana wa mita 200 katika lango la kuingia na kugeuzia meli kwa ajili ya kupokea meli kubwa katika Bandari yetu ya Dar es Salaam. Kadhalika Serikali itaendelea na ujenzi wa Bandari Kavu ya Kwala, ambayo kwa sasa utekelezaji wake umeshafikia asilimia 96. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuimarisha usafiri wa anga ikiwemo ujenzi wa viwanja vya ndege, Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Msalato ambapo ujenzi umeshafikia sasa asilimia 56.9 kwa *package* ya kwanza, ambayo ni ya miundombinu na asilimia 22.56 kwa *package* ya pili, ambayo ni majengo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa ujenzi Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, imeendelea kuimarisha huduma za usafiri na usafirishaji nchini pamoja na kuwezesha wananchi kutekeleza shughuli zao za kimaendeleo. Hii ni kwa upande wa barabara zote ambazo zinajengwa kupitia *TANROADS'* na zile ambazo zinajengwa kupitia *TARURA*.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua kuwa barabara za vijijini ni barabara za muhimu kwa uchumi wetu na usalama wa Watanzania tulio wengi, Serikali ya Awamu ya Sita imeendelea kuboresha bajeti ya *TARURA* kutoka shilingi bilioni 710 hadi kufikia bilioni 825 kwa mwaka wa fedha 2023 na kufikia bilioni 841 kwa mwaka wa fedha 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na ukarabati wa miundombinu na usafirishaji yakiwemo na madaraja makubwa ambayo yanajengwa kupitia *TANROADS* likiwepo Daraja la Kigongo – Busisi, lenye urefu wa kilometa tatu na barabara unganishi zenye urefu wa kilometa 1.66 kwa viwango vya lami ambavyo vimeshafikia zaidi ya asilimia 88. Hii inatuambia nini? Hii inatuambia Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, anatosha kuiongoza Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Sekta ya Nishati, Mheshimiwa Rais alipokea Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Maji ya Bwawa la Mwalimu Julius Nyerere unaoweza kuzalisha *megawatt* 2,115 ukiwa takribani asilimia 37 ambapo hadi Aprili, 2024 kwa taarifa ambazo zilikuwa zimetolewa, utekelezaji ulishafika zaidi ya asilimia 97.43. Kwa sasa utekelezaji umeshakamilika upo hatua za mwisho za ukamilishwaji na tayari umeshajaribiwa na tayari tumeanza kupata *megawatt* takribani 235 na hivyo kuongezwa kwenye upatikanaji wa umeme na ndiyo maana nchi imetoka kwenye katika katika ya umeme na mgao wa umeme ambao ulishaanza kulikumba Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Sita imekamilisha pia ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa *kilovolt* 400 na kujenga kituo kipya cha kupoza umeme cha Chalinze cha *kilovolt* 400, 220 na 132 na kimeanza kutumika kuingiza umeme katika Gridi ya Taifa. Kwa upande mwingine, Serikali imekamilisha Mradi wa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa *kilovolt* 400 yenye urefu wa kilometa 414 kutoka Singida hadi Namanga kupitia Babati na Arusha. Gharama za mradi huu ukiwa ni takribani dola za Marekani milioni 258. Aidha, miundombinu yote ya kusafirisha umeme imekamilika na umeme umeanza kusafirishwa kutoka Singida hadi Arusha. Hadi muda huu utekelezaji wa mradi huu umewezesha Gridi hiyo ya upande wa mashariki *(Eastern Africa Power Pool)* kukamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mradi wa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa *kilovolt* 400 kutoka Iringa kupitia Mbeya, Tunduma hadi Sumbawanga pamoja na ujenzi wa vituo vya

kupoza umeme vya Kisada (Iringa), Iganjo (Mbeya), Tunduma na Sumbawanga umefikia asilimia zaidi ya 27 ya utekelezaji. Gharama za mradi huu ni zaidi ya dola za Kimarekani milioni 615. Mradi huu unalenga kuunganisha Gridi ya Taifa na nchi za Kusini mwa Afrika *(Southern Africa Power Pool)*.

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine, Serikali imeanza kutekeleza mradi wa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa *kilovolt* 132 kutoka Malagarasi hadi Kidahwe Mkoani Kigoma. Kazi hii inaenda sambamba na kazi ya ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme wa *megawatt* 49.5 kwa kutumia maporomoko ya maji ya Mto Malagarasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, si kazi hii tu ya usafirishaji lakini hadi kufikia Mei 2024, Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini imeunganisha umeme katika vijiji 11,973, sawa na asilimia 97.2 ya vijiji vyote nchini na wakandarasi wanaendelea kukamilisha uunganishaji wa umeme katika vijiji vilivyobaki. Vilevile, vitongoji 32,827 kati ya 64,359 nchi nzima vimefikishiwa huduma ya umeme. Kazi hiyo inaendelea hadi vitongoji vyote vitakapokamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki, Serikali kupitia *TPDC* inamiliki asilimia 15 ya hisa. Hadi mwezi Mei 2024, Serikali imelipa jumla ya Dola za Marekani milioni 307.3, sawa na asilimia 99.8 ya kiasi kinachotakiwa kulipwa. Kazi mbalimbali zinaendelea kutekelezwa ambapo shehena za mabomba ya mradi yenye jumla ya urefu wa kilometa 600 zimewasili hapa nchini. Kazi hiyo ya kulaza mabomba itaendelea na inatarajiwa kuanza mwezi Agosti 2024 na mradi huu unatarajiwa kukamilika Desemba 2025.

Mheshimiwa Spika, mafanikio haya katika Sekta ya Nishati ni ishara kwamba Mama yetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amedhamiria kwa dhati upatikanaji wa umeme wa uhakika nchi nzima uweze kukamilika. Hakika Mama anatosha, mitano tena. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Spika, sio tu kwamba, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameendeleza miradi ya kimkakati na kuleta mipya, bali ameweza kuweka historia ya kukwamua miradi sugu. Miradi ya maji iliyoshindikana kwa miaka mingi imeweza sasa kutatuliwa na kutimiza azma ya kumtua Mama ndoo kichwani. Serikali imetekeleza miradi mikubwa ya kimkakati yenye lengo la kuimarisha upatikanaji wa huduma ya maji mijini na vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa msisitizo zaidi, Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan nikitoa mfano, imeweza kumaliza ujenzi wa mradi ambao ulikuwa umekwama kwa muda mrefu sana katika Mji wa Orkesumet kwa upande wa Simanjiro. Serikali imeendelea na utekelezaji wa Mradi wa Ujenzi wa mtambo wa kutibu maji Butimba ambao nao ulikuwa umekwama kwa muda mrefu sana na sasa umefikia asilimia 99; Mradi wa Maji Mugango - Kiabakari - Butiama asilimia umeshafika 99; Mradi wa Maji Same - Mwanga – Korogwe umeshafika asilimia 92; Mradi wa Maji kutoka Mto Kiwira kwenda jijini Mbeya umeshafika asilimia 20; Mradi wa Maji wa Miji 28 umeshafika asilimia 25; na Mradi wa Ujenzi wa Bwawa la Kidunda umeshafika asilimia 20. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu na wananchi kwa ujumla kuwa hadi kufikia Desemba 2023, hali ya upatikanaji wa huduma ya maji safi unafikia sasa asilimia 79.6 katika maeneo ya vijijini na asilimia 90 maeneo ya mijini. Kwa ujumla, mafanikio hayo yamechangiwa na kukamilika kwa utekelezaji wa miradi 1,633 ya maji vijijini na miradi 213 ya maji mijini na kazi hii inaendelea. Hii inatuambia nini? Inatuambia kuwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, anajali mahitaji ya lazima ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Sekta ya Kilimo, Mheshimiwa Rais alipokea nchi hii ikiwa na eneo la umwagiliaji lenye ukubwa wa hekta 726,000 tu za tangu kutoka uhuru. Kwa kipindi chake takribani miaka mitatu anatekeleza miradi mipya yenye ukubwa wa hekta 543,366 yenye thamani ya shilingi trilioni 1.18 na

ameanza ujenzi wa mabwawa makubwa 14 na kukamilisha upembuzi yakinifu wa mabonde 22. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Sekta ndogo ya Mbegu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan alipokea nchi ikiwa inajitosheleza kwa mahitaji ya mbegu bora kwa asilimia 22 tu na sasa ndani ya miaka mitatu tumefikia utoshelevu wa zaidi ya asilimia 78 na ifikapo 2026/2027 tutakuwa tumejitosheleza kwa asilimia 100. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa uhifadhi wa chakula, nchi yetu ilikuwa na uwezo wa tani 250,000 tu. Sasa katika kipindi cha miaka mitatu tumefikia tani zaidi ya tani 500,000 na mauzo ya nje yamefikia zaidi ya bilioni 2.3 dola za kimarekani kutoka bilioni 1.2 ambayo ni takribani mara mbili. Hii siyo tu inatuambia kuwa Mama yetu anajali kilimo bali Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan anapambana kwa vitendo kuwaondolea umasikini wa Watanzania na ndiyo maana anaweka bajeti kubwa kwenye Sekta ya Kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa uvuvi Serikali imeendelea kuongeza Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kutoka shilingi bilioni 66 mwaka 2020/2021 hadi kufikia bilioni 295.9 mwaka 2023/2024; na kazi hiyo inaendelea kwa kuwa na Wizara hiyo pia ipo kwenye mageuzi ya mifugo pamoja na Sekta ya Uvuvi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Sekta ya Afya, Serikali imeendelea na jitihada za kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora za afya katika ngazi zote za upatikanaji wa huduma hapa nchini. Sote tunafahamu kuwa huduma za uchunguzi wa magonjwa ni nguzo muhimu katika utoaji wa huduma za tiba ya magonjwa kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua hilo, Serikali imeendelea kuimarisha huduma hizo kwa kufanya uwekezaji mkubwa katika upatikanaji wa vifaa vya uchunguzi ikiwemo *X–rays* ambazo zimeshafika 346, *ultrasound* 677 na mashine za *CT scan* ambazo

zimeshafika 31. Aidha, Serikali imekamilisha upatikanaji wa *MRI* nne ambazo sasa zinawasaidia wananchi kupata huduma hiyo pande zote za Tanzania.

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na changamoto ya uhaba wa wataalamu wa afya katika kipindi hiki, Serikali imetoa kibali cha kuajiri jumla ya watumishi 13,187. Aidha, katika kuimarisha na kuzisogeza huduma za kibingwa na ubingwa bobevu karibu na wananchi wetu, Serikali imeendelea kutoa ufadhili wa masomo katika fani hizo. Mathalan, kupitia Mpango wa *Dkt. Samia Afya Scholarship,* jumla ya wataalamu 1,251 wamesomea ubingwa huo. Hii nayo inatuambia kuwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ana upendo wa dhati na Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa elimu uwekezaji katika elimu unaendelea vizuri na katika Hotuba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI na Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia yalielezewa vizuri. Kwa hiyo sitaweza kuyarudia yote lakini tuna mambo mapya ambayo yameshakuja. Mfano mafunzo ya amali yatakayotolewa ni nyanja ya ufundi yaani *technical secondary schools*, kama ilivyo *Tanga Technical School*, *Moshi Technical School* na nyingine kutaja kwa mfano chache. Huu ni mwanzo mzuri wa ujenzi wa vyuo 64 vya *VETA* katika wilaya 64 ambazo zilikuwa hazina vyuo hivyo pamoja na baadhi ya mikoa ikiwemo Mkoa wa Songwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, chini ya uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita, siyo tu kwamba mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu imeongezwa, lakini pia kiasi cha fedha anachopata mwanafunzi kimeongezeka. Zaidi ya hapo sasa Serikali imeanza kutoa mikopo hata kwa wanafunzi wanaosoma vyuo vya kati pamoja na Vyuo vya Elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hadi Aprili, 2024 jumla ya shilingi trilioni 1.98 zimetolewa kwa ajili ya mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu na vyuo vya kati. Kadhalika, Serikali imeondoa ada ya wanafunzi kwa kidato cha tano na cha sita sambamba na kufuta ada ya mitihani. Aidha, Serikali imeendelea kugharamia Programu ya Elimu ya Msingi

na Sekondari bila Ada ambapo jumla ya shilingi bilioni 766.1 zimetolewa. Hii ina maana gani? Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania yupo kazini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kati ya mambo ambayo ameyafanya na yatawekwa katika historia ni mageuzi haya na ni mageuzi makubwa, magumu na yanaweza kufanywa tu na kiongozi mwenye uthubutu na mwenye upendo na wananchi wake. Ni mageuzi ambayo kiongozi ameangalia maslahi ya vizazi vijavyo na akayapa kipaumbele. Kuna msemo ambao huwa unasemwa *"a politician looks at the next election but a statesman looks at the next generation"*. Nimesema *a stateman* kwa lugha ya kibiblia. Hivyo, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan sio tu kwamba ni mwanasiasa shupavu bali ni kiongozi jasiri mwenye maono makuu ya kulijenga Taifa analojali vizazi na vizazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa madini katika kipindi cha Awamu ya Sita kumekuwa na mafanikio makubwa katika Sekta ya Madini ikiwemo kuendelea kuongezeka kwa mchango wa Sekta ya Madini kwenye Pato la Taifa kutoka asilimia 7.3 mwaka 2021 hadi asilimia tisa mwaka 2023, kuongezeka kwa vituo vya ununuzi wa madini kutoka 61 mwaka 2020/2021 hadi vituo kufikia 100 mwaka 2023/2024 pamoja na kuanzishwa kwa soko jipya moja la madini hivyo kufikia masoko 42.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali imenunua mitambo mitano ya uchorongaji kwa ajili ya wachimbaji wadogo wadogo inayotumika katika maeneo mbalimbali hapa nchini. Vilevile, Serikali kupitia Benki Kuu ya Tanzania imeanzisha utaratibu wa kununua dhahabu kwa ajili ya akiba ya Taifa *(National Gold Reserve)* kwa lengo la kuimarisha akiba ya fedha za kigeni na kusaidia katika utekelezaji wa Sera ya Fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Sekta ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji. Sekta ya Viwanda imepata mafanikio makubwa ikiwemo kuendelea na ulipaji wa fidia kwa wananchi

wanaoishi katika miradi unganishi kwa mfano Mradi wa Mchuchuma na Liganga fidia yake ilishalipwa, kukamilisha maandalizi ya kuanza utekelezaji wa Mradi wa Magadi Soda Engaruka, kufufua kiwanda cha *Kilimanjaro Machines Tools Company (KMTC),* kufanya usanifu na kuendeleza utengenezaji wa vifaatiba na kuvisambaza katika hospitali mbalimbali nchini na kuchakata alizeti kwa kutumia teknolojia mpya itakayosaidia kupunguza uhaba wa mafuta ya kula na kusimamia utekelezaji wa mfumo wa stakabadhi ghalani kwa uendeshaji wa ghala pamoja dhamana za mazao mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Sekta ya Maliasili na Utalii Serikali pia imeendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ya kutangaza utalii ndani na nje ya nchi ikiwemo programu ya Tanzania - *The Royal Tour* ili kuongeza mapato yatokanayo na utalii. *The Royal Tour* iliongeza mapato yatokanayo na utalii na kutokana na mikakati hiyo, idadi ya watalii iliongezeka hadi kufikia milioni 1.8 kwa mwaka 2023 kutoka watalii 922,692. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mawasiliano Serikali inatambua umuhimu wa Sekta ya Mawasiliano. Katika kuhakikisha hivyo, Serikali imeendelea na kutekeleza programu na majukumu mbalimbali na kwa kipindi cha miaka mitatu Serikali ya Awamu ya Sita, mafanikio mbalimbali yamepatikana katika Sekta hiyo ikiwemo kuongeza ya operesheni ya anwani za makazi ambapo makazi takribani 12,800,000 yamesajiliwa na kuongeza wigo wa miundombinu ya mkongo wa Taifa wa mawasiliano kwa kujenga kilometa 3,000 na kufika jumla ya kilometa 11,000 za mkongo wa Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa ardhi Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, imeendelea kutenga fedha kwa ajili ya kuongeza kasi ya upangaji, upimaji na umilikishaji wa ardhi ambapo hatua mbalimbali zimechukuliwa na kazi hii inaendelea kwa kasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa utawala bora, ulinzi na usalama Serikali ya Chama Cha Mapinduzi inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, imeendelea kuimarisha mifumo ya utoaji haki ikijumuisha ujenzi wa miundombinu na kuimarisha matumizi ya *TEHAMA* katika uendeshaji wa mashauri ya mahakama. Aidha, kutokana na umahiri wa Serikali katika kujali haki za binadamu na kuheshimu utawala wa sheria nchini, Tanzania imefanikiwa kuwa mwenyeji wa mikutano ya kimataifa ya masuala haya ikiwemo Kikao cha 77 cha Kamisheni ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu pamoja na Mkutano wa Mawaziri wa Sheria wa nchi za Jumuiya ya Madola. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile, katika jitihada za kukuza na kuimarisha demokrasia nchini, Bunge lako Tukufu limetunga Sheria ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi ya Mwaka 2024 na Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani ya Mwaka 2023 pamoja na kufanya marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa, Sura 258. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa michezo, sanaa na burudani, Serikali inatambua umuhimu wa michezo kwa vijana. Kwa kuzingatia hilo Serikali inaendelea kuwaunganisha wasanii wa Kitanzania na soko la kimataifa. Pia, Serikali ya Awamu ya Sita imeendelea kujenga misingi ya uibuaji na uendelezaji wa vipaji kuanzia mashuleni ambayo imesaidia kuongeza ajira kwa vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kufuatia hatua hiyo ya uendelezaji wa vipaji, imewezesha Timu ya Taifa ya Mpira wa Miguu *(Taifa Stars)* kushiriki mashindano ya Kombe la Mataifa ya Afrika *(AFCON)*. Kufuatia jitihada za makusudi za Mama katika kuimarisha Sekta ya Michezo nchini, Tanzania itakuwa mwenyeji wa michuano ya kombe la *AFCON* ya mwaka 2027 kwa kushirikiana na Uganda pamoja na Kenya. Nipende kuwahakikishia kuwa, Serikali imejipanga vyema kuendelea na maandalizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maandalizi ya timu yanahitaji uwepo wa viwanja bora. Serikali imejiandaa kujenga viwanja vipya na kukarabati baadhi ya viwanja vilivyopo. Kuhusu ubora wa eneo la kuchezea *(pitch)* kwenye viwanja mbalimbali, tayari Serikali ilitunga Sheria ya kutoa msamaha wa uingizaji wa nyasi bandia kwa ajili ya nyasi na vifaa vyake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa, msimu ujao wa Ligi Kuu ya Tanzania tutaanza kutumia *VAR* ili kuhakikisha matokeo yanayopatikana uwanjani yanakuwa ya haki. Tuna timu zimezidi msimu mmoja penati 10, zikifungwa zenyewe magoli yanakataliwa. Ili tuwe na *VAR* za kutosha viwanja vyote viwe na *VAR*, naleta pendekezo la msamaha kwenye uingizaji wa mashine za *VAR* na vifaa vyake na mambo haya yanawezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu maslahi ya watumishi wa Umma pamoja na wastaafu. Serikali imeendelea kuhakikisha kuwa malimbikizo ya mshahara na yasiyo ya kimshahara ya watumishi wa Umma yanalipwa kwa wakati. Katika kipindi cha miaka mitatu ya Serikali ya Awamu ya Sita, jumla ya shilingi bilioni 98.63 zimelipwa kama malimbikizo mbalimbali ya watumishi wa Umma.

Mheshimiwa Spika, aidha, katika kipindi hicho, Serikali imelipa jumla ya shilingi bilioni 160.04 kwa ajili ya kugharamia upandishwaji wa vyeo kwa watumishi wa umma wapatao 126 katika kada mbalimbali. Hata hivyo, kumekuwepo na kilio kikubwa kutoka kwa wastaafu kuhusu kikokotoo. Kama asemavyo Naibu Waziri wa Fedha Mheshimiwa Chande kuwa mara zote mtoto akilia, mama huwa anajua analilia nini. Kwa kutumia sauti mtoto akilia atasema hapo ameshiba sana, akilia anasema hapo ana usingizi, akilia sana anasema hapo ana usingizi, akilia sana anasema hapo nguo zimembana tu au akilia sana anasema huyu anaumwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali yetu sikivu inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan imekisikia kilio cha watumishi wa nchi hii, imeyafanyia kazi suala la maslahi ya wastaafu wetu.

Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ameelekeza kuongezwa kwa malipo ya mkupuo yaliyokuwa yanatolewa kwa watumishi wetu wa umma kwa wale waliokuwa wanapokea 33% iliyopo sasa hadi kufikia 40% kwa kundi la watumishi walioshushwa kutoka 50% hapo awali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameelekeza; naomba kurudia.

Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ameelekeza kuongezewa kwa malipo yanayotolewa kwa mkupuo kwa watumishi walioshushwa kutoka 50% hapo awali na kufikia 33% sasa watapokea 40%. Wale waliokuwa wakipokea 25% hapo awali na kuongezewa kufikia 33% sasa watapandishwa mpaka kufikia 35% kuanzia mwaka huu wa fedha. Wale wote walioathirika na mabadiliko yaliyojitokeza watakuwa sehemu ya mabadiliko haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuliangalia kwa ukaribu jambo la maslahi ya wastaafu kwa kuzingatia tathmini ya uhai na uendelevu wa mifuko yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuimarisha upatikanaji wa fedha za kigeni, kama ilivyokuwa kwa nchi nyingi duniani nchi yetu pia ilikabiliwa na changamoto za upungufu wa fedha za kigeni kwa mwaka 2023/2024. Changamoto hii imesababishwa na mambo mbalimbali ikiwemo athari za UVIKO-19 pamoja na mambo mengine yanayoendelea Ulaya ya Mashariki.

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na changamoto hizo, changamoto nyingi hapa nchini zikiwemo na nchi kubwa zimepita katika changamoto hii. Serikali imefanikiwa kukabiliana nayo kwa kushirikiana na sekta binafsi pamoja na washirika wa maendeleo ili kuendelea kuwa na akiba ya kutosha ya fedha za kigeni. Hadi Machi, 2024 akiba yetu ya fedha ya kigeni ni dola za Kimarekani bilioni 5.3, kiasi ambacho kinakidhi uingizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa zaidi ya miezi 4.4.

Mheshimiwa Spika, pamoja na sababu nilizozitaja hapo awali, sisi wenyewe Watanzania tunalikuza tatizo hili la upungufu wa dola kwa baadhi ya watu kudai malipo au kufanya malipo ya bidhaa na huduma zinazotolewa ndani ya nchi kwa kutumia fedha ya kigeni (dola). Hii kwa lugha ya kitaalamu inaitwa *dollarization*.

Mheshimiwa Spika, taasisi ipo Tanzania na pengine hata ni taasisi ya Serikali, inamuuzia huduma Mtanzania na inamwambia alipe kwa dola. Taasisi nyingine zinataka Mtanzania alipe ada, kodi ya nyumba, vibali vya kazi au leseni kwa dola na kadhalika, kila kitu kingine ambacho kinaweza kupatikana kwa shilingi kama leseni kwa dola. Tunawafanya Watanzania wahangaike kuitafuta fedha ya kigeni kununua huduma zinazotolewa ndani ya nchi yao badala ya kuwafanya wageni wahangaike kuitafuta shilingi ya Kitanzania wanapotaka kupata huduma ndani ya nchi. Jambo hili linasababisha kuongezeka kwa mahitaji yasiyo ya lazima ya fedha za kigeni na kuwanyima fursa wanaohitaji fedha za kigeni kwa ajili ya kulipia bidhaa ama huduma muhimu kutoka nje. Kitendo cha kuuza bidhaa au huduma ndani kwa kutumia fedha za kigeni ni kosa kwa mujibu wa kifungu cha 26 cha Sheria ya Benki Kuu ya mwaka 2006 ambacho kinabainisha kwamba shilingi ya Tanzania ndiyo fedha pekee ya malipo ya ndani ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuanzia tarehe 01 Julai, 2024 naelekeza wadau wote wa ndani, taasisi za umma, wafanyabiashara, asasi za kiraia, mashirika ya kimataifa na watu wote waliopo nchini Tanzania wenye tabia ya kuweka bei kwenye huduma au kuuza bidhaa kwa fedha za kigeni kuacha mara moja na mwongozo wake utatolewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwongozo wake utatolewa ili jambo hili liweze kufanyika kwa ufanisi bila kusababisha matatizo na bila kuleta taharuki. Hata mgeni akija na fedha ya kigeni ni vyema akaibadilisha kuwa fedha ya Kitanzania ili aweze kupata huduma. Tunapofanya kila malipo kwa fedha ya kigeni tunasababisha shilingi ikose thamani na badala yake tunasababisha dola iwe na thamani kubwa ndani ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawahimiza Watanzania wenzangu na wadau wote mliopo nchini kuacha kununua ama kulipa vitu vilivyomo kwenye nchi yetu kwa fedha za kigeni, hususani vifaa vya kielektroniki, ada za shule kama chuo, kodi za nyumba, viwanja, bidhaa ama huduma mbalimbali kwa kuwa ni haki yetu kisheria kulipa bidhaa hizo kwa kutumia fedha yetu ya Kitanzania. Endapo una fedha za kigeni unatakiwa uzibadilishe, hivyo ndivyo mataifa mengine wanavyofanya.

Mheshimiwa Spika, ninaendelea kuielekeza Benki Kuu pamoja na vyombo vingine kuliratibu jambo hili ili liweze kufanyika kwa ufanisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na hatua ambazo zinachukuliwa, napenda kuwakumbusha wananchi wote kuwa suluhisho la kudumu katika kuimarisha thamani ya sarafu yetu ni kuongeza uzalishaji na ubora wa bidhaa zetu na huduma tunazozitoa nje ya nchi. Ikumbukwe kuwa thamani ya sarafu yetu ni kielelezo cha uwezo wa uchumi wetu wa kukidhi mahitaji yake ya msingi, ikiwemo kulipa mahitaji ambayo hayana budi kuagizwa kutoka katika nchi nyingine. Tutaendelea kutekeleza programu ambayo imeshapitishwa na Serikali ya kuongeza fedha za kigeni.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa maendeleo ya sekta ya fedha imeendelea kukua ambapo utafiti wa *FinScope* kwa mwaka 2023 unaonesha kuwa 76% ya Watanzania sasa wanatumia huduma rasmi za kifedha ikilinganishwa na 65% hapo mwaka 2017.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa matumizi ya mifumo ya malipo ya kidijitali, Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Dkt. Samia Suluhu Hassan ina lengo mahususi la kupandisha hadhi uchumi wa nchi yetu ili kuwa uchumi wa kidijitali. Mojawapo ya hatua kubwa zinazochukuliwa ni kuhakikisha tunakuwa na mifumo madhubuti ya kidijitali inayotuwezesha wananchi kufanya malipo kwa urahisi popote walipo na kwa gharama nafuu. Katika kutekeleza hilo Serikali kupitia Benki Kuu ya Tanzania iliunda na kuzindua Mfumo wa Malipo wa Papo kwa Papo *(TIPS)* katika mwaka

2023/2024. Lengo lake lilikuwa ni kufanikisha gharama ziwe nafuu za kufanya hatua hizo za kulipa kwa kutumia kidijitali. Watumiaji wa mitandao ya kielekroniki kwa kutuma na kupokea walifika zaidi ya milioni 51.7 kwa mwaka 2023 baada ya mageuzi hayo.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa pia na ongezeko la mashine za kituo cha mauzo kufikia 8,652 ambacho kimefanya miamala zaidi ya milioni 9.9 yenye thamani ya shilingi trilioni 1.922.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na changamoto ya watu kushindwa kufanya miamala kwa kisingizio kwamba mitandao ipo chini. Hata hivyo matumizi ya mifumo ya kielektroniki katika kufanya miamala yameendelea kuboreshwa ambapo sasa unaweza kutumia simu yako kulipia huduma popote pale ulipo kwa kutumia Mfumo wa Lipa Namba ambao hauhitaji kuwa na mtandao wa *internet*. Hivyo napenda nitoe rai kwa Watanzania wote kujiunga na Mfumo huo wa Lipa Namba ili kurahisisha ufanyaji wa miamala kiganjani. Hii itatuwezesha kwenda kwenye uchumi wa kidijitali na kwenda kwenye *cashless economy* ambao Bunge lako Tukufu limesisitiza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa masuala ya Muungano; ili kuendeleza ustawi wa Tanzania na kukuza uchumi wa nchi yetu, umoja wa kitaifa, amani, mshikamano na undugu ni jambo muhimu sana. Serikali inatambua kuwa Muungano wetu ndio Utaifa wetu. Bila Tanzania Bara hakuna Taifa linaitwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na vivyo hivyo, bila Zanzibar hakuna Taifa linaitwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ndio utambulisho wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, zaidi ya hayo yote, sasa Muungano umepiga hatua kutoka kwenye karatasi na mchanga vilivyofanyika kama kielelezo yaani ishara wakati wa Muungano na kwenda kwenye Muungano wa damu. Sasa Watanzania wameoleana kabila kwa kabila, hakuna hata kabila moja ambalo watu wake hawajaoleana na kabila lingine na wala hakuna upande mmoja wa

Muungano ambao upande huo watu wake haujaoleana na upande mwingine wa Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa kumezuka baadhi ya wanasiasa, kwa sababu za kufilisika tu kisiasa na kutotambua unyeti wa suala hili wamekuwa wakitoa lugha zinazopandikiza chuki dhidi ya Watanzania wa pande hizi za Muungano. Sote tumeshuhudia lugha za kibaguzi zikitolewa na baadhi ya viongozi wa vyama vya siasa ambazo zinahatarisha Muungano wetu. Kauli hizi zikiachwa bila kukemewa na kila mmoja wetu zina uelekeo wa kuvunja Muungano wetu na zinatishia kuvunja utaifa na undugu wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tukumbuke, Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alisema kuwa; "dhambi ya ubaguzi ni kama dhambi ya kula nyama ya mtu, ukila mara moja hauiachi." *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tutakapomaliza kubaguana kwa misingi ya Muungano na baada ya hapo tutaamua kubaguana kikabila, tutachomeana vibanda vyetu, tutanyang'anyana viwanja, tutafukuzana na kufukuziana mifugo, tutauvunja utaifa wetu. Tukatae ajenda hizo na tuwakatae wale wanaotupeleka katika njia hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuzikatae wote ajenda za viongozi wabaguzi hao waliofilisika kisera, hawana ajenda inayoweza kuwapa uhalali kwa Watanzania mpaka watoe lugha za kibaguzi. Lugha hizo ni za hovyo kabisa na za aibu kutolewa na kiongozi yeyote wa chama cha siasa chenye usajili wa kudumu. Ikumbukwe kuwa hata vyama vyetu vya siasa vilivyosajiliwa, vimesajiliwa kwa sharti la lazima kuwa vimeungwa mkono na pande zote za Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, inawezekana wenzetu hawa kwa tamaa za madaraka hawajatilia maanani suala hili. Viongozi hao wanafikiri kuwa lugha hizo zinazohatarisha Muungano zinawapa umaarufu ama uhalali kwa wapiga kura wao. Kuligawa Taifa kwa ajili ya kufanikisha ajenda ya kisiasa tu ni jambo la hatari kwa nchi yetu.

Ndugu zangu Watanzania, viongozi wote wa vyama vyote vya siasa wanaotaka kuligawa Taifa letu kwa maslahi mepesi, ambao wanatafuta uhalali wa kisiasa kwa ubaguzi; Watanzania, watu wa aina hiyo hawastahili na hawafai kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninarejea tena, kwa wanasiasa wanaotafuta uhalali wa kisiasa kwa misingi ya ukabila, Utanganyika ama Uzanzibar ni wanasiasa waliofilisika kiasera na hawafai kabisa. Jambo hili ni la hatari na linatakiwa likataliwe na kila Mtanzania. Vyombo na mamlaka zote zinazohusika zitoe onyo kali kwenye kauli hizi na zichukue hatua kali, haya mambo yatajirudia. Tutaulinda Muungano kwa gharama yoyote, tutailinda nchi yetu kwa gharama yoyote na Serikali hatutatoa nafasi kwa yeyote mwenye chokochoko kama hizo kufanikisha ajenda zake za hovyo za aina hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa usalama barabarani; takwimu zetu za ajali zinazotokana na vyombo vya moto zinaashiria hatari kubwa sana kwa uchumi wetu. Watanzania wengi bado hatuheshimu sheria za barabarani, hatuna nidhamu na matumizi ya vyombo vya moto pamoja na alama za barabarani, madhara yake tunapoteza nguvu kazi kubwa sana. Wakati mwingine kwa uzembe unaoweza kuepukika tunapoteza nguvu kazi ya nchi yetu, tunapoteza watu wanaotegemewa. Katika kipindi cha miaka mitano (2019 – 2024) ajali za barabarani ni 10,093, ambapo zimetugharimu vifo 7,639 na majeruhi 12,663, na miongoni mwao wamepata ulemavu wa kudumu.

Mheshimiwa Spika, hebu fikiria, magari binafsi ajali 3,250, vifo 2,090, majeruhi 3,177; hebu fikiria, mabasi ajali 790, vifo 782, majeruhi 2,008; hebu fikiria, daladala ajali 820, vifo 777, majeruhi 1,800 na hebu fikiria, *taxi* ajali 93, vifo 97, majeruhi 173. Jambo hili lilisababisha nikakosa kazi nikiwa Waziri wa Mambo ya Ndani, ni idadi kubwa mno hii. Hii ni idadi inayotuondolea nguvu kazi ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, ilivyo sasa wengi wetu huona usumbufu na wakati mwingine mpaka tunaweka chuki na uadui

tunapokumbushwa na Jeshi la Polisi tunapokuwa barabarani, tunavunja sana sheria. Wakati mwingine hata magari ya Serikali yanafanya vivyo hivyo na wakati mwingine tunawagonga waenda kwa miguu. Ni wakati sasa jambo hili likaazimiwa na jamii nzima lisiwe jambo la askari polisi. Ni jambo ambalo linatumalizia nguvu kazi yetu. Hatuwezi kuendelea kushuhudia nguvu kazi yetu ikipukutika kirahisi namna hiyo. Askari barabarani msiwe na huruma hata kidogo kwa wazembe wote wanaokiuka sheria katika magari yenye namba zozote hata yale ambayo yana usajili wa namba za Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama sheria zetu ni rafiki sana tuyaondoe makosa haya ya ajali za barabarani kwenye *traffic cases* tuyapeleke kwenye makosa makubwa zaidi ikiwepo hata makosa ya kuua bila kukusudia au makosa ya kuua, kwa sababu anayeua kwa risasi na anayeendesha mwendokasi anajua mwisho wake ni kuwaua abiria aliowabeba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Sheria za Ununuzi wa Umma; utakumbuka Bunge lako Tukufu lilipitisha upya Sheria ya Ununuzi ya Umma Na.10 ya mwaka 2023. Moja ya maboresho hayo ni pamoja na ukomo wa upendeleo kwa bidhaa zilizochimbwa au kuzalishwa ndani ya nchi ambapo sasa tumepeleka 15%. Hivyo, zabuni zote zinazohusu bidhaa, kandarasi na huduma ambazo thamani yake inazidi shilingi bilioni 50 zimewekwa kwa wazawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka 2024 zimeweka masharti mahsusi na ya kipekee yatakayotumiwa na wauzaji wa bidhaa, wakandarasi au watoa huduma wa ndani ili kuweza kuhakikisha kwamba tunarahisisha masharti yale yaliyokuwa yanatukwamisha. Kwa zabuni ambazo kampuni za kigeni zitaruhusiwa kushiriki, kanuni mpya za Ununuzi wa Umma pia zimetoa upendeleo maalumu kwa kampuni ya kigeni ambayo itatoa mikataba midogo *(sub-contracts)* kwa kampuni ndogo za ndani.

Mheshimiwa Spika, katika zabuni hizo, kanuni mpya za ununuzi wa umma zimeweka sharti kwa taasisi nunuzi kulipa moja kwa moja kwa kampuni ya ndani malipo ya mkataba mdogo ulioingiwa baina ya kampuni pamoja na kampuni ya kigeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika eneo hili, sheria mpya ya ununuzi wa umma imeruhusu watu au kampuni binafsi za ndani kuingia katika ushirika na kampuni za nje ili kuweza kukuza ujuzi wa makampuni ya ndani. Endapo ushirika utakaoanzishwa utahusisha kampuni za kigeni, sheria imeelekeza kuwa kampuni ya ndani itakuwa ndiyo kampuni inayoongoza ama inaweza na yenyewe kuwa kampuni inayoongoza katika mradi husika. Hatua hii inatarajia kuleta mageuzi makubwa ikiwa ni pamoja na kujenga uwezo wa kampuni za ndani ili kuwa sawa na nchi nyingine ambazo zimejenga uwezo wa makandarasi wao.

Mheshimiwa Spika, sheria imeruhusu wazawa kupata kazi kubwa ama kutoa *sub-contract* kwa wageni, msione uoga kuwapa kazi kubwa wazawa kwa sababu wao ndio wenye utajiri wa nchi hii na hata mbuyu ulianza kama mchicha. Kwa hiyo, itakuwa jambo la kusikitisha sana endapo tutamuangusha Mheshimiwa Rais ambaye ametoa fursa kwa Watanzania kujenga uwezo wa kiuchumi ndani ya nchi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa ushirika wa wazawa katika shughuli za kiuchumi, nimeelezea Serikali imeweka kiasi kikubwa cha fedha kutelekeza miradi ya maendeleo bado sehemu kubwa ya fedha hizo zitaenda kwa wazawa na hivyo kujenga uchumi mkubwa na huu ni mkakati kwa kujenga Uchumi wa ndani ya nchi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande mabadiliko ya tabianchi, mabadiliko ya tabianchi yameendelea kuleta athari za kijamii na kiuchumi, hivi karibuni, tumeshuhudia mafuriko yaliyosababisha uharibifu mkubwa na ile ni moja ya jambo ambalo tumeliweka kwenye kipaumbele katika bajeti yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwenendo wa Deni la Serikali, hadi kufikia Machi, 2024 Deni la Serikali lilikuwa shilingi bilioni 91,000. Kati ya kiasi hicho, deni la nje ni shilingi bilioni 60,000 na deni la ndani ni shilingi bilioni 30,000. Kumekuwa na mjadala kuhusu Deni la Serikali ambalo mara nyingi limepotoshwa na limetumika kisiasa. Mara kwa mara, tunajadili ongezeko la deni bila kutaja sababu zake halisi na bila kutaja fedha hizo zimetumika wapi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni kweli deni limeongezeka lakini ni vizuri tukajielekeza kwenye sababu za kuongezeka kwa deni, na fedha zimetumika wapi? Tujadiliane kuhusu fedha zimetumika wapi. Ongezeko la deni letu la Taifa limegawanyika katika sababu kadhaa za msingi kabisa za kimaendeleo; kwanza, tumepokea fedha za mikopo ya zamani pamoja na mikopo mipya. Fedha hizo zimeelekezwa kwenye miradi ya kimaendeleo yenye manufaa kwa Taifa letu, ikiwa ni pamoja na ujenzi wa miundombinu ya barabara, reli ya kisasa, viwanja vya ndege, pamoja na miradi ya umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sababu ya pili ambayo imesababisha deni kuongezeka ni kupungua kwa thamani ya shilingi dhidi ya dola ya Kimarekani, ambayo imechangiwa na kuyumba kwa uchumi wa Dunia. Kuanzia tarehe 31 Machi, 2021 hadi 31 Machi, 2024, thamani ya shilingi dhidi ya dola moja imepungua kutoka shilingi 2,300 hadi shilingi 2,500 ambayo ni sawa na asilimia 11.24%. Kwa sababu madeni yanalipwa na madeni yanapimwa kwa *exchange rate* ya sasa hii imesababisha bila mkopo wowote deni limeongezeka kwa zaidi ya trilioni tano zimetokana na kuchafuka kwa uchumi wa Dunia ambao umesababisha *exchange rate* kubadilika.

Mheshimiwa Spika, tatu, ongezeko la deni letu lilisababishwa pia na kutoa hatifungani maalum yenye shilingi bilioni 2.17 ambazo tulizitoa kwa ajili ya kulipa mifuko ya hifadhi ya jamii kwa watumishi wa umma.

Mheshimiwa Spika, huu ni uamuzi sahihi kwa sababu wazee wetu wale walishafanya kazi na walikuwa wanahainga kupata

malipo yao. Tumebadilisha madeni ya Watanzania, wazee wetu ambao walishafanya kazi na kuwapa hatifungani huu si mkopo mpya lakini kwa kuwa ni hatifungani imeonekana kwenye deni jipya kwamba limeongezeka. Kwa muktadha huo ni muhimu kuelewa sababu za kuongezeka kwa deni na hizo ni sababu ambazo nimezitaja.

Mheshimiwa Spika, kipindi cha Serikali ya Awamu ya Sita, tumekopa jumla ya shilingi bilioni 17,000 kutoka vyanzo vya nje kwa lengo la kugharamia miradi. Tumekopa na hizi zimeongeza deni tunatakiwa tujadiliane kama miradi tuliyofanya kwa wale wanaopinga waone kama haukuwa na maana. Moja ya fedha ambazo tumepeleka kwenye mikopo hiyo bilioni 17,000 tulipeleka kwenye mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa *SGR* vipande mbalimbali, manunuzi ya mabehewa. Mikoa itakayonufaika na miradi hii ni kama ambavyo mmeona hii ni reli ambayo ni uti wa mgongo kwa Taifa letu kuanzia Dar es Salaam mpaka Kigoma na Mwanza na nchi za jirani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa sekta ya ujenzi tumetumia bilioni 4,164, fedha hizo tulizozikopa zimeelekezwa kwenye miundombinu bilioni 4000 hizi ni trilioni 4.164 fedha hizo zimepelekwa kwenye ujenzi wa miundombinu ya barabara.

Mheshimiwa Spika, huu ni ufunguzi wa matatizo ambayo yalikuwa yanajitokeza kwenye upande wa ujenzi wa barabara. Tumepata mradi mwingine wa viwanja vya ndege, miradi hiyo ikiwa na thamani ya dola za Kimarekani bilioni 2.8 sawa na shilingi za Kitanzania trilioni 7.37 ikijumulisha mkopo nafuu kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika ambayo sasa tunauelekeza kwenye ujenzi wa uwanja wa ndege wa Msalato, tunaamini ni jambo lenye busara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, fedha zingine zimeenda kwenye ujenzi wa barabara za mabasi ya *BRT* awamu ya pili ya Kariakoo – Mbagala, awamu ya tatu ya Gongolamboto, barabara za mzunguko hapa Dodoma, Barabara ya Mnivata - Masasi – Newala, Barabara ya

Tanzania kuunganisha na Burundi, Barabara Kasulu – Manyovu, Barabara ya kikanda ya Bagamoyo – Horohoro, Barabara za Malagarasi - Ilunde - Uvinza, Kazilambwa - Chagu, Kasekese - Ikola – Karema, Barabara ya Kahama -Bulyanhulu – Kakola, Barabara za Rusahunga - Rusumo, Barabara Mtwara - Mingoyo - Masasi, Rutukila - Songea, Iringa – Msembe pamoja na daraja la ujenzi wa Jangwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa wale ambao wamezoea kupita kwenye barabara nzuri wanaweza wasione umuhimu wa kukopa na kuwajengea barabara nzuri Watanzania hawa ambao hawajawahi kuonja barabara za lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivyo hivyo tulichukua takribani dola bilioni 4000 ambazo zilielekezwa kwenye miundombinu sehemu yake ikiwa ni fedha za Uviko, fedha hizo zimejenga madarasa nchi nzima hakuna wilaya ambayo haikuguswa na hii imetoa watoto waliokuwa wanasomea chini ya miti na imewatengenezea mazingira bora watoto wetu ya kusomea hii ikiwa ni kwa nchi nzima. Bilioni 2,427 zilielekezwa kwenye miradi ya elimu ikiwemo miradi ya maboresho ya elimu ya juu, mageuzi ya kiuchumi ambayo imeelekezwa kwenye vyuo vikuu na hivi vyote vimeenda kwenye mikoa ambayo hata haikuwahi kuwa na vyuo vikuu.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa sekta ya maji, shilingi bilioni 1,000 yaani trilioni moja zilielekezwa kwenye miradi ya maji, miradi hiyo inajumuisha mradi wa maji safi na usafi wa mazingira vijijini ambao umeenda katika maeneo mengi yote kwa Tanzania Bara pamoja na Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, katika juhudi za kuimarisha miundombinu nchini, shilingi bilioni 2,000 kwa upande wa nishati, bilioni 2051, zilielekezwa kutekeleza miradi mbalimbali ya nishati. Hii imesaidia katika kuhakikisha vijiji vingi vinapata umeme ulio imara ambao baadhi ya fedha zimeenda kwenye *stabilization* ya *grid*.

Mheshimiwa Spika, kwa kilimo, shilingi bilioni 1,379 zimeelekezwa katika mikoa yote ya Tanzania Bara na Zanzibar, ikiwemo mradi wa Tanzania *Food Systems Resilience Program* na *Agricultural Inputs Support Project*, ambao inalenga kuongeza uzalishaji na usalama wa chakula, hii itatutoa kwenye mnyororo wa umaskini. Watanzania wasitiwe hofu kwenye masuala haya ya deni, wataalam wa kukagua masuala ya madeni kampuni ya *Moody's Analytics* pamoja na *Fitch Ratings* ambazo zimeifanyia tathimini nchi yetu zimesema kwamba nchi yetu bado ipo imara kwa nchi zote za Afika Mashariki pamoja na Nchi za *SADC*. Ambapo Tanzania ilipanda kutoka *B2* na kwenda Daraja la *B1 positive* ikiwa na *stable outlook*, daraja hili ni la juu sana na inaongoza kwa nchi zote hizi za Afrika Mashariki pamoja na za *SADC*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa niende katika mwenendo wa mapato, kwa upande wa mwenendo wa mapato tumeweka mchanganuo ambao mapato yaliyokusanywa katika mwaka wa fedha uliopita yalifika trilioni 21.31 sawa na 79.7%, mapato yasiyo ya kikodi yalifika trilioni 1.91% sawa na 54%, mapato yaliyokusanywa na Mamlaka za Serikali za Mitaa yalifika bilioni 931 sawa na 81% misaada na mikopo yalifika trilioni 4.93 sawa na 90%, mikopo ya kibiashara ilikuwa trilioni 4.61 sawa na 84.8% ya lengo na mikopo ya kibiashara ilikuwa trilioni 1.56 sawa na 35% kwa upande wa matumizi ni kama ambavyo nimetoka kufafanua katika baadhi ya maeneo. Naomba taarifa yangu yote iingie kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mikakati ya kuongeza mapato, katika kuongeza wigo wa mapato Serikali inaendelea kuboresha vyanzo vya mapato kwa huhakikisha vinaakisi misingi ya ukusanyaji wa mapato. Aidha utoaji wa elimu kwa umma kuhusu ulipaji kodi utakuwa endelevu ili kuweza kuongeza kulipa kodi kwa hiyari.

Mheshimiwa Spika, katika kurahisisha ulipaji kodi, ada na tozo mbalimbali na kuongeza uhiari wa ulipaji wa kodi ya Serikali, Serikali inaendelea kufanya maboresho ya mifumo ya taasisi zenye sura ya utoaji wa huduma kwa pamoja ili kutoa ankara jumuishi ya malipo ili

kuhakikisha kwamba yunapunguza usumbufu wakati wa kulipa na kunufaika na matumizi ya *TEHAMA*.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kumekuwa na tabia kwa baadhi ya wafanyabiashara kukwepa kulipa kodi kwa kutumia mbinu mbalimbali. Jambo hili linasikitisha na naomba nimnukuu Mheshimiwa Rais kama alivyosema wakati alipozungumza katika Baraza la Eid mwezi Aprili, 2024, naomba ninukuu "Inasikitisha kuona kwamba baadhi ya wafanyabiashara wanatumia mbinu mbalimbali kukimbia kulipa kodi, hawatoi risiti wanapouza au wakitoa risiti wanatoa risiti zenye upungufu, na wanunuzi wa bidhaa nao hawadai risiti wanaponunua bidhaa au wanaponunua huduma. Naomba mniruhusu nitumie jukwaa hili kusema kwamba ulipaji wa kodi ni jambo la halali kidini, Mwenyezi Mungu ametuwekea mfumo madhubuti wa kiuchumi unaoeleza namna ya *bait-ul-mal* au hazina ya Serikali zinavyopaswa kukusanya kodi ili ziwe na uwezo wa kuwahudumia wananchi wake". Mwisho wa kunukuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kukemea vikali wale wenye tabia hizo ambazo wanaikosesha Serikali mapato inayostahili kuyapata.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kuwa malengo ya ukusanyaji mapato ya Serikali yanafikiwa, nielekeze taasisi zilizopewa dhamana ya kukusanya mapato ya Serikali kuhakikisha mapato yanakusanywa kupitia mfumo rasmi na kodi stahiki inayopaswa kulipwa kwa mujibu wa sheria kama alivyosisitiza Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, nanukuu "Ahadi yangu kwa watanzania ni kuendelea kusimamia haki kwenye ukusanyaji wa kodi, kuboresha mifumo na kuleta wepesi katika ulipaji na ukusanyaji wa kodi na kuhakikisha kuwa kodi inayokusanywa inatumika ipasavyo kwa manufaa ya wananchi", mwisho wa kunukuu. Hata hivyo nawaomba Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote kwa ujumla muunge mkono jitihada za Mheshimiwa Rais katika kulipa kodi kwa sababu kulipa bila shuruti, kodi ndiyo maendeleo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kufuatia mvua za *El-Nino* zilizonyesha nchini Septemba, 2023 pamoja na kimbunga Hidaya, barabara zetu zimeharibika sana. Barabara 68 zilikuwa zimejifunga, barabara 106 zilikuwa hazipitiki kwa shida na barabara 168 ziliathirika lakini kwa sasa zinaendelea kupitika kwa muda. Maeneo yaliyoathirika katika barabara hizo yanakadiriwa kufikia kilometa 528.

Mheshimiwa Spika, aidha, madaraja na makalavati yapatayo 189 yalikuwa pia yamekatika na mengine yameharibika vibaya. Tathmini iliyofanywa inaonesha gharama ya kurejesha miundombinu hiyo ni shilingi trilioni 1.07, kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 728 ni kwa ajili ya kufanya matengenezo ya kurejesha miundombinu ya barabara ili zirudi katika hali yake na shilingi bilioni 158 ni kwa ajili ya matengenezo ya dharura ili barabara hizo ziweze kupitika.

Mheshimiwa Spika, aidha, shilingi bilioni 184.14 ni kwa ajili kurejesha miundombinu iliyoathiriwa na kimbunga Hidaya. Mahitaji hayo ya kurejesha miundombinu iliyoharibika ili iwe katika hali yake ya kawaida, kwenye bajeti ya Mwaka 2023/2024 hayakuwepo. Tunaliomba Bunge lako Tukufu liangalie uwezekano wa kutupitishia mapendekezo ili tuwe na mfuko wa Serikali kwa ajili ya kujiandaa na majanga vipindi vijavyo.

Mheshimiwa Spika, napendekeza kurekebisha Sheria ya Mfuko wa Dharura *(Contingency Fund)* ili uwe na sifa za mfuko maalum kwa ajili ya kugharamia matengenezo ya dharura ya miundombinu ya barabara iliyoharibika tukianza na Mwaka huu wa Fedha ambapo miundombinu ya barabara imeharibika kutokana na athari nilizozitaja hapo juu.

Mheshimiwa Spika, napendekeza vyanzo vya mfuko huu kuwe na tozo ya miundombinu *(infrastructure levy)*, mapato yatokanayo na tofauti ya kushuka kwa bei za mafuta (*the windfall gain in fuel price decrease)* na asilimia moja ya matumizi ya Serikali, undani zaidi nitaelezea kwenye hatua za kikodi tutakapoanza kwenye majedwali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kadhalika nchi inatekeleza miradi mikubwa ya kimkakati kwa mara moja kuliko nchi yeyote Afrika Mashariki na pengine kwenye ukanda huu wa Afrika. Kwa mfano reli hii ya kisasa, reli ya kisasa hii tunayoijenga itakuwa ni reli ya tano duniani kwa urefu itakapokuwa imekamilika ikifuata baada ya Ufaransa yenye kilometa 2,700, Japan yenye kilometa 3,146 Hispania yenye kilometa 3,917 na China yenye kilometa 40,000 ikifuatiwa na nchi zingine ambazo zinafuata zenye kilometa 1,000 kama Ujerumani, Uturuki kilometa 1,200, Finland kilometa 1,100. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii itakuwa reli ndefu zaidi kwa nchi zote zinazoendelea hapa Duniani na itakuwa reli ndefu zaidi kwa nchi zote za Afrika. Aidha Tanzania inatekeleza miradi mingine mikubwa ya umwagiliaji, miradi ya uzalishaji mbegu na tunatekeleza pia mabadiliko makubwa ya mitaala kwa kiwango kikubwa kufanyika katika historia yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile tunatelekeza maandalizi ya Bima ya Afya kwa wote, tunatelekeza *program* kubwa zaidi kwenye sekta ya afya pamoja na sekta zingine. Programu hizi zote kubwa ikiwemo *program* ya kufua na kusambaza umeme, kutengeneza barabara mpaka za vijijini hayo ni baadhi tu. Hii inatuambia nini mambo haya yote yanahitaji kwanza Watanzania tujivunie kama Watanzania tusijidharau wenyewe. Sote kazi hii tunaifanya na kazi hizi tumeshaona ambazo tumezifanya na zikakamilika ikiwemo Bwawa la Mwalimu Nyerere, hii inatupa jukumu la kila mmoja wetu anayestahili kulipa kodi kutimiza wajibu huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivyo niendelee kutoa rai kwa Watanzania wote kwa kila mmoja wetu kuona umuhimu wa kulipa kodi kwa kuwa kodi ni yako na kodi ni maendeleo ya Taifa, kodi ni yako na Taifa ni lako, kodi ni yetu na Taifa ni letu, kodi ni yako na Taifa ni lako, kila mtu aone wajibu wa kulipa kodi.

Mheshimiwa Spika, Sheria za ukusanyaji wa kodi tulizozitunga zinatoa jukumu hilo kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania na linataka kila mwananchi anayestahili kulipa kodi alipe kodi inayostahili. Zipo

aina mbili za kodi, aina ya kwanza ni ile ya moja kwa moja yaani *direct taxes* ambazo zinatozwa kwa Sheria za Kodi na aina nyingine ni kodi zile ambazo ni *indirect taxes.*

Mheshimiwa Spika, *indirect taxes* mathalani *pay as you earn* kodi kwa mtumishi siyo kodi kwa mwajiri ni kodi ya mtumishi, mwajiri kama ni kampuni au shirika linawajibika kumlipa mtumishi mshahara wake kisha kuzuia sehemu ambayo ilikuwa ni mshahara wa mtumishi siyo fedha yake yeye aliyezuia ni fedha ya mtumishi ambaye amelipa kodi hiyo kwa Mujibu wa Sheria ili iende Serikalini kwa Mujibu wa Sheria ya Mapato sura namba 332 na kuiwasilisha *return* ya malipo yaliyokatwa kama kodi kwa mtumishi.

Mheshimiwa Spika, hivyo hivyo kodi ya ongezeko la thamani *VAT* ni kodi inayotozwa kwa Mujibu wa Sheria ya ongezeko la thamani sura namba 148 kwa mwananchi wa kawaida anaponunua bidhaa hii siyo ya muuza bidhaa aliyelipa ni mwananchi. Kodi hii hukusanywa na wauzaji ambao Sheria inawapa wajibu wa kuikusanya na kuiwasilisha *TRA* ifikapo tarehe 20 mwezi unaofuata. Hii si kodi ya kampuni wala si kodi ya muuza huduma hivyo hivyo kama ile ya *pay* si kodi ya mwajiri ni mtumishi amelipa.

Mheshimiwa Spika, Serikali imebaini uwepo wa wimbi la wafanyabiashara na taasisi ambao wanawajibu wa uwakala wa kukusanya kodi ambao siyo waaminifu katika kutimiza wajibu huo. Mawakala hao wamekuwa wakikusanya kodi kutoka kwa wananchi na kutokuziwasilisha zinapotakiwa kwa mujibu wa Sheria. Vyema ifahamike kuwa kodi hiyo siyo kodi ya mfanyabiashara wala wakala yoyote ambaye amekusanya.

Mheshimiwa Spika, pia, sio yeye anayelipa hiyo kodi na hivyo, anapotumia kodi hiyo kwa kuwa aliitumia anaiibia Serikali. Ifahamike kuwa, wafanyabiashara hawa wenye wajibu wa uwakala wanapoamua kwa makusudi kwenda kinyume na utaratibu wa Sheria Na Kwa kuwa, wanafanya hivyo, wanazitumia kodi za walipa kodi hawa wa kawaida ambao walishalipa fedha hiyo, kwa ajili ya kwenda Serikalini na kuleta maendeleo katika nchi yetu. Hii sio fedha

binafsi ya biashara zao na hatimaye inaonekana kuwa, ndio matajiri kumbe wametumia fedha za Watanzania wenzao. Mawakala hawa wanaofanya hivyo wanaihujumu Serikali, wanaihujumu nchi na wanahujumu jitihada za Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, katika kuwaletea Watanzania maendeleo.

Mheshimiwa Spika, ninatoa rai kwa hao mawakala iwe ni waajiri binafsi au Taasisi za Serikali wakiwemo wale waliosajiriwa kwenye Kodi ya Ongezeko la Thamani (*VAT*), Kodi ya Zuio *(Withholding)* au Ushuru wa Bidhaa (*Excise Duty)* kuacha mara moja tabia hiyo ya kuzuia kodi zilizokusanywa kwa wengine na kuzitumia wao wenyewe badala ya kuziwasilisha Serikalini. Pia, naelekeza Mamlaka ya Mapato Tanzania kuchukua hatua kali za Kisheria kwa mawakala wote watakaojikopesha fedha ambazo zilitakiwa ziende Serikalini kwa kutumia fursa ya kuwa wakala wa kukusanya, kuchukua fedha za walipa kodi wa Tanzania na kutumia kwa matumizi binafsi, kinyume na Sheria. Hatua hizi zitasaidia kukomboa kodi ya Serikali kwa wakati na kuhamasisha ulipaji wa kodi kwa hiari, ili kutekeleza miradi yetu ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, hatutakuwa na utani na mtu ambaye atakusanya fedha, kama wakala, inayotakiwa kwenda Serikalini na yeye akajikopesha ama akajipa mamlaka ya kutumia fedha ya Watanzania bila kuzifikisha zilikotakiwa kufika. Kwa mfano, kodi ni wajibu wa kila mmoja anayestahili kulipa kodi. Pia, kuna mazingira yamekuwa yakijitokeza ambayo hayana usawa ambayo tumeendelea kuyasema na haya yanatumika tu kwa mazoea.

Mheshimiwa Spika, mfano, mtu mwenye kima cha chini cha mshahara anayelipwa shilingi laki tatu kwa mwezi anatozwa kodi sawa na hivyo, kuna wafanyabiashara wengine wenye mapato ghafi yasiyozidi shilingi laki tatu na thelathini kwa mwezi wanatozwa kodi. Inatokea makundi mengine kwenye sekta za uzalishaji ambayo kimsingi yanatumia kodi za walipa kodi wengine kuboresha huduma katika maeneo yao. Hii inatokea na hawalipi kodi, hii na yenyewe haiko sawa. Au kwa mfano, mtu mwenye ng'ombe elfu tisa kutokulipa kodi na akataka kujengewa josho lake ama bwawa lake

kwa kutumia mifuko ya kodi ya watu waliotozwa kodi wanaopokea shilingi laki tatu kwa mwezi, shilingi milioni tatu na laki sita kwa mwezi hii na yenyewe haiko sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napendekeza kila Halmashauri hivyo hivyo, mtu mwenye kipato cha shilingi milioni mia mbili au milioni mia tatu kutokana na kuuza mazao yake ama bidhaa zake kutokulipa kodi na kupokea ruzuku ya mbolea ama mbegu au skimu ya umwagiliaji ikajengwa kwa kutumia kodi ya mtu anayelipwa laki tatu na akalipa kodi hii na yenyewe haiko sawa.

Mheshimiwa Spika, napendekeza Halmashauri zetu zenye idadi kubwa ya mifugo kuratibu ushirika wa mifugo na kuanzisha mifuko ya kuendeleza huduma za ugani za mifugo, miundombinu ya mifugo na majosho kwa kutumia mifuko hiyo. Bahati nzuri magari ya kuchimba mabwawa yapo kila kona ya Tanzania, kila ukanda umepata magari haya na hii, vyama vya wafugaji wakubaliane wao wenyewe na utaratibu wa uendeshaji wa mifuko hiyo ikifanyiwa uratibu na vyama vya wafugaji wenyewe kwenye ushirika wao, kama tunavyofanya kwenye korosho, tunavyofanya kwenye tumbaku na tunavyofanya kwenye pamba na mazao mengine.

Mheshimiwa Spika, sasa najielekeza kwenye Mapendekezo ya Mifumo ya Kodi. Napendekeza kufanya maboresho kwenye Sheria zifuatazo kwa kuwa, orodha ni ndefu na ziko kwenye vishikwambi, ni kama ambavyo inasomeka:-

(i) Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, SURA 148;

(ii) Sheria ya Kodi ya Mapato, SURA 332;

(iii) Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, SURA 147;

(iv) Sheria ya Usimamizi wa Kodi, SURA 438;

(v) Sheria ya Ufundi Stadi, SURA 82;

(vi) Sheria ya Kodi ya Majengo, SURA 289;

(vii) Sheria ya Benki Kuu, SURA 197;

(viii) Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha, SURA 342;

(ix) Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha, SURA 407;

(x) Sheria ya Hifadhi ya Jamii na Watumishi wa Umma, Mwaka 2018;

(xi) Sheria ya Ushuru wa Barabara na Mafuta, SURA 220;

(xii) Sheria ya Mtoto (hii nimeifuta);

(xiii) Sheria ya Bandari, Mwaka 2004;

(xiv) Sheria ya Sukari, Namba 6;

(xv) Sheria ya Korosho, Namba 18;

(xvi) Sheria ya Madini, SURA 123;

(xvii) Sheria ya Michezo ya Kubahatisha, SURA 41;

(xviii) Sheria ya Reli, Mwaka 2017;

(xix) Sheria ya Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, SURA 157;

(xx) Sheria ya Magari na Usajili wa magari, SURA 124;

(xxi) Sheria ya Usimamizi wa Forodha ya mwaka 2004;

(xxii) Sheria ya Kudhibiti Uingizwaji wa Bidhaa Nchini, SURA 276;

(xxiii) Sheria ya Usafirishaji Bidhaa Nje ya Nchi, SURA 196;

(xxiv) Maboresho ya Ada na Tozo mbalimbali za Taasisi;

(xxv) Marekebisho madogo madogo katika baadhi ya Sheria za Kodi pamoja na Sheria nyingine mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura Namba 148; napendekeza:-

(i) Kufanya marekebisho ya Kipengele cha 18, Sehemu ya Kwanza, Jedwali la Msamaha, ili kujumuisha magari pamoja na vifaa vinavyotumiwa na Jeshi la Wananchi, *The Military and Armed Forces*. Lengo la hatua hii ni kuwezesha Jeshi la Wananchi kutekeleza majukumu yake ya ulinzi na usalama kwa ufanisi. *(Makofi)*

(ii) Kujumuisha wazalishaji na waunganishaji wa ndege nchini kwenye wigo wa msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani unaotolewa kwenye ongezeko la kinga ya ndege, *The Aircraft Maintenance*, uuzaji na ukodishaji wa ndege, injini pamoja na vifaa vyake hapa nchini. Hatua hii itatupunguzia, Serikali, kiasi cha mapato takribani shilingi milioni 7.1.

(iii) Kusamehe kodi ya ongezeko la thamani kwenye dawa za kutibu na kusafisha maji, dira za maji, huduma na uondoshaji wa maji taka *(sewage)*. Msamaha unatolewa na Mamlaka ya Maji baada ya kupata ridhaa ya Waziri mwenye dhamana ya masuala ya maji.

(iv) Kusamehe kodi ya ongezeko la thamani kwenye uingizaji wa vifaa vya kiteknolojia, kwa ajili ya kuwasaidia waamuzi *(Video Assistance Referees Equipment's and Accessories)*. Kama nilivyotoka kusema pale mwanzo kwamba, tutatoa msamaha kwenye *VAR* na tunatarajia Ligi Kuu ianze kutumia *VAR,* kwa ajili ya kujiandaa na michuano mikubwa na ubora wa ligi.

(v) Kuweka takwa la marejesho ya kodi ya ongezeko la thamani *(VAT Refund)* kulipwa ndani ya siku 30 kutoka tarehe ya kuwasilishwa kwa maombi ya marejesho haya. Hatua hii inalenga kuchochea ulipaji kodi wa hiari na kuongeza uwajibikaji wa Mamlaka ya Mapato Tanzania.

(vi) Kujumuisha trekta lenye ekseli moja *(single axle tractors/power tiller)* linalotambulika kwa *HS Code 8701.10.00* kwenye wigo wa zana na vifaa vya kilimo vinavyopata msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani. Marekebisho haya yanalenga kuakisi mawanda ya bidhaa zilizosamehewa pamoja na kuoanisha *H.S Codes* zilizomo kwenye vitabu vinginevyo.

(vii) Kufanya marekebisho kwenye Sehemu ya Kwanza ya Jedwali la Misamaha ya Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa kuondoa baadhi ya vifaa vyenye matumizi mbadala kwenye wigo wa vifaa vya kilimo vinavyopata msamaha wa kodi. Vifaa hivyo ni vile ambavyo vinatambuliwa kwa *HS Code 8201.10.00* pamoja na *8201.30.00*. Hatua hii inalenga kutuongezea mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi milioni 4,250;

(viii) Kutoza Kodi ya Ongezeko la Thamani la kiwango cha asilimia 0 kwenye madini ya dhahabu yanayouzwa kwa Benki Kuu ya Tanzania. Lengo la hatua hii ni kuhamasisha uuzaji wa dhahabu kwa Benki Kuu.

(ix) Kutoza Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa kiwango cha asilimia 0 kwenye bidhaa za nguo zinazotengenezwa kwa kutumia pamba inayolimwa hapa nchini kwa kipindi cha mwaka mmoja. Lengo la hatua hii ni kuleta unafuu kwa wakulima wa pamba pamoja na viwanda vinavyotengeneza nguo hapa nchini.

(x) Kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye mafuta ya kula yanayozalishwa ndani ya nchi kwa kutumia mbegu zinazozalishwa nchini kwa muda wa mwaka mmoja. Hapo awali, msamaha huu ulitolewa kwa kipindi cha mwaka mmoja

(1) kupitia Sheria ya Fedha ya Mwaka 2023 kwa hiyo, ilikuwa inafikia ukomo. Lengo la hatua hii ni kuendeleza unafuu wa bei ya mafuta ya kula iliyokuwa imepanda kutokana na mdororo wa uchumi baada ya Uviko-19 na vita ya Ulaya Mashariki.

(xi) Kutoza Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye huduma za *data* zinazotolewa mtandaoni *(online data service)*. Mabadiliko haya yanaenda sambamba na kuweka tafsiri ya *online data services* na kujumuisha huduma hiyo kwenye wigo wa utozaji wa huduma za kidijitali. Lengo la hatua hii ni kuongeza wigo wa kodi kuendana na mabadiliko ya kiteknolojia. Hatua hii inalenga kuiongezea Serikali kiasi cha takribani shilingi milioni 16,397.

Mheshimiwa Spika, kwa hatua zote za Kodi ya Ongezeko la Thamani tunatarajia kuongeza shilingi milioni 22,393.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Kodi ya Mapato, SURA 332; napendekeza:-

(i) Kuzijumuisha taasisi zinazofanya shughuli za uboreshaji wa huduma za afya *(advancement of health)* na utunzaji wa mazingira kwenye wigo wa taasisi zinazotoa huduma za hisani *(charitable organizations),* ili ziweze kupata nafuu ya ukokotoaji wa Kodi ya Mapato kulingana na matakwa ya Sheria. Lengo la hatua hii ni kuchochea huduma za hisani kwenye eneo la afya na utunzaji wa mazingira, hususan katika kipindi hiki ambacho dunia inakabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

(ii) Kufanya marekebisho ya Kifungu cha 4(8) cha Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura. Na. 332, ili kuondoa takwa la kulipa Kodi ya Mapato Mbadala *(Alternative Minimum Tax)* kwa kampuni inayochakata mazao ya chai ambayo yanatengeneza hasara kwa kipindi cha miaka mitatu. Lengo la hatua hii ni kuleta unafuu kwenye Sekta ya Chai ambayo kwa sasa inakabiliana na changamoto mbalimbali ikiwemo upatikanaji wa hasara

unaosababishwa na bei ya zao hilo kushuka katika soko la dunia.

(iii) Kufanya marekebisho kwenye Kifungu cha 11 cha Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura 332, kwa kuweka takwa la risiti za kielektroniki kutumika katika kuthibitisha manunuzi yaliyofanywa kwenye mwaka husika wa mapato ambayo yamechangia katika uzalishaji wa mapato.

(iv) Kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Kodi ya Mapato, ili kuruhusu michango ya asilimia 15 inayolipwa na Taasisi za Serikali kwenda Mfuko Mkuu wa Serikali kuwa miongoni mwa sehemu ya gharama za taasisi hizo katika ukokotoaji wa kodi. Hatua hii inatarajia kupunguza Mapato ya Serikali kwa kiasi cha Shilingi milioni 1,000.

(v) Kufanya marekebisho kwenye Jedwali la Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura 332, kwa kurekebisha viwango elekezi vya kodi vinavyotumika kwa wasafirishaji wa abiria ambako mauzo ghafi yanazidi kiasi cha shilingi milioni mia moja ambao hawawajibiki kuandaa hesabu za Kisheria. Hatua hii ni, hususan, usafirishaji kupitia daladala pamoja na maeneo mengine kama hayo. Hatua hii itatupunguzia Mapato ya Serikali kwa takribani shilingi milioni 2,265.

Mheshimiwa Spika, Jedwali lenyewe ni kama linavyoonekana kwenye vishikwambi vyetu ambavyo tumeelezea siti zisizozidi 15, 16 hadi 25, 26 hadi 45, 46 hadi 65 na zaidi ya 65 na viwango ni shilingi laki sita na nusu, milioni moja na laki moja, milioni moja na laki sita, milioni mbili na laki mbili ambapo huo ndio utaratibu unaopendekezwa.

(i) Kuweka takwa kwa raia wa kigeni kukusanya kodi ya zuio kwa kiwango cha asilimia 5 kwenye malipo yanayofanywa kwenda kwa watengeneza maudhui wakaazi *(Digital content creator)*. Lengo la hatua hii ni kuongeza wigo wa kodi na kuzingatia

kanuni za usawa na utozaji wa kodi. Hatua hii inatarajiwa kuongeza fedha za Serikali takribani shilingi milioni 675.

(ii) Kuweka Kodi ya Zuio kwa kiwango cha asilimia mbili kwenye malipo yanayotokana na ununuzi wa madini ya viwandani *(industrial minerals)*. Aidha, utozaji huu hautahusisha chumvi, madini ya metaliki au madini mengine ya thamani kama yalivyotafsiriwa kwenye Sheria ya Madini, Sura 123, yatakayouzwa kwa mmiliki wa Leseni ya Uchimbaji Mdogo wa Madini *(Primary Mining License)* au mchimbaji mdogo wa madini *(Artisanal Miners)*. Lengo la hatua hii ni kuongeza wigo wa kodi na kuzingatia kanuni za usawa za utozaji kodi.

(iii) Kutoza Kodi ya Zuio kwa kiwango cha asilimia 3 kwenye mapato yatokanayo na uhamishaji au ubadilishanaji wa mali za kidijitali *(digital assets)*. Mabadiliko haya yanaenda sambamba na kuweka tafsiri ya maneno "mali za kidijitali". Aidha, Mmiliki wa jukwaa au mtu yeyote atakayefanikisha zoezi la uhamishaji au ubadilishanaji, atawajibika kwa wakala wa kukusanya kodi hiyo na kuiwasilisha kwa Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato. Hatua hii inatarajia kutuongeza fedha kwa takribani shilingi milioni 465.

(iv) Kutoza Kodi ya Zuio kwa kiwango cha asilimia 5 kwenye malipo ya biashara ya kutengeneza maudhui ya kidijitali *(digital content creators)* yanayofanywa kwa wakaazi *(resident business)*. Lengo la hatua hii ni kuongeza kodi na kuzingatia kanuni za usawa katika utozaji wa kodi. Hatua hii itatuongezea takribani shilingi milioni 968.

(v) Kutoza Kodi ya Mapato kwa kiwango cha asilimia 2 kwenye malipo yatakayofanywa na *intermediaries*, wafanyabiashara wanaofanya biashara za kati kutokana na ununuzi wa bidhaa za kilimo, ufugaji, uvuvi na misitu kama inavyofanyika kwenye upande wa madini. Kodi inayopendekezwa itakuwa kodi ya mwisho kwa wafanyabiashara wa kati wanaofanya biashara kwenye bidhaa zinazoangukia kwenye sekta hizo.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Ushuru wa Bidhaa, Sura 147; Serikali kupitia Sheria ya Fedha ya mwaka 2023 ilifanya marekebisho ya viwango maalum vya ushuru *(specific duty rates)* kwa kiwango cha asilimia 10 ya bei kwenye bidhaa zisizo za petroli na asilimia 20 ya bei kwa bidhaa za bia na tumbaku ikiwa na lengo la kuakisi mabadiliko ya thamani ya mapato ya Serikali kulingana na mfumuko wa bei. Maboresho hayo hayakujumuisha Utozaji Ushuru wa Bidhaa kwa kiwango cha asilimia 30 ya bidhaa *(advalorem rates)* kwa kuwa, thamani ya bidhaa inazingatia mfumuko wa bei. Vilevile, Serikali inaanzisha utaratibu wa kurekebisha viwango vya ushuru kila baada ya miaka mitatu, ili kuweza kuweka stability. Kwa minajili hiyo, napendekeza:-

(i) Kupunguza ushuru wa bidhaa kutoka shilingi 63.80 kwa lita hadi shilingi 56 kwa lita ya maji ya kunywa yanayosindikwa kwenye chupa zinazozalishwa hapa nchini kwenye *HS Codes* zile tulizozitaja.

(ii) Kuongeza ushuru wa bidhaa kwa kiwango cha shilingi 7,000 kwenye *Un-denatured Ethyl Alcohol* yenye kilevi cha asilimia 80 au zaidi inayotoka nje ya nchi na asilimia tano kwa ile inayotoka ndani ya nchi yenye asilimia 80 au zaidi inayozalishwa ndani ya nchi. Bidhaa hiyo inatambulika kwa *HS Code 2207.10.00*. Utozaji huo hautahusisha *Un-denatured Ethyl Alcohol* inayotumika kwa matumizi mengine yasiyohusu uzalishaji wa vilevi. Hatua hii inalenga kutuongezea shilingi milioni 154,550.

(iii) Kutoza ushuru wa bidhaa kwa kiwango cha asilimia 10 kwenye thamani ya dau la kamari *(value of the stake on betting)* kwenye Michezo ya Kubahatisha na Bahati Nasibu ya Taifa. Mapato yatakayokusanywa kutoka chanzo hiki yatapelekwa moja kwa moja kwenye mfuko wa kuendeleza masuala ya afya.

(iv) Kutoza ushuru wa bidhaa kiwango cha asilimia 10 kwenye ada ya matangazo ya biashara na Michezo ya Kubahatisha

ikiwemo na Bahati Nasibu kupitia vituo vya televisheni, tasnia ya uchapishaji. Lengo hatua hii ni kuongeza wigo wa mapato.

(v) Kutoza ushuru wa bidhaa kwa kiwango cha Shilingi 300 kwa kilo ya *tomato sauce* au *tomato ketchup* za kutoka nje. Lengo la hatua hii ni kuongeza mapato ya Serikali na kupata fedha kufidia athari hasi zinazotokana na matumizi yake.

(vi) Kutoza ushuru wa bidhaa kwa kiwango cha Shilingi 500 kwa kilo moja ya rangi za mafuta zinazozalishwa kutoka nje. Rangi hizo zinatambulika kwa *HS Code 32.08.* Lengo la hatua hii ni kuongeza mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa sheria ya usimamizi wa kodi:-

(i) Kuongeza kiwango cha *currency points* kutoka shilingi 15,000 hadi shilingi 20,000. Lengo la hatua hii ni kuakisi mabadiliko ya thamani ya mapato ya Serikali kwa kuwa utozaji wa *currency point* kwa kutumia kiwango maalum *(specific rates)* usiporekebishwa hupoteza thamani ya fedha na hivyo kupunguza mapato ya Serikali.

(ii) Kufanya marekebisho kwenye Kifungu cha 86(1) cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi kwa kuweka ukomo wa faini ya juu ya kosa la kutokutoa risiti ambayo tumepunguza kwa kiasi cha *currency points* 1000 (sawa na shilingi 15,000). Lengo la hatua hii ni kuleta nafuu kwa walipakodi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Sheria za Serikali za Mitaa, napendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Serikali za Mitaa ya Utozaji wa Kodi ya Majengo, Sura 289 ili kuelekeza 20% ya mapato yanayokusanywa kutoka kwenye kodi ya majengo na kodi ya pango la ardhi ipelekwe moja kwa moja kwenye akaunti za Mamlaka ya Serikali za Mitaa (halmashauri) ambazo zimehusika kukusanya, badala ya utaratibu wa sasa ambapo mapato yote yanaingia Mfuko Mkuu wa Serikali na kisha halmashauri kuomba

kurejeshewa hiyo 20%. Lengo la hatua hii ni kuwezesha Mamlaka ya Serikali za Mitaa kugharamia masuala ya ufuatiliaji na ukusanyaji wa Kodi ya Majengo na Kodi ya Pango la Ardhi kwa ufanisi na kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania, Sura 197, napendekeza kufanya marekebisho kwenye Vifungu vya 32(2)(b), 35(1), 41 na 42(2) vya Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania, Sura 197 kwa kuongeza maneno *'return' or 'profit'* katika vifungu hivyo.

Mheshimiwa Spika, kwenye upande wa Sheria ya Benki na Taasisi zake, napendekeza kufanya marekebisho kwenye Kifungu cha 24(g)(iv) cha Sheria ya Benki Kuu na Taasisi za Fedha Sura 342 kwa kuongeza maneno *'return' or 'profit'*. Kwa upande wa Sheria ya Huduma Ndogondogo za Fedha, napendekeza kufanya marekebisho kwenye Kifungu cha 4(3) cha Sheria ya Benki Kuu kwa kuongeza maneno *'return' or 'profit'*.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma, napendekeza kufanya marekebisho ya muda mfupi wa kugharamia malipo ya nyongeza ya mkupuo kwa kufikia 40% kwa kundi ambalo lilikuwa linalipwa 33% na kuongeza kwa kundi lililokuwa linalipwa 25% na baadaye 33% kuifikisha 35%. Nyongeza hizo zitaanza kulipwa kwa wastaafu walioanza 2022/2023. Hatua hii inatarajia kutupunguzia mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi 155,000,400.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Sheria ya Sheria wa Barabara na Mafuta, napendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Ushuru wa Barabara na Mafuta, Sura 220 ili kutoza shilingi 382 kwa kila gesi asilia inayotumika kwenye magari. Lengo la hatua hii ni kuongeza mapato yatakayotumika katika kufanya matengenezo ya barabara pamoja na kuleta usawa kwa kuwa magari yanayotumia mafuta tayari yanachangia mapato kwa ajili ya matengenezo ya barabara. Hatua hii tunatarajia ituongezee fedha kwa takribani shilingi milioni 9,500.

Mheshimiwa Spika, napendekeza pia kuweka utaratibu wa kutenga fedha kwa ajili ya maendeleo ya miundombinu katika kipindi ambacho kutakuwa na punguzo la bei ya mafuta kama nilivyosema hapo awali katika kipindi ambacho kutakuwa na punguzo la mafuta ya petroli, *diesel* pamoja na mengine sokoni. Mafuta hayo badala yaweze moja kwa moja kwenda kwenye Mfuko wa Barabara, utaratibu huu utatekelezwa na Kamati maalumu itakayoundwa na Waziri mwenye dhamana ya masuala ya Nishati kwa kushirikiana na Waziri mwenye dhamana ya masuala ya Fedha kwa lengo la kupendekeza kiasi kitakachotengwa kwa kuzingatia wastani wa bei iliyopo katika Soko la Dunia. Aidha, mapato yatakayotokana na utaratibu huu yatapelekwa moja kwa moja kwenye mfuko wa dharura wa kutengeneza barabara zilizoharibika tukianza na utaratibu wa barabara zilizoharibika mwaka huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Sheria ya Bandari, napendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Bandari ya mwaka 2004 ili kurejesha jukumu la kukusanya Tozo ya Matumizi ya Miundombinu ya Bandari *(wharfage)* kwa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania *(TPA)*. Aidha, mapato yatakayotokana na tozo hizo yatawekwa katika akaunti maalumu ya *TPA* iliyopo Benki Kuu ya Tanzania na matumizi yake yatafanyika baada ya kuomba na kupata kibali cha Mlipaji Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Sukari, Namba 6, napendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Sukari, Namba 6 kama ifuatavyo: -

(i) Kuiwezesha Wakala wa Hifadhi ya Chakula *(NFRA)* kununua na kuhifadhi sukari kwenye hifadhi ya chakula ya Taifa. Lengo la hatua hii ni kuwezesha upatikanaji wa sukari nchini na kuondoa uhodhi kwa baadhi ya viwanda bila kuathiri dhamira ya Serikali ya kulinda viwanda; *(Makofi)*

(ii) Kufanya marekebisho kwenye Kanuni ya *NFRA* kwa kuijumuisha sukari kuwa sehemu ya usalama wa chakula; na

(iii) Kutoza shilingi 50 kwa kilo ya mabaki *(by products)* yanayotakana na uzalishaji wa sukari. Lengo la hatua hii ni kuongeza mapato yatakayoiwezesha Bodi ya Sukari kutekeleza majukumu yake ikiwemo kuendeleza mafunzo na kukuza ujuzi.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Korosho Namba 18, napendekeza kufanya marekebisho ya Sheria ya Korosho ili mapato yatokanayo na tozo ya kusafirisha korosho ghafi nje ya nchi yapelekwe Bodi ya Korosho moja kwa moja kwa kipindi cha miaka mitano. Lengo la hatua hii ni kuchochea maendeleo ya sekta ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa michezo ya kubahatisha napendekeza kuanzisha ada ya maombi ya cheti cha uwakala *(dealer's certificate)* ya michezo ya kubahatisha ya shilingi 10,000 na ada ya cheti ya shilingi 20,000. Lengo la hatua hii ni kuongeza mapato yatokanayo na ufanisi wa udhibiti bora wa watu binafsi na mawakala wanaofanya biashara hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Reli, napendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Reli ya mwaka 2017 kwa kuongeza kiwango kwenye Tozo ya Maendeleo ya Reli kinachotozwa kwenye bidhaa zote zinazoingia na kutumika nchini kutoka asilimia tano hadi asilimia mbili. Aidha, 50% ya mapato yatakayotokana na chanzo hicho yatapelekwa kwenye Mfuko wa Maendeleo ya Reli na 50% nyingine itatumika kwenye matengenezo ya barabara yakienda kwenye mfuko ambao tumeupendekeza.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Sheria ya Mamlaka ya Hali ya Hewa, napendekeza kufanya marekebisho ya kuanzisha ada ya matumizi ya huduma mahsusi za hali ya hewa katika shughuli za ujenzi ya shilingi 500,000 kwa mradi wenye thamani kuanzia shilingi milioni 500 hadi shilingi bilioni moja na ada ya shilingi 1,500,000 kwa

mradi wenye thamani kuanzia shilingi bilioni moja hadi shilingi bilioni 10; na ada ya shilingi 5,000,000 kwa mradi wenye thamani zaidi ya shilingi bilioni 10. Lengo la hatua hii ni kuongeza mapato yatakayowezesha utoaji wa huduma mahsusi kwenye masuala ya hali ya hewa.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa magari, napendekeza kufanya marekebisho ya Sheria ya Magari Namba 24 kwa kujumuisha magari ya umeme kwenye wigo wa ulipaji wa ada ya usajili wa magari. Lengo la hatua hii ni kuzingatia kanuni za usawa za utozaji wa kodi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, napenda kukufahamisha kwamba kikao cha Mawaziri wa Fedha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki cha Maandalizi *(Pre-Budget)* kilichofanyika tarehe 17 Mei, Jijini Arusha, pamoja na masuala mengine kilipendekeza kufanya marekebisho kwenye baadhi ya sheria.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo ya Mawaziri ya kufanya marekebisho kwenye Viwango vya Pamoja vya Ushuru wa Forodha ni kama ifuatavyo, mapendekezo ya hatua mpya ni kama ifuatavyo:-

(i) Kutoa unafuu wa Ushuru wa Forodha kwa utaratibu wa *Duty Remission* kwa kiwango cha asilimia sifuri badala ya 25% kwa mwaka mmoja kwenye betri za umeme *(Lithium-ion Electric accumulators)* zinazotambulika kwa *HS Code* 8507.60.00;

(ii) Kutoa unafuu wa Ushuru wa Forodha kwa utaratibu wa *Duty Remission* kwa kiwango cha asilimia sifuri badala ya 10% kwa mwaka mmoja kwenye runinga ambazo hazijaunganishwa;

(iii) Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zimekubaliana kutoa unafuu wa Ushuru wa Forodha kwa

utaratibu wa *Duty Remission* kwa kiwango cha asilimia sifuri kwenye malighafi zinazotumika katika uzalishaji au uunganishaji wa simu za mkononi;

(iv) Kutoa unafuu wa Ushuru wa Forodha kwa utaratibu wa *Duty Remission* kwa kiwango cha 10% badala ya 25% kwa mwaka mmoja kwenye karatasi zinazotambulika kwa *HS Code* 4811.90.00;

(v) Kutoa unafuu wa Ushuru wa Forodha kwa utaratibu wa *Duty Remission* kwa kiwango cha 10% badala ya 35% kwa mwaka mmoja kwenye malighafi za kutengeneza vioo vigumu zinazotambulika kwa *HS Codes* 7005.10.00; 7005.21.00; 7005.29.00; na 7005.30.00. Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu kwa watengenezaji wa vioo hapa nchini;

(vi) Nchi wanachama za Jumuiya ya Afrika Mashiriki zimekubaliana kutoa unafuu wa Ushuru wa Forodha kwa utaratibu wa *Duty Remission* kwa viwango vya 10% badala ya 25% kwenye malighafi *(input)* zinazotambulika kwa *HS codes* 2106.90.20 zinazotumika kwenye uzalishaji wa vyakula na vinywaji. Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu kwa uzalishaji wa vyakula na vinywaji kwenye Jumuiya ya Afrika Masharikí;

(vii) Kutoza Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha 35% badala ya 10% kwenye vioo vya kawaida na vigumu vinavyotambulika kwa *HS Codes* 7005.10.00; 7005.21.00; 7008.00.00; 7007.29.00 na 7007.19.00; kwa mwaka mmoja. Hatua hii inalenga kulinda wazalishaji wa vioo hapa nchini;

(viii) Kutoza Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha 10% au Dola za Kimarekani 300 kwa kila tani moja ya ujazo kwa kutegemea kiwango kitakachokuwa kikubwa badala ya 10% kwa mwaka mmoja kwenye bidhaa za mabati zinazotambulika kwa *HS code* 7212.60.00;

(ix) Kutoza Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha 25% au Dola za Kimarekani 300 kwa kila tani moja ya *metric ton* kutegemeana na kiwango kitakachokuwa kikubwa katika kiwango cha 10% kwenye bidhaa zinazotambulika kwa *HS code* 7225.91.00; 7225.92.00 na 7225.99.00;

(x) Kwa upande wa Ushuru wa Forodha kwa utaratibu wa *Duty Remission* umetolewa pia kwa kiwango cha asilimia sifuri badala ya 10% kwa 25% kwa mwaka mmoja kwenye malighafi za kutengeneza sabuni zinazotambulika kwa *HS Codes* 3402.31.00 na 3402.39.00. Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu kwa wazalishaji wa sabuni za unga hapa nchini.

(xi) Napendekeza kutoa unafuu wa Ushuru wa Forodha kwa utaratibu wa *Duty Remission* kwa kiwango cha asilimia sifuri badala ya 25% kwa mwaka mmoja kwenye vifungashio vya tumbaku iliyochakatwa vinavyotambulika kwa *HS Code* 5310.10.00. Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu kwa wachakataji; na

(xii) Kutoa unafuu wa Ushuru wa Forodha kwa utaratibu wa *Duty Remission* kwa kiwango 10% badala 25% kwa mwaka mmoja kwenye bidhaa zinazotambulika kwa *HS Code* 8704.21.90. Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu kwa waunganishaji wanaozalisha hapa ndani.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Sheria ya Udhibiti wa Uingizaji Bidhaa Nchini Sura Namba 276, napendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Kudhibiti Uingizwaji wa Bidhaa Nchini, Sura 276 kwa kuanzisha Tozo ya Marekebisho ya Viwanda *(industrial Development Levy)* kwa baadhi ya bidhaa zinazoingizwa nchini kama ifuatavyo: -

(i) Kiwango cha 10% kwenye *wire rods* zinazotambulika kwa *HS Code* 7213.91.10 na 7213.99.90; 10% kwenye bidhaa

zinazotambulika kwa *heading* 22.03 pamoja na mvinyo asilimia tano na kwenye bidhaa zisizo na kilevi *(non-alcoholic beer)* zinazotambulika kwa *HS Code* 2202.91.00 na asilimia tano kwenye vinywaji vinavyoongeza nguvu *(energy drinks)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Sheria ya Usafirishaji wa Bidhaa Nje ya Nchi, Sura 196, napendekeza yafuatayo: -

(i) Kutoza ushuru kwa kiwango cha 10% kwenye mafuta ghafi ya kula ya alizeti *(Crude Sunflower Oil),* mashudu yanayotokana na mbegu za alizeti pamoja na mbegu za alizeti zinazosafirishwa kwenda nje ya nchi. Lengo la hatua hii ni kuwezesha upatikanaji wa bidhaa za mafuta kwa bei nafuu hapa nchini; na

(ii) Kutoza Ushuru wa kiwango cha asilimia sita kwenye malighafi ya dhahabu.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa maboresho ya ada na tozo mbalimbali za taasisi za serikali pamoja na utekelezaji wa mpango wa kuboresha mazingira ya kufanya biashara *(blueprint),* napendekeza kufanya marekebisho ya kuweka takwa la kutoza kiwango cha 0.1% ya malipwani kwenye bidhaa za mifugo na chakula inayosafirishwa kwenda nje ya nchi. Kupunguza ada ya mionzi kutoka 0.4% ya Malipwani hadi 0.2% ya malipwani kwa bidhaa ambazo zinaingizwa nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Jeshi la Zimamoto, napendekeza kufanya marekebisho ya Sheria ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Sura 427 kwa kupunguza tozo ya mafunzo ya kinga na tahadhari ya moto kwa wasimamizi kutoka shilingi 500,000 kwenda shilingi 200,000.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Mamlaka za Usafiri wa Anga, kutoza ada ya kuhuisha leseni za uendeshaji wa ndege

zinazohusisha kiusalama kwa kiwango cha Dola za Kimarekani 600,000.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa sekta za uvuvi na mifugo, kufanya marekebisho kwenye ada ya kibali cha kusafirisha mifugo katika minada kutoka shilingi 30,000 hadi shilingi 31,000. Kwa upande wa sekta ya uvuvi:-

(i) Kupunguza ada ya kibali cha kusafirisha samaki na mazao ya uvuvi: dagaa, samaki wakavu, wabichi na waliounganishwa kutoka shilingi 100 kwenda shilingi 50;

(ii) Kupunguza ada ya kibali cha kusafirisha mazao ya mabondo kutoka shilingi 2,500 hadi shilingi 2,000; na

(iii) Kuongeza ushuru wa kusafirisha mabondo nje ya nchi kutoka Dola za Kimarekani 2.7 hadi Dola za Kimarekani 3.0.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa kuanza kutekeleza sheria mpya, hatua hizi za kikodi zinazopendekezwa kuanza kutekelezwa tarehe 1 Julai, 2024, isipokuwa pale itakapoelezwa vinginevyo.

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo sura ya bajeti, mapato ya ndani yanakadiriwa kuwa jumla ya shilingi trilioni 34.61, sawa na 70.1% ya bajeti yote na 15.7% ya Pato la Taifa. Kati ya mapato hayo, mapato yatakayokusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania yanakadiriwa kuwa shilingi trilioni 29.41, mapato yasiyo ya kikodi yatakayokusanywa na Wizara, Taasisi na Idara zinazojitegemea yanatarajiwa kuwa shilingi trilioni 3.84 na mapato yatakayokusanywa na Mamlaka za Serikali za Mitaa shilingi trilioni 1.36. Mikakati ya kufikia malengo haya ya mapato ni kama nilivyoeleza pale awali.

Mheshimiwa Spika, misaada na mikopo kutoka kwa washirika wa maendeleo inakadiriwa kuwa ni trilioni 5.13. Pia, naomba nizitambue nchi wahisani ambazo tunatarajia kushirikiana nazo kwa

mwaka huu ikiwa ni: Australia, Austria, Canada, China, Denmark, Finland, India, Ireland, Italia, Japan, Korea ya Kusini, Marekani, Norway, Poland, Sweden, Ubelgiji, Ufaransa, Hispania, Uholanzi, Uingereza, Ujerumani na Uswisi. Aidha, Taasisi na Mashirika ya Kimataifa ambayo tunatarajia kushirikiana nayo ni pamoja na: Benki ya Dunia, Shirika la Fedha la Kimataifa *(IMF)*, Benki ya Maendeleo ya Afrika, Benki ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Kiuchumi katika Afrika *(BADEA),* Benki ya Uwekezaji ya Ulaya, Mfuko wa Abu Dhabi, Mfuko wa Kuwait, Mfuko wa Kimataifa wa Kusaidia Mapambano Dhidi ya Ukimwi, Kifua Kikuu na Malaria, Mfuko wa *OPEC* kwa Maendeleo ya Kimataifa, Mfuko wa Mazingira Duniani, *Adaptation Fund*, Mfuko wa *GRMF*, Umoja wa Mataifa na mashirika yote yaliyopo chini yake, Umoja wa Ulaya na Shirikisho la *GAVI*.

Mheshimiwa Spika, Serikali inakadiria kukopa shilingi trilioni 6.6 kutoka soko la ndani ambapo shilingi trilioni 4.02 ni kwa ajili ya kulipia hatifungani na dhamana za Serikali zinazoiva na shilingi trilioni 2.6 kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa matumizi katika mwaka wa fedha 2024/2025, Serikali imepanga kutumia jumla ya shilingi trilioni 49.35. Kiasi hicho kikiwa kinajumuisha gharama za mfuko mkuu shilingi trilioni 11 kwa ajili ya mishahara ikiwemo ajira mpya, upandishaji wa madaraja kwa watumishi pamoja na shilingi trilioni 2.17 kwa ajili ya mifuko ya reli, barabara, maji, *REA* na *TARURA*. Bajeti nzima ni kama inavyoonekana kwenye jedwali. Nikiwa naelekea kumaliza utekelezaji wa bajeti kwa mwaka 2024 ni kama nilivyoelezea kwenye utekelezaji wa bajeti.

Mheshimiwa Spika, katika kuhitimisha, ni dhahiri kwamba Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, imepata mafanikio makubwa sana kama nilivyotoka kuelezea pale mwanzo ikiwepo uongozi madhubuti wa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Sera madhubuti za Serikali ya Chama Cha Mapinduzi zinazolenga kuimarisha uchumi na katika kipindi cha miaka mitatu uongozi wake umedhihirisha kuwa ni kiongozi mwadilifu, msikivu, makini, shupavu, mchapakazi na aliye

na dhamira thabiti ya kuendelea kutuletea maendeleo nchi yetu. *(Makofi)*.

Mheshimiwa Spika, tunapozungumzia mafanikio haya ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hasssan hatuwezi kumsahau Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hivyo hivyo, nitumie fursa hii kumpongeza kwa kumsaidia vema Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nitumie fursa hii pia kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa uongozi wake thabiti alioonesha tangu kuchaguliwa kwake, hakika Zanzibar ya Uchumi wa Buluu imemeremeta! Hakika Dkt. Mwinyi mitano tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninatoa pongezi za dhati pia kwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Mbunge wa Jimbo la Ruangwa kwa kumsaidia vema Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Sambamba na hivyo nitoe pongezi pia kwa Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati na Mbunge wa Jimbo la Bukombe, kwa kuendelea kuratibu na kusimamia vema shughuli za Serikali kwa weledi na umahiri mkubwa. Hakika safu hii imesheheni viongozi makini na kazi inandelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii pia kukupongeza wewe mwenyewe Dkt. Tulia Ackson, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani, kwa kuendelea kuliongoza vema Bunge letu na umeliletea heshima Taifa letu ulipochaguliwa kuwa Rais wa Mabunge Duniani. Pia ninampongeza Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mbunge wa Ilala kwa kazi nzuri anayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninampongeza Mheshimiwa Prof. Ibrahim Hamis Juma - Jaji Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Mustapher Mohamed Siyani - Jaji Kiongozi wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Prof. Elisante Ole Gabriel - Mtendaji

Mkuu wa Mahakama na Katibu wa Tume ya Utumishi wa Mahakama na niwapongeze Viongozi Wakuu wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama kwa kazi kubwa wanazozifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia ninawapongeza Wabunge ambao walipata uteuzi baada ya mwaka wa fedha huu kuwa umeshapita nikianza na Mheshimiwa Doto Mashaka Biteko - Naibu Waziri Mkuu, Mheshimiwa Deogratius John Ndejembi - Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Mheshimiwa William Jerry Silaa - Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Zainab Katimba - Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Mheshimiwa Stanslaus Nyongo - Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – Mipango na Uwekezaji, Mheshimiwa Daniel Sillo Baran - Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Judith Kapinga - Naibu Waziri wa Nishati, Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile -Naibu Waziri Uchukuzi, Mheshimiwa Alexander Pastory Mnyeti - Naibu Waziri Kilimo, Mheshimiwa Dunstan Luka Kitandula - Naibu Waziri Maliasili na Utalii na wengine wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee kabisa na kwa namna ya pekee kabisa ninampongeza Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi kwa kuaminiwa na kuteuliwa kuwa Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi na kazi anaifanya njema sana, hakika uzoefu wake na umahiri wake katika siasa na diplomasia ya kimataifa hauna shaka yoyote na atasimamia vyema utekelezaji wa mipango ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninawapongeza Mheshimiwa Deo Mwanyika, Mbunge wa Jimbo la Njombe Mjini, Mheshimiwa Joseph Kizito Mhagama pamoja na Najma Giga kwa kukusaidia vyema katika kutekeleza majukumu haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru viongozi wenzangu wote wa Wizara ya Fedha kwa ushirikiano mkubwa na watumishi wenzangu wote wa Wizara ya Fedha kwa ushirikiano mkubwa wanaonipa nikianza na Mheshimiwa Hamad Hassan Chande, Naibu Waziri wa viwango, Naibu vya Naibu Waziri wa Fedha Mbunge wa

Jimbo la Kojani, Dkt. Natu El-maamry Mwamba, Katibu Mkuu Hazina na Mlipaji Mkuu wa Serikali pamoja na Naibu Makatibu Wakuu wote wanaomsaidia pamoja na watendaji wote wa Serikali na Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nizipongeze timu za Azam na Coastal Union kwa kukata tikezi ya kucheza mashindano ya kimataifa. Coastal Union imefuzu kucheza mashindano ya kimataifa na Azam imefuzu kucheza mashindano ya Klabu Bingwa. Katika hili kipekee ninampongeze kwa dhati Mheshimiwa Ummy Mwalimu - Mbunge wa Tanga Mjini, kwa kujitoa kwake kwa hali na mali wakati Coastal Union inapanda daraja alikuwa hakosi katika Uwanja wa Mkwakwani. Ni vema kujikumbusha tulikotoka na tuwakumbushe Wanatanga maana kiubinadamu nyumba ikipendeza huwa kuna wakati anasahaulika yule aliyejenga msingi anafahamika zaidi yule aliyepaka rangi, ni hakika Mheshimiwa Ummy amechangia pakubwa kuipeleka Coastal Union Ligi Kuu na hivi sasa imeenda kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa umaalum naipongeza pia timu ya Simba, ni kweli kabisa Simba amekuwa mwanzilishi wa kufanya vema kwenye mashindano ya kimataifa, hata hivi sasa ambavyo mwenendo haujaridhisha sana hatuwezi kusahau kwamba Simba wamefanya vizuri sana kwenye mashindano ya kimataifa. Rai yangu wawe na umoja waache kulumbana wakati wa usajili kwa sababu wakati wa usajili ndiyo wakati wa kutengeneza timu bora, Simba ni marafiki zangu wasingekuwa marafiki nisingewapa ushauri huo. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa umaalum kabisa ninaupongeza uwekezaji ambao umefanywa na Azam, siku hizi tunapoangalia mpira ni Azam, tunavyocheza ni Azam na tunapoongea ni Azam. Wamefanya uwekezaji mkubwa ambao umetangaza tasnia ya mpira wa miguu hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa umaalum pia nimpongeze *GSM* kwa uwekezaji mzuri alioufanya ambao umebadilisha taswira na uwezo

wa timu ya Yanga. *GSM* amebadilisha taswira ya Yanga na ameleta mafanikio, *GSM* wewe ni mwamba, ujengewe mnara pale Makao Makuu ya Yanga. Ninaipongeza pia Menejimenti inayoongozwa na Eng. Hersi kwa kazi kubwa ambayo wameifanya. Yanga imefanya mambo makubwa ukuwauliza wachezaji wa Mamelodi Sundowns watakuambia kile walichokipata. Kuna wakati natamani kumshauri Gavana aangalie uwezekano wa kuiweka nembo ya Yanga kwenye shilingi mia na noti ya shilingi mia kama ipo. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mafanikio haya yaliyopatikana kwenye vilabu vya mpira pamoja na timu za Taifa yamechangiwa kwa kiwango kikubwa na hamasa iliyofanywa na Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alipokuwa akitoa milioni tano kwa kila goli linalofungwa kwa hatua ya makundi na alipotoa milioni kumi kwa hatua ya robo fainali na kuendelea, hakika Mama yetu ni mbunifu na ametengeneza historia mpya ya nchi yetu kwenye upande wa masuala ya michezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla muda haujaisha kwa namna ya kipekee kabisa nitumie fursa hii kumshukuru Mungu kwa kuendelea kunipa nguvu hata nimesoma hotuba kwa leo, naomba pia nimshukuru mke wangu na rafiki yangu kipenzi Ndugu Neema Mwigulu Nchemba na leo yuko hapa pamoja na watoto ambao leo wameungana nami, wamekuwa wakinipa faraja na kuniombea na kuniwezesha kutekeleza wajibu niliopewa wa kuwatumikia watanzania kwenye nafasi hii ambayo niliaminiwa na Mheshimiwa Rais, ahsanteni sana nawashukuru sana na muendelee kuniunga mkono hivyo hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee niwashukuru wapigakura wa Jimbo la Iramba, nawashukuru sana kwa kuendelea kuniamini na nawashukuru sana kwa kuendelea kuniombea, leo hii tumesoma hotuba mbili, hotuba iliyosomwa na Kaka yangu Profesa Kitila Mkumbo na hii ambayo nimesoma mimi leo mmenipatia *message* kwamba sisi ni miti inayostahimili ukame nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge, viongozi na wananchi wote kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maneo hayo naomba sasa kutoa hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa ngoja, hebu msaidizi kuna *paragraph* moja hivi mpelekee Mheshimiwa Waziri, anakuletea hapo ili utuwekee vizuri, hiyo sehemu ya tatu tu kuhusu hapo kwenye *currency points* lakini unaweza kuisoma *paragraph* yote.

Mheshimiwa Waziri unaweza kuisoma hiyo iliyo kwenye kitabu kwa sababu ulivyokuwa unasoma imeenda sawasawa na maneno yako isipokuwa hapo kwenye kiasi, kwa hiyo tusomee tu hiyo ya kwenye kitabu haina shida.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, kufanya marekebisho kwenye Kifungu cha 86 (1) cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi kwa kuweka ukomo wa faini ya juu ya kosa la kutotoa risiti wa kiasi cha *currency points* 1,000 sawa na shilingi 15,000,000 lengo la hatua hii ni kuleta unafuu kwa walipakodi na kuchochea ulipaji kodi kwa hiari. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, sasa unaweza kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya naomba sasa kutoa hoja, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**13 JUNI, 2024**

**HOTUBA YA WAZIRI WA FEDHA, MHESHIMIWA DKT. MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU (MB), AKIWASILISHA BUNGENI MAPENDEKEZO YA SERIKALI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA 2024/25 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

## I. UTANGULIZI

**1. Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu lipokee, lijadili na kukubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2024/25. Bajeti hii inawasilishwa kwa mujibu wa Ibara ya 137 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, ikisomwa pamoja na Kifungu cha 23 (3) cha Sheria ya Bajeti, Sura 439 na Kifungu cha 124 (4) cha Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari 2023.

**2. Mheshimiwa Spika**, pamoja na hotuba hii ninawasilisha vitabu vinne vinavyoelezea kwa kina makadirio ya Bajeti ya Serikali. Kitabu cha Kwanza ni Makadirio ya Mapato; Kitabu cha Pili ni Makadirio ya Matumizi ya Kawaida kwa Wizara, Idara Zinazojitegemea na Wakala wa Serikali; Kitabu cha Tatu ni Makadirio ya Matumizi ya Kawaida kwa Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa; na Kitabu cha Nne ni Makadirio ya Matumizi ya Maendeleo kwa Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala wa Serikali, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Aidha, Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2024 pamoja na Muswada wa Sheria ya Matumizi ya Serikali wa Mwaka 2024 kwa pamoja ni sehemu ya bajeti hii.

**3. Mheshimiwa Spika**, niruhusu kwa moyo wa simanzi nitoe pole kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, waheshimiwa wabunge pamoja na watanzania kwa ujumla kwa kuondokewa na wapendwa wetu Hayati Alhaj Ali Hassan Mwinyi, aliyekuwa Rais wa Awamu ya Pili wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Hayati Edward Ngoyai Lowassa, aliyewahi kuwa Mbunge wa Jimbo la Monduli na Waziri Mkuu Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, natoa pole kwa kuondokewa na Mheshimiwa Francis Leonard

Mtega, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Mbarali, na Mheshimiwa Ahmed Yahya Abdulwakil, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Kwahani, pamoja na Viongozi wengine wa Serikali waliofariki katika mwaka huu wa fedha. Mwenyezi Mungu azilaze roho zao mahala pema peponi. **Amina!**

4. **Mheshimiwa Spika**, niruhusu pia nitumie fursa hii kutoa pole kwa wananchi wote walioathiriwa na majanga mbalimbali ikiwemo ajali na mafuriko yaliyotokea maeneo mbalimbali nchini kutokana na mvua za *El-Nino*. Majanga haya yamesababisha athari mbalimbali ikiwemo vifo, majeruhi pamoja na uharibifu wa mali na miundombinu. Nawapa pole wananchi wote waliopoteza ndugu, jamaa na marafiki pamoja na mali zao kutokana na majanga hayo na nawaombea kwa Mwenyezi Mungu majeruhi wote wapone haraka na kurejea katika majukumu yao na awajalie marehemu wote pumziko jema la milele. **Amina!**

## II. BAJETI YA MWAKA 2024/25

5. **Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo, naomba niwasilishe makadirio ya Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2024/25 ambayo imeandaliwa kwa kuzingatia: Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025; Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2020; Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22 - 2025/26); Dira ya Maendeleo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki 2050; Ajenda ya Maendeleo ya Afrika 2063; Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030; pamoja na nyaraka, miongozo na makubaliano mengine ya kikanda na kimataifa ambayo Tanzania imeridhia.

6. **Mheshimiwa Spika**, Bajeti ya Serikali ya Mwaka 2024/25 ni ya nne katika utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22 - 2025/26), wenye dhima ya Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu. Aidha, dhima kuu ya Bajeti ya Mwaka 2024/25 kama ilivyokubaliwa na nchi wanachama wa

Jumuiya ya Afrika Mashariki ni "**Mageuzi Endelevu ya Kiuchumi kupitia Uimarishaji wa Sera za Kibajeti na Uwekezaji katika Kuhimili na Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi kwa Maendeleo ya Wananchi**".

**Shabaha za Uchumi Jumla**

**7. Mheshimiwa Spika**, kutokana na nyaraka na miongozo iliyozingatiwa katika uandaaji wa Bajeti hii, shabaha za uchumi jumla ni kama ifuatavyo:

i. Kuongeza kasi ya ukuaji wa Pato la Taifa kufikia asilimia 5.4 mwaka 2024 kutoka ukuaji wa asilimia 5.1 mwaka 2023;

ii. Kuendelea kudhibiti kasi ya mfumuko wa bei na kuhakikisha kuwa unabaki kwenye wigo wa tarakimu moja ya wastani wa asilimia kati ya 3.0 - 5.0 katika muda wa kati;

iii. Mapato ya ndani kufikia asilimia 15.8 ya Pato la Taifa mwaka 2024/25 ikilinganishwa na matarajio ya asilimia 15.4 mwaka 2023/24;

iv. Mapato ya kodi kufikia asilimia 12.9 ya Pato la Taifa mwaka 2024/25 kutoka matarajio ya asilimia 12.6 mwaka 2023/24;

v. Kuwa na nakisi ya bajeti (ikijumuisha misaada) isiyozidi asilimia 3.0 ya Pato la Taifa; na

vi. Kuwa na akiba ya fedha za kigeni kwa kiwango cha kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi minne (4).

**Misingi ya Bajeti**

**8. Mheshimiwa Spika**, uandaaji wa shabaha za uchumi jumla kwa mwaka 2024/25 umezingatia misingi (assumptions) ifuatayo:

i. Kuongezeka kwa ushiriki wa sekta binafsi kwenye shughuli za uwekezaji na biashara;
ii. Kuendelea kuhimili athari za majanga ya asili na yasiyo ya asili ikiwemo ukame, vita, magonjwa ya mlipuko, mafuriko;
iii. Kuimarika kwa uchumi wa dunia na utulivu wa bei katika masoko ya fedha na bidhaa;
iv. Kuendelea kuimarika kwa upatikanaji na usalama wa chakula nchini; na
v. Uwepo wa amani, usalama, umoja na utulivu wa ndani na nchi jirani.

**Maeneo ya Vipaumbele kwa Mwaka 2024/25**

**9. Mheshimiwa Spika**, bajeti ya Serikali ya mwaka 2024/25 imelenga kutekeleza vipaumbele vilivyozingatia maeneo yaliyoainishwa kwenye Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 - 2025/26 wenye dhima ya " ***Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu***" pamoja na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2024/25. Maeneo ya vipaumbele yaliyoainishwa katika Mpango ni pamoja na: kuchochea uchumi shindani na shirikishi; kuimarisha uwezo wa uzalishaji viwandani na utoaji huduma; kukuza biashara na uwekezaji; kuchochea maendeleo ya watu; na kuendeleza rasilimali watu.

**10. Mheshimiwa Spika**, baadhi ya maeneo mahsusi yatakayopewa kipaumbele ni pamoja na: kukamilisha miradi ya KIELELEZO na ile ya KIMKAKATI; kuimarisha sekta za UZALISHAJI; kuimarisha rasilimali watu hususani katika sekta za HUDUMA ZA JAMII; kuongeza matumizi ya TEHAMA; na kuboresha mazingira ya ufanyaji biashara na uwekezaji wa sekta binafsi. Aidha, maeneo mengine ya muhimu katika utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2024/25 ni kugharamia: mishahara ya watumishi wa umma; deni la serikali; Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa Mwaka 2024; maandalizi ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025; maandalizi ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050; na maandalizi ya michuano ya mpira wa miguu

ya mataifa ya Afrika (AFCON) ya mwaka 2027 ikiwa ni pamoja na ujenzi na ukarabati wa viwanja.

**11. Mheshimiwa Spika**, miradi mahsusi katika maeneo ya kipaumbele ambayo Serikali itatekeleza kupitia Bajeti ya mwaka 2024/25 imeainishwa kwa kina katika hotuba iliyowasilishwa leo asubuhi na Mheshimiwa Prof. Kitila Alexander Mkumbo (Mb), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - Mipango na Uwekezaji, alipokuwa akiwasilisha taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2023 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2024/25.

**Usimamizi wa Matumizi ya Fedha za Umma**

**12. Mheshimiwa Spika**, Serikali imefanya uwekezaji mkubwa kwenye mifumo ya uendeshaji wa shughuli zake ili kudhibiti matumizi ya fedha za umma. Hata hivyo, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali amekuwa akitoa hoja zinazohusu matumizi ya fedha za umma. Nipende kulihakikishia Bunge lako Tukufu na watanzania wote kuwa, Serikali makini ya Chama Cha Mapinduzi itaendelea kusimamia nidhamu ya matumizi ya fedha za umma kwa kuzingatia Sheria ya Bajeti, Sura 439; Sheria ya Fedha za Umma, Sura 348; Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura 290; Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura 410; na Sheria ya Matumizi ya Fedha za Umma ya Mwaka 2024. Aidha, Serikali itaendelea kuhakikisha Sheria hizo zinasimamiwa na kutekelezwa ipasavyo ikiwa ni pamoja na kujibu hoja zilizotolewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na hoja za wakaguzi wa ndani. Na endapo itabainika Afisa Masuuli wa Fungu husika ameshindwa kutekeleza matakwa ya Sheria hizo, **hatua kali za kinidhamu zitachukuliwa**.

**13. Mheshimiwa Spika**, niendelee kuwasisitiza Maafisa Masuuli kuzingatia Waraka wa Mkuu wa Utumishi wa Umma Na. 2 wa mwaka 2021 kuhusu utaratibu wa kutumia magari, aina na stahili za magari kwa viongozi katika utumishi wa umma kwa lengo la kupunguza matumizi. Aidha, hatua nyingine zitakazochukuliwa ni pamoja na kupunguza safari za ndani na nje na kupunguza ukubwa wa uwakilishi kwenye mikutano ya ndani na nje ya nchi. Vilevile,

niendelee kuwasisitiza Maafisa Masuuli wote kuendelea kufanya vikao/mikutano kwa njia ya mtandao na kupunguza matumizi ya karatasi.

**14. Mheshimiwa Spika**, Serikali inaendelea kuchukua hatua kwa taasisi za Serikali zinazokiuka taratibu za ununuzi ikiwemo kufanya ununuzi bila kupata ridhaa ya bodi za zabuni. Nitoe wito kwa taasisi zote za Serikali kufuata taratibu za ununuzi wa umma na kuhakikisha kuwa ununuzi wote unaidhinishwa na Bodi za Zabuni. Hii itaongeza uwazi na uwajibikaji katika mchakato wa ununuzi na hivyo, kudhibiti matumizi mabaya ya rasilimali za umma. Aidha, nawaelekeza Maafisa Masuuli kuendelea kutumia Mfumo wa Kielektroniki wa Ununuzi wa Umma katika ununuzi wa bidhaa, huduma na kandarasi pamoja na kuzingatia bei ya soko wakati wa ununuzi.

**15. Mheshimiwa Spika**, Serikali itaendelea kutekeleza Mkakati wa Kugharamia Miradi ya Maendeleo kwa Kutumia Vyanzo Mbadala (Alternative Project Financing - APF) ili kuongeza wigo wa upatikanaji wa fedha za utekelezaji wa miradi ya maendeleo na kupunguza utegemezi wa bajeti ya Serikali Kuu. Mfano halisi wa utekelezaji wa mkakati huo ni kufanikiwa kwa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Tanga (TANGA UWASA) kutoa hatifungani ya kijani yenye thamani ya shilingi bilioni 53.1. Aidha, Serikali itaendelea kutoa mafunzo katika Mamlaka za Serikali za Mitaa, sekta binafsi na taasisi za fedha kuhusu ugharamiaji wa miradi kwa njia mbadala ikiwemo utekelezaji wa miradi kwa ubia baina ya sekta ya umma na sekta binafsi (PPP).

**16. Mheshimiwa Spika**, utakumbuka kuwa, mwaka 2023/24, Serikali ilianzisha vitengo vya ufuatiliaji na tathmini katika wizara na taasisi zake ili kuimarisha usimamizi wa utekelezaji wa majukumu ya taasisi husika. Nipende kuwahakikishia kuwa Serikali itaendelea kuviongezea nguvu vitengo hivyo kwa kuvipatia rasilimali watu, fedha na vitendea kazi ili kuhakikisha shughuli zinazotekelezwa zinaakisi thamani halisi ya fedha.

**17. Mheshimiwa Spika**, tukitekeleza hatua hizo za kudhibiti matumizi ya fedha za umma, tutaokoa fedha ambazo zitaweza kuelekezwa kwenye miradi itakayosaidia jamii kama vile ujenzi wa barabara, vituo vya afya, miundombinu ya maji na shule. Aidha, niwasihi viongozi wenzangu kuona umuhimu wa kusimamia matumizi ya fedha za umma ili kuweza kuleta maendeleo kwa wananchi. Na niwaonye wale wachache wanaotumia vibaya fedha za umma **waache mara moja!** Na wale watakaobainika hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yao.

**MAFANIKIO YA SERIKALI YA AWAMU YA SITA**

**18. Mheshimiwa Spika**, napenda kutumia fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa uongozi wake shupavu ambao umedhihirishwa wazi na majira ambayo nchi imepitia. Ikumbukwe kuwa, Mheshimiwa Rais alipokea usukani wa kuiongoza nchi ikiwa imepatwa na tukio la huzuni la kuondokewa na aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, tukio ambalo halikuwahi kutokea hapa nchini lakini **MAMA** hakuyumba na hata sasa tunasonga mbele, nchi haijakwama kwenye jambo lolote, Nchi inasonga mbele!

**19. Mheshimiwa Spika**, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, alipokea nchi katika kipindi ambacho dunia ilikuwa inapita katika msukosuko wa kiuchumi kufuatia UVIKO – 19 na baadae kidogo mzozo wa kisiasa kule Ulaya ya mashariki, msukosuko wa kiuchumi ambao uliyumbisha hata chumi za mataifa makubwa, sababu ambazo zingetosha kuachana na miradi mikubwa ya maendeleo, lakini bado Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, akasema ataendeleza miradi yote iliyokuwa inatekelezwa na awamu zilizopita na ataleta miradi mingine mipya.

**20. Mheshimiwa Spika**, licha ya misukosuko hiyo, Serikali ya Chama Cha Mapinduzi chini ya uongozi mahiri wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, imeendelea kuboresha maeneo yafuatayo: sekta za uzalishaji

ikiwemo kilimo, mifugo, uvuvi na madini; miundombinu wezeshi hususan utekelezaji wa miradi ya reli, barabara, viwanja vya ndege, usafiri wa anga na mawasiliano; na huduma za kijamii ikiwemo maji, afya na elimu. Kwa ujumla, Serikali ya Awamu ya Sita imekuwa na mafanikio makubwa katika kipindi hiki cha miaka mitatu ambayo hayahitaji "***VAR***" kuyang'amua. **Mheshimiwa Spika**, naomba uniruhusu sasa nielezee baadhi ya mafanikio hayo kama ifuatavyo:

**Sekta ya Uchukuzi**

**21. Mheshimiwa Spika**, kama nilivyosema, Mheshimiwa Rais aliahidi kuendeleza utekelezaji wa miradi ya awamu zilizopita na kuleta miradi mipya. Ni dhahiri sasa, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan hakusema tu bali ametekeleza kauli hiyo. Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, alipokea mradi wa reli ya kisasa (SGR) ukiwa umetekelezwa kwa asilimia 83.55 kwa *Lot* 1 na asilimia 57.57 kwa *Lot* 2 ambazo sasa zimekamilika na kufanyiwa majaribio. Sasa hata nauli zimeshatangazwa Dar es Salaam - Dodoma bei ya jogoo wawili tu yaani shilingi 31,000. **Hii inatuambia nini Mheshimiwa Spika? Dkt. Samia Suluhu Hassan, Ameweza pasipo mashaka kuiongoza Tanzania.**

**22. Mheshimiwa Spika,** itakumbukwa kuwa, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, aliahidi kuanzisha miradi mingine mipya. Hilo hakuliahidi tu, limetekelezwa kikamilifu kwani alianzisha ujenzi wa reli *Lot* 3 (Makutupora -Tabora), *Lot* 4 (Tabora -Isaka), *Lot* 6 (Tabora - Kigoma) na *Lot* 7 (Uvinza - Musongati) ambazo hazikuwepo wakati Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan akipokea kijiti. Kazi kwenye vipande vyote hivi inaendelea kwa usimamizi wa upatikanaji wa fedha kupitia *Standard Chartered Bank* kwa *Lot* 3, *Lot* 4 na *Lot* 5, na Benki ya Maendeleo ya Africa (AfDB) kwa *Lot* 6 na *Lot* 7 ikiwa ni ushiriki wa kwanza kwa benki hii kushiriki kwenye mradi kama huu kwenye ukanda wetu.

**23. Mheshimiwa Spika**, Serikali imeendelea kuboresha miundombinu ya bandari ikiwemo kuongeza kina kufikia mita 15.5 na upana mita 200 katika lango la kuingia na kugeuza meli kwa ajili

ya kupokea meli kubwa katika bandari ya Dar es Salaam. Kadhalika, Serikali inaendelea na ujenzi wa Bandari Kavu ya Kwala ambapo utekelezaji umefikia asilimia 96.0.

**24. Mheshimiwa Spika**, Serikali imeendelea kuimarisha usafiri wa anga ikiwemo: ujenzi wa kiwanja cha ndege cha kimataifa cha Msalato ambapo ujenzi umefikia asilimia 56.9 kwa Package I - Miundombinu na asilimia 22.56 kwa Package II - Majengo. Aidha, Serikali inaendelea na ukarabati, upanuzi na uboreshaji wa viwanja vya ndege vya Iringa, Musoma, Tabora, Shinyanga, Sumbawanga na Moshi ambavyo vipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Vilevile, Serikali imeendelea kuboresha miundombinu ya hali ya hewa nchini kwa kukamilisha ufungaji wa rada mbili (2) za hali ya hewa katika Mikoa ya Mbeya na Kigoma. Kadhalika, ndege mpya saba (7) zimenunuliwa na hivyo kuifanya ATCL kuwa na jumla ya ndege 16.

**Sekta ya Ujenzi**

**25. Mheshimiwa Spika**, ili kurahisisha huduma za usafiri na usafirishaji nchini pamoja na kuwawezesha wananchi kutekeleza shughuli zao za kiuchumi na kijamii, Serikali ya awamu ya sita imeendelea na ujenzi na ukarabati wa barabara kuu, barabara za mikoa na madaraja kupitia TANROADS pamoja na barabara za mijini na vijijini kupitia TARURA. Ni dhahiri MAMA hasemi tu, bali anatekeleza! Niwape mfano mmoja, utekelezaji wa ujenzi wa Daraja la Kigongo – Busisi lenye urefu wa kilometa 3 na barabara unganishi yenye urefu wa kilometa 1.66 kwa kiwango cha lami umefikia asilimia 88.0 na jumla ya shilingi bilioni 426.1 zimetumika. Mradi huu unatarajiwa kukamilika mwaka 2024/25.

**26. Mheshimiwa Spika**, kwa kutambua kuwa barabara za vijijini ni maisha, uchumi na usalama kwa watanzania tulio wengi, Serikali ya Awamu ya Sita imeendelea kuiongeza bajeti ya TARURA kutoka shilingi bilioni 710.31 mwaka 2022/23, shilingi bilioni 825.09 mwaka 2023/24 hadi kufikia shilingi bilioni 841.19 kwa mwaka 2024/25. Bajeti hii itawezesha TARURA kuendelea na ujenzi, matengenezo pamoja

na ukarabati wa miundombinu ya usafiri na usafirishaji wa vijijini na mijini. **Hii nayo inatuambia nini Mheshimiwa Spika? Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Anatosha kuiongoza Tanzania.**

**Sekta ya Nishati**

**27. Mheshimiwa Spika**, MAMA alipokea Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Maji wa Julius Nyerere (JNHPP) utakaozalisha jumla ya MW 2,115 ukiwa na takribani asilimia 37 ambapo hadi Aprili 2024 utekelezaji ulikuwa umefikia asilimia 97.43 na kuanza uzalishaji kupitia mtambo namba tisa (9) unaoingiza katika Gridi ya Taifa jumla ya MW 235 na hivyo, kuimarisha upatikanaji wa umeme. Hadi kufikia hatua hii jumla ya shilingi trilioni 6.01 zimetumika. Kwa sasa kazi inaendelea ili kukamilisha ufungaji wa mitambo saba (7) yenye uwezo wa kuzalisha MW 235 kila mmoja. Aidha, Serikali imekamilisha Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Rusumo kwa kutumia maporomoko ya maji ya Mto Kagera ambapo mradi huu unahusisha nchi tatu (3) za Tanzania, Burundi na Rwanda ambao unachangia MW 26.7 katika Gridi ya Taifa. Kwa upande wa mwingine, Serikali imeanza kutekeleza mradi wa ujenzi wa mitambo ya kuzalisha umeme wa MW 150 kwa kutumia nguvu ya jua katika eneo la Kishapu mkoani Shinyanga. Vilevile, Serikali inaendelea na ujenzi na ukarabati wa njia za kusafirisha na kusambaza umeme ambazo zinaunganisha maeneo mbalimbali nchini na nchi jirani.

**28. Mheshimiwa Spika**, Serikali ya Awamu ya Sita imekamilisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme ya msongo wa Kilovoti 400 na kituo kipya cha kupoza umeme cha Chalinze cha Kilovoti 400/220/132 na kimeanza kutumika kuingiza umeme katika Gridi ya Taifa. Kwa upande mwingine, Serikali imekamilisha Mradi wa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa Kilovoti 400 yenye urefu wa kilometa 414 kutoka Singida hadi Namanga kupitia Babati na Arusha. Gharama za mradi huu ni dola za Marekani milioni 258.82. Aidha, miundombinu yote ya kusafirisha umeme imekamilika na umeme unasafirishwa kutoka Singida hadi Arusha. Mradi huu utawezesha kuiunganisha Gridi ya Taifa na Nchi za Afrika Mashariki (*Eastern Africa Power Pool - EAPP)*.

**29. Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa mradi wa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa Kilovoti 400 kutoka Iringa kupitia Mbeya, Tunduma hadi Sumbawanga pamoja na ujenzi wa vituo vya kupoza umeme vya Kisada (Iringa), Iganjo (Mbeya), Tunduma na Sumbawanga umefikia asilimia 27 ya utekelezaji. Gharama za mradi huu ni dola za Marekani milioni 615. Mradi huu unalenga kuunganisha Gridi ya Taifa na nchi za Kusini mwa Afrika *(Southern Africa Power Pool – SAPP)*. Kwa upande mwingine, Serikali imeanza kutekeleza mradi wa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa Kilovoti 132 kutoka Malagarasi hadi Kidahwe mkoani Kigoma. Kazi hii inaenda sambamba na kazi ya ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme wa MW 49.5 kwa kutumia maporomoko ya maji ya Mto Malagarasi.

**30. Mheshimiwa Spika**, hadi Mei 2024, Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini (REA) imeunganisha umeme katika vijiji 11,973, sawa na asilimia 97.2 ya vijiji vyote nchini na wakandarasi wanaendelea kukamilisha uunganishaji wa umeme katika vijiji vilivyobaki. Vilevile, vitongoji 32,827 kati ya 64,359 nchi nzima vimefikishiwa huduma ya umeme. Kazi hiyo inaendelea hadi vitongoji vyote vitakapopata umeme.

**31. Mheshimiwa Spika**, katika Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki, Serikali kupitia TPDC inamiliki asilimia 15 ya hisa. Hadi mwezi Mei 2024, Serikali imelipa jumla ya Dola za Marekani milioni 307.3, sawa na asimilia 99.8 ya kiasi kinachotakiwa kulipwa cha Dola za Marekani milioni 308. Kazi mbalimbali zinaendelea kutekelezwa ambapo shehena za mabomba ya mradi yenye jumla ya urefu wa kilometa 600 zimewasili nchini na mradi unatarajia kuendelea kupokea shehena ya mabomba yenye jumla ya urefu wa kilometa 100 kila mwezi kwa miezi 11 ijayo. Kazi ya kulaza mabomba inatarajiwa kuanza mwezi Agosti 2024 na mradi kukamilika Desemba 2025. ***Mafanikio haya katika sekta ya nishati ni ishara kwamba MAMA amedhamiria upatikanaji wa umeme wa uhakika nchi nzima. Hakika MAMA Mitano Tena!***

**Sekta ya Maji**

**32**. **Mheshimiwa Spika**, sio tu kwamba, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameendeleza miradi ya kimkakati na kuleta mipya, bali ameweza kuweka historia ya kukwamua miradi sugu ya maji iliyoshindikana kwa miaka mingi. Katika kutimiza azma ya kumtua mama ndoo kichwani, Serikali imeendelea kutekeleza miradi mikubwa na ya kimkakati yenye lengo la kuimarisha upatikanaji wa huduma ya maji mijini na vijijini. Kwa msisitizo zaidi Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan imekamilisha Mradi wa ujenzi wa tekeo (intake) Kigoma na Mradi wa Maji wa Orkesumet Manyara. Aidha, Serikali iliendelea na utekelezaji wa: Mradi wa Ujenzi wa mtambo wa kutibu maji Butimba ambao utekelezaji umefikia asilimia 99; Mradi wa Maji Mugango - Kiabakari - Butiama asilimia 99; Mradi wa Maji Same - Mwanga - Korogwe asilimia 92; Mradi wa Maji kutoka Mto Kiwira kwenda jijini Mbeya asilimia 20; Mradi wa Maji wa Miji 28 asilimia 25; na Mradi wa Ujenzi wa Bwawa la Kidunda asilimia 20. **Mheshimiwa Spika**, napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu na wananchi kwa ujumla kuwa hadi Desemba 2023, hali ya upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama ulifikia asilimia 79.6 katika maeneo ya vijijini na asilimia 90.0 mijini. Kwa ujumla, mafanikio hayo yamechangiwa na kukamilika kwa utekelezaji wa miradi 1,633 ya maji vijijini na miradi 213 ya maji mijini. **Hii inatwambia nini Mheshimiwa Spika? Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, anajali mahitaji ya lazima ya wananchi wa Tanzania.**

**Sekta ya Kilimo**

**33. Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa sekta ya kilimo, Mheshimiwa Rais alipokea nchi ikiwa na eneo la umwagiliaji la ukubwa wa hekta 726,000 tokea tunapata uhuru. Kwa kipindi chake takribani miaka mitatu anatekeleza miradi mipya yenye ukubwa wa hekta 543,366 yenye thamani ya shilingi trilioni 1.18 na ameanza ujenzi wa mabwawa makubwa 14 na kukamilisha upembuzi yakinifu wa mabonde 22. Kwa upande wa sekta ndogo ya mbegu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan alipokea nchi ikiwa

inajitosheleza kwa mahitaji ya mbegu bora kwa asilimia 22 tu na sasa ndani ya miaka mitatu ya uongozi wake tumefikia utoshelevu wa asilimia 78 na ifikapo 2026/27 tutakuwa tumejitosheleza kwa asilimia 100. Kwa upande wa uhifadhi wa chakula, nchi ilikuwa na uwezo wa tani 250,000 tu sasa katika kipindi cha miaka mitatu tumefikia tani 500,000. Mauzo ya nje yalikuwa wastani wa dola za Marekani bilioni 1.2 leo tuna wastani wa dola za Marekani bilioni 2.3. Utoshelevu wa chakula umefikia asilimia 124 mwaka 2023/24 na kutarajiwa kufikia asilimia 130 mwaka 2024/25. **Hii nayo inatwambia nini Mheshimiwa Spika? Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, anapambana kwa vitendo kuondoa umasikini wa watanzania.**

**34. Mheshimiwa Spika**, kwa kutambua umuhimu wa sekta ya kilimo, Serikali ya Awamu ya Sita imeendelea kuongeza bajeti ya Wizara ya Kilimo kutoka shilingi bilioni 294.0 mwaka 2021/22 hadi shilingi bilioni 970.8 mwaka 2023/24. Kuongezeka kwa bajeti hiyo kumewezesha kuendelea na utekelezaji wa Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (ASDP II) yenye lengo la kuboresha sekta ya kilimo ili kuongeza tija katika kilimo ikijumuisha kuinua wakulima wadogo, kuimarisha usalama wa chakula na lishe pamoja na kuongeza mchango katika Pato la Taifa. Aidha, Serikali ilitoa ruzuku ya mbolea kiasi cha shilingi bilioni 389.9.

**Sekta ya Mifugo na Uvuvi**

**35**. **Mheshimiwa Spika**, Serikali imeendelea kuongeza Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kutoka shilingi bilioni 66.8 mwaka 2020/21 hadi bilioni 295.9 mwaka 2023/24. Ongezeko hilo ni mara 4 zaidi ya bajeti iliyokuwa ikitengwa awali. Kutokana na ongezeko hilo na utekelezaji mzuri wa sera na miongozo iliyopo, mafanikio mbalimbali yamepatikana ikijumuisha: kuongezeka kwa mauzo ya mazao ya mifugo na uvuvi nje ya nchi; ujenzi na uboreshaji wa miundombinu ya mifugo na uvuvi ikiwemo Bandari ya Uvuvi Kilwa Masoko ambapo ujenzi umefikia asilimia 53; ujenzi wa miundombinu ya ukuzaji viumbe maji, mialo na masoko ya samaki, ujenzi wa miundombinu ya maabara ya uzalishaji wa chanjo za mifugo, minada ya kisasa 51; ujenzi wa majosho 746 na mabwawa 15; uzalishaji wa malisho na

pembejeo ikiwa ni pamoja na kuongezeka kwa maeneo ya malisho hadi kufikia hekta milioni 3.5; kuboresha huduma za ugani nchini kwa kutoa mafunzo na vitendea kazi kwa wataalamu; uboreshaji wa mbari za mifugo na upatikanaji wa vifaranga vya samaki; kuboresha shughuli za uvuvi katika bahari kuu; na kuwawezesha wakulima wa mwani, wafugaji na wavuvi kupata mikopo ya vitendea kazi na fedha taslimu.

**Sekta ya Afya**

**36. Mheshimiwa Spika**, Serikali imeendelea na jitihada za kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora za afya katika ngazi zote za utoaji huduma nchini. Jitihada hizo zinahusisha uboreshaji wa miundombinu ya vituo vya kutolea huduma vilivyopo pamoja na ujenzi wa vituo vipya zaidi ya 1,324. Waheshimiwa Wabunge na watanzania wenzangu, sote ni mashahidi kuwa katika kipindi cha mwaka 2023/24, vituo vya kutolea huduma za afya viliongezeka na kufikia 12,266 kutoka vituo 11,040 vilivyokuwepo mwaka 2022/23.

**37. Mheshimiwa Spika**, sote tunafahamu kuwa, huduma za uchunguzi wa magonjwa ni nguzo muhimu katika utoaji wa huduma za tiba ya magonjwa kwa wananchi. Kwa kutambua hilo, Serikali imeendelea kuimarisha huduma hizo kwa kufanya uwekezaji mkubwa katika upatikanaji wa vifaa vya uchunguzi wa magonjwa ambapo *digital X – ray* zimefikia 346, *ultrasound* 677 na mashine za *CT scan* 31 ambazo zimeanza kutumika kutoa huduma katika Hospitali za Rufaa za Mikoa. Aidha, Serikali imekamilisha usimikaji wa MRI 4. Kuanza kupatikana kwa huduma hizo kumewawezesha wananchi kuokoa gharama za kufuata huduma hizo umbali mrefu ikiwemo kwenda nje ya nchi. Haya ni mapinduzi makubwa yaliyofanywa na Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

**38. Mheshimiwa Spika**, Serikali imeendelea kutoa kipaumbele katika upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi vya maabara kwenye vituo vya kutolea huduma za afya vinavyomilikiwa na Serikali. Aidha, katika kuijengea uwezo Bohari ya Dawa (MSD)

kuwa na dawa na bidhaa za afya za kutosha, kwa mara ya kwanza na katika historia ya Tanzania Serikali imetoa jumla ya shilingi bilioni 100 ikiwa ni sehemu ya mtaji wa MSD. Fedha hizo zimewezesha upatikanaji wa bidhaa muhimu za afya.

**39. Mheshimiwa Spika**, katika kukabiliana na changamoto ya uhaba wa wataalam wa afya, katika kipindi hiki, Serikali imetoa kibali cha kuajiri jumla ya watumishi 13,187. Aidha, katika kuimarisha na kuzisogeza huduma za kibingwa na ubingwa bobezi karibu zaidi na wananchi, Serikali imeendelea kutoa ufadhili wa masomo katika fani hizo. Mathalan, kupitia **Mpango wa Dkt. Samia Afya Scholarship**, jumla ya wataalam 1,251 wanaosomea ubingwa na ubingwa bobezi katika vyuo mbalimbali ndani na nje ya nchi walipata ufadhili wa masomo kwa gharama ya shilingi bilioni 9 zilizotolewa na Serikali. **Hii nayo inatwambia nini Mheshimiwa Spika? Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ana upendo wa dhati kwa watanzania.**

**Sekta ya Elimu**

**40. Mheshimiwa Spika**, sasa naomba nizungumzie mageuzi makubwa kwenye sekta ya elimu ambayo yameanza kutekelezwa mwaka huu kwa awamu. Awali ya yote naomba kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuweka kipaumbele kwenye sekta ya elimu. Katika kipindi cha takribani miaka mitatu cha uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Serikali imeongeza uwekezaji mkubwa katika sekta ya elimu ikiwemo uwekezaji kwenye miundombinu, vitendea kazi, ajira, maslahi ya wanafunzi na kuanzisha mageuzi makubwa ya elimu. Serikali ya Awamu ya Sita imeendelea kuimarisha utoaji wa elimu ya msingi na sekondari kwa kuboresha miundombinu ya elimu ikijumuisha ujenzi na ukarabati wa vyumba vya madarasa, mabweni, mabwalo na uzio wa shule ambapo jumla ya shilingi trilioni 1.29 zimetolewa.

**41. Mheshimiwa Spika**, uwekezaji katika elimu umeelezwa vizuri katika hotuba za Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, na Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia - kwa hiyo sitarudia kwa undani. Hata

hivyo, tukumbuke hiki ndicho kipindi ambacho ujenzi na ukarabati wa shule za awali, shule za msingi na shule za sekondari umeongezeka kwa kasi kubwa. Kwa mfano, kama ilivyoelezwa na Mawaziri hao wa sekta ya elimu, Serikali itaanza kujenga shule mia moja za sekondari za mkondo wa amali kuanzia mwaka ujao wa fedha. Mafunzo ya amali yatakayotolewa ni ya nyanja ya ufundi, yaani *technical secondary schools*, kama ilivyo Tanga Technical School, Moshi Technical School na kadhalika. Na huu ni mwanzo tu. Kadhalika, ujenzi wa vyuo 64 vya VETA katika wilaya 64 ambazo zilikuwa hazina vyuo hivyo pamoja na ujenzi wa chuo cha VETA cha Mkoa wa Songwe unaendelea.

**42. Mheshimiwa Spika**, chini ya uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita, siyo tu kwamba mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu imeongezwa, lakini pia kiasi cha fedha anachopata mwanafunzi kimeongezeka na zaidi ya hapo sasa Serikali imeanza kutoa mikopo hata kwa wanafunzi wanaosoma vyuo vya kati. Hadi Aprili 2024, jumla ya shilingi trilioni 1.98 zimetolewa kwa ajili ya mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu na vyuo vya kati. Kadhalika, Serikali imeondoa ada ya wanafunzi kwa kidato cha tano na cha sita sambamba na kufuta ada ya mitihani. Aidha, Serikali imeendelea kugharamia Programu ya Elimumsingi na Sekondari bila Ada ambapo jumla ya shilingi bilioni 766.1 zimetolewa.

**43. Mheshimiwa Spika**, kati ya jambo ambalo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan atakumbukwa nalo daima katika historia ya Taifa letu ni jinsi alivyoagiza na anavyosimamia mageuzi makubwa ya elimu hapa nchini. Mageuzi haya ni makubwa sana, ni magumu sana na yatakuwa na uhitaji mkubwa wa fedha, rasilimali watu na umakini mkubwa. Matunda ya mageuzi haya ni makubwa sana lakini hatutayaona haraka. Haya ni mageuzi ambayo kiongozi anaeangalia tu uchaguzi ujao angeogopa kuyaanzisha. Ni mageuzi ambayo kiongozi anaeangalia maslahi ya vizazi vijavyo angeyapa kipaumbele. Kuna msemo usemao kuwa "***a politician looks at the next election but a stateman looks at the next generation*".** Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan siyo tu kwamba ni

mwanasiasa shupavu bali pia ni kiongozi jasiri mwenye maono makuu ya kulijenga Taifa letu kwa vizazi na vizazi.

**44. Mheshimiwa Spika**, katika mageuzi haya ya elimu, ifikapo mwaka 2027 kila mtoto wa Kitanzania atalazimika kusoma mpaka kidato cha nne. Kwa maana hiyo kila mtoto itabidi akae shuleni si chini ya miaka kumi. Labda niseme tu, sasa hivi vijana wetu wanamaliza elimu ya lazima, yaani darasa la saba, wakiwa na miaka 13 - umri ambao hawawezi kujiajiri wala hawaajiriki. Kwa mageuzi haya, sasa mtoto wa Kitanzania atamaliza elimu ya lazima akiwa na miaka kumi na sita. Hatua hii inaendana na nchi nyingi duniani na ni hatua nzuri kiuchumi kuandaa nguvu kazi. Zaidi ya hapo, sasa elimu ya kidato cha kwanza mpaka cha sita itakuwa imegawanyika katika mikondo miwili, mkondo wa elimu jumla na mkondo wa elimu ya amali. Wale watakaopitia mkondo wa elimu ya amali watapata elimu ya sekondari sambamba na ujuzi kama unaotolewa kwenye vyuo vya VETA na vyuo vya ufundi. Haya ni baadhi tu ya mambo yaliyoko kwenye mageuzi ya elimu na mitaala.

**45. Mheshimiwa Spika**, swali ambalo kila mtu anauliza ni je, tutatenga fedha za kuwezesha utekelezaji wa mageuzi haya ya sera ya elimu na mitaala mipya? Napenda kuwahakikishia waheshimiwa wabunge na watanzania wote kwamba mageuzi haya ni maelekezo ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, hivyo sisi na Mawaziri wote tunatoa kipaumbele katika kutekeleza mageuzi haya. Fedha zitapatikana na zitatolewa kwa wakati. Tunaharakisha kutumia fedha za Programu ya Kuboresha Upatikaji Fursa Sawa katika Ujifunzaji Ngazi ya Elimu ya Awali na Msingi (BOOST) na Mradi wa Kuboresha Elimu ya Sekondari (SEQUIP) ili tuwe na miundombinu ya kutosha kuhakikisha ifikapo mwaka 2027 watoto wote watasoma mpaka kidato cha nne na mafunzo ya amali yatatolewa kwa wanafunzi wengi kwa viwango vinavyotakiwa. Bajeti ya sekta ya elimu kwa mwaka ujao imeongezwa ili kuweza kugharamia mageuzi haya makubwa. Tutafanya kila tuwezalo kufanikisha mageuzi haya makubwa ambayo ni kielelezo hata kwa nchi nyingine za Afrika. **Mheshimiwa Spika, hii ndio Tanzania ijayo inayojengwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.**

## Sekta ya Madini

**46**. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Awamu ya Sita kumekuwa na mafanikio katika sekta ya madini ikiwemo: kuendelea kuongezeka kwa mchango wa sekta ya madini kwenye Pato la Taifa kutoka asilimia 7.3 mwaka 2021 hadi asilimia 9.0 mwaka 2023; kuongezeka kwa vituo vya ununuzi wa madini kutoka 61 mwaka 2020/21 hadi vituo 100 mwaka 2023/24; pamoja na kuanzishwa kwa soko jipya moja (1) la madini hivyo kufikia masoko 42. Aidha, Serikali imenunua mitambo mitano (5) ya uchorongaji kwa ajili ya wachimbaji wadogo inayotumika katika maeneo mbalimbali nchini. Vilevile, Serikali kupitia Benki Kuu ya Tanzania imeanzisha utaratibu wa kununua dhahabu kwa ajili ya akiba ya Taifa (National Gold Reserve) kwa lengo la kuimarisha akiba ya fedha za kigeni na kusaidia katika utekelezaji wa Sera ya Fedha. Hadi Aprili 2024, Benki Kuu ya Tanzania imenunua dhahabu yenye thamani ya dola za Marekani milioni 26 ambapo malengo ya Serikali ni kununua tani sita (6) za dhahabu yenye thamani ya dola za Marekani milioni 400. Kadhalika, Serikali inaendelea kuhamasisha viwanda vya ndani vya kuchenjua dhahabu kufanya taratibu za kupata Ithibati ya *London Bullion Market Association* (LBMA) ili kuwezesha dhahabu inayosafishwa kutambuliwa kwenye masoko ya kimataifa na kuweza kununuliwa kwa ajili ya kuhifadhiwa kama fedha.

## Sekta ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji

**47**. **Mheshimiwa Spika**, sekta ya viwanda imepata mafanikio mbalimbali ikiwemo: kuendelea na ulipaji wa fidia kwa wananchi wanaopisha Mradi Unganishi wa Mchuchuma na Liganga; kukamilisha maandalizi ya kuanza utekelezaji wa mradi wa Magadi Soda Engaruka; kufufua kiwanda cha Kilimanjaro Machines Tools Company (KMTC); kufanya usanifu na kuendeleza utengenezaji wa vifaa tiba na kuvisambaza katika hospitali mbalimbali nchini; kukamilisha utafiti na kutengeneza teknolojia kwa ajili ya kuchakata alizeti itakayosaidia kupunguza uhaba wa mafuta ya kula; kusimamia utekelezaji wa mfumo wa stakabadhi za ghala kwa waendesha ghala na meneja dhamana wa mazao mbalimbali; na

kuratibu majadiliano ya kikanda na kimataifa ili kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji.

**Sekta ya Maliasili na Utalii**

**48**. **Mheshimiwa Spika**, Serikali pia imeendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ya kutangaza utalii ndani na nje ya nchi ikiwemo programu ya *Tanzania - The Royal Tour* ili kuongeza mapato yatokanayo na utalii. Kutokana na mikakati hiyo, idadi ya watalii walioingia nchini iliongezeka hadi 1,808,205 mwaka 2023 kutoka watalii 922,692 mwaka 2021. Aidha, mapato ya utalii yameongezeka kutoka dola za Marekani bilioni 1.31 mwaka 2021 hadi dola za Marekani bilioni 3.37 mwaka 2023. Ni matumaini yangu kuwa, filamu ya *Amazing Tanzania* iliyozinduliwa mwezi Mei 2024 itaongeza zaidi mapato yatokanayo na sekta ya utalii.

**Sekta ya Mawasiliano**

**49**. **Mheshimiwa Spika**, Serikali inatambua umuhimu wa sekta ya mawasiliano katika kuhakikisha uwepo wa jamii yenye habari sahihi na iliyowezeshwa kidijitali kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Katika kipindi cha miaka mitatu ya uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita, mafanikio mbalimbali yamepatikana katika sekta hii ikiwemo: kufanyika kwa operesheni ya anwani za makazi ambapo anwani za makazi takribani 12,810,353 zimesajiliwa; na kuongeza wigo wa miundombinu ya mkongo wa Taifa wa mawasiliano kwa kujenga kilometa 3,000 na kufanya jumla ya kilometa 11,319 za mkongo wa Taifa ambazo zitawezesha upatikanaji wa mawasiliano ya kasi na ubora na uhakika katika Wilaya 99 nchini hivyo kuchochea maendeleo ya jamii na uchumi.

**Sekta ya Ardhi**

**50**. **Mheshimiwa Spika**, Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano ya Tanzania, imeendelea kutenga fedha kwa ajili ya kuongeza kasi ya upangaji, upimaji na umilikishaji wa ardhi ambapo

hatua mbalimbali zimechukuliwa. Hatua hizo ni pamoja na: utekelezaji wa Mradi wa Usalama wa Milki za Ardhi; kutekeleza Programu ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi kwa kushirikiana na sekta binafsi na taasisi za umma; na kuendelea kuboresha mifumo ya TEHAMA katika utoaji wa huduma. Aidha, kwa kuzingatia umuhimu wa upangaji, upimaji na umilikishaji wa ardhi nchini, Serikali imeridhia kurejeshwa kwa matumizi ya akaunti ya Mfuko wa Maendeleo ya Ardhi ambapo Serikali imetoa mtaji wenye thamani ya shilingi bilioni 15.4 na imeridhia marejesho ya fedha kiasi cha shilingi bilioni 50 za kupanga, kupima na kumilikisha zinazodaiwa kwenye mikopo ya halmashauri ziingizwe kwenye Mfuko huu. Hatua nyingine iliyochukuliwa ni uendeshwaji wa kliniki za ardhi katika mikoa 22 nchini. Kliniki hizi zimekuwa na mafanikio makubwa kutokana na wananchi wengi kujitokeza kusikilizwa kwa uhuru na uwazi changamoto zao na kupatiwa ufumbuzi ambapo hadi Mei 2024, wananchi 35,963 walihudumiwa. Aidha, migogoro na malalamiko 7,444 yalipokelewa ambapo migogoro 4,565 ilitatuliwa na migogoro 2,879 inaendelea kushughulikiwa.

**Utawala Bora, Ulinzi na Usalama**

**51. Mheshimiwa Spika**, Serikali ya Chama Cha Mapinduzi chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, imeendelea kuimarisha mifumo ya utoaji haki ikijumuisha ujenzi wa miundombinu na kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika uendeshaji wa mashauri ya mahakama. Aidha, kutokana na umahiri wa Serikali katika kujali haki za binadamu na kuheshimu utawala wa sheria nchini, Tanzania imefanikiwa kuwa mwenyeji wa mikutano ya kimataifa ya masuala haya ikiwemo Kikao cha 77 cha Kamisheni ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu pamoja na Mkutano wa Mawaziri wa Sheria wa nchi za Jumuiya ya Madola. Vilevile, katika jitihada za kukuza na kuimarisha demokrasia nchini, Bunge lako Tukufu lilitunga Sheria ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi ya Mwaka 2024 na Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani ya Mwaka 2023 pamoja na kufanya marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa, Sura 258.

**52. Mheshimiwa Spika**, Serikali imeendelea kuimarisha na kusimamia hali ya ulinzi na usalama wa mipaka ya nchi yetu. Katika kuimarisha usalama wa raia na mali zao, Serikali imejenga jumla ya vituo 26 vya polisi vya daraja A, B na C kwa gharama ya shilingi bilioni 9.63; ofisi 6 za makamanda wa polisi wa mikoa shilingi bilioni 9.46; na ujenzi na ukarabati wa nyumba 57 za mapumziko na makazi shilingi bilioni 7.2. Aidha, Tanzania imeendelea kutoa mchango katika ulinzi wa amani chini ya Umoja wa Mataifa na jumuiya za kikanda kupitia Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ). Jukumu hili limeongeza sifa kwa nchi kimataifa, kuimarisha uhusiano wa kidiplomasia na nchi mbalimbali pamoja na kulipa jeshi letu uzoefu wa kimataifa.

**Michezo, Sanaa na Burudani**

**53. Mheshimiwa Spika**, Serikali ya Awamu ya Sita inatambua umuhimu wa michezo, sanaa na burudani katika kukuza ajira hususani kwa vijana. Kwa kuzingatia hilo, Serikali imeendelea kuwaunganisha wasanii wa Tanzania na soko la kimataifa kupitia mikutano na matamasha mbalimbali na kuhakikisha kuwa kazi za ubunifu wao zinalindwa. Aidha, kwa upande wa michezo, Serikali ya awamu ya Sita imeendelea kujenga misingi ya uibuaji na uendelezaji wa vipaji kuanzia mashuleni ambayo imesaidia kuongeza ajira na kipato kwa wachezaji wanaosajiliwa katika timu mbalimbali ndani na nje ya nchi. Kufuatia hatua hiyo ya uendelezaji wa vipaji, imewezesha timu ya taifa ya mpira wa miguu Taifa Stars kushiriki mashindano ya Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON) kwa mara ya tatu katika historia ya Taifa letu na Timu ya Taifa ya wanawake ya mpira wa miguu Twiga Stars kufuzu kucheza mashindano ya WAFCON ambayo yatafanyika mwaka 2024 nchini Morocco.

**54. Mheshimiwa Spika**, kufuatia jitihada za makusudi za MAMA katika kuimarisha sekta ya michezo nchini, Tanzania itakuwa mwenyeji wa michuano ya kombe la AFCON ya mwaka 2027 kwa kushirikiana na nchi za Uganda na Kenya. Nipende kuwahakikishia kuwa, Serikali imejipanga vyema juu ya maandalizi ya michuano

hiyo ikiwemo ujenzi wa uwanja wa mpira wa Samia jijini Arusha kama alivyowasilisha Mheshimiwa Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo. Nitoe rai kwa Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania kuanza maandalizi ya timu yetu ya Taifa mapema ili hatimaye tulibakize kombe hilo hapa nyumbani.

**55.** **Mheshimiwa Spika**, maandalizi ya timu yanahitaji uwepo wa viwanja bora. Serikali imejiandaa kujenga viwanja vipya na kukarabati baadhi ya viwanja vilivyopo. Kuhusu ubora wa eneo la kuchezea, yaani *pitch* kwenye viwanja mbalimbali, tayari Serikali ilitunga sheria inayotoa msamaha kwenye uingizaji wa nyasi bandia na vifaa vyake. **Mheshimiwa Spika**, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa, msimu ujao wa Ligi Kuu ya Tanzania tutaanza kutumia **"VAR"** ili kuhakikisha matokeo yanayopatikana uwanjani yanakuwa ya haki maana kuna timu zimezidi - msimu mmoja penati 10, halafu zikifungwa zenyewe magoli yanakataliwa. Na ili tuwe na "**VAR"** za kutosha katika viwanja vyote, naleta pendekezo la kutoa msamaha kwenye uingizaji wa mashine za **"VAR"** na vifaa vyake kwa ufafanuzi utakaotolewa hapo baadae. **INAWEZEKANA!**

**Maslahi ya Watumishi na Wastaafu**

**56.** **Mheshimiwa Spika**, Serikali imeendelea kuhakikisha kuwa malimbikizo ya kimshahara na yasiyo ya kimshahara ya watumishi wa umma yanalipwa kwa wakati. Katika kipindi cha miaka mitatu ya Serikali ya Awamu ya Sita, jumla ya shilingi bilioni 98.63 zimelipwa kama malimbikizo mbalimbali ya watumishi wa umma. Aidha, katika kipindi hicho, Serikali imelipa jumla ya shilingi bilioni 160.04 kwa ajili ya kugharamia upandishwaji wa vyeo kwa watumishi wa umma wapatao 126,814 katika kada mbalimbali. Hata hivyo, kumekuwa na kilio kikubwa kutoka kwa wastaafu kuhusu kikokotoo. Kama asemavyo Naibu Waziri wa Fedha Mheshimiwa Chande kuwa mara zote mtoto akilia mama hujua kwa sauti kuwa hapo mtoto analilia nini. Akilia anasema hapo ameshiba, akilia anasema hapo ana usingizi, akilia anasema hapo nguo zimembana au akilia anasema apelekwe hospitali.

**57. Mheshimiwa Spika, mabadiliko ya kikokotoo yalishusha kundi la wafanyakazi waliokuwa wakipokea mkupuo wa asilimia 50 mpaka asilimia 33, na kundi waliokuwa wakipokea asilimia 25 walipandishwa mpaka asilimia 33.**

**58. Mheshimiwa Spika**, Serikali yetu sikivu inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, imesikia kilio hicho na imekifanyia kazi kwa maslahi mapana ya wastaafu wetu na wanaotarajiwa kustaafu. Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ameelekeza kuongezwa malipo ya mkupuo kutoka asilimia 33 iliopo sasa hadi asilimia 40. Hili ndio kundi kubwa la watumishi wanaofanya kazi nzuri sana kwa taifa letu wakiwepo, Walimu, kada ya afya, Polisi, Magereza, Uhamiaji, Zimamoto na makundi mengine yalioko Serikali kuu na Serikali za Mitaa. Vilevile, Mheshimiwa Rais ameelekeza kuongezewa zaidi kundi lililokuwa likipokea asilimia 25 hapo awali na kupandishwa kwenda asilimia 33 sasa itakuwa asilimia 35 kuanzia mwaka wa fedha huu. Watumishi takriban 17 walioathirika na mabadiliko haya watazingatiwa katika mabadiliko haya. Serikali itaendelea kuangalia maslahi ya wastaafu kwa kuzingatia tathmini ya uhai na uendelevu wa mifuko.

**59. Mheshimiwa Spika**, mafanikio hayo yote yamepatikana chini ya uongozi mahiri na thabiti wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi, kupitia mchango wa watanzania wakiwemo wakulima, wafanyakazi, wafanyabiashara na wazalishaji. Hii inadhihirisha kuwa MAMA anawapenda sana watanzania, hivyo basi na sisi watanzania **Tusimame na MAMA** kwa kumpatia wasaidizi makini kutoka Chama Cha Mapinduzi watakaoendeleza gurudumu la maendeleo kupitia uchaguzi wa Serikali za mitaa unaotarajiwa kufanyika Novemba 2024.

**Kuimarisha Upatikanaji wa Fedha za Kigeni**

**60. Mheshimiwa Spika**, kama ilivyokuwa kwa nchi nyingi duniani, nchi yetu pia ilikabiliwa na changamoto ya upungufu wa fedha za kigeni mwaka 2023/24. Changamoto hii ilisababishwa na mambo

mbalimbali ikiwemo: athari za UVIKO–19; vita vinavyoendelea nchini Ukraine na katika ukanda wa Gaza; mabadiliko ya tabianchi; na kubadilika kwa sera za fedha katika nchi zilizoendelea. Changamoto hizo zilisababisha kupanda kwa riba za fedha kwenye nchi zilizoendelea na masoko ya kimataifa ili kukabiliana na mfumuko wa bei kwenye nchi hizo. Hali hiyo ilipunguza ukwasi na mzunguko wa fedha za kigeni katika uchumi wa dunia kwa ujumla.

**61. Mheshimiwa Spika**, pamoja na changamoto hii kuwa kubwa katika nchi nyingi duniani, Serikali ilifanikiwa kukabiliana nayo kwa kushirikiana na sekta binafsi na washirika wa maendeleo ili kuendelea kuwa na akiba ya kutosha ya fedha za kigeni. Hadi Machi 2024, akiba ya fedha za kigeni ilikuwa dola za Marekani bilioni 5.3, kiasi ambacho kinakidhi uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa miezi 4.4, ambacho kiko juu ya lengo la nchi la muda usiopungua miezi 4.0. Aidha, Serikali iliendelea kutekeleza mkakati wa kupunguza nakisi ya urari wa biashara uliopelekea kupungua kwa nakisi hiyo kutoka dola za Marekani bilioni 5.3 mwaka 2022 hadi dola za Marekani bilioni 2.7 kwa mwaka ulioishia Februari 2024 kwa kuongeza mauzo nje na kupunguza uagizaji wa bidhaa zinazozalishwa nchini.

**62. Mheshimiwa Spika**, pamoja na sababu nilizozitaja hapo awali, sisi watanzania pia tunalikuza tatizo la upungufu wa dola kwa baadhi ya watu kudai malipo au kufanya malipo ya bidhaa na huduma zinazotolewa ndani ya nchi kwa kutumia fedha za kigeni yaani, *dollarization*. Taasisi ipo Tanzania na pengine hata taasisi ya Serikali, inamuuzia huduma mtanzania inamwambia alipe kwa dola, taasisi zingine zinataka mtanzania alipe ada kwa dola, alipe kodi ya nyumba kwa dola, vibali vya kazi, leseni na kadhalika kwa dola. Tunawafanya watanzania wahangaike kuitafuta fedha ya kigeni kununua huduma zinazotolewa ndani ya nchi yao badala ya kuwafanya wageni wahangaike kuitafuta shilingi ya Tanzania wanapotaka huduma ndani ya nchi. Jambo hili linasababisha kuongezeka kwa mahitaji yasiyo ya lazima ya fedha za kigeni na kuwanyima fursa watu wanaohitaji fedha za kigeni kwa ajili ya kulipia bidhaa na huduma muhimu kutoka nje ya nchi. Kitendo cha

kuuza bidhaa au huduma za ndani kwa kutumia fedha za kigeni ni kosa kwa mujibu wa kifungu cha 26 cha Sheria ya Benki Kuu ya mwaka 2006, ambacho kinabainisha kwamba Shilingi ya Tanzania ndiyo fedha halali pekee kwa malipo ya ndani ya nchi.

**63. Mheshimiwa Spika**, kuanzia tarehe 1 Julai, 2024, naelekeza wadau wote wa ndani, taasisi za umma, wafanyabiashara, asasi za kiraia, mashirika ya kimataifa na watu wote waliopo nchini Tanzania wenye tabia ya kuweka bei kwenye huduma au kuuza bidhaa kwa fedha za kigeni kuacha mara moja na kuhakikisha bei za bidhaa na huduma hizo zinatangazwa na kulipwa kwa Shilingi ya Tanzania. Aidha, nazielekeza taasisi zote za Serikali zinazotoza ushuru, ada na tozo mbalimbali kwa fedha za kigeni kurekebisha kanuni zao ili tozo hizo zilipwe kwa shilingi. Hata mgeni akija na fedha za kigeni ni vyema akaibadilisha kuwa fedha ya kitanzania ili aweze kupata huduma. Tunafanya kila malipo kwa fedha za kigeni, halafu shilingi ikishuka thamani tunajiuliza tumekosea wapi.

**64. Mheshimiwa Spika,** nawahimiza watanzania wenzangu na wadau wote waliopo nchini kuacha kununua/kulipia vitu vilivyomo nchini kwa fedha za kigeni, hususan vifaa vya kielektroniki, ada za shule/chuo, kodi za nyumba, viwanja, na bidhaa au huduma mbalimbali kwa kuwa ni haki yetu kisheria kulipa bidhaa na huduma kwa sarafu yetu, na ukikubali kulipa kwa fedha za kigeni ni kosa la uhujumu uchumi. Endapo una fedha za kigeni, unatakiwa kuzibadilisha kupitia benki au maduka halali ya kubadilishia fedha ndipo ufanye malipo kwa kutumia shilingi ya Tanzania. Naielekeza Benki Kuu pamoja na vyombo vingine vinavyohusika kuendelea kudhibiti suala hili, kufuatilia kwa ukaribu ili kubaini wote wanaoendelea kufanya makosa hayo, na kuchukua hatua stahiki kwa mujibu wa sheria.

**65. Mheshimiwa Spika**, pamoja na sababu za upungufu wa fedha za kigeni nilizozitaja, takribani asilimia 80 ya bidhaa zinazozalishwa nchini kwa ajili ya soko la nje ni bidhaa ghafi. Hali hii inadhihirisha kuwa nchi yetu bado haitumii ipasavyo fursa ya kuongeza thamani ya bidhaa zinazozalishwa nchini kabla ya kuuzwa nje ili kuongeza

fedha za kigeni. Kwa upande mwingine, uzalishaji wa bidhaa na huduma nchini haukidhi mahitaji ya ndani na hivyo kulazimika kutumia kiasi kikubwa cha fedha za kigeni kuagiza bidhaa kutoka nje.

**66. Mheshimiwa Spika**, katika kuimarisha upatikanaji wa fedha za kigeni, Serikali imeandaa Mkakati wa Taifa wa Kuimarisha Upatikanaji wa Fedha za Kigeni wenye malengo ya: kuimarisha uzalishaji na kuongeza thamani ya bidhaa na huduma ili kuongeza mapato ya fedha za kigeni; kuzalisha bidhaa na huduma mbadala zinazoagizwa kutoka nje ili kupunguza matumizi ya fedha za kigeni; na kuimarisha mazingira ya uwekezaji ili kuvutia wawekezaji kutoka nje ya nchi na sekta binafsi. Nitoe rai kwa sekta husika kutekeleza Mkakati huo ili kufikia matokeo yanayotarajiwa. Aidha, nisisitize taasisi zote za Serikali kuzingatia matakwa ya kifungu cha 60 cha Sheria ya Ununuzi wa Umma Namba 10 ya Mwaka 2023 kinachoelekeza kutoa kipaumbele kwa bidhaa au huduma zinazotengenezwa au kuzalishwa ndani ya nchi katika mikataba inayotolewa kwa misingi ya ushindani wa zabuni za kitaifa au kimataifa ili kupunguza matumizi ya fedha za kigeni na kukuza viwanda vya ndani.

**67. Mheshimiwa Spika**, pamoja na hatua nilizoziainisha hapo juu, napenda pia kuwakumbusha wananchi kuwa suluhisho la kudumu katika kuimarisha thamani ya sarafu yetu ni kuongeza uzalishaji na ubora wa bidhaa na huduma tunazouza nje ya nchi na kukubali kutumia zaidi bidhaa na huduma zinazozalishwa hapa nchini. Ikumbukwe kuwa, thamani ya sarafu ni kielelezo cha uwezo wa uchumi kukidhi mahitaji yake ya msingi, ikiwemo kulipia mahitaji ambayo hayana budi kuagizwa kutoka katika nchi nyingine. Hivyo, kwa kutekeleza hayo, tutakuwa tumechangia kuimarisha sarafu yetu. Kila mmoja wetu ana mchango wa kutoa katika suala hili.

**Uendelezaji wa Sekta ya Fedha**

**68. Mheshimiwa Spika**, sekta ya fedha imeendelea kukua na watumiaji wa huduma rasmi za kifedha wameendelea kuongezeka.

Utafiti wa *Finscope* wa mwaka 2023 unaonesha kuwa asilimia 76 ya watanzania wanatumia huduma rasmi za kifedha ikilinganishwa na asilimia 65 ya mwaka 2017. Pamoja na mafanikio haya, kumekuwa na changamoto mbalimbali katika sekta ya fedha, ikiwemo utoaji wa mikopo yenye riba kubwa inayowaumiza wananchi na kuwarudisha nyuma kimaendeleo (maarufu kama mikopo-umiza, mikopo kausha-damu, mikopo kuzimia, mikopo chuma ulete na kadhalika). Wako baadhi ya watanzania wenzetu wasio na huruma na ambao wanawapa wenzao mikopo yenye masharti ya dhuluma ikiwemo riba kubwa sana na kuuza mali za wakopaji bila kufuata taratibu za kisheria. Aidha, wako baadhi ya watu wanaotoa mikopo hii kwa njia ya vitu badala ya fedha, ila kwa masharti yanayoumiza pia.

**69. Mheshimiwa Spika,** wako watu wanaowakopesha wakulima kopo la mbegu la kilogramu 2 halafu wanamtaka mkulima atakapovuna alipe gunia la mazao lenye takribani kilogramu 100, hii ni sawa na riba ya asilimia 5,000. Hii ni dhuluma na ni wizi kama wizi mwingine. Aidha, wapo watu wanaokopeshana fedha kwa makubaliano ya riba ya shilingi 800,000 kwa mwezi ambapo ukikopa shilingi milioni 4 utatakiwa urudishe shilingi milioni 28 baada ya miezi 30, hii ni sawa na riba ya asilimia 240 kwa mwaka. Hii nayo ni dhuluma na ni wizi kama wizi mwingine. Viwango hivi ni vikubwa sana na vinawarudisha nyuma wananchi ambao wakati mwingine wanafanya makubaliano bila kuwa na elimu ya fedha. Hii si huruma, ni dhuluma, ni kuiba kwa kutumia matatizo aliyonayo mtanzania mwenzako.

**70. Mheshimiwa Spika**, natoa onyo kwa watu binafsi na kampuni zinazojihusisha na utoaji wa mikopo ya namna hii kuacha mara moja kwani jambo hili linarudisha nyuma wananchi wetu kiuchumi na kuwaingiza katika lindi la umaskini. Aidha, nawakumbusha wananchi wote kuwa na nidhamu ya fedha ikiwemo: kukopa kwa ajili ya mahitaji yenye tija na ikiwezekana kuchukua mikopo kwa ajili ya shughuli za uzalishaji mali badala ya matumizi ya kawaida; kuwa makini katika masharti ya mikataba ya mikopo mnayoingia; na kuhakikisha mikopo mnayopewa inarejeshwa kwa wakati ili msiingie

katika mitego ya wakopeshaji wenye nia mbaya ya kuuza dhamana zao. Vilevile, naielekeza Benki Kuu na taasisi zote zinazohusika katika usimamizi wa sekta ya fedha ikiwemo: kamati zote za ulinzi na usalama kuendelea kufuatilia suala hili kwa ukaribu; kuchukua hatua kali dhidi ya wote wanaotoa huduma za fedha bila kuwa na leseni; na kuwanyang'anya leseni wote watakaobainika kuwa wanatoa mikopo bila kuzingatia masharti ya leseni na kuwaumiza wananchi.

**71. Mheshimiwa Spika**, katika kutatua changamoto hiyo, Serikali imeendelea kutekeleza programu ya Elimu ya Fedha kwa Umma ya mwaka 2021/22 - 2025/26 pamoja na kuhamasisha usajili na kutoa elimu ya uendeshaji wa vikundi vya kijamii vya huduma ndogo za fedha. Hadi Februari 2024, Serikali imesajili jumla ya vikundi vya kijamii 49,168 vya huduma ndogo za fedha na wahamasishaji 500. Aidha, Serikali imeteuwa maafisa dawati 212 katika ngazi ya wizara, mkoa, na halmashauri na kuwapatia mafunzo ya uratibu na usimamizi wa biashara ya huduma ndogo za fedha katika maeneo yao. Vilevile, Serikali imetoa leseni kwa watoa huduma za fedha daraja la pili wapatao 1,726 na Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo 759. **Mheshimiwa Spika**, sekta ya fedha inasimamiwa na sheria mbalimbali ikiwemo Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya Mwaka 2006 na Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha ya Mwaka 2018. Kwa msingi huo, ili kampuni au taasisi iweze kutoa mikopo kwa wananchi inapaswa kukidhi matakwa ya sheria tajwa. Hivyo, nasisitiza watanzania kutumia watoa huduma za fedha waliosajiliwa

**72. Mheshimiwa Spika**, Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali ili kuwezesha upatikanaji wa mikopo yenye riba rafiki. Hatua hizo ni pamoja na: kufanya mashauriano na benki ili kupunguza gharama za uendeshaji; Benki Kuu kuimarisha mazingira ya ushindani katika sekta ya fedha; na kuimarisha kanzidata ya taarifa za wakopaji na mwenendo wao katika urejeshaji wa mikopo. Aidha, Serikali itaendelea kutoa elimu ya fedha kwa wananchi ikiwemo umuhimu wa kupanga bajeti pamoja na usimamizi wa fedha binafsi na mikopo ili kuwaepusha kukopa bila kuwa na mipango madhubuti.

**Matumizi ya Mifumo ya Malipo ya Kidijitali**

**73. Mheshimiwa Spika**, Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, ina lengo mahsusi la kuupandisha hadhi uchumi wa nchi yetu ili kuwa uchumi wa kidijitali. Mojawapo ya hatua kubwa tunazochukua ni kuhakikisha tunakuwa na mifumo madhubuti ya kidijitali, itakayowawezesha wananchi kufanya malipo kwa urahisi popote walipo na kwa gharama nafuu. Katika kutekeleza azma hiyo, Serikali kupitia Benki Kuu ya Tanzania iliunda na kuzindua Mfumo wa Malipo ya Papo kwa Papo (Tanzania Instant Payment System - TIPS) katika mwaka 2023/24. Lengo la kuundwa kwa TIPS ni kuwezesha miamala kutoka benki na mitandao ya simu kufanyika kwa urahisi zaidi (interoperability), kuongeza ufanisi katika kufanya miamala na kupunguza gharama za miamala. **Mheshimiwa Spika**, napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa, benki zote za biashara na kampuni zote zinazotoa huduma za fedha kwa njia ya simu zimejiunga kwenye mfumo wa TIPS. Hadi sasa, TIPS inawezesha kufanyika kwa miamala yote ikiwemo kati ya *mtu na mtu*, *mtu na biashara*, na *biashara na biashar*a. Serikali imeanza hatua nyingine ya utekelezaji wa TIPS itakayowezesha kufanya malipo ya bidhaa na huduma kwa njia ya msimbo wa haraka (QR code).

**74. Mheshimiwa Spika,** watumiaji wa mitandao ya kielektroniki kutuma na kupokea fedha walifikia milioni 51.7 mwaka 2023 kutoka watumiaji milioni 38.3 mwaka 2022. Kwa kutumia mfumo wa TIPS, miamala milioni 364.4 baina ya mtu na mtu ilifanyika mwaka 2023 ikiwa na thamani ya shilingi bilioni 11,323.78 ikilinganishwa na miamala milioni 235.5 yenye thamani ya shilingi bilioni 7,369.3 mwaka 2022. Aidha, miamala iliyofanywa na watumiaji wa mitandao ya kielektroniki kununua bidhaa na huduma (mtu na biashara) ilifikia milioni 1,350.8 yenye thamani ya shilingi bilioni 18,250.3 mwaka 2023 kutoka miamala milioni 788.1 yenye thamani ya shilingi bilioni 10,819.7 mwaka 2022. Miamala iliyofanywa na wananchi kupata huduma zinazotolewa na Serikali (mtu na Serikali) ilifikia milioni 10.54 yenye thamani ya shilingi bilioni 426.28 mwaka 2023 ikilinganishwa na

miamala milioni 9.5 yenye thamani ya shilingi bilioni 357.2 mwaka 2022.

**75. Mheshimiwa Spika**, kulikuwa pia na ongezeko la mashine za kituo cha mauzo (Point of Sales - POS) kufikia 8,652 zilizofanya miamala milioni 9.9 yenye thamani ya shilingi bilioni 1,922.2 mwaka 2023 ikilinganishwa na mashine 7,317 zilizofanya miamala milioni 6.7 iliyokuwa na thamani ya shilingi bilioni 1,343.9 mwaka 2022. Matumizi ya mifumo ya kielektroniki yameendelea kuboreshwa ambapo sasa unaweza kutumia simu yako kulipia huduma popote ulipo kwa kutumia mfumo wa "lipanamba" (merchant payment). Mfumo huu wa lipanamba sasa unapatikana nchi nzima na idadi ya watoa huduma hii wamefikia 657,346 na miamala iliyofanyika kupitia lipa namba ilikuwa milioni 301.2 yenye thamani ya shilingi bilioni 17,918.12 mwaka 2023 ikilinganishwa na watoa huduma 393,977 na miamala milioni 166.4 mwaka 2022 ikiwa na thamani ya shilingi bilioni 12,103.43. Takwimu hizo zinatuonesha kwamba kuna mwamko mkubwa wa wananchi kufanya miamala kwa kutumia mifumo ya kielektroniki kwani inarahisisha upatikanaji wa huduma.

**76. Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na changamoto ya watu kushindwa kufanya miamala kwa kisingizio kuwa mtandao uko chini. Hata hivyo, matumizi ya mifumo ya kielektroniki katika kufanya miamala yameendelea kuboreshwa ambapo sasa unaweza kutumia simu yako kulipia huduma popote ulipo kwa kutumia mfumo wa "lipanamba" (merchant payment) ambao hauhitaji kuwa na mtandao wa intaneti. Hivyo, napenda nitoe rai kwa watanzania wote kujiunga na mfumo huo wa lipa namba ili kurahisisha ufanyaji wa miamala kiganjani mwako.**

**77. Mheshimiwa Spika**, katika kurahisisha ufanyaji wa malipo ya kidijitali kwa wananchi, Serikali ilifanya marekebisho kwenye tozo za uwekaji wa miundombinu kwenye hifadhi ya barabara (Right of Way) kwa kupunguza ada ya awali (Initial Fee) ya usimikaji wa nyaya za mawasiliano kutoka dola za Marekani 1,000 kwa kilometa hadi dola za Marekani 200 kwa kilometa na ada ya mwaka (annual fee) kutoka dola za Marekani 1,000 kwa kilometa hadi dola za

Marekani 100 kwa kilometa. Lengo la hatua hii ni kufanikisha usambazaji wa miundombinu ya mawasiliano kutoka mkoani kwenda wilayani na kutoka wilayani kwenda kwa wateja ili kuwezesha upatikanaji wa huduma za mawasiliano zilizo bora. Hivyo, natoa rai kwa wananchi kuongeza matumizi ya mifumo ya kidijitali katika kufanya malipo na kupunguza matumizi ya fedha taslimu. Serikali itaendelea kuboresha na kuimarisha mifumo ya malipo ya kidijitali, na kuweka mazingira rafiki ya kufanya malipo, biashara na uwekezaji inayotumia teknolojia za kidijitali kwa ajili ya maendeleo ya watu wetu.

**Masuala ya Muungano**

**78. Mheshimiwa Spika**, ili kuendeleza ustawi wa watanzania na kukuza uchumi wa nchi yetu, umoja wa kitaifa, amani, mshikamano na undugu ni jambo muhimu sana. Serikali inatambua kuwa muungano wetu ndio utaifa wetu. Bila Tanzania Bara hakuna Taifa linaitwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na vivyo hivyo, bila Zanzibar hakuna Taifa linaitwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ndio utambulisho wetu duniani. **Mheshimiwa Spika**, zaidi ya hayo yote, sasa muungano umepiga hatua zaidi kutoka kwenye karatasi na mchanga vilivyofanyika wakati ule wa ishara ya muungano na kwenda kwenye muungano wa damu, sasa watanzania wameoleana kabila kwa kabila, hakuna kabila moja sasa ambalo hawajaoleana na kabila lingine na wala hakuna upande mmoja wa muungano ambao upande huo watu wake haujaoleana na upande mwingine wa muungano.

**79. Mheshimiwa Spika**, sasa kumezuka baadhi ya wanasiasa, kwa sababu za kufilisika kisiasa na kutotambua unyeti wa suala hili wamekuwa wakitoa lugha zinazopandikiza chuki dhidi ya watanzania. Sote tumeshuhudia lugha za kibaguzi zikitolewa na baadhi ya viongozi wakuu wa vyama vya siasa ambazo zinahatarisha muungano wetu. Kauli hizi zikiachwa bila kukemewa na kila mmoja wetu zina uelekeo wa kuvunja muungano wetu na zinatishia kuvunja utaifa wetu na undugu wetu.

**80. Mheshimiwa Spika**, tukumbuke, Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alituasa kuwa, dhambi ya ubaguzi ni kama dhambi ya kula nyama ya mtu, ukila mara moja hauachi. Tutamaliza kubaguana kwa misingi ya muungano na baada ya hapo tutahamia kubaguana kikabila, tutachomeana vibanda, tutanyang'anyana viwanja, tutafukuziana mifugo, tutavunja utaifa wetu. Tuzikatae wote agenda za viongozi wabaguzi hawa waliofilisika kisera, hawana agenda inayoweza kuwapa uhalali kwa watanzania mpaka watoe lugha za kibaguzi. Lugha hizo ni za hovyo kabisa na za aibu kutolewa na viongozi wa vyama vya siasa. Ikumbukwe kuwa, vyama hivyo vya siasa vimesajiliwa kwa sharti la lazima kuwa viwe vimeungwa mkono na pande mbili za muungano.

**81. Mheshimiwa Spika**, inawezekana wenzetu hawa kwa tamaa za madaraka hawajatilia maanani suala hili. Viongozi hao wanafikiri kuwa lugha hizo za kuhatarisha muungano zina mashiko kwa wapiga kura wao na kana kwamba hawajawahi kunufaika na uwepo wa muungano. Kuligawa Taifa kwa ajili ya kufanikisha agenda ya kisiasa ni jambo la hatari sana. Ndugu watanzania, viongozi wa vyama vya siasa vya upinzani wanaotaka kuligawa Taifa letu kwa maslahi mepesi hawastahili kuaminiwa kupewa uongozi wa nchi, ukiwajaribishia hawa watauvunja muungano wetu, wataiua nchi yetu. **Hawafai kabisa!!**

**82. Mheshimiwa Spika**, narejea tena, kwa hawa wanasiasa wanaotafuta uhalali wa kisiasa kwa misingi ya ukabila au utanganyika au uzanzibar, ni wanasiasa waliofilisika kisera, hawafai, na jambo hili ni la hatari sana kwa Taifa letu. Jambo hili halikubaliki hata kidogo na wala halina afya kwa demokrasia yetu. Vyombo na mamlaka zote zinazohusika zitoe onyo kali kwenye kauli hizi na zichukue hatua kali haya mambo yakijirudia. Tutaulinda muungano kwa gharama yeyote, tutailinda nchi yetu kwa gharama yeyote wala Serikali hatutatoa nafasi kwa yeyote mwenye chokochoko kama hii kufanikisha agenda ovu kama hizo. **Mheshimiwa Spika**, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa, Serikali zote mbili zina nia ya dhati na thabiti katika kuhakikisha kuwa, hoja za muungano zilizopo na zitakazojitokeza zinashughulikiwa kwa wakati

na kuufanya muungano kuwa na maslahi kwa kila mmoja ili kuulinda na kuudumisha muungano wetu adhimu.

**Usalama Barabarani**

**83. Mheshimiwa Spika**, takwimu zetu za ajali zitokanazo na vyombo vya moto zinaashiria hatari kubwa sana ambayo kila mtu anapaswa kuongeza umakini. Watanzania wengi bado hatuheshimu sheria za barabarani, hatuna nidhamu na matumizi ya vyombo vya moto na alama za barabarani. Madhara yake tunapoteza nguvu kazi ya nchi yetu kutokana na ajali za barabarani ambazo zinatuondolea watu wanaotegemewa katika jamii zetu, wakati mwingine kwa uzembe unaoweza kuepukika. Katika kipindi cha miaka mitano yaani kutokea mwaka 2019 hadi Mei 2024, ajali za barabarani zilikuwa 10,093 ambapo vifo vilikuwa 7,639 na majeruhi 12,663 miongoni mwao wakipata ulemavu wa kudumu. Hebu fikiria, magari binafsi - ajali 3,250, vifo 2,090, majeruhi 3,177. Hebu fikiria, mabasi - ajali 790, vifo 782, majeruhi 2,508. Hebu fikiria, daladala - ajali 820, vifo 777, majeruhi 1,810. Hebu fikiria, taxi - ajali 93, vifo 97, majeruhi 173. Hebu fikiria, magari ya kukodi (sherehe, misiba, na shughuli maalum) - ajali 326, vifo 263, majeruhi 302. Idadi hii kubwa ya majeruhi na vifo vya watu kutokana na ajali utadhani nchi iko kwenye vita vya wenyewe kwa wenyewe. **Jambo Hili Halikubaliki!**

**84. Mheshimiwa Spika**, ilivyo sasa wengi huona usumbufu na wakati mwingine mpaka tunaweka chuki na uadui tunapokumbushwa kuhusu usalama wetu na Jeshi la Polisi tuwapo barabarani. Tunavunja sana sheria barabarani, hata magari ya Serikali hivyo hivyo, wakati mwingine tunawagonga waenda kwa miguu. Ni wakati sasa jambo hili kuazimiwa na jamii nzima ya watanzania kwa kuweka mtazamo wa kuchukia ajali. Hatuwezi kuendelea kushuhudia nguvu kazi yetu ikipukutika kirahisi tu kama nyumbu anavyouawa mbugani. Askari barabarani msiwe na huruma hata kidogo kwa wazembe wote wanaokiuka sheria hata kama gari ina usajili wa namba za Serikali. **Mheshimiwa Spika**, kama sheria zetu ni rafiki sana, tuyaondoe makosa yote ya ajali barabarani

kwenye inayoitwa *traffic case*, tupeleke kwenye makosa makubwa zaidi ikiwezekana huu uwe ni uuaji kama uuaji mwingine kwa maana mtu anayekufyatulia risasi kwa kukusudia ana uhakika kuwa atakujeruhi au kukuua na hata anayefanya uzembe na vyombo vya moto ana uhakika wa kukujeruhi au kuua kwa makusudi kabisa.

**Sheria ya Ununuzi wa Umma**

**85. Mheshimiwa Spika**, utakumbuka Bunge lako tukufu lilitunga upya Sheria ya Ununuzi ya Umma Na.10 ya Mwaka 2023. Baadhi ya mambo yaliyozingatiwa katika sheria hii mpya na kanuni zake ni pamoja na maboresho katika masharti yahusuyo upendeleo wa kitaifa (National Preference), upendeleo wa kipekee kwa watu au kampuni za ndani (Exclusive Preference) pamoja na maeneo mengine ya upendeleo wa ndani.

**86. Mheshimiwa Spika**, moja ya maboresho hayo, ni ukomo wa upendeleo (Margin of Preference) kwa bidhaa zilizochimbwa au kuzalishwa ndani ya Tanzania kuendelea kuwa **asilimia 15** pamoja na kuwekwa masharti mapya yatakayohakikisha uzingatiwaji wa sharti hili. Aidha, kiwango cha upendeleo wa kipekee (Exclusive Preference) kwa wauzaji wa bidhaa, wakandarasi au watoa huduma wa ndani kimepandishwa kwa kiasi kikubwa hadi kufikia shilingi bilioni 50. Hivyo, zabuni zote zinazohusu bidhaa, kandarasi na huduma ambazo thamani yake haizidi shilingi bilioni 50 zimetengwa kwa wazawa pekee.

**87. Mheshimiwa Spika**, Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2024 zimeweka masharti mahsusi kuwa upendeleo wa kipekee utatumika kwa wauzaji wa bidhaa, wakandarasi au watoa huduma wa ndani na ushirika wa ndani na wa kigeni ikiwa mchango wa wauzaji wa bidhaa, wakandarasi, au watoa huduma wa ndani katika ushirika ni zaidi ya **asilimia 75**. Aidha, Sheria imeweka masharti mahsusi yatakayopaswa kuzingatiwa na wazabuni ili kunufaika na upendeleo huu na hivyo kuziba mianya ya matumizi mabaya ya masharti haya.

**88. Mheshimiwa Spika**, kwa zabuni ambazo Kampuni za kigeni zitaruhusiwa kushiriki, Kanuni mpya za ununuzi wa umma pia zimetoa upendeleo maalum kwa kampuni za kigeni ambazo zinatoa mikataba midogo (Sub-contracts) kwa kampuni ndogo za ndani. Katika zabuni hizo, Kanuni mpya za Ununuzi wa Umma zimeweka sharti kwa Taasisi nunuzi kulipa moja kwa moja kwa kampuni ya ndani malipo ya mkataba mdogo ulioingiwa baina ya kampuni ya ndani na kampuni ya kigeni kwa kuzingatia masharti ya Mkataba husika.

**89. Mheshimiwa Spika**, katika eneo hili, Sheria mpya ya ununuzi wa umma imeruhusu watu au kampuni binafsi za ndani kuingia katika ushirika na kampuni za nje endapo hazina uwezo wa kutekeleza mikataba ya ununuzi wa umma hususan miradi mikubwa ya ujenzi. Endapo ushirika utakaoanzishwa utahusisha kampuni ya kigeni, Sheria imeelekeza kuwa kampuni ya ndani itakuwa ndiyo kampuni kiongozi katika utekelezaji wa mradi husika. Hatua hii inatarajiwa kuleta mageuzi makubwa ikiwemo kujenga uwezo kwa kampuni za ndani ili kuwa sawa na nchi nyingine ambazo miradi mikubwa ya ujenzi katika nchi hizo hufanywa na kampuni za wazawa ambazo zina uwezo mkubwa wa kutekeleza miradi hiyo. Nitoe rai kwa ndugu zangu wakandarasi na watoa huduma pamoja na wauzaji wa bidhaa kutumia fursa hii adhimu na kuitekeleza kwa uaminifu. Sasa sheria imeruhusu wazawa kupata kazi kubwa na kutoa *sub contracts* kwa wageni, msione woga kuwapa kazi kubwa wazawa ili wao ndio waajiri wageni kwani **hata mbuyu ulianza kama mchicha**!. Itakuwa ni jambo la kusikitisha sana endapo tutamuangusha Mheshimiwa Rais aliyetupa fursa hii, kwa kutekeleza miradi chini ya kiwango na isioendana na thamani ya fedha.

**90. Mheshimiwa Spika**, ili kuongeza uwajibikaji na ufanisi katika ununuzi wa umma, sheria na kanuni za ununuzi wa umma zimeweka viwango vya uidhinishaji kwa Bodi za Zabuni. Ununuzi wowote ambao thamani yake inaangukia chini ya ukomo huo utashughulikiwa na Afisa Masuuli. Viwango hivyo vinategemea ukubwa wa kiwango cha ununuzi wa mwaka kwa taasisi husika

(Annual Procurement Volume) na pia umezingatia mahitaji mahsusi ya Taasisi zinazojiendesha kibiashara.

**91. Mheshimiwa Spika**, eneo lingine muhimu lililozingatiwa katika Sheria na Kanuni za ununuzi wa umma ni uwepo wa sehemu mahsusi ya usimamizi wa mikataba ya ununuzi inayohusu: uhakiki wa ubora wa bidhaa na huduma; udhibiti wa ongezeko la gharama na muda; mabadiliko na usitishwaji wa mikataba; mgawanyo wa majukumu; na utaratibu wa malipo. Aidha, PPRA imepewa jukumu la kuandaa bei kikomo kwa bidhaa, huduma na kandarasi zenye viwango na vigezo vya kiufundi kwa kuzingatia taarifa za bei kutoka kwa taasisi husika zenye mamlaka ya kuandaa bei hizo. Aidha, Mtendaji yeyote wa Serikali atakayefanya ununuzi juu ya bei kikomo, atachukuliwa hatua za kinidhamu pamoja na kutakiwa kulipa tofauti kati ya gharama halisi ya ununuzi na gharama ambayo ingepatikana kupitia bei kikomo.

**92. Mheshimiwa Spika**, kuhusu upendeleo kwa makundi maalum, kila Taasisi nunuzi itatoa upendeleo wa kipekee wa **asilimia 30** katika ununuzi wake wa mwaka kwa ajili ya makundi maalumu yaliyopo katika eneo lake. Kwa kuzingatia utekelezaji hafifu katika eneo hili, Kanuni za Ununuzi wa Umma zimetamka bayana kuwa **Afisa masuuli ambaye atakiuka kanuni hii atawajibika kwa hatua za kinidhamu kwa mamlaka husika.** Aidha, PPRA itatoa miongozo kwa ajili ya utekelezaji wa masharti ya Sheria na kanuni ikiwemo upendeleo kwa makundi maalum.

**93. Mheshimiwa Spika**, maeneo mengine muhimu yaliyozingatiwa katika sheria na kanuni mpya za ununuzi wa umma ni pamoja na: sharti la lazima la matumizi ya mfumo wa kielektroniki wa ununuzi wa umma, ambapo yeyote atakayekiuka atakuwa ametenda kosa la jinai na atawajibika binafsi baada ya kutiwa hatiani; na kupunguzwa kwa muda wa utekelezaji wa shughuli za ununuzi ili kuongeza ufanisi. Kuhusu masharti ya utekelezaji wa miradi ya ujenzi kwa utaratibu wa *force account*, kanuni mpya za ununuzi wa umma zimeweka ukomo wa thamani ya shilingi milioni 100 ambapo ununuzi wowote unaozidi thamani hiyo hautatumia njia hiyo ya *force account.* Aidha, Sheria

na Kanuni za ununuzi wa umma zimeweka masharti madhubuti yanayopaswa kuzingatiwa katika utekelezaji wa miradi ya ujenzi kwa utaratibu wa *force account*.

**94. Mheshimiwa Spika**, lengo la hatua hizi ni kujenga sekta binafsi iliyo imara na kutengeneza walipa kodi wakubwa hapa nchini. **Sheria ni hatua moja, utekelezaji ni hatua nyingine, nitoe rai kwa kamati zetu za ununuzi kuzingatia mwongozo huu**. Utaratibu wa kuwapa masharti ya upendeleo wageni na kuwapa masharti yanaoumiza wazawa yanafanya nchi yetu kuendelea kuwa na sekta binafsi changa yenye wigo mdogo wa walipakodi wakubwa. Tunatekeleza miradi wakati mwingine kwa fedha za mikopo, tunapogawa kazi hizo zote kwa wageni tunafanya fedha hiyo ipitilize kwenda nchi nyingine na kuwaachia watanzania mzigo wa deni. Hivyo, nitoe rai pia kwa **Maafisa Masuuli wote mnapoingia mikataba hakikisheni mnalinda maslahi ya watanzania**.

**95. Mheshimiwa Spika**, umekuwepo utaratibu inapoingiwa mikataba na wageni, inawekwa kwenye mkataba, muda wa kulipwa hati za madai zilizoiva na kwamba ikichelewa hata siku moja inatengeneza riba. Hata hivyo, mikataba hiyo haioneshi wazi wajibu wa makandarasi hawa kulipa riba pindi watakapochelewesha malipo ya makandarasi wazawa walio chini yao (sub contract). Na hivyo, tunakuwa na shinikizo la kuwalipa wageni fedha ambazo wao wanapitisha hata miezi minne mpaka sita bila kuwalipa wazawa. Maafisa

Masuuli wote mnapoingia mikataba na makandarasi wageni, wekeni masharti ambayo yatatumika pia kwa wakandarasi wazawa kwenye mikataba midogo wanaopata kutoka kwao.

**Ushiriki wa Wazawa katika Shughuli za Kiuchumi**

**96. Mheshimiwa Spika**, pamoja na Serikali kutenga kiasi kikubwa cha fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo, bado sehemu kubwa ya fedha hizo haziwanufaishi wazawa ipasavyo. Sababu kubwa zinazochangia kuwepo kwa hali hiyo ni uwezo mdogo wa kifedha kwa makandarasi wa ndani, mitambo na

wataalam ikilinganishwa na kampuni za nje. Kwa kutambua changamoto hizo, Serikali itaendelea kutoa elimu ili kuwajengea uwezo wazawa kwenye utekelezaji wa miradi mbalimbali hasa katika sekta ya ujenzi hapa nchini. Aidha, Serikali imedhamiria kuwawezesha makandarasi wazawa kushiriki kwenye kazi kubwa za ujenzi katika hatua na taratibu zote kuanzia mipango, usanifu, ununuzi, ujenzi na ukarabati. Katika kufanikisha hilo, Serikali imeandaa mkakati wa kuongeza ushiriki wa wazawa katika utekelezaji wa miradi (Local Content Strategy) pamoja na kufanya marekebisho katika Sheria ya Ununuzi wa Umma Namba 10 ya Mwaka 2023 kwa kuongeza wigo wa thamani ya miradi ya kutekelezwa na wazawa peke yao. Nitoe rai kwa sekta zote kuhakikisha kuwa zinazingatia Sheria hiyo na pia mikataba inayosainiwa na makampuni ya nje ihakikishe inazingatia sera ya uwezeshaji ikiwemo kutumia huduma na rasilimali zinazopatikana hapa nchini pamoja na kutoa ajira za moja kwa moja kwenye utekelezaji wa miradi husika. Vilevile, Serikali itaanzisha utaratibu wa Mfuko wa Mtaji (Venture Capital Fund) kwa lengo la kutoa mtaji kwa biashara zinazoanza na ndogondogo (Start-ups na SMEs) kwa utaratibu utakaowekwa.

**97. Mheshimiwa Spika,** uwezeshaji wa wazawa utaleta manufaa ikiwemo: faida inayopatikana kutokana na utekelezaji wa miradi kubaki nchini na kutumika kukuza biashara za wazawa; kupunguza matumizi ya fedha za kigeni; kuongeza ajira na ujuzi kwa wataalam wa ndani pamoja na kujenga uwezo wa kampuni za ndani kuweza kushindana kimataifa.

**Mabadiliko ya Tabianchi**

**98. Mheshimiwa Spika**, mabadiliko ya tabianchi yameendelea kuleta athari za kijamii na kiuchumi hasa kwa nchi zinazoendelea ikiwemo Tanzania. Hivi karibuni, tumeshuhudia mafuriko nchini yaliyosababisha uharibifu wa miundombinu pamoja na kuathiri shughuli za uzalishaji. Athari hizo zimeendelea kuongeza gharama za utekelezaji wa bajeti, kupunguza kasi ya ukuaji wa uchumi na kuathiri maisha ya wananchi.

**99. Mheshimiwa Spika**, kwa kutambua athari za mabadiliko ya tabianchi, Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali ikiwemo kutenga bajeti kwa ajili ya kutekeleza programu za uhifadhi na usimamizi wa mazingira pamoja na kufanya mazungumzo na Washirika wa Maendeleo ili kupata fedha za kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi. Mathalan, kwa sasa Serikali ipo katika majadiliano na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) ili kunufaika na mkopo nafuu kupitia dirisha la *Resilience and Sustainability Facility (RSF)* kwa ajili ya kuimarisha uwezo wa nchi katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Aidha, nitumie fursa hii kuzielekeza taasisi zote kujumuisha masuala ya uhifadhi na usimamizi wa mazingira wakati wa kupanga na kutekeleza sera na programu mbalimbali.

**100. Mheshimiwa Spika**, katika kuunga mkono juhudi za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, napenda nitambue juhudi zinazochukuliwa na Serikali yetu ikiongozwa na Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan za kupunguza uchafuzi wa mazingira kupitia hewa ya kaboni. Mheshimiwa Rais katika mkutano wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi uliofanyika Dubai mwaka 2023 (COP 28) alizindua rasmi mpango wa utekelezaji wa *Mradi wa Nishati Safi ya kupikia kwa Wanawake Afrika* (African Women Clean Cooking Support Programme - AWCCSP) ambao una lengo la kuleta mageuzi ya nishati ya kupikia na kumkomboa mwanamke na kulinda mazingira yetu. Aidha, Mheshimiwa Rais alizindua Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia (2024 - 2034) ikiwa ni moja ya hatua za awali za kitaifa za utekelezaji wa programu hiyo. Mkakati huu unalenga kukuza matumizi ya nishati safi ya kupikia kwa watanzania kwa kuimarisha upatikanaji wa malighafi na miundombinu ya uhakika ya nishati safi ya kupikia. Hivyo, napenda kutoa rai kwa wananchi na wadau wote kumuunga mkono

Mheshimiwa Rais katika jitihada za kufanikisha utekelezaji wa mkakati huu.

**Mwenendo wa Deni la Serikali**

**101. Mheshimiwa Spika**, hadi Machi 2024, deni la Serikali lilikuwa shilingi bilioni 91,708.28. Kati ya kiasi hicho, deni la nje ni shilingi bilioni

60,954.31 na deni la ndani ni shilingi bilioni 30,753.97. Tathmini ya uhimilivu wa deni iliyofanyika Desemba 2023 imeonesha kuwa deni ni himilivu katika kipindi cha muda mfupi, wa kati na mrefu. Katika tathmini hiyo, viashiria vinaonesha kuwa kwa mwaka 2023/24: thamani ya sasa ya deni la Serikali kwa Pato la Taifa ni asilimia 35.6 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 55; thamani ya sasa ya deni la nje kwa Pato la Taifa ni asilimia 19.0 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 40; na thamani ya sasa ya deni la nje kwa mauzo ya nje ni asilimia 113.2 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 180.

**102. Mheshimiwa Spika**, kumekuwa na mijadala kuhusu Deni la Serikali ambalo mara nyingi limepotoshwa na kutumiwa kisiasa kama silaha ya kuwatia hofu watanzania kuhusu mwenendo wa deni letu. Mara kwa mara, ongezeko la deni limekuwa likitajwa bila kueleza sababu zake halisi na jinsi fedha hizo zinavyotumika. **Napenda kusahihisha rekodi hiyo leo ili kuweka kumbukumbu sawa. Mheshimiwa Spika**, ongezeko la deni letu la Taifa limechangiwa na sababu kadhaa za msingi na za kimaendeleo. **Kwanza**, tumepokea fedha kutoka mikopo ya zamani pamoja na mikopo mipya. Fedha hizo, zimeelekezwa kwenye miradi ya maendeleo yenye manufaa kwa Taifa letu, ikiwa ni pamoja na ujenzi wa miundombinu ya barabara, reli ya kisasa, viwanja vya ndege, na miradi ya umeme, elimu na afya. Kwa kipindi cha kuanzia tarehe 1 Aprili 2021 hadi 31 Machi 2024, Serikali ilipokea (*net inflow*) jumla ya shilingi bilioni 17,218.21.

**Pili**, kupungua kwa thamani ya Shilingi dhidi ya dola ya Marekani kumechangia ongezeko la deni la nje. Kuanzia tarehe 31 Machi 2021 hadi 31 Machi 2024, thamani ya shilingi dhidi ya dola moja imepungua kutoka shilingi 2,309.96 hadi shilingi 2,569.66, sawa na kupungua kwa thamani kwa asilimia 11.24. Hii imesababisha ongezeko la deni la nje kwa shilingi bilioni 5,428.92.

**Tatu**, ongezeko la deni la ndani lilisababishwa na kutoa hatifungani maalumu zenye thamani ya shilingi bilioni 2,176.7 mwaka 2021/22 kwa ajili ya kulipa deni la Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi

wa Umma (PSSSF), linalohusu michango ya watumishi waliokuwa kwenye utumishi kabla ya mwaka 1999.

**103. Mheshimiwa Spika**, kwa muktadha huo, ni muhimu kuelewa sababu za ongezeko la deni kabla ya kutoa hukumu au kueneza hofu. Serikali yetu inaendelea kuchukua hatua za makusudi kuhakikisha kwamba mikopo inayochukuliwa inatumika kwa malengo yaliyokusudiwa na kwa manufaa ya taifa letu. Hatua hizi zinaenda sambamba na juhudi zetu za kulipa madeni kwa wakati, hali inayotuweka katika nafasi nzuri ya kifedha na kuendeleza uaminifu wetu kimataifa.

**104. Mheshimiwa Spika,** ni dhahiri kwamba uwiano wa maendeleo ndani ya nchi yetu haukuwa sawa kwa muda mrefu. Baadhi ya mikoa imekuwa na miundombinu bora zaidi, kama vile barabara nzuri, idadi kubwa ya shule za msingi na sekondari, vyuo vingi, na huduma bora za maji na umeme ikiwemo umeme unaofika hadi kwenye mabanda ya mifugo. Wakati huo huo, mikoa mingine inakabiliwa na changamoto nyingi ikiwemo ukosefu wa umeme katika makazi ya watu. Katika kutatua tofauti hizi, Serikali ya Awamu ya Sita imechukua hatua madhubuti kwa kuingia mikataba ya mikopo ya fedha ili kufadhili miradi mbalimbali ya maendeleo katika sekta tofauti. Nitaeleza kwa undani zaidi kuhusu miradi hiyo na jinsi fedha hizo zilivyotumika, hivi punde.

**105. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Sita, tumekopa jumla ya shilingi bilioni 17,218.21 kutoka katika vyanzo vya nje kwa lengo la kugharamia shughuli mbalimbali za maendeleo. Fedha hizo zimeelekezwa kwenye miradi mikubwa ya kimkakati ikiwemo: Mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa (SGR) kwa vipande mbalimbali pamoja na ununuzi wa mabehewa na vichwa vya treni. Mikoa itakayonufaika na mradi huu ni pamoja na Dar es Salaam, Morogoro, Dodoma, Singida, Tabora, Shinyanga, Mwanza, Katavi na Kigoma. Miradi hii pia itafungua fursa za kiuchumi kutoka nchi jirani kama vile Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo.

**106. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2023/24, sekta ya ujenzi ilitengewa jumla ya shilingi bilioni 4,164.96. Fedha hizo zimeelekezwa kwenye miradi mbalimbali ya ujenzi inayotekelezwa katika mikoa tofauti nchini. Chini ya uongozi wa **Mama yetu, Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,** na kwa ushirikiano na washirika wetu wa maendeleo, tumeweza kuendelea na utekelezaji wa ujenzi wa miradi ya barabara na viwanja vya ndege zaidi ya 14. Miradi hiyo ina thamani ya dola za Marekani bilioni 2.81, sawa na shilingi trilioni 7.34, ikijumuisha mikopo nafuu na misaada kutoka kwa Washirika wa Maendeleo kama Benki ya Maendeleo Afrika (AfDB), Benki ya Dunia, JICA, Mfuko wa Maendeleo wa Kuwait, na Mfuko wa Maendeleo wa OPEC.

**107. Mheshimiwa Spika,** baadhi ya barabara zinazojengwa kwa fedha za washirika hawa ni pamoja na: Ujenzi wa Barabara ya Mabasi ya Haraka (BRT) Awamu ya Pili (Kariakoo - Mbagala), Tatu (Posta - Gongolamboto) na Nne (Posta - Tegeta) Jijini Dar es Salaam; Mradi wa Barabara za Mzunguko kwa Jiji la Dodoma; barabara ya Mnivata - Masasi - Newala; barabara ya kikanda ya Tanzania - Burundi, Rumonge Gitaza kabingo - Kasulu Manyovu; barabara ya kikanda ya Bagamaoyo - Horohoro/Lunga Lunga - Malindi; barabara za Malagarasi - Ilunde - Uvinza, Kazilambwa - Chagu, Kasekese - Ikola - Karema; Barabara ya Kahama -Bulyanhulu - Kakola; barabara za Rusahunga - Rusumo, Mtwara - Mingoyo - Masasi, Rutukila - Songea, Iringa - Msembe; pamoja na ujenzi wa daraja la Jangwani. Ujenzi huu, unaenda sambamba na ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Msalato na viwanja vya ndege vya Tanga, Ziwa Manyara na Iringa. Miradi hii ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji wake na baadhi yake inategemewa kukamilika katika mwaka 2024/25.

**108. Mheshimiwa Spika**, katika jitihada za kuboresha huduma za jamii, jumla ya shilingi bilioni 4,063.31 zilielekezwa kwa ajili ya kupambana na athari za UVIKO-19. Fedha hizi zimeelekezwa katika ujenzi wa madarasa ya shule za msingi na sekondari, kuboresha huduma za afya, na ufufuaji wa sekta ya utalii, miradi ambayo imetekelezwa nchi nzima.

**109. Mheshimiwa Spika**, katika **sekta ya elimu**, shilingi bilioni 2,427.42 zilielekezwa kwenye miradi muhimu ikiwemo Mradi wa Maboresho ya Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi, ambao unatekelezwa na vyuo vikuu vyote vya umma Tanzania Bara na Zanzibar. Aidha, tunaendeleza Mradi wa Kuboresha Elimu Msingi Zanzibar ili kuimarisha misingi ya elimu katika eneo hilo.

**110. Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa **sekta ya maji**, shilingi bilioni 1,012.06 zilikopwa kwa ajili ya miradi ya maji inayotekelezwa Tanzania Bara na Zanzibar. Miradi hii inajumuisha Mradi wa Maji Safi na Usafi wa Mazingira Vijijini - *Sustainable Rural Water Supply and Sanitation* kwa upande wa bara, na Mradi wa Usambazaji Maji Mijini kwa upande wa Zanzibar.

**111. Mheshimiwa Spika,** katika juhudi za kuimarisha miundombinu ya nishati nchini, shilingi bilioni 2,051.32 zilielekezwa kutekeleza miradi mbalimbali ya **sekta ya nishati**. Kwenye **sekta ya mawasiliano**, shilingi bilioni 1,631.84 zimeelekezwa kwenye miradi kama *Mradi wa Digital Tanzania*, unaotekelezwa nchi nzima kuboresha upatikanaji na ubora wa mawasiliano.

**112. Mheshimiwa Spika**, katika **sekta ya kilimo**, shilingi bilioni 1,379.68 zimeelekezwa kutekeleza miradi katika mikoa yote ya Tanzania Bara na Zanzibar, ikiwemo mradi wa *Tanzania Food Systems Resilience Program* na *Agricultural Inputs Support Project*, ambayo inalenga kuongeza uzalishaji na usalama wa chakula. Aidha, jumla ya shilingi milioni 2,433.98, zimeelekezwa katika sekta nyingine kama **ardhi, afya, utawala bora, maendeleo ya jamii na sekta ya fedha** ili kuboresha huduma na miundombinu muhimu.

**113. Mheshimiwa Spika,** kwa maelezo haya, ni dhahiri kwamba Serikali ya Awamu ya Sita imeingia mikataba ya mikopo ya fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo kwa kiasi kikubwa ukiachilia mbali ile sehemu ya deni iliyoongezeka kwa sababu za msukosuko wa uchumi duniani.

**114. Mheshimiwa Spika**, pamoja na hayo, kampuni kubwa za kimataifa za *Moody's Analytics* na *Fitch Ratings* ziliifanyia nchi yetu tathmini ya uwezo wa nchi kukopa na kulipa madeni. Matokeo ya tathmini ya awamu ya kwanza ya mwaka 2023 yalibainisha kuwa Tanzania inakopesheka na ina uwezo wa kulipa madeni. Kampuni ya *Moody's* ilifanya mapitio ya pili ya mwenendo wa uchumi wa Tanzania Machi 2024. Kufuatia mapitio hayo, Tanzania imepandishwa Daraja la uwezo wa nchi kukopesheka kutoka B2 ikiwa na mtazamo chanya (Positive Outlook) hadi B1 ikiwa na mtazamo thabiti (Stable Outlook). Daraja hili ni la juu kabisa katika ukanda wa Afrika Mashariki na inatokana na jitihada za Serikali ya Chama cha Mapinduzi chini ya uongozi thabiti wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, katika kuboresha mazingira ya ufanyaji biashara na uwekezaji pamoja na ukuaji wa uchumi. Faida za kupandishwa daraja kwa Tanzania ni pamoja na: kuvutia uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje; na kuongeza upatikanaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya Serikali na sekta binafsi katika masoko ya fedha ya kimataifa. Aidha, Kampuni ya *Fitch* imeanza kufanya mapitio kama haya mwezi Mei 2024.

## IV. TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA 2023/24

### Mwenendo wa Mapato

**115**. **Mheshimiwa Spika**, katika bajeti ya mwaka 2023/24, Serikali ilitarajia kukusanya jumla ya shilingi trilioni 44.39 kutoka katika vyanzo vya ndani na nje. Hadi Aprili 2024, jumla ya shilingi trilioni 35.25 zilipatikana kutoka vyanzo hivyo, sawa na asilimia 79.4 ya lengo la mwaka. Mchanganuo wa mapato yaliyopatikana ni kama ifuatavyo:

(i) Mapato yaliyokusanywa kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania yalikuwa ni shilingi trilioni 21.31, sawa na asilimia 79.7 ya lengo la mwaka;

(ii) Mapato yasiyo ya kodi yanayokusanywa na Wizara, Wakala na Taasisi za Serikali yalifikia shilingi trilioni 1.91, sawa na asilimia 54.4 ya lengo la mwaka;
(iii) Mapato yanayokusanywa na Mamlaka za Serikali za Mitaa yalifikia shilingi bilioni 931.0, sawa na asilimia 81.4 ya lengo la mwaka;
(iv) Misaada na mikopo nafuu kutoka kwa Washirika wa Maendeleo ilifikia shilingi trilioni 4.93, sawa na asilimia 90.1 ya lengo la mwaka;
(v) Mikopo ya kibiashara kutoka vyanzo vya ndani ilikuwa shilingi trilioni 4.61, sawa na asilimia 84.8 ya lengo la mwaka; na
(vi) Mikopo ya kibiashara kutoka vyanzo vya nje ilikuwa shilingi trilioni 1.56, sawa na asilimia 74.5 ya lengo la mwaka.

**Mwenendo wa Matumizi**

**116. Mheshimiwa Spika,** makadirio ya matumizi yaliyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu kwa mwaka 2023/24 ni shilingi trilioni 44.39, ambapo shilingi trilioni 30.31 ni matumizi ya kawaida na shilingi trilioni 14.08 ni matumizi ya maendeleo. Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Aprili 2024, jumla ya shilingi trilioni 35.63 zimetolewa, sawa na asilimia 80.3 ya lengo la mwaka. Kati ya kiasi hicho, shilingi trilioni 23.29, sawa na asilimia 76.8 ya lengo la mwaka zilikuwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Aidha, jumla ya shilingi trilioni 12.34, sawa na asilimia 87.7 ya lengo la mwaka zimetolewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

**117. Mheshimiwa Spika**, baadhi ya maeneo yaliyopelekewa fedha katika kipindi cha marejeo ni pamoja na: ulipaji wa deni la Serikali shilingi trilioni 8.84; ulipaji wa mishahara ya watumishi shilingi trilioni 8.28; ujenzi wa barabara, madaraja, na viwanja vya ndege shilingi trilioni 1.27; ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya reli ikiwemo mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa (SGR) shilingi trilioni 1.71; utekelezaji wa mradi wa Kufua Umeme katika Bwawa la Julius Nyerere (JNHPP) MW 2,115 na mradi wa kusambaza umeme vijijini kupitia Wakala wa Nishati Vijijini (REA) shilingi trilioni 1.02; ugharamiaji wa mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu na vyuo vya kati shilingi bilioni 570.3;

ugharamiaji wa Programu ya Elimumsingi na Sekondari bila Ada shilingi bilioni 333.0; utekelezaji wa mradi wa Kuboresha Shirika la Ndege la Tanzania (ATCL) ikijumuisha ununuzi wa ndege shilingi bilioni 244.8; na utekelezaji wa miradi ya maji mijini na vijijini shilingi bilioni 457.4.

**118. Mheshimiwa Spika**, utakumbuka kuwa nchi yetu ilikumbwa na janga la mvua za El-Nino ambazo ziliharibu kwa kiasi kikubwa miundombinu ya barabara, madaraja na reli. Kufuatia hali hiyo, Serikali makini ya Awamu ya Sita ilifanya jitihada za makusudi kurejesha hali ya awali ya miundombinu hiyo kwa kutoa jumla ya shilingi bilioni 136.2 kupitia TANROADS na TARURA. Nipende kuwahakikishia watanzania kuwa Serikali itaendelea kutoa fedha kwa ajili ya kugharamia ukarabati wa miundombinu iliyoharibiwa. Aidha, nazielekeza taasisi zote zinazohusika na ujenzi wa miundombinu kuhakikisha zinafanya usanifu wa miradi kwa kuzingatia mabadiliko ya tabianchi.

**Ulipaji wa Malimbikizo ya Madeni**

**119**. **Mheshimiwa Spika**, hadi Aprili 2024, Serikali imelipa madeni yaliyohakikiwa ya jumla ya shilingi trilioni 1.19. Kati ya kiasi hicho, madeni yatokanayo na mashauri ya kimahakama na hati za makubaliano (deed of settlement) ni shilingi bilioni 535.8, wazabuni shilingi bilioni 268.0, makandarasi shilingi bilioni 263.3, watumishi shilingi bilioni 106.7 na watoa huduma shilingi bilioni 14.6. Ulipaji huu wa madeni umesaidia kuongeza ukwasi na hivyo kuchochea shughuli za kiuchumi. Aidha, ili kuipunguzia Serikali gharama za malipo ya madeni, nazielekeza taasisi zote za Serikali kuhakikisha zinawasilisha hati za madai Wizara ya Fedha kwa wakati na kufuata taratibu inapolazimu kuvunja mikataba.

**V. MIKAKATI YA KUONGEZA MAPATO KWA MWAKA 2024/25**

**120. Mheshimiwa Spika**, Serikali ya Awamu ya Sita, chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, itaendelea na jitihada za kuongeza mapato ya ndani ikiwa ni pamoja na kuanza utekelezaji wa Mkakati

wa Muda wa Kati wa Kuongeza Mapato (2024/25 - 2026/27) kwa lengo la kupunguza utegemezi wa kibajeti na kuzidi kuliletea maendeleo Taifa letu. Mkakati huo umejikita katika kuongeza wigo wa kodi, kuendelea kuimarisha mifumo ya usimamizi na ukusanyaji wa mapato pamoja na kuhamasisha umma juu ya umuhimu wa kulipa kodi kwa hiari.

**121. Mheshimiwa Spika**, katika kuongeza wigo wa mapato, Serikali itaendelea kuboresha vyanzo vya mapato kwa kuhakikisha vinaakisi misingi ya ukusanyaji mapato. Aidha, utoaji elimu kwa umma kuhusu ulipaji kodi utakuwa endelevu ili kuongeza uhiari na kuhakikisha kodi stahiki inakusanywa. Vilevile, kupitia fursa za uwekezaji zinazoibuliwa, Serikali itaendelea kutambua walipakodi wapya ikiwemo kusajili kampuni za kimataifa zinazoendesha biashara kidijitali hapa nchini kupitia mfumo wa usajili uliorahisishwa.

**122. Mheshimiwa Spika**, katika kurahisisha ulipaji kodi, ada na tozo mbalimbali na kuongeza uhiari wa ulipaji wa kodi, Serikali inaendelea kufanya maboresho ya mifumo ya taasisi zenye sura ya utoaji wa huduma kwa pamoja ili kutoa ankara jumuishi ya malipo itakayorahisisha upatikanaji wa mapato kwa wakati na kupunguza muda wa utoaji wa huduma kwa wananchi. Aidha, Serikali imeendelea kuwekeza kwenye matumizi ya TEHAMA ili kuhakikisha mifumo ya Serikali inabadilishana taarifa kwa usahihi, kuondoa urudufu na kuimarisha ufuatiliaji na usimamizi wa fedha za umma. Niendelee kuzihimiza taasisi kuhakikisha malipo yote yanakusanywa kwa kutumia **Kumbukumbu Namba ya Malipo** ili kudhibiti upotevu wa mapato.

**123. Mheshimiwa Spika**, kumekuwa na tabia kwa baadhi ya wafanyabiashara kukwepa kulipa kodi kwa kutumia mbinu mbalimbali. Jambo hili linamsikitisha sana Mheshimiwa Rais kama alivyozungumza katika Baraza la Eid mwezi Aprili 2024, naomba ninukuu ***"Inasikitisha kuona kwamba baadhi ya wafanyabiashara wanatumia mbinu mbalimbali kukimbia kulipa kodi, hawatoi risiti wanapouza au wakitoa risiti ni zenye upungufu, na wanunuzi wa bidhaa nao hawadai risiti wanaponunua bidhaa au huduma.***

***Naomba mniruhusu nitumie jukwaa hili kusema kwamba ulipaji wa kodi ni jambo la halali kidini. Mwenyezi Mungu ametuwekea mfumo madhubuti wa kiuchumi unaoeleza namna ya bait-ul-mal au hazina ya Serikali zinavyopaswa kukusanya kodi ili ziwe na uwezo wa kuwahudumia wananchi wake*"**. Mwisho wa kunukuu. Nitumie fursa hii kukemea vikali tabia hiyo na Serikali itachukua hatua kali za kisheria dhidi ya wale wote watakaobainika kujihusisha na vitendo vya ukwepaji kodi.

**124. Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya pekee, napenda kuwashukuru wananchi wanaoendelea kulipa kodi kwa hiari. Hakika moyo huu wa kizalendo unawezesha Serikali kutekeleza majukumu yake ya kuleta maendeleo ya nchi yetu. ***Kwa Pamoja Tujenge Taifa Letu!*** Aidha, Serikali inakusudia kuanzisha Tuzo ya Uzalendo kupitia Mfumo wa Usimamizi wa Risiti za Kielektroniki ili kuhamasisha tabia ya wananchi kudai risiti stahiki pindi wanapofanya ununuzi, na wafanyabiashara kutoa risiti kwa hiari pale wanapofanya mauzo. Tuzo hizo zitatolewa kwa mtindo wa bahati nasibu ambapo zawadi mbalimbali zitakuwa zinatolewa kwa kuchezesha droo ili kuwapata washindi waliotoa na waliodai risiti kwa kipindi husika. Vilevile, Serikali inaendelea kuhimiza juu ya umuhimu wa kuzingatia sheria za kodi pale taasisi za umma, mashirika, watu binafsi na makampuni yanapofanya ununuzi ama kuuza bidhaa na huduma.

**125. Mheshimiwa Spika**, Serikali itaendeleza juhudi za kuboresha mazingira wezeshi ya ufanyaji biashara na uwekezaji kwa kurahisisha taratibu na kanuni za uanzishaji na uendeshaji. Aidha, kwa kutambua umuhimu wa biashara ya kimataifa na uwekezaji wa kigeni, Serikali itaendelea kuimarisha na kukuza uhusiano na mataifa mengine, taasisi za kimataifa na jumuiya za kikanda pamoja na kuimarisha utekelezaji wa sera ya diplomasia ya uchumi.

**126. Mheshimiwa Spika**, Serikali imekuwa ikitoa misamaha ya kodi kwa lengo la kuvutia uwekezaji nchini. Hata hivyo, kumekuwa na changamoto ya matumizi yasiyo sahihi ya misamaha hiyo. Hivyo, Serikali inaendelea kuhimiza matumizi sahihi ya misamaha inayotolewa katika uwekezaji na miradi mbalimbali nchini. Aidha,

katika kuhakikisha uwazi na ufanisi wa misamaha inayotolewa, Serikali itaendelea kufanya mapitio ya misamaha na vivutio vya kodi vinavyotolewa kwa wawekezaji na kwenye utekelezaji wa miradi mbalimbali. Lengo likiwa ni kubaini faida na umuhimu wake kwa ukuaji wa uchumi wa Taifa, na pale itakapobainika kuwa misamaha hiyo imetumika kinyume na malengo yaliyokusudiwa **itafutwa mara moja** ili kunusuru upotevu wa mapato.

**127. Mheshimiwa Spika**, kama ilivyobainishwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuwa, baadhi ya taasisi na mashirika ya umma yamekuwa yakipata hasara mwaka hadi mwaka na kusababisha Serikali kutopata mapato stahiki na kuiongezea mzigo kwa kuendelea kupewa ruzuku. Hivyo, nazielekeza taasisi na mashirika ya umma kuweka mikakati ya kuongeza ufanisi ili kusaidia kurejesha fedha za uwekezaji na kuongeza mapato na hatimaye kupunguza mzigo kwa Serikali. Aidha, Serikali itaendelea kuimarisha mifumo ya usimamizi na tathmini ya utendaji wa taasisi na mashirika ya umma ili kuongeza ufanisi.

**128. Mheshimiwa Spika**, katika kuhakikisha malengo ya ukusanyaji mapato ya Serikali yanafikiwa, nazielekeza taasisi zilizopewa dhamana ya kukusanya mapato ya Serikali kuhakikisha mapato yanakusanywa kupitia mifumo rasmi na kodi stahiki inalipwa kwa mujibu wa sheria kama alivyosisitiza Mheshimiwa Rais, naomba kunukuu **"*Ahadi yangu kwa watanzania ni kuendelea kusimamia haki kwenye ukusanyaji wa kodi, kuboresha mifumo na kuleta wepesi katika ulipaji na ukusanyaji wa kodi na kuhakikisha kuwa kodi inayokusanywa inatumika ipasavyo kwa manufaa ya wananchi*"**. Mwisho wa kunukuu. Hivyo, nawaomba Waheshimiwa Wabunge na watanzania wote kwa ujumla tumuunge mkono Mheshimiwa Rais katika kulipa kodi bila shuruti kwa maendeleo ya Taifa letu.

**129. Mheshimiwa Spika**, kufuatia mvua za *El-Nino* zilizonyesha nchini kuanzia Septemba, 2023 pamoja na kimbunga Hidaya, barabara mbalimbali za kitaifa katika mikoa 26 zimeathirika. Barabara 68

zilikuwa zimejifunga, barabara 106 zilikuwa zinapitika kwa shida na barabara 168 ziliathirika lakini zinaendelea kupitika kwa shida baada ya kufanyiwa matengenezo ya dharura. Maeneo yaliyoathirika katika barabara hizo yanakadiriwa kufikia kilometa 520. Aidha, madaraja na makalavati yapatayo 189 yalikuwa yamekatika na mengine kuharibika vibaya. Tathmini iliyofanyika inaonesha gharama za kurejesha miundombinu hiyo ni shilingi trilioni 1.07. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 728.0 ni kwa ajili ya kufanya matengenezo ya kurejesha miundombinu ya barabara ili zirudi katika hali yake ya awali na shilingi bilioni 158.0 ni kwa ajili ya matengenezo ya dharura ili barabara hizo ziweze kupitika. Aidha, shilingi bilioni 184.14 ni kwa ajili kurejesha miundombinu iliyoathiriwa na kimbunga Hidaya. Mahitaji hayo ya kurejesha miundombinu iliyoharibika katika hali yake ya kawaida hayakuwepo kwenye bajeti ya mwaka 2023/24 yaliyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu na upo uwezekano majanga kama haya kuendelea kujitokeza miaka ijayo.

**130. Mheshimiwa Spika**, napendekeza kurekebisha Sheria ya Mfuko wa Dharura (Contigency Fund) ili uwe na sifa za mfuko maalum kwa ajili ya kugharamia matengenezo ya dharura ya miundombinu ya barabara inayoharibika tukianza na mwaka huu wa fedha ambapo miundombinu ya barabara imeharibika kutokana na athari za mabadiliko ya tabianchi. Napendekeza vyanzo vya mfuko huu iwe tozo ya miundombinu (infrstructure levy), mapato yatokanayo na tofauti ya kushuka kwa bei za mafuta (the windfall gain in fuel price decrease, asilimia moja ya matumizi ya Serikali kila mwezi na vyanzo vingine vitakavyopangwa na Waziri mwenye dhamana ya Fedha). Undani zaidi utaelezwa kwenye majedwali ya hatua za kikodi.

## VI. MABORESHO YA MFUMO WA KODI, ADA, TOZO NA HATUA NYINGINE ZA MAPATO

**131. Mheshimiwa Spika**, nchi inatekeleza miradi mikubwa ya kimkakati kwa mara moja kuliko nchi yeyote ukanda wa Afrika kwa mfano, reli yetu ya kisasa SGR itakuwa reli ya tano duniani kwa urefu baada tu ya China km 40,493, Hispania km 3,917, Japani km 3,146, Ufaransa km 2,735 na Tanzania km 2,080, ikifuatiwa na Ujerumani km

1,631, Uturuki km 1,232 na Finland km 1,120. Na itakuwa reli ndefu kuliko reli zote duniani kwa nchi zinazoendelea. Aidha, Tanzania inatekeleza mradi mkubwa wa umwagiliaji na uzalishaji wa mbegu. Tunatekeleza pia mabadiliko makubwa ya mitaala kwa kiwango kikubwa kufanyika katika historia ya nchi yetu na mpango wa elimu bila ada na ruzuku kwenye elimu ngazi zote kwa idadi kubwa ya wanafunzi kuliko kipindi chochote katika historia ya nchi yetu. Vilevile, tunatekeleza maandalizi ya Bima ya Afya kwa wote ambapo Bunge lako Tukufu lilipitisha Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote Na. 13 ya Mwaka 2023 ambayo ni programu kubwa zaidi kwenye sekta ya afya katika historia ya nchi yetu. Kadhalika, tunatekeleza programu kubwa ya miradi ya kufua na kusambaza umeme nchini na tunajenga barabara mijini na kufungua barabara nyingi vijijini kuliko kipindi chochote katika historia ya nchi yetu. **Hayo ni baadhi tu!**

**132. Mheshimiwa Spika**, hii inatuambia nini? haya ni mambo ya kujivunia kwa kila mtanzania. Tusijidharau wenyewe na kwamba sote tuna kazi ya kufanya kukamilisha haya yote. Hii inatupa jukumu la kila mmoja anayestahili kulipa kodi kutimiza wajibu huu kikamilifu. Hivyo, niendeleee kutoa rai kwa watanzania wote kwa kila mmoja wetu kuona umuhimu wa kulipa kodi kwa kuwa kodi yako ndio inayoenda kufanikisha hayo yote. **Mheshimiwa Spika**, Sheria za ukusanyaji wa kodi zilizotungwa na Bunge lako Tukufu na kusimamiwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) zinamtaka kila mwananchi kulipa kodi stahiki. Zipo aina mbili za kodi. Aina ya kwanza ni ile ya moja kwa moja (direct taxes) ambazo zinatozwa na sheria za kodi kutoka kwa mlipakodi na kumtaka yeye awasilishe ritani na kulipa kodi husika kwa wakati uliowekwa kisheria. Lakini pia zipo aina za kodi ambazo sio za moja kwa moja (indirect taxes) ambazo Serikali kupitia TRA hukusanya kwa kutumia mawakala.

**133. Mheshimiwa Spika** Mathalani, kodi ya PAYE ni kodi kwa mtumishi sio kodi kwa mwajiri. Mwajiri kama ni Kampuni au Shirika linaowajibu wa kumlipa mtumishi mshahara wake na kisha kuzuia shehemu ya mshahara wake kwa mujibu wa Sheria ya Kodi ya Mapato SURA Na. 332 na kuiwasilisha ritani na malipo yaliyokatwa

kama kodi kwa mtumishi kila ifikapo tarehe 7 ya mwezi unaofuata. Kadhalika, Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) ni kodi inayotozwa kwa mujibu wa Sheria ya Ongezeko la Thamani SURA Na. 148 kwa wananchi wa kawaida kila wanaponunua bidhaa ama kununua huduma. Kodi hii hukusanywa na wauzaji ambao sheria inawapa wajibu wa kuikusanya na kuiwasilisha TRA kila ifikapo tarehe 20 ya mwezi unaofuata.

**134.** Mheshimiwa Spika, Serikali imebaini kuwepo kwa wimbi la wafanyabiashara na Taasisi ambao wana wajibu wa uwakala wa ukusanyaji wa kodi ambao sio waaminifu katika kutimiza wajibu wao uliowekwa kisheria. Mawakala hao wamekuwa wakikusanya kodi hizo na kutokuziwasilisha inavyotakiwa kwa mujibu wa sheria za kodi. Ni vyema ikafahamika kuwa kodi hii sio kodi ya mfanyabiashara au wakala yeyote, na pia si yeye anayelipa ila yeye anatumika kama mkusanyaji wa kodi ya Serikali na anatakiwa kuiwasilisha Serikali ndani ya muda unaotakiwa kwa mujibu wa sheria, taratibu na kanuni za kodi. Ifahamike kuwa, wafanyabiashara hawa wenye wajibu wa uwakala wanaamua kwa makusudi kwenda kinyume na utaratibu wa kisheria, na kwa kufanya hivyo, wanazitumia kodi za walipakodi hawa wa kawaida kwa matumizi binafsi ya biashara zao na hatimae kuonekana kuwa ndio matajiri kumbe wanatumia fedha za watanzania wenzao. Mawakala wanaofanya vitendo hivi wanaihujumu Serikali na jitihada za **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** katika kuiletea maendeleo nchi yetu.

**135. Mheshimiwa Spika**, ninatoa rai kwa mawakala hao iwe ni waajiri binafsi au Taasisi za Serikali wakiwemo wale waliosajiliwa kwenye Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT), Kodi ya Zuio (Withholding Tax) na Ushuru wa bidhaa (Excise Duty) **kuacha mara moja tabia hiyo** ya kuzuia kodi zilizokusanywa kwa wengine na kuzitumia wao badala ya kuziwasilisha TRA kwa mujibu wa sheria. Pia, naelekeza Mamlaka ya Mapato Tanzania kuchukua hatua kali za kisheria kwa mawakala ambao hawatawasilisha ritani na malipo ya kodi hizi ndani ya wakati ikibidi kuwapeleka mahakamani. Hatua

hizi zitasaidia kukomboa kodi ya Serikali kwa wakati na kuhamasisha ulipaji kodi kwa hiari ili kuiletea maendeleo nchi yetu.

**136. Mheshimiwa Spika**, kodi ni wajibu wa kila mmoja anayestahili kulipa kodi. Kuna mazingira yasio na usawa ambayo yamezoeleka katika utozaji wa kodi. Mfano, mtu mwenye kima cha chini cha mshahara anayepata shilingi 300,000 kwa mwezi anatozwa kodi sawa na ilivyo kwa mfanyabiashara mdogo mwenye mapato ghafi yanayozidi shilingi 330,000 kwa mwezi. Inatokea makundi mengine kwenye sekta za uzalishaji ambayo kimsingi yanatumia kodi kuboresha shughuli zao lakini hayalipi kodi. Hii haiko sawa na haina usawa. Kwa mfano, mtu mwenye ng'ombe 9,000 kutokulipa kodi na kutaka kujengewa josho au bwawa kwa ajili ya mifugo yake kwa kodi ya mtu mwenye kipato cha shilingi 300,000 kwa mwezi, **sio sawa**. Mtu mwenye kipato cha milioni 200 au 300 kutokana na kuuza mazao yake kutokulipa kodi na kupokea ruzuku ya mbolea, mbegu au skimu ya umwagiliaji kutokana na kodi ya mtu mwenye kipato cha shilingi 300,000, **sio sawa**.

**137. Mheshimiwa Spika,** napendekeza kila halmashauri zenye idadi kubwa ya mifugo kuratibu ushirika wa mifugo na kuanzisha mfuko wa kuendeleza huduma za ugani za mifugo na miundombinu ya mifugo kama majosho kwa kutumia mifuko hiyo na magari ya Serikali ya kuchimba mabwawa na visima yalioko mikoani mwetu. Vyama vya wafugaji na wafugaji wakubaliane kuhusu utaratibu wa uendeshaji wa mifuko hiyo kama inavyofanyika kwenye vyama vya ushirika kwenye mazao ya kilimo mfano korosho, tumbaku pamba na kadhalika.

**138. Mheshimiwa Spika**, sasa nijielekeze kwenye mapendekezo ya maboresho ya mfumo wa kodi, ada na tozo mbalimbali kwa mwaka 2024/25. Maboresho hayo yanatarajiwa kujibu maswali na kukidhi kiu ya jamii ya Watanzania katika kuchachua uwekezaji kwenye shughuli mbalimbali za uzalishaji mali ndani ya nchi na kuweka mkazo katika sekta za kimkakati kama vile viwanda, kilimo, madini, utalii, ufugaji na uvuvi, miundombinu ya umeme, uchukuzi na usafirishaji na sekta za kijamii za elimu na afya. Maboresho haya

yanalenga pia kukuza uchumi jumla, kukuza ajira na hatimaye kupunguza ukali wa maisha ya wananchi(" Macro economic objectives for inclusive economic growth" ). Aidha, Hatua hizo zinalenga pia kuimarisha usimamizi, ukusanyaji wa mapato ya ndani ya nchi na kudhibiti upotevu wa mapato ya Serikali ("Domestic Revenue Mobilization and Improvements in Tax Administration"). Marekebisho yanayopendekezwa yanahusu Sheria zifuatazo:

1. Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, SURA 148;
2. Sheria ya Kodi ya Mapato, SURA 332;
3. Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, SURA 147;
4. Sheria ya Usimamizi wa Kodi, SURA 438;
5. Sheria ya Kuendeleza Ufundi Stadi, SURA 82;
6. Sheria ya Serikali za Mitaa ya Utozaji wa Kodi ya Majengo, SURA 289;
7. Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania, SURA 197;
8. Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha, SURA 342;
9. Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha, SURA 407;
10. Sheria ya Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma, Mwaka 2018;
11. Sheria ya Ushuru wa Barabara na Mafuta, SURA 220;
12. Sheria ya Mtoto, SURA 13;
13. Sheria ya Bandari, Mwaka 2004;
14. Sheria ya Sukari, Namba 6;
15. Sheria ya Korosho, Namba 18;
16. Sheria ya Madini, SURA 123;
17. Sheria ya Michezo ya Kubahatisha, SURA 41;
18. Sheria ya Reli, Mwaka 2017;
19. Sheria ya Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, SURA 157;
20. Sheria ya Magari (Ada ya Usajili na Uhamishaji), SURA 124;
21. Sheria ya Usimamizi wa Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya mwaka 2004;
22. Sheria ya Kudhibiti Uingizwaji wa Bidhaa Nchini, SURA 276;
23. Sheria ya Usafirishaji Bidhaa Nje ya Nchi, SURA 196;

24. Maboresho ya Ada na Tozo mbalimbali za Taasisi za Serikali pamoja na Utekelezaji wa Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Kufanya Biashara (Blueprint); na
25. Marekebisho madogo madogo katika baadhi ya Sheria za Kodi na Sheria nyingine mbalimbali.

**1. Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, SURA 148**

**139.** ***Mheshimiwa Spika,*** napendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura 148 kama ifuatavyo:

i. Kufanya marekebisho kwenye Kipengele cha 18 cha Sehemu ya Kwanza ya Jedwali la Msamaha ili kujumuisha magari pamoja na vifaa vinavyotumiwa na Jeshi la Wananchi (military and armed forces). Lengo la hatua hii ni kuwezesha Jeshi la Wananchi kutekeleza majukumu yake ya ulinzi na usalama wa nchi. Aidha, msamaha utatolewa baada ya kupata uthibitisho wa Waziri mwenye dhamana ya masuala ya Ulinzi ili kuhakikisha msamaha husika unatumika kwa manufaa ya Jeshi la Wananchi na si vinginevyo;

ii. Kujumuisha wazalishaji na waunganishaji wa ndege nchini kwenye wigo wa msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani unaotolewa kwenye matengenezo kinga ya ndege (aircraft maintenance), uuzaji na ukodishaji wa ndege, injini za ndege na vifaa vyake vinavyouzwa nchini. Lengo la hatua hii ni kufanya wazalishaji na waunganishaji wa ndege nchini kuwa shindani sokoni, kuvutia uwekezaji nchini, kuchochea ukuaji wa tasnia ya Anga pamoja na kuunga mkono juhudi za kuhamasisha Sekta ya Utalii Hatua hii inatarajiwa **kupunguza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi **milioni 7.1**;

iii. Kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye madawa ya kutibu na kusafisha maji, dira za maji na huduma ya uondoshaji wa maji taka (sewage). Msamaha utatolewa kwa Mamlaka za Maji baada ya kupata ridhaa ya Waziri mwenye dhamana ya

masuala ya Maji. Lengo la hatua hii ni kufanikisha utoaji wa huduma ya maji safi na salama nchini;

iv. Kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye uingizwaji wa vifaa vya kiteknolojia kwa ajili ya kuwasaidia waamuzi (Video Assistant Referee equipment and accessories). Lengo la hatua hii ni kuhakikisha nchi inapata vifaa muhimu vya michezo kwa kuzingatia kuwa, Tanzania ni moja ya nchi mwenyeji zitakazohusika katika maandalizi ya michuano ya fainali ya kuwania kombe la mataifa ya Afrika (AFCON) mwaka 2027 na hivyo kunufaika na ongezeko la akiba ya fedha za kigeni, kukuza taswira ya nchi kimataifa na uwepo wa fursa kwa makampuni ya ndani kutangaza biashara zao. Aidha, msamaha utatolewa baada ya vifaa hivyo kupata idhini ya Waziri mwenye dhamana ya masuala ya michezo ili kuhakikisha kuwa msamaha huo unatumika kama ilivyokusudiwa na si vinginevyo;

v. Kuweka takwa la marejesho ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT Refunds) kulipwa ndani ya siku 30 kutoka tarehe ya kuwasilishwa kwa maombi ya marejesho hayo. Hatua hii inalenga kuchochea ulipaji kodi wa hiari na kuongeza uwajibikaji kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania;

vi. Kujumuisha trekta lenye ekseli moja (single axle tractors/ power tiller) linalotambulika kwa HS Code 8701.10.00 kwenye wigo wa zana na vifaa vya kilimo vinavyopata msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani. Marekebisho haya yanalenga kuakisi mawanda ya bidhaa zilizosamehewa pamoja na kuoanisha H.S Codes zilizomo kwenye kitabu cha Viwango vya Pamoja vya Ushuru cha Jumuiya ya Afrika Mashariki (East African Community Common External Tariff) cha mwaka 2017 na zile zilizomo kwenye kitabu cha mwaka 2022;

vii. Kufanya marekebisho kwenye Sehemu ya Kwanza ya Jedwali la Misamaha ya Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa kuondoa baadhi ya vifaa vyenye matumizi mbadala kwenye wigo wa

vifaa vya kilimo vinavyopata msamaha wa kodi. Vifaa hivyo vinatambulika kwa HS Code 8201.10.00 (chepe); 8201.30.00 (sururu). Lengo la hatua hii ni kuendana na azma ya Serikali ya kupunguza misamaha isiyo na tija kwa lengo la kulinda mapato ya Serikali na kupunguza matumizi yanayohusiana na utoaji wa misamaha ya kodi (tax expenditure). Aidha, tathmini iliyofanywa imebaini kuwa, msamaha husika haujafikia malengo kutokana na vifaa hivyo kuwa na matumizi mbadala. Hatua hii inatarajiwa **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi **milioni 4,250;**

viii. Kutoza Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa kiwango cha asilimia 0 kwenye madini ya dhahabu yatakayouzwa kwa Benki Kuu ya Tanzania. Lengo la hatua hii ni kuhamasisha uuzaji wa dhahabu kwa Benki Kuu ya Tanzania, na hivyo kuongeza akiba ya nchi ya fedha za kigeni na kupunguza tatizo la uhaba wa dola za Marekani. Aidha, hatua hii inalenga pia kuchochea ukuaji wa viwanda vya kusafisha madini (refineries) nchini kwa kuwa Benki Kuu ya Tanzania hununua dhahabu baada ya kusafishwa na viwanda hivyo pekee;

ix. Kutoza Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa kiwango cha asilimia 0 kwenye madini ya dhahabu yatakayouzwa kwa Viwanda vya Kusafishia Dhahabu Nchini (refineries). Lengo la hatua hii ni kuchochea ukuaji wa viwanda hivyo nchini kwa kuhakikisha kuwa vinapata malighafi za kutosha (feed stock). Aidha, pendekezo hili pia linalenga kutimiza azma ya Serikali ya kuhakikisha kuwa madini ghafi ya dhahabu yanasafishwa nchini na kuongezewa thamani kabla ya kusafirishwa kwenda nje ya nchi;

x. Kufuta Msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye madini ya thamani, madini ya vito na madini mengine ya thamani yanayouzwa kwenye vituo vya kusafishia dhahabu (refineries) vilivyopo nchini. Lengo la hatua hii ni kuongeza mchango wa Sekta ya Madini katika ukuaji wa Pato la Taifa.

Hatua hii inatarajiwa **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi **milioni 18,150;**

xi. Kutoza Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa kiwango cha asilimia 0 kwenye mbolea inayozalishwa ndani ya nchi kwa kipindi cha mwaka mmoja. Lengo la hatua hii ni kuleta unafuu kwa wakulima na walaji hasa katika kipindi hiki cha mdororo wa uchumi duniani;

xii. Kutoza Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa kiwango cha asilimia 0 kwenye bidhaa za nguo zinazotengenezwa kwa kutumia pamba inayolimwa nchini kwa kipindi cha mwaka mmoja. Lengo la hatua hii ni kuleta unafuu kwa wakulima wa pamba na viwanda vinavyotengeneza nguo nchini hasa katika kipindi hiki cha mdororo wa uchumi;

xiii. Kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye mafuta ya kula yanayozalishwa ndani ya nchi kwa kutumia mbegu zinazozalishwa nchini kwa muda wa mwaka mmoja. Hapo awali, msamaha huu ulitolewa kwa kipindi cha mwaka mmoja (1) kupitia Sheria ya Fedha ya mwaka 2023 na ukomo wake ni tarehe 30 June 2024. Lengo la hatua hii ni kuendeleza unafuu wa bei ya mafuta ya kula iliyopanda kutokana na mdororo wa uchumi pamoja na vita ya Urusi na Ukraine vilivyosababisha uhaba wa mafuta hayo; na

xiv. Kutoza Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye huduma ya data zinazotolewa mtandaoni (online data service). Mabadiliko haya yanaenda sambamba na kuweka tafsiri ya maneno *online data services* na kujumuisha huduma hiyo kwenye wigo wa utozaji wa huduma za kidijitali. Lengo la hatua hii ni kuongeza wigo wa kodi na kuendana na mabadiliko ya kiteknolojia. Hatua hii inatarajia **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi **milioni 16,397.**

Hatua zote za Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa ujumla wake zinatarajiwa **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi **milioni 22,393.**

**2. Sheria ya Kodi ya Mapato, SURA 332**

**140**. ***Mheshimiwa Spika,*** napendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura 332 kama ifuatavyo:

i. Kujumuisha Taasisi zinazofanya shughuli za uboreshaji wa huduma za afya (advancement of health) na utunzaji wa mazingira kwenye wigo wa Taasisi zinazotoa huduma za hisani (Charitable Organisations) ili ziweze kupata nafuu ya ukokotoaji wa Kodi ya Mapato kulingana na matakwa ya Sheria. Lengo la hatua hii ni kuchochea huduma za hisani kwenye eneo la afya na utunzaji wa mazingira hususan katika kipindi hichi ambacho dunia inakabiliana na athari za mabadiliko ya Tabianchi;

ii. Kufanya marekebisho ya kifungu cha 4(8) cha Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura. Na. 332, ili kuondoa takwa la kulipa kodi ya mapato mbadala (Alternative Minimum Tax) kwa makampuni yanayochakata mazao ya Chai, ambayo yanatengeneza hasara kwa kipindi cha miaka mitatu (3). Lengo la hatua hii ni kuleta unafuu kwenye Sekta ya Chai ambayo kwa sasa inakabiliana na changamoto mbalimbali ikiwemo upatikanaji wa hasara unaosababishwa na bei ya zao hilo kushuka katika soko la dunia;

iii. Kufanya marekebisho kwenye Kifungu cha 11 cha Sheria ya Kodi ya Mapato, SURA 332 kwa kuweka takwa la risiti za kielektroniki kutumika katika kuthibitisha manunuzi yaliyofanywa kwenye mwaka husika wa mapato ambayo yamechangia katika uzalishaji wa mapato. Hatua hii haitahusisha muuza bidhaa au mtoa huduma ambaye ni raia wa kigeni na hayupo Tanzania au mtu yeyote ambaye hayupo katika wigo wa kutoa risiti za kielektroniki. Lengo la hatua hii ni kuhimiza utoaji risiti za kielektroniki na kulinda mapato ya Serikali;

iv. Kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura 332 kwa kuruhusu michango ya asilimia 15 inayolipwa na Taasisi za Serikali kwenda Mfuko Mkuu wa Serikali kuwa miongoni mwa sehemu ya gharama za Taasisi kwenye ukokotoaji wa kodi ya mapato (deductible expenditure). Lengo la hatua hii ni kupunguza changamoto zilizopo katika ukokotoaji wa kodi hiyo kwa kuwa fedha hizo huingizwa Mfuko Mkuu wa Serikali. Hatua hii inatarajiwa **kupunguza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha Shilingi **milioni 1,000;**

v. Kufanya maboresho kwenye Jedwali la Kwanza la Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura 332, kwa kurekebisha viwango elekezi vya kodi vinavyotumika kwa wasafirishaji wa abiria ambao mauzo ghafi yao hayazidi kiasi cha shilingi milioni mia moja na ambao hawawajibiki kuandaa hesabu kisheria. Maboresho haya yanalenga kutoa unafuu wa kodi kwa wafanyabishara wa Kundi/ Daraja A na kuendana na hali halisi ya utekelezaji wa shughuli hizo hususan za usafirishaji kupitia daladala. Hatua hii inatarajia **kupunguza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi **milioni 2,265;**

***Jedwali:*** Utaratibu wa kukadiria kodi ya mapato unaopendekezwa kwa wasafirishaji wa Abiria kwa kutumia viwango elekezi vya kodi kwa kila Gari

| **A** | **Daraja A: Magari ya Abiria** | | | |
|---|---|---|---|---|
| | **Utaratibu wa sasa** | | **Utaratibu Unaopendekezwa** | |
| | ***Idadi ya Abiria*** | ***Kiwango*** | ***Idadi ya Abiria*** | ***Kiwango*** |
| 1 | Wasiozidi 15 | 250,000 | Wasiozidi 15 | 250,000 |
| 2 | 16 hadi 25 | 550,000 | 16 hadi 30 | 650,000 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 3 | 26 hadi 45 | 1,100,000 | 31 hadi 45 | 1,100,000 |
| 4 | 46 hadi 65 | 1,600,000 | 46 hadi 65 | 1,600,000 |
| 5 | Zaidi ya 65 | 2,200,000 | Zaidi ya 65 | 2,200,000 |

vi. Kuweka takwa kwa raia wa kigeni (non-resident) kukusanya kodi ya zuio kwa kiwango cha asilimia 5 kwenye malipo yanayofanywa kwenda kwa mtengeneza maudhui mkaazi (resident digital content creator). Lengo la hatua hii ni kuongeza wigo wa kodi na kuzingatia kanuni za usawa za utozaji wa kodi. Hatua hii inatarajia **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi **milioni 675;**

vii. Kutoza Kodi ya Zuio kwa kiwango cha asilimia mbili kwenye malipo yanayotokana na ununuzi wa madini ya viwandani (industrial minerals). Aidha, utozaji huu hautahusisha chumvi, madini ya metaliki au madini mengine ya thamani kama yalivyotafsiriwa kwenye Sheria ya Madini, SURA 123 yatakayouzwa na mmiliki wa Leseni ya Uchimbaji Mdogo wa Madini (Primary Mining Licence) au mchimbaji mdogo wa madini (Artisanal Miner). Lengo la hatua hii ni kuongeza wigo wa kodi na kuzingatia kanuni za usawa za utozaji kodi;

viii. Kutoza Kodi ya Zuio kwa kiwango cha asilimia 3 kwenye mapato yatokanayo na uhamishaji au ubadilishanaji wa mali za kidijitali (digital assets). Mabadiliko haya yanaenda sambamba na kuweka tafsiri ya maneno "mali za kidijitali". Aidha, Mmiliki wa jukwaa au mtu yeyote atakayefanikisha zoezi la uhamishaji au ubadilishanaji, atawajibika kuwa wakala wa kukusanya kodi hiyo na kuiwasilisha kwa Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania. Raia wa kigeni anayemiliki jukwaa linalotumika kufanikisha uhamishaji au ubadilishanaji wa mali za kidijitali, atapaswa kujisaliji chini ya mfumo uliopo wa *simplified tax regime*. Lengo la hatua hii ni kuongeza wigo wa kodi na kuzingatia kanuni za usawa za utozaji wa kodi. Hatua hii

inatarajia **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi **milioni 465;**

ix. Kutoza Kodi ya Zuio kwa kiwango cha asilimia 5 kwenye malipo ya biashara ya kutengeneza maudhui ya kidijitali (digital content creators) yanayofanywa na wakaazi (resident business). Lengo la hatua hii ni kuongeza wigo wa kodi na kuzingatia kanuni za usawa za utozaji wa kodi. Hatua hii inatarajia **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi **milioni 968;**

x. Kutoza Kodi ya Mapato kwa kiwango cha asilimia 2 kwenye malipo yatakayofanywa na WAFANYABIASHARA WA KATI kutokana na ununuzi wa bidhaa za kilimo, ufugaji, uvuvi na misitu. Kodi inayopendekezwa itakuwa ni kodi ya mwisho na mpokeaji wa mapato hatawajibika kukatwa tena kodi kwa mapato ambayo yameshakatwa kodi hiyo;

xi. Kufanya marekebisho kwenye Kifungu cha 56(5)(a) cha Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura 332 ili kubainisha kuwa, mabadiliko ya umiliki wa Kampuni iliyopo nchini (resident entity) uliosababishwa na ugawaji wa hisa mpya hautatozwa Kodi ya Mapato kwa mujibu wa Kifungu cha 56. Lengo la hatua hii ni kutoa ufafanuzi wa kifungu hicho na kuondoa changamoto zilizopo katika utekelezaji na usimamizi wa kifungu hicho baada ya kufanyiwa marekebisho kupitia Sheria ya Fedha ya 2023;

xii. Kufanya marekebisho ya Kifungu cha 19 (2) cha Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura 332 ili kuongeza wigo wa faida itakayotozwa kodi kuanzia mwaka wa nne kwa mfanyabiashara anayepata hasara mfululizo kutoka asilimia 30 hadi asilimia 40. Lengo la hatua hii ni kuiwezesha Serikali kukusanya kodi mapema zaidi bila kuathiri hasara za nyuma za biashara zitakazobakia ambazo mfanyabiashara ataruhusiwa kuzidai kwenye miaka ya mapato itakayofuatia;

xiii. Kutoa msamaha wa Kodi ya Zuio kwenye malipo ya riba yanayofanywa na Taasisi za Kifedha za ndani ya nchi (Resident Financial Institutions) kwenda Taasisi za Kifedha au Mifuko ya Kifedha ya nje ya nchi (Non Resident Financial Institutions or Funds) zenye mikataba na Serikali ya kutoa mikopo ya riba nafuu kwa Taasisi za Kifedha za ndani ya nchi. Aidha, msamaha utatolewa pale ambapo mkataba uliosainiwa umekidhi matakwa ya Sheria za nchi na una kipengele kinachobainisha msamaha wa kodi hiyo. Lengo la hatua hii ni kuchochea ukuaji wa uchumi kwa kuhakikisha upatikanaji wa mikopo yenye riba nafuu kwa wananchi pamoja na kuwezesha benki za ndani ya nchi kupata mikopo kwa gharama nafuu kutoka Benki za nje ya nchi; na

xiv. Kuweka utaratibu kupitia Kanuni wa utambuzi na ufutaji wa mikopo chechefu kwa taasisi za Kibenki nchini. Lengo la hatua hii ni kutatua changamoto zinazojitokeza katika utambuzi na ufutaji wa mikopo chechefu hususani wakati wa ukokotoaji wa kiasi cha Kodi ya Mapato kinachopaswa kulipwa na Benki husika;

Hatua hizi za Kodi ya Mapato kwa ujumla wake zinatarajiwa **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi **milioni 31,738;**

**3. Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, SURA 147**

**141**. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Sheria ya Fedha ya mwaka 2023 ilifanya marekebisho ya viwango maalum vya ushuru (specific duty rates) kwa kiwango cha asilimia 10 ya bei kwenye bidhaa zisizo za petroli, na asilimia 20 ya bei kwenye bidhaa za bia na tumbaku ikiwa na lengo la kuakisi mabadiliko ya thamani ya mapato ya Serikali kulingana na mfumuko wa bei. Maboresho hayo hayakujumuisha utozaji Ushuru wa Bidhaa kwa kiwango cha asilimia ya thamani ya bidhaa (advalorem rates) kwa kuwa thamani ya bidhaa inazingatia mfumuko wa bei. Vilevile, Serikali ilianzisha utaratibu wa kurekebisha viwango vya Ushuru wa Bidhaa kila baada ya miaka mitatu (3) kuanzia mwaka wa fedha 2023/24 ili kuiwezesha

nchi kuwa na sera za kodi zinazotabirika na kuweka mazingira bora ya uwekezaji nchini. Aidha, napendekeza pia kufanya marekebisho kwa bidhaa nyingine kama ifuatavyo: -

i. Kupunguza Ushuru wa Bidhaa kutoka shilingi 63.80 kwa lita hadi shilingi 56 kwa lita ya maji ya kunywa yaliyosindikwa kwenye chupa yanayozalishwa nchini. Maji hayo yanatambulika kwa *Hs Code* 2201.10.00 na 2201.90.00. Lengo la hatua hii ni kuchochea ukuaji wa viwanda vidogo vinavyozalisha maji nchini, kupunguza gharama kwa walaji na kuchochea matumizi ya maji safi na salama. Hatua hii inatarajia **kupunguza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi **milioni 474;**

ii. Kutoza Ushuru wa bidhaa kwa kiwango cha shilingi 7,000 kwa kila lita ya *Un-denatured Ethyl Alcohol* yenye kilevi cha asilimia 80 au zaidi inayotoka nje ya nchi, na shilingi 5,000 kwa kila lita ya *Un-denatured Ethyl Alcohol* yenye kilevi cha asilimia 80 au zaidi inayozalishwa ndani ya nchi. Bidhaa hiyo inatambulika kwa HS Code 2207.10.00. Utozaji huo hautahusisha *Un-denatured Ethyl Alcohol* inayotumika kwa matumizi mengine yasiyohusu uzalishaji wa vilevi baada ya kupata ridhaa ya Waziri mwenye dhamana ya masuala husika. Aidha, viwango tofauti vinapendekezwa kwa lengo la kulinda viwanda vya ndani. Lengo la hatua hii ni kuongeza mapato ya Serikali. Hatua hii inatarajia **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi **milioni 154,550;**

iii. Kutoza Ushuru wa Bidhaa kwa kiwango cha asilimia 10 kwenye thamani ya dau la kamari (value of the stake on betting) kwenye Michezo ya Kubahatisha na Bahati Nasibu ya Taifa. Mapato yatakayokusanywa kutoka chanzo hiki ni kwa ajili ya kugharamia bima ya afya kwa watu wasio na uwezo na makundi maalum hususan wanawake wajawazito na watoto wa umri chini ya miaka mitano. Hatua hii inatarajia kupeleka kiasi cha shilingi **milioni 29,522** katika Mfuko huo;

iv. Kutoza Ushuru wa Bidhaa kwa kiwango cha asilimia 10 kwenye ada ya matangazo ya biashara za Michezo ya Kubahatisha na

Bahati Nasibu ya Taifa yanayotangazwa kupitia vituo vya televisheni, redio, na tasnia ya uchapishaji. Lengo la hatua hii ni kuongeza wigo wa kodi. Hatua hii inatarajia **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi **milioni 9,150;**

v. Kutoza Ushuru wa Bidhaa kwa kiwango cha Shilingi 300 kwa kilo ya *tomato sauce* na *tomato ketchup* (HS Code 2103.20.00), pamoja na *chilli sauce* na *chilli ketchup* (*HS Code* 2103.90.00) zile zinazotoka nje ya nchi. Lengo la hatua hii ni kuongeza mapato ya Serikali na kupata fedha za fidia ya athari hasi zinazotokana na matumizi ya sukari na chumvi iliyopo katika bidhaa hizo. Hatua hii inatarajia **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi **milioni 634;**

vi. Kutoza Ushuru wa Bidhaa kwa kiwango cha Shilingi 500 kwa kilo moja ya rangi za mafuta (solvent based paints and vanishes) zinazotoka nje ya nchi. Rangi hizo zinatambulika kwa *heading* 32.08. Lengo la hatua hii ni kuongeza mapato ya Serikali na kupata fedha za fidia ya athari hasi zinazotokana na matumizi ya bidhaa hizo. Hatua hii inatarajia **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi **milioni 2,433;**

vii. Kutoza Ushuru wa Bidhaa kwa kiwango cha Shilingi 963.90 kwa lita ya bia isiyochujwa, yaani *opaque* ya mfano wa Kibuku (HS Code 2206.00.20) zinazoingizwa kutoka nje ya nchi, na Shilingi 2,959.74 kwa lita ya pombe zenye mchanganyiko wa matunda (HS Code 2206.00.90) zinazotoka nje ya nchi. Lengo la hatua hii kuleta usawa katika utozajiKodi. Hatua hii inatarajia **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi **milioni 327**;

viii. Kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura 147 ili kuelekeza asilimia 2 ya mapato ya Ushuru wa Bidhaa yanayokusanywa kutoka kwenye bidhaa za urembo, vinywaji laini (carbonated drinks) na vileo (bia na pombe kali) kwenye Bima ya Afya kwa wote. Lengo la hatua hii ni kuongeza fedha zitakazotumika kwa ajili ya kugharamia bima ya afya kwa watu wasio na uwezo na makundi maalum hususan wanawake wajawazito na watoto wa umri chini ya miaka mitano.

Hatua hii inatarajia kupeleka kiasi cha shilingi **milioni 18,800** katika Mfuko huo; na

ix. Kuweka takwa kwenye Kanuni za Stempu ya Kodi Kielektroniki za mwaka 2018, linaloelekeza Leseni ya uzalishaji wa bidhaa zinazotozwa Ushuru wa Bidhaa kutolewa baada ya mfumo wa kutoa stempu za kielektroniki kusimikwa na kiwanda kuanza uzalishaji. Takwa hili litaenda sambamba na ukaguzi utakaokuwa ukifanyika mara kwa mara ili kuhakikisha bidhaa zote zinazozalishwa zinawekwa stempu za kielektroniki na kulipiwa kodi stahiki. Lengo la hatua hii ni kulinda viwanda vya ndani dhidi ya biashara ya bidhaa feki sokoni, kuboresha usimamizi wa ukusanyaji wa ushuru wa bidhaa na kuzuia upotevu wa mapato ya Serikali.

Hatua hizi za Ushuru wa Bidhaa kwa ujumla wake zinatarajiwa **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi **milioni 196,142.**

i. Kuongeza kiwango cha *currency points* kutoka shilingi 15,000 hadi shilingi 20,000. Lengo la hatua hii ni kuakisi mabadiliko ya thamani ya mapato ya Serikali kwa kuwa utozaji wa *currency point* kwa kutumia kiwango maalum (specific rates) usiporekebishwa hupoteza thamani ya fedha na hivyo kupunguza mapato ya Serikali. Njia bora inayotumika kuondoa mapungufu hayo ni kurekebisha kiwango hicho ili kuendana na thamani ya fedha; na

ii. Kufanya marekebisho kwenye Kifungu cha 86(1) cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi kwa kuweka ukomo wa faini ya juu ya kosa la kutokutoa risiti wa kiasi cha *currency points* 1000 (sawa na shilingi 15,000,000). Lengo la hatua hii ni kuleta unafuu kwa walipakodi na kuchochea ulipajikodi kwa hiari.

**4. Sheria ya Kuendeleza Ufundi Stadi, SURA 82**

**142**. ***Mheshimiwa Spika,*** Kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Kuendeleza Ufundi Stadi, Sura 82 ili kutokujumuisha gharama za vibarua wanaotumika katika utekelezaji wa miradi ya maji inayosimamiwa na Mamlaka za Maji katika wigo wa kukokotoa Kodi

ya Kuendeleza Ufundi Stadi. Lengo la hatua hii ni kupunguza gharama za utekelezaji wa miradi na kuongeza ufanisi wa usambazaji wa maji nchini.

**5. Sheria ya Serikali za Mitaa ya Utozaji wa Kodi ya Majengo, SURA 289**

**143**. ***Mheshimiwa Spika,*** Napendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Serikali za Mitaa ya Utozaji wa Kodi ya Majengo, Sura 289 ili kuelekeza asilimia 20 ya mapato yanayokusanywa kutoka kwenye kodi ya majengo na kodi ya pango la ardhi ipelekwe moja kwa moja kwenye akaunti za Mamlaka ya Serikali za Mitaa (Halmashauri) husika badala ya utaratibu wa sasa ambapo mapato yote yanaingia Mfuko Mkuu wa Serikali na kisha Halmashauri kuomba kurejeshewa asilimia 20 ya mapato hayo. Lengo la hatua hii ni kuwezesha Mamlaka ya Serikali za Mitaa kugharamia masuala ya ufatiliaji na ukusanyaji wa Kodi ya Majengo na Kodi ya Pango la Ardhi kwa ufanisi na kwa wakati.

**6. Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania, SURA 197;**

**144**. ***Mheshimiwa Spika,*** Napendekeza kufanya marekebisho kwenye vifungu vya 32(2)(b); 35(1); 41 na 42(2) vya Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania, Sura 197 kwa kuongeza maneno *‘ return’ or ‘ profit’* katika vifungu hivyo. Lengo la hatua hii ni kuwezesha benki na taasisi za fedha zisizo toza riba kutumia fursa zinazotolewa kama ilivyo kwa benki na taasisi zinazotoa huduma za kibenki kwa kufuatia mfumo wa kawaida wa kibenki.

**7. Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha, SURA 342**

**145**. ***Mheshimiwa Spika,*** Napendekeza kufanya marekebisho kwenye kifungu cha 24(g)(iv) cha Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha, Sura 342 kwa kuongeza maneno *‘ return’ or ‘ profit’* . Lengo la hatua hii ni kuruhusu benki zisizo toza riba kufanya biashara kwa kutumia akaunti zao au akaunti za wateja kwenye hati zinazotumika kuzalisha.

**8. Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha, SURA 407**

**146.** ***Mheshimiwa Spika,*** Napendekeza kufanya marekebisho kwenye kifungu cha 4(3) cha Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania, Sura 407 kwa kuongeza maneno *' return' or ' profit'* ili kuwezesha taasisi au makampuni yanayojihusisha na utoaji wa huduma ndogo za fedha kuweza kutoa huduma hizo kwa misingi ya kutotoza riba.

**9. Sheria ya Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma, Mwaka 2018.**

**147.** ***Mheshimiwa Spika,*** Napendekeza kufanya maamuzi ya muda mfupi ya kugharamia malipo ya nyongeza ya mkupuo kwa asilimia 7 ili kufikia asilimia 40 kwa kundi ambalo lilikuwa linalipwa asilimia 50 kabla ya kuunganishwa kwa mifuko ya pensheni. Vile vile, napendekeza kuongeza kikokotoo kwa asilimia 2 ili kufikia asilimia 35 kwa kundi ambalo lilikuwa linalipwa asilimia 25 kabla ya kuunganishwa kwa mifuko ya pensheni. Nyongeza hizo zitaanza kulipwa kwa wastaafu waliostaafu kuanzia mwaka 2022/23 na kuendelea hadi watakaostaafu mwaka 2029/30 na baada ya hapo mfuko wa PSSSF uchukue jukumu la kuendelea kuwalipa mafao. Lengo la hatua hii ni kutoathiri mfumo mzima wa pensheni kwa kuwa na uwiano wa mafao kwa wanachama na kuupa Mfuko muda wa kuangalia uhimilivu wake. Hatua hii inatarajiwa **kupunguza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi **milioni 155,400.**

**10. Sheria ya Ushuru wa Barabara na Mafuta, SURA 220**

**148.** ***Mheshimiwa Spika,*** Napendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Ushuru wa Barabara na Mafuta, Sura 220 ili kutoza shilingi 382 kwa kila kilo ya gesi asilia inayotumika kwenye magari. Lengo la hatua hii ni kuongeza mapato yatakayotumika katika kufanya matengenezo ya barabara pamoja na kuleta usawa kwa kuwa magari yanayotumia mafuta tayari yanachangia mapato kwa ajili ya matengenezo ya miundombinu ya barabara. Mapato yatakayotokana na chanzo hiki yatapelekwa Mfuko wa Barabara.

Hatua hii inatarajia kuongeza Mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi **milioni 9,500.**

**149.** ***Mheshimiwa Spika,*** Napendekeza pia Kuweka utaratibu wa kutenga fedha kwa ajili ya maendeleo ya miundombinu ya barabara katika kipindi ambacho kutakuwa na punguzo la bei ya mafuta ya petroli sokoni ambapo badala ya bei hizo kushuka fedha hizo zitaelekewa kwenye Mfuko wa Barabara. Utaratibu huu utatekelezwa na Kamati Maalum itakayoundwa na Waziri mwenye dhamana ya masuala ya Nishati kwa kushirikiana na Waziri mwenye dhamana ya masuala ya Fedha kwa lengo la kupendekeza kiasi kitakachotengwa kwa kuzingatia wastani wa bei iliyopo sokoni. Aidha, mapato yatakayotokana na utaratibu huu yatapelekwa Mfuko wa Barabara. Lengo la hatua hii ni kuongeza mapato ya Serikali yatakayotumika katika ujenzi na uboreshaji wa miundombinu ya barabara nchini.

**11. Sheria ya Bandari, Mwaka 2004**

**150.** ***Mheshimiwa Spika***, napendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Bandari ya mwaka 2004 ili kurejesha jukumu la kukusanya tozo ya matumizi ya miundombinu ya bandari (wharfage) kwa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA). Aidha, mapato yatakayotokana na tozo hizo yatawekwa katika akaunti maalum ya TPA iliyopo Benki Kuu ya Tanzania na matumizi yake yatafanyika baada ya kuomba na kupata idhini ya Mlipaji Mkuu wa Serikali. Lengo la hatua hii ni kuiwezesha Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania kupata fedha kwa wakati kwa ajili ya maboresho ya miundombinu ya Bandari na hivyo kuongeza ufanisi wake.

**12. Sheria ya Sukari, Namba 6**

**151**. ***Mheshimiwa Spika,*** Napendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Sukari, Namba 6 kama ifuatavyo:

i. Kuiwezesha Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) kununua kuratibu na kuhifadhi pengo la sukari kwenye hifadhi ya chakula ya Taifa. Lengo la hatua hii ni kuwezesha upatikanaji wa Sukari nchini na kuondoa uhodhi kwa baadhi ya wenye viwanda bila kuathiri dhamira ya Serikali ya kulinda viwanda vya ndani;

ii. Kufanya marekebisho kwenye kanuni ya NFRA kwa kuijumuisha sukari kuwa sehemu ya usalama wa chakula; na

iii. Kutoza shilingi 50 kwa kilo ya mabaki (by products) yanayotakana na uzalishaji wa sukari. Lengo la hatua hii ni kuongeza mapato yatakayoiwezesha Bodi ya Sukari kutekeleza majukumu yake ikiwemo kuendeleza mafunzo na kukuza ujuzi katika sekta ya sukari pamoja na kusimamia uzalishaji wa sukari nchini kupitia upanuzi wa viwanda vilivyopo na kuhamasisha uwekezaji mpya.

**13. Sheria ya Korosho, Namba 18**

**152.** ***Mheshimiwa Spika,*** napendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Korosho ili mapato yatokanayo na tozo ya kusafirisha korosho ghafi nje ya nchi yapelekwe Bodi ya Korosho kwa asilimia 100 kwa kipindi cha miaka mitano. Lengo la hatua hii ni kuchochea maendeleo ya Sekta ya kilimo na kusaidia upatikanaji wa rasilimali fedha kwa ajili ya ruzuku na tafiti pamoja na kuongeza mchango wa zao katika ukuaji wa uchumi wa nchi.

**153.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile ninapendekeza kuipa Mamlaka ya Mapato Tanzania jukumu la kukusanya tozo za kusafirisha mazao nje ya nchi na tozo za kuingiza mazao nchini pamoja na kubainisha mgawanyo wa mapato yatokanayo na tozo hizo kama ifuatavyo: asilimia 70 pelekwe mfuko wa kilimo (ADF); na asilimia 30 ipelekwe mfuko mkuu wa Serikali. Lengo la hatua hii ni kuongeza ufanisi katika ukusanyaji, kuchochea maendeleo ya Sekta ya kilimo na kusaidia upatikanaji wa rasilimali fedha kwa ajili ya majukumu mbalimbali ya Serikali.

## 14. Sheria ya Madini, SURA 123

**154**. ***Mheshimiwa Spika***, Napendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Madini, Sura 123 kama ifuatavyo:

i. Kufanya marekebisho kwenye Kifungu cha 90A (3) cha Sheria ya Madini, SURA 123 ili kutoa msamaha kwa Benki Kuu ya Tanzania wa kulipa ada ya ukaguzi ya asilimia 1. Lengo la hatua hii ni kupunguza gharama za ununuaji wa madini na kuhamasisha uuzaji wa dhahabu kwa Benki ya Tanzania ili kuongeza akiba ya nchi ya fedha za kigeni kwa lengo la kupunguza tatizo la upatikanaji wa dola zinazotumika kwa ajili ya majukumu mbalimbali;

ii. Kupunguza mrabaha unaotozwa kwenye madini ya dhahabu yatakayouzwa kwa Benki Kuu ya Tanzania kutoka asilimia sita (6) hadi asilimia mbili (4) . Marekebisho haya yanaenda sambamba na kuweka takwa la malipo ya mrabaha unaolipwa kwenye madini ya dhahabu yanayouzwa kwa Benki Kuu ya Tanzania kuwa ni malipo ya mwisho (final payments). Lengo la hatua hii ni kuhamasisha uuzaji wa dhahabu kwa Benki Kuu ya Tanzania kwa lengo la kuongeza akiba ya nchi ya fedha za kigeni na kupunguza tatizo la upatikanaji wa dola zinazotumika kwa ajili ya majukumu mbalimbali. Vile vile, hatua hii inalenga kuleta usawa baina ya vituo vya kusafishia madini (refineries) na Benki Kuu ya Tanzania kwa kuwa tayari vituo hivyo vinanufaika na msamaha;

iii. Kuweka takwa la wamiliki wa leseni za uchimbaji wa madini na wafanyabiashara wa madini kutenga kiasi cha madini kwa ajili ya kuchakatwa, kuyeyushwa, kusafishwa na kuuzwa nchini. Aidha, kiasi kitakachopaswa kutengwa kitabainishwa na Waziri mwenye dhamana ya masuala ya madini kwenye Kanuni za Masoko ya Madini za mwaka 2019 ambapo kwa kuanzia kiasi cha asilimia 20 ya sehemu ya dhahabu inayozalishwa nchini kitapaswa kutengwa.
Aidha, takwa hili halitahusisha Kampuni za Uchimbaji wa Madini zilizoingia mikataba na Serikali kwa lengo la kutekeleza miradi ya uchimbaji wa madini ya dhahabu nchini ili kuheshimu makubaliano hayo. Serikali itafanya majadiliano na Kampuni hizo ili kuona

uwezekano wa kutekeleza takwa la kutenga kuanzia asilimia 20. Hatua hii inalenga kuongeza akiba ya fedha za kigeni nchini na kupunguza tatizo la uhaba wa dola zinazotumika kwa ajili ya majukumu mbalimbali. Vile vile, hatua hii inalenga pia kuchochea ukuaji wa viwanda vya kusafisha madini kwa kuhakikisha vinapata dhahabu ya kusafisha ikiwa ni moja ya hatua za kupata ithibati za kimataifa; na

iv. Kuitambua Benki Kuu ya Tanzania kama mnunuzi wa madini nchini. Lengo la hatua hii ni kuondoa mkinzano uliopo baina ya Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania na Sheria ya Madini na kuiwezesha Benki Kuu ya Tanzania kutekeleza jukumu lake la kisheria la kununua madini ya dhahabu kwa ajili ya kuongeza akiba ya nchi ya fedha za kigeni.

Hatua hizi kwa pamoja zinatarajia **kupunguza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi **milioni 114,519.**

**15. Sheria ya Michezo ya Kubahatisha, SURA 41.**

**155**. ***Mheshimiwa Spika,*** napendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Michezo ya Kubahatisha, Sura 41 kama ifuatavyo:

i. Kuanzisha ada ya maombi ya cheti cha uwakala (dealer' s certificate) wa michezo ya kubahatisha ya shilingi 10,000 na ada ya cheti ya shilingi 20,000.
Lengo la hatua hii ni kuongeza mapato yatakayowezesha ufanisi na udhibiti bora wa watu binafsi au mawakala wanaofanya biashara katika tasnia ya michezo ya kubahatisha;

ii. Kuanzisha ada ya usajili wa vituo vya bahati nasibu ikiwemo Bahati Nasibu ya Taifa kwa kiwango cha shilingi 30,000. Lengo la hatua hii ni kuongeza mapato yatokanayo na Bahati Nasibu ya Taifa yatakayowezesha ufanisi na udhibiti bora wa michezo ya kubahatisha; na

iii. Kuanzisha ada ya leseni ya uuzaji au usambazaji wa tokeni zinazotumika kwenye mashine za sloti kwa kiasi cha shilingi 500,000 ikiwa ni ada ya maombi ya leseni, na shilingi 1,000,000 ikiwa ada ya leseni kwa mwaka. Lengo la hatua hii ni kuongeza mapato yatakayowezesha Bodi ya Michezo ya Kubahatisha kuongeza ufanisi na udhibiti wa tasnia ya michezo ya kubahatisha.

Hatua hizi kwa pamoja zinatarajia **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi **milioni 180.**

**16. Sheria ya Reli, ya Mwaka 2017**

**156**. ***Mheshimiwa Spika,*** Napendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Reli ya mwaka 2017 kwa kuongeza kiwango cha Tozo ya Maendeleo ya Reli (Railway Development Levy) kinachotozwa kwa bidhaa zote zinazoingia na kutumika nchini kutoka asilimia 1.5 ya thamani ya mzigo (CIF) hadi asilimia 2 ya thamani ya mzigo (CIF). Aidha, asilimia 50 ya mapato yatakayotokana na chanzo hicho yatapelekwa kwenye Mfuko wa Maendeleo ya Reli na asilimia 50 itapelekwa kwenye Mfuko wa Barabara. Lengo la hatua hii ni kuongeza mapato yatakayotumika katika kuboresha na kujenga miundombinu ya reli na barabara zilizoathiriwa na mvua za El-Nino. Hatua hii inatarajia **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi **milioni 216,898;**

**17. Sheria ya Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania SURA 157**

**157**. ***Mheshimiwa Spika***, Napendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Sura 157 kama ifuatavyo:

i. Kuanzisha ada ya matumizi ya huduma mahsusi za hali ya hewa katika shughuli za ujenzi ya shilingi 500,000/= kwa mradi wenye thamani kuanzia milioni 500 hadi bilioni 1; ada ya shilingi 1,500,000 kwa mradi wenye thamani kuanzia shilingi bilion 1.1 hadi bilioni 10; na ada ya shilingi 5,000,000 kwa mradi wenye

thamani zaidi ya bilion 10. Lengo la hatua hii ni kuongeza mapato yatakayowezesha utoaji wa huduma mahsusi za hali ya hewa kwa lengo la kuongeza ufanisi wa utendaji kazi na kuboresha usalama wa watu na mali katika maeneo ya miradi/ujenzi. Hatua hii inatarajia **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi **milioni 1,600**; na

ii. Kuanzisha ada ya matumizi ya huduma mahsusi za hali ya hewa katika shughuli za usimamizi wa rasilimali maji kwa kiwango cha shilingi 500,000 kwa mwezi kwa kila Bodi ya Maji ya Bonde yenye uwezo mkubwa kifedha na shilingi 200,000 kwa mwezi kwa kila Bodi ya Maji ya Bonde yenye uwezo mdogo kifedha. Lengo la hatua hii ni kuongeza mapato yatakayowezesha utoaji wa huduma mahsusi za hali ya hewa kwa ufanisi kwenye mabonde ya maji pamoja na kuboresha utendaji kazi kwa kuongeza ufanisi katika usimamizi wa rasilimali maji. Hatua hii inatarajia **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi **milioni 36.**

**18. Sheria ya Magari (Ada ya Usajili na Uhamishaji), SURA 124**

**158**. ***Mheshimiwa Spika***, Napendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Magari (Ada ya Usajili na Uhamishaji) Sura 124 kwa kujumuisha magari ya umeme kwenye wigo wa ulipaji wa ada ya usajili wa magari. Lengo la hatua hii ni kuzingatia kanuni za usawa za utozaji wa kodi na kuendana na mabadiliko ya teknolojia.

**19. Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya mwaka 2004**

**159. *Mheshimiwa Spika*,** Napenda kukufahamisha kwamba, kikao cha Mawaziri wa Fedha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki cha Maandalizi ya Bajeti (EAC Pre-Budget Consultative Meeting of Ministers of Finance) kilichofanyika tarehe 17 Mei 2024 jijini Arusha, pamoja na masuala mengine kilipendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Usimamizi wa Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya mwaka 2004 pamoja na Viwango vya Pamoja vya

Ushuru wa Forodha vya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC Common External Tariff) kwa mwaka wa Fedha 2024/25. Mapendekezo hayo yanalenga kuendeleza mageuzi ya kiuchumi kupitia uimarishaji wa Sera za bajeti na uwekezaji katika kuhimili na kukabiliana na mabadiliko ya Tabianchi kwa maendeleo ya wananchi.

**160.** ***Mheshimiwa Spika,*** mapendekezo ya Mawaziri wa Fedha ya kufanya marekebisho kwenye Viwango vya Pamoja vya Ushuru wa Forodha yanahusisha hatua mpya na zinazoendelea ambazo zimekuwa zikitekelezwa katika Mwaka wa Fedha 2023/24. Hatua hizo ni kama zifuatazo:

i. Mapendekezo ya hatua mpya za Viwango vya Ushuru wa Forodha ni kama ifuatavyo: -

a. Kutoa unafuu wa Ushuru wa Forodha kwa utaratibu wa *Duty Remission* kwa kiwango cha asilimia 0 badala ya asilimia 25 kwa mwaka mmoja kwenye betri za umeme (Lithium-ion Electric accumulators) zinazotambulika kwa HS Code 8507.60.00 zinazotumiwa na wazalishaji au waunganishaji wa magari na pikipiki nchini. Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu pamoja na kuchochea uwekezaji katika uzalishaji au uunganishaji wa magari na pikipiki hapa nchini ili kuwezesha upatikanaji wa bidhaa ya mwisho kwa bei nafuu;

b. Kutoa unafuu wa Ushuru wa Forodha kwa utaratibu wa *Duty Remission* kwa kiwango cha asilimia 0 badala ya asilimia 10 kwa mwaka mmoja kwenye runinga ambazo hazijaunganishwa (Unassembled Television (CKD)) zinazotambulika kwa HS Codes 8528.72.10; 8528.73.10. Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu kwa waunganishaji wa runinga nchini ili kurahisisha upatikanaji wa bidhaa hiyo kwa gharama nafuu, kuongeza ajira pamoja na kuhamasisha uwekezaji nchini;

c. Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zimekubaliana kutoa unafuu wa Ushuru wa Forodha kwa

utaratibu wa *Duty Remission* kwa kiwango cha asilimia 0 kwenye malighafi (inputs) zinazotumika katika uzalishaji au uunganishaji wa simu za mkononi. Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu kwa wazalishaji na waunganishaji wa simu ndani ya Jumuiya ili kurahisisha upatikanaji wa bidhaa hiyo kwa gharama nafuu, kuongeza ajira pamoja na kuhamasisha uwekezaji;

d. Kutoa unafuu wa Ushuru wa Forodha kwa utaratibu wa *Duty Remission* kwa kiwango cha asilimia 10 badala ya asilimia 25 kwa mwaka mmoja kwenye karatasi zinazotambulika kwa HS Code 4811.90.00 zinazotumiwa na wazalishaji wa lebo na karatasi za kutolea risiti za kielektroniki. Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu wa ushuru wa forodha kwenye viwanda vinavyotumia malighafi hii;

e. Kutoa unafuu wa Ushuru wa Forodha kwa utaratibu wa *Duty Remission* kwa kiwango cha asilimia 10 badala ya asilimia 35 kwa mwaka mmoja kwenye malighafi za kutengeneza vioo vigumu (toughened glass) zinazotambulika kwa HS Codes 7005.10.00; 7005.21.00; 7005.29.00; na 7005.30.00. Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu kwa watengenezaji wa vioo hivyo nchini;

f. Kutoa unafuu wa Ushuru wa Forodha kwa utaratibu wa *Duty Remission* kwa kiwango cha asilimia 0 badala ya asilimia 25 au asilimia 35 kwa mwaka mmoja kwenye vifungashio vinavyotumiwa na wazalishaji wa maziwa kwa joto la juu yanayodumu kwa muda mrefu (UHT Milk), *yoghurt* na maziwa ya unga vinavyotambulika kwa HS codes 3923.50.90; 4819.20.90; 4819.30.00; 4819.50.00; 4821.90.00; 7607.19.90. Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu kwa wazalishaji wa maziwa hapa nchini, kuongeza ajira pamoja na kuhamasisha uwekezaji kwenye sekta ya maziwa nchini;

g. Kutoa unafuu wa Ushuru wa Forodha kwa utaratibu wa *Duty Remission* kwa kiwango cha asilimia 0 kwa mwaka

mmoja kwenye malighafi zinazotumiwa na wazalishaji wa *Optical Fiber Cables* zinazotambulika kwa HS codes 3215.19.00; 3403.99.00; 3506.91.00; 3818.00.00;3907.99.00;3907.99.00;3916.90.00;3917.39.00;3919.90.90;3920.69.90; 3920.99.90;3921.14.90; 3921.90.90; 5402.11.00;5404.90.00; 7019.90.90; 8536.90.00; 8544.49.00. Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu kwa wazalishaji wa *Optical Fiber Cables* hapa nchini ili kurahisisha upatikanaji wa mawasiliano kwa gharama nafuu, kuongeza ajira pamoja na kuhamasishauwekezaji kwenye sekta ya mawasiliano;

h. Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zimekubaliana kutoa unafuu wa Ushuru wa Forodha kwa utaratibu wa *Duty Remission* kwa kiwango cha asilimia 0 kwenye malighafi (inputs) zinazotambulika kwa HS Codes 4817.30.00; 4819.10.00; 5407.51.00; 3921.19.90 zinazotumika katika uzalishaji dawa za mbu (mosquito repelants). Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu kwa wazalishaji wa dawa hizo ndani ya Jumuiya ili kurahisisha upatikanaji wa bidhaa hiyo kwa gharama nafuu, kuongeza ajira, kuhamasisha uwekezaji pamoja na kuongeza juhudi za kupambana dhidi ya malaria;

i. Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zimekubaliana kutoa unafuu wa Ushuru wa Forodha kwa utaratibu wa *Duty Remission* kwa kiwango cha asilimia 10 badala ya asilimia 25 kwenye malighafi (inputs) zinazotambulika kwa HS Code 2106.90.20 zinazotumika kwenye uzalishaji wa vyakula na vinywaji. Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu kwa wazalishaji wa vyakula na vinywaji ndani ya Jumuiya;

j. Kutoza Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha asilimia 35 badala ya asilimia 10 kwenye vioo vya kawaida na vigumu (float, toughened and multiple-walled insulating units of glass) vinavyotambulika kwa HS Codes 7005.10.00; 7005.21.00; 7005.29.00; 7005.30.00; 7007.19.00; 7007.29.00 na 7008.00.00 kwa mwaka mmoja. Hatua hii inalenga kulinda

wazalishaji wa vioo hivyo hapa nchini ili viweze kuwa shindani dhidi ya vioo kutoka nje ya nchi;

k. Kutoza Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha asilimia 35 au dola za Marekani 3.0 kwa kila mita moja ya mraba (square meter) kutegemea kiwango kitakachokuwa kikubwa badala ya asilimia 35 pekee kwa mwaka mmoja kwenye marumaru zinazotambulika kwa HS Codes 6907.21.00; 6907.22.00; na 6907.23.00. Lengo la hatua hii ni kulinda viwanda vya ndani vinavyozalisha marumaru, pamoja na kudhibiti udanganyifu wa thamani halisi ya bidhaa hizo kutoka nje;

l. Kutoza Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha asilimia 25 au dola za Marekani 300 kwa kila tani moja ya ujazo (metric ton) kutegemea kiwango kitakachokuwa kikubwa badala ya ushuru wa asilimia 25 au dola za Marekani 200 kwa kila tani moja ya ujazo (metric ton) kwa mwaka mmoja kwenye bidhaa za mabati zinazotambulika kwa HS codes 7210.49.00; 7210.61.00; 7210.69.00; 7210.70.00; 7210.90.00; na 7212.30.00. Lengo la hatua hii ni kulinda viwanda vya ndani, kuongeza ajira pamoja na mapato ya Serikali;

m. Kutoza Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha asilimia 25 au dola za Marekani 300 kwa kila tani moja ya ujazo (metric ton) kutegemea kiwango kitakachokuwa kikubwa badala ya asilimia 35 kwa mwaka mmoja kwenye bidhaa za mabati zinazotambulika kwa HS codes 7212.40.00; na 7212.50.00. Lengo la hatua hii ni kulinda viwanda vya ndani, kuongeza ajira pamoja na mapato ya Serikali;

n. Kutoza Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha asilimia 10 au dola za Marekani 300 kwa kila tani moja ya ujazo (metric ton) kutegemea kiwango kitakachokuwa kikubwa badala ya asilimia 10 kwa mwaka mmoja kwenye bidhaa za mabati zinazotambulika kwa HS code 7212.60.00. Lengo la hatua hii

ni kulinda viwanda vya ndani, kuongeza ajira pamoja na mapato ya Serikali;

o. Kutoza Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha asilimia 25 au dola za Marekani 300 kwa kila tani moja ya ujazo *(metric ton)* kutegemea kiwango kitakachokuwa kikubwa badala ya kiwango cha asilimia 10 kwenye bidhaa za chuma zinazotambulika kwa HS Codes 7225.91.00; 7225.92.00; na 7225.99.00 kwa mwaka mmoja. Lengo la hatua hii ni kulinda viwanda vinavyozalisha nondo hapa nchini, kuongeza ajira pamoja na mapato ya Serikali;

p. Kutoza Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha asilimia 35 au dola za Marekani 500 kwa kila tani moja ya ujazo *(metric ton)* kutegemea kiwango kitakachokuwa kikubwa badala ya kiwango cha asilimia 35 kwenye mabati yanayotambulika kwa HS Codes 7210.41.00 kwa mwaka mmoja. Lengo la hatua hii ni kulinda viwanda vinavyozalisha mabati hayo ndani ya nchi, kuongeza ajira pamoja na mapato ya Serikali;

q. Kutoza Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha asilimia 50 badala ya kiwango cha asilimia 35 au asilimia 25 kwenye chumvi inayotambulika kwa *Heading* 25.01 kwa mwaka mmoja. Lengo la hatua hii ni kulinda wazalishaji wa chumvi nchini;

r. Kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia 10 au dola za Marekani 300 kwa kila tani moja *(Metric ton)* kutegemea kiwango kitakachokuwa kikubwa kwenye bidhaa za chuma zinazotambulika kwa HS Code 7226.99.00 kwa mwaka mmoja badala ya ushuru wa asilimia 10 pekee. Lengo la hatua hii ni kulinda viwanda vya ndani, kuongeza ajira, kuvutia uwekezaji, kuongeza mapato ya Serikali pamoja na kudhibiti udanganyifu wa thamani halisi ya bidhaa hizo kutoka nje;

s. Kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia 35 au dola za Marekani 500 kwa kila tani moja ya ujazo *(Metric ton)* kutegemea

kiwango kitakachokuwa kikubwa badala ya asilimia 35 kwa mwaka mmoja kwenye mafuta ya kula yaliyochakatwa kwa kiwango cha mwisho (refined edible oils) yanayotambulika kwa HS codes 1507.90.00; 1508.90.00; 15.09; 15.10; 1511.90.30;1511.90.90;1512.19.00;1512.29.00;1513.19.00;1513.29.00; 1514.19.00; 99.00; 1515.19.00; 1515.29.00; 50.00; 1515.60.00 na 1515.90.00. Lengo la hatua hii ni kulinda viwanda vya ndani na kuhamasisha uchakataji wa mbegu na mafuta ghafi yaliyoingizwa nchini ili kuongeza thamani ya bidhaa (value addition), kukuza ajira, pamoja na kuongeza mapato ya Serikali; na

t. Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zimekubaliana kufanya marekebisho kwenye muundo wa *tariff lines* za magari yanayotumia nishati ya umeme na mafuta (hybrid) zinazotambulika kwenye HS Codes 8703.40.00; 8703.50.00; 8703.60.00; na 8703.70.00 ili magari yanayoingizwa nchini yakiwa hayajaunganishwa (unassembled) yatozwe ushuru wa forodha kwa kiwango cha asilimia 0. Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu kwa waunganishaji wa magari hayo nchini na kuhamasisha uwekezaji.

ii. Mapendekezo ya kuendelea na utekelezaji wa Viwango vya Ushuru wa Forodha vya mwaka 2023/24 ni kama ifuatavyo:

a. Kupunguza Ushuru wa Forodha kutoka asilimia 10 hadi asilimia 0 kwa mwaka mmoja kwenye mashine za kielektroniki zinazotumika kukusanya mapato ya Serikali *(Cash registers, Electronic Fiscal Device (EFD) Machines and Point of Sale (POS)* machines) zinazotambulika kwa HS Codes 8470.50.00 na 8470.90.00. Lengo la hatua hii ni kuhamasisha matumizi ya vifaa hivi katika kuhasibu mapato ya Serikali;

b. Kutoa unafuu wa Ushuru wa Forodha kwa utaratibu wa *Duty Remission* kwa kiwango cha asilimia 0 badala ya asilimia 10 kwa mwaka mmoja kwenye vifuniko vya chupa za mvinyo (corks and stoppers) vinavyotambulika kwa HS Code 4503.10.00. Hatua

hii inalenga kuwapunguzia gharama wazalishaji wa mvinyo ili kuhamasisha na kuendeleza kilimo cha zao la zabibu nchini pamoja na kuongeza ajira;

c. Kutoza Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha asilimia 10 badala ya asilimia 0 kwa mwaka mmoja kwenye unga wa kakao unaoingizwa kutoka nje unaotambulika kwa HS Code 1805.00.00. Lengo la hatua hii ni kuhamasisha kilimo cha zao la kakao nchini pamoja na kuongeza mapato ya Serikali;

d. Kutoa unafuu wa Ushuru wa Forodha kwa utaratibu wa *Duty Remission* kwa kiwango cha asilimia 0 badala ya asilimia 25 kwa mwaka mmoja kwenye vifungashio vya kuhifadhia kahawa vinavyotambulika kwa HS codes 7310.21.00; 6305.10.00; 3923.50.10; 3923.50.90 na 3920.30.90 vinavyotumiwa na viwanda vya kusaga kahawa nchini. Hatua hii inalenga kuongeza thamani kwenye zao la kahawa na kutoa unafuu wa gharama kwenye viwanda vinavyosaga kahawa hapa nchini;

e. Kutoa unafuu wa Ushuru wa Forodha kwa utaratibu wa *Duty Remission* kwa kiwango cha asilimia 0 badala ya asilimia 25 kwa mwaka mmoja kwenye vifungashio vya kuhifadhia korosho vinavyotambulika kwa HS code 3923.21.00. Hatua hii inalenga kuongeza thamani katika zao la korosho na kupunguza gharama kwenye viwanda vinavyochakata korosho hapa nchini;

f. Kutoa unafuu wa Ushuru wa Forodha kwa utaratibu wa *Duty Remission* kwa kiwango cha asilimia 0 badala ya asilimia 25 kwa mwaka mmoja kwenye vifungashio vya kuhifadhia pamba (cotton lint) vinavyotambulika kwa HS codes 3920.30.90; 6305.39.00 na 7217.90.00. Hatua hii inalenga kuvutia uwekezaji ili kuongeza thamani ya zao la pamba nchini;

g. Nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zimekubaliana kuendelea kutoa unafuu wa Ushuru wa Forodha kwa utaratibu wa *Duty Remission* kwa kiwango cha asilimia 0

badala ya asilimia 10 au asilimia 25 kwenye malighafi mbalimbali za kutengeneza taulo za kike pamoja na taulo za watoto. Hatua hii inalenga kutoa unafuu wa gharama za uzalishaji na kuongeza ajira;

h. Kutoa unafuu wa Ushuru wa Forodha kwa utaratibu wa *Duty Remission* kwa kiwango cha asilimia 0 badala ya asilimia 25 kwa mwaka mmoja kwenye vifungashio vya mbegu vinavyotambulika kwa HS codes 3923.29.00; 6305.10.00; 4819.40.00; 7310.29.90; 6305.33.00; 6305.20.00; 6304.91.90 na 7607.19.90. Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu kwa wazalishaji wa mbegu hapa nchini;

i. Kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia 10 au dola za Marekani 125 kwa kila tani moja ya ujazo *(Metric ton)* kutegemea kiwango kitakachokuwa kikubwa badala ya ushuru wa asilimia 10 pekee kwenye bidhaa za chuma kwa mwaka mmoja. Bidhaa hizi zinatambulika kwa HS Codes 7209.16.00; 7209.17.00; 7209.18.00; 7209.25.00 7209.26.00; 7209.27.00; 7209.28.00; 7209.90.00; 7211.23.00; 7211.90.00; 7225.50.0 na 7226.92.00. Lengo la hatua hii ni kulinda viwanda vya ndani vinavyozalisha bidhaa hizo pamoja na kukuza ajira;

j. Kutoza Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha asilimia 25 au dola za Marekani 250 badala ya kiwango cha asilimia 25 au dola za Marekani 200 kwa kila tani moja ya ujazo *(metric ton)* kutegemea kiwango kitakachokuwa kikubwa kwenye bidhaa za chuma zinazotambulika kwa HS Codes 7213.10.00; 7213.20.00; 7213.99.00; 7306.30.00; 7306.50.00; 7306.61.00; 7306.69.00; na 7306.90.00 kwa mwaka mmoja. Lengo la hatua hii ni kulinda viwanda vinavyozalisha nondo hapa nchini, kuhamasisha uwekezaji, kuongeza ajira pamoja na mapato ya Serikali;

k. Kutoza Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha asilimia 10 badala ya asilimia 0 kwa mwaka mmoja kwenye fito za plastiki zijulikanazo kama *PVC Profiles* zinazotambulika kwa HS Codes 3916.10.00; 3916.20.00; na 3916.90.00 zinazotumika

kutengenezea fremu za milango, madirisha. Lengo la hatua hii ni kuongeza mapato ya Serikali;

l. Kutoza Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha asilimia 25 badala ya asilimia 10 kwa mwaka mmoja kwenye karatasi zinazotambulika kwa HS code 4804.29.00. Lengo la hatua hii ni kulinda viwanda vinavyozalisha karatasi hizo hapa nchini;

m. Kutoa unafuu wa Ushuru wa Forodha kwa utaratibu wa *Duty Remission* kwa kiwango cha asilimia 10 badala ya asilimia 35 kwa mwaka mmoja kwenye ngano inayotambulika kwa HS Codes 1001.99.10 na 1001.99.90. Lengo la hatua hii ni kupunguza gharama kwa Viwanda vinavyozalisha unga wa ngano;

n. Kutoa unafuu wa Ushuru wa Forodha kwa utaratibu wa *Duty Remission* kwa kiwango cha asilimia 0 badala ya asilimia 10 kwa mwaka mmoja kwenye malighafi ya kutengeneza sabuni ijulikanayo kama *RBD Palm Stearin* zinazotambulika kwa HS Code 1511.90.40 kwa viwanda vinavyotengeneza sabuni nchini. Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu kwa viwanda vya kuzalisha sabuni nchini;

o. Kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia 25 au dola za Marekani 1.35 kwa kila kilo moja ya viberiti *(safety match boxes)* vinavyotambuliwa kwenye HS code 3605.00.00 kutegemea kiwango kitakachokuwa kikubwa badala ya asilimia 25 pekee kwa mwaka mmoja. Lengo la hatua hii ni kulinda viwanda vinavyozalisha viberiti nchini dhidi ya bidhaa zenye ruzuku kutoka nje na hivyo kuwa na ushindani sawa katika soko;

p. Kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia 60 badala ya asilimia 35 kwa mwaka mmoja kwenye maji ya kunywa *(mineral water)* yanayotambulika kwa HS code 2201.10.00. Hatua hii inalenga kulinda viwanda vinavozalisha maji ya kunywa nchini;

q. Kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia 10 badala ya asilimia 0 kwenye *Gypsum Powder* inayotambulika kwa HS code

2520.20.00 kwa mwaka mmoja. Lengo la hatua hii ni kulinda wazalishaji wa *Gypsum Powder* nchini;

r. Kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia 35 badala ya asilimia 35 au dola za Marekani 0.40 kwa kilo moja kutegemea kiwango kitakachokuwa kikubwa kwa mwaka mmoja kwenye mitumba inayotambulika kwa HS Codes 6309.00.10; 6309.00.20; na 6309.00.90 inayoingia kutoka nje. Hatua hii inalenga kutoa unafuu kwa watumiaji wa bidhaa hii hapa nchini;

s. Kutoa unafuu wa Ushuru wa Forodha kwenye malighafi, vipuri na mashine vinavyotumika katika kutengeneza viatu vya ngozi na nguo. Lengo la hatua hii ni kuhamasisha ukuaji wa sekta ya nguo na viatu vya ngozi nchini;

t. Kutoza ushuru wa Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha asilimia 25 badala ya asilimia 10 kwa mwaka mmoja kwenye matairi mapya ya pikipiki (new pneumatic tyres of rubber) yanayotambulika kwa HS Code 4011.40.00. Lengo la hatua ni kuhamasisha uzalishaji wa matairi hayo nchini kwa kuwa kuna malighafi za kutosha;

u. Kupunguza Ushuru wa Forodha kutoka asilimia 25 hadi asilimia 0 kwa mwaka mmoja kwenye mikebe ya kubebea maziwa (milk cans) inayotambulika kwa HS Codes 7310.10.00 na 7310.29.90. Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu wa vifungashio vya kuhifadhia maziwa ili kuwalinda walaji nchini;

v. Kutoa unafuu wa Ushuru wa Forodha kwa utaratibu wa *Duty Remission* kwa kiwango cha asilimia 0 badala ya asilimia 10 au asilimia 25 kwa mwaka mmoja kwenye malighafi za kutengeneza sabuni (Organic surface-active agents) zinazotambulika kwa HS Codes 3402.31.00; 3402.39.00; 3402.49.00. Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu kwa wazalishaji wa sabuni za unga na maji nchini;

w. Kutoa unafuu wa Ushuru wa Forodha kwa utaratibu wa *Duty Remission* kwa kiwango cha asilimia 0 badala ya asilimia 25 au asilimia 10 kwa mwaka mmoja kwenye malighafi za kuchakata ngozi zinazotambulika kwa HS Codes 3208.20.10; 3208.20.20; 3208.90.20 na 3210.00.10. Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu kwa wachakataji wa ngozi nchini;

x. Kutoa unafuu wa Ushuru wa Forodha kwa utaratibu wa *Duty Remission* kwa kiwango asilimia 0 badala ya asilimia 25 au asilimia 10 mwaka mmoja kwenye malighafi za kutengeneza mbolea zinazotambulika kwa HS Codes 2710.99.00, 2528.00.00 na 3505.20.00. Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu kwa wazalishaji wa mbolea nchini;

y. Kutoa unafuu wa Ushuru wa Forodha kwa utaratibu wa *Duty Remission* kwa kiwango asilimia 0 badala ya asilimia 25 kwa mwaka mmoja kwenye vifungashio vya tumbaku iliyochakatwa vinavyotambulika kwa HS Code 5310.10.00. Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu kwa wachakataji wa tumbaku nchini;

z. Kutoa unafuu wa Ushuru wa Forodha kwa utaratibu wa *Duty Remission* kwa kiwango asilimia 0 badala asilimia 25 kwa mwaka mmoja kwenye vifungashio vya chai iliyochakatwa vinavyotambulika kwa HS Codes 4819.20.90, 5407.44.00 na 3923.29.00. Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu kwa wachakataji wa chai (tea blenders) nchini;

aa. Kutoa unafuu wa Ushuru wa Forodha kwa utaratibu wa *Duty Remission* kwa kiwango asilimia 10 badala ya asilimia 25 kwa mwaka mmoja kwa waunganishaji wa pikipiki za matairi matatu bila kujumuisha fremu ili ziweze kutengenezwa na kuunganishwa hapa nchini (CKD for three-wheel motorcycles excluding chassis and its components) zinazotambulika kwa HS Code 8704.21.90. Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu kwa waunganishaji wa pikipiki hizo nchini ili kurahisisha usafirishaji wa mizigo; bb. Kutoa unafuu wa Ushuru wa Forodha kwa utaratibu wa *Duty Remission* kwa kiwango asilimia 0 badala ya asilimia 25 au asilimia 10 kwa

mwaka mmoja kwenye malighafi za kutengeneza mabomba ya plastiki (glass reinforced plastic pipes) zinazotambulika kwa HS Codes 3920.61.10, 7019.39.00, 7019.31.00, 6006.90.00, 7019.12.00, 3920.10.10, 4016.93.00, na 3907.91.00. Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu kwa watengenezaji wa mabomba hayo nchini ili kupunguza gharama za uzalishaji na kuwezesha ujenzi wa miundombinu ya maji;

cc. Nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zimekubaliana kuendelea kutoa unafuu wa Ushuru wa Forodha kwa utaratibu wa *Duty Remission* kwa kiwango cha asilimia 10 badala ya asilimia 100 au dola za Marekani 460 kwa kila tani moja ya ujazo (metric tone) kutegemea kiwango kitakachokuwa kikubwa kwenye sukari ya matumizi ya viwandani (sugar for industrial use) inayotambulika kwa HS Codes 1701.99.10 na 1701.99.20. Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu kwenye viwanda vinavyotumia bidhaa hii kama malighafi;

dd. Kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia 10 au dola za Marekani 125 kwa kila tani moja *(Metric ton)* kutegemea kiwango kitakachokuwa kikubwa kwenye mabati yanayotambulika kwa HS Code 7212.20.00 kwa mwaka mmoja badala ya ushuru wa asilimia 10 pekee. Lengo la hatua hii ni kulinda viwanda vya ndani, kuongeza ajira pamoja na mapato ya Serikali;

ee. Kutoza Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha asilimia 35 badala ya asilimia 25 kwa mwaka mmoja kwenye taulo za watoto *(Baby* Diapers) zinazotumbulika kwa HS code 9619.00.90. Lengo la hatua hii ni kulinda viwanda vinavyozalisha bidhaa hii nchini, kuongeza ajira pamoja na mapato ya Serikali;

ff. Kutoza Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha asilimia 25 badala ya asilimia 10 kwa mwaka mmoja kwenye nyuzi za pamba (cotton yarn) zinazotambulika kwa *Headings* 52.05, 52.06 na 52.07 isipokuwa nyuzi za pamba zinazotambulika kwa HS Code 5205.23.00. Lengo la hatua ni kulinda viwanda vinavyozalisha

bidhaa hiyo na kuongeza thamani ya zao la pamba (value addition) nchini;

gg. Kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia 35 badala ya asilimia 25 kwenye bidhaa za mbogamboga na matunda zinazotambulika kwa HS code 0604.20.00; 0604.90.00; 0808.10.00; 0808.30.00 kwa mwaka mmoja. Hatua hii inalenga kilinda wazalishaji wa bidhaa za mbogamboga na matunda hapa nchini;

hh. Kutoa unafuu wa Ushuru wa Forodha kwa utaratibu wa *Duty Remission* kwa kiwango cha asilimia 0 badala ya asilimia 10 kwa mwaka mmoja kwenye malighafi za kutengeneza viongeza ladha kwenye vyakula na vinywaji (food flavors) zinazotambulika kwa HS Code 1901.90.10; 3302.10.00; na 3505.10.00. Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu kwa watengenezaji wa vyakula na vinywaji nchini;

ii. Kutoa unafuu wa Ushuru wa Forodha kwa utaratibu wa *Duty Remission* kutoka asilimia 25 au asilimia 10 hadi asilimia 0 kwa mwaka mmoja kwenye karatasi zinazotambulika kwa HS Codes 4804.39.00; 4805.11.00; 4805.19.00; 4805.24.00; 4805.25.00; zinazotumika kama malighafi ya kutengeneza vifungashio aina ya maboksi (corrugated boxes). Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu kwa wazalishaji wa vifungashio hivyo hapa nchini ili wananchi waweze kuvipata kwa urahisi na kwa bei nafuu;

jj. Kutoa unafuu wa Ushuru wa Forodha kwa utaratibu wa *Duty Remission* kutoka asilimia 35 hadi asilimia 10 kwa mwaka mmoja kwenye malighafi za kutengeneza sabuni (toilet soap) zinazotambulika kwa HS Code 3401.20.10. Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu kwa wazalishaji wa sabuni nchini, kuhamasisha uwekezaji, kuongeza ajira pamoja na mapato ya Serikali;

kk. Kutoa unafuu wa Ushuru wa Forodha kwa utaratibu wa *Duty Remission* kwa kiwango cha asilimia 0 badala ya asilimia 25 au asilimia 10 kwa mwaka mmoja kwenye malighafi za kutengeneza nyaya za umeme (electrical cables)

zinazotambulika kwa HS Codes 7312.10.00; 7217.20.00; 7408.19.00; 7409.11.00; 7605.21.00; 2710.19.56; 3815.90.00; 5402.19.00; 5903.90.00; 7907.00.00; na 2712.10.00. Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu kwa watengenezaji wa nyaya hizo pamoja na kuvutia uwekezaji nchini;

ll. Kutoza Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha asilimia 25 badala ya asilimia 10 kwenye kamba zinazotengenezwa kwa nyuzi zenye asili ya plastiki (Twine of other synthetic fibers) zinazotambulika kwa HS Code 5607.50.00 kwa mwaka mmoja. Lengo ni kulinda viwanda vinavyozalisha bidhaa mbadala hapa nchini pamoja na kuongeza ajira;

mm. Kupunguza Ushuru wa Forodha kutoka asilimia 25 hadi asilimia 0 kwa mwaka mmoja kwenye kadi janja (smart cards) zinazotambulika kwa HS Code 8523.52.00 zitakazoingizwa nchini na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA). Hatua hii inalenga kupunguza gharama za uingizaji wa kadi hizo ili kurahisisha upatikanaji wa vitambulisho vya Taifa kwa wananchi;

nn. Kutoza Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha asilimia 25 au dola za Marekani 250 kwa kila tani moja ya ujazo (metric ton) kutegemea kiwango kitakachokuwa kikubwa badala ya ushuru wa asilimia 25 kwa mwaka mmoja kwenye mabati yanayotambulika kwa HS code 7210.30.00. Lengo la hatua hii ni kulinda viwanda vya ndani, kuongeza ajira pamoja na mapato ya Serikali;

oo. Kupunguza Ushuru wa Forodha kutoka kiwango cha asilimia 50 hadi asilimia 35 kwa mwaka mmoja kwenye vitenge vinavyotambulika kwa HS Codes 5208.51.10; 5208.52.10; 5209.51.10; 5210.51.10; 5211.51.10; 5212.15.10; 5212.25.10; 5513.41.10; na 5514.41.10. Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu kwenye uagizaji wa vitenge ili kulinda walaji;

pp. Kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia 25 au dola za Marekani 0.25 kwa kila mita moja kutegemea kiwango kitakachokuwa

kikubwa badala ya asilimia 25 pekee kwa mwaka mmoja kwenye vitambaa vya pamba (cotton grey fabric) vinavyotambulika kwa HS Codes 5208.11.00; 5208.12.00; 5208.13.00; 5208.19.00; 5209;11.00; 5209.12.00; 5209.19.00; 11.00; 5210.19.00; 5211.11.00; 5211.12.00; 5211.19.00; 5212.11.00; na 5212.21.00. Lengo la hatua hii ni kuchochea uzalishaji wa vitambaa hivyo kwa kutumia pamba inayozalishwa hapa nchini, kuongeza ajira pamoja na mapato ya Serikali;

qq. Kutoza Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha asilimia 25 badala ya asilimia 10 kwenye karatasi za kutolea risiti za kielektroniki zinazotambulika kwa HS Code 4811.90.00 kwa mwaka mmoja. Lengo la hatua hii ni kulinda viwanda vya ndani vinavyozalisha bidhaa hii;

rr. Kupunguza Ushuru wa Forodha kutoka asilimia 25 hadi asilimia 0 kwa mwaka mmoja kwenye mabasi ya abiria yanayotambulika kwa HS Codes 8702.10.99 na 8702.20.99 yanayoingizwa nchini kwa ajili ya mradi wa mabasi yaendayo haraka. Hatua hii inalenga kupunguza gharama za uingizaji wa mabasi hayo ili kurahisisha huduma ya usafiri kwa wananchi;

ss. Kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia 35 au dola za Marekani 350 kwa kila tani moja ya ujazo (Metric ton) kutegemea kiwango kitakachokuwa kikubwa badala ya asilimia 35 pekee kwa mwaka mmoja kwenye misumari zinazotambulika kwa HS code 7317.00.00. Hatua hii inalenga kulinda viwanda vinavyozalisha bidhaa hizo nchini, kuhamasisha uwekezaji wa bidhaa za chuma, kuongeza ajira pamoja na mapato ya Serikali;

tt. Kutoza Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha asilimia 35 badala ya kiwango cha asilimia 100 au dola za Marekani 460 kwa kila tani moja ya ujazo kutegemea kiwango kitakachokuwa kikubwa kwa mwaka mmoja kwenye sukari ya matumizi ya kawaida (consumption sugar) inayotambulika kwa HS Code 1701.14.90 inayoagizwa kutoka nje ya nchi kwa vibali maalum kwa lengo la kuziba pengo (gap) la uzalishaji hapa nchini;

uu. Kutoa unafuu wa Ushuru wa Forodha kwa utaratibu wa *Duty Remission* kutoka asilimia 35, asilimia 25 au asilimia 10 hadi asilimia 0 kwa mwaka mmoja kwenye malighafi za kuzalisha bidhaa mtaji (capital goods) zinazotumika viwandani zinazotambulika kwa headings 72.14;
72.15; 72.16; 32.08; 73.07; 83.11; 85.44; 68.06; 74.19; 72.08; 73.06; 73.12; 73.15; 73.18; 84.82; 84.83; 72.22; 73.04; 84.81; 84.84; 73.25; 40.10; na 76.06. Hatua hii inalenga kutoa unafuu kwa wazalishaji wa bidhaa mtaji hapa nchini ili bidhaa hizo ziweze kupatikana kwa unafuu kwa viwanda vya ndani pamoja na kuchochea uwekezaji wa kuzalisha bidhaa hizo hapa nchini;

vv. Kutoa unafuu wa Ushuru wa Forodha kwa utaratibu wa *Duty Remission* kwa kiwango cha asilimia 0 badala ya asilimia 35, asilimia 25 au asilimia 10 kwa mwaka mmoja kwenye malighafi za kutengeneza rejeta (radiators) za vyombo vya moto zinazotambulika kwa HS Codes 7409.11.00; 7409.19.00; 7410.11.00; 7410.12.00; 7409.21.00; 8001.10.00; 3810.90.00. Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu pamoja na kuchochea uwekezaji katika uzalishaji wa rejeta hapa nchini;

ww. Kutoa unafuu wa Ushuru wa Forodha kwa utaratibu wa *Duty Remission* kwa kiwango cha asilimia 0 badala ya asilimia 10 au asilimia 25 kwa mwaka mmoja kwenye malighafi za kutengeneza *wiring harnesses* za vyombo vya moto zinazotambulika kwa HS Codes 8538.90.00; 4016.99.00; 8205.59.00; 8536.10.00; 8536.69.00; 8536.90.00; 8547.20.00; 3926.90.90; 3917.32.00; na 8544.30.00. Hatua hii inalenga kutoa unafuu kwa wazalishaji pamoja na kuchochea uwekezaji katika uzalishaji wa *wiring harnesses* nchini; na

xx. Kutoza Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha asilimia 10 kwa mwaka mmoja badala ya asilimia 0 kwenye mafuta ghafi ya soya, karanga, nazi, mnyonyo, haradali n.k yanayotambulika kwa HS codes 1507.10.00; 1508.10.00; 1513.11.00; 1513.21.00; 1514.11.00; 1514.91.00; na 1515.11.00. Lengo la hatua hii ni

kuoanisha viwango vya mafuta ghafi haya vifanane na viwango vya mafuta ghafi ya alizeti, pamba, mahindi na mafuta ghafi mengineyo ambayo viwango vyake ni asilimia 10. Aidha, hatua hii pia inalenga kulinda na kuhamasisha uzalishaji wa mbegu za mafuta ya kula nchini, kuongeza ajira pamoja na kulinda fedha za kigeni zinazotumika kuagiza mafuta hayo nje ya nchi.

**161.** ***Mheshimiwa Spika,*** Napendekeza kuanzisha utaratibu wa Serikali kusaini Mikataba ya Utekelezaji (Performance Agreement) na viwanda vinavyolindwa na Serikali kwa kupewa unafuu wa kodi ikiwemo Ushuru wa Forodha kupitia utaratibu wa *Duty Remission*, Kodi ya Ongezeko la Thamani kupitia utoaji wa msamaha au utozaji wa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa kiwango cha asilimia sifuri (Exemption au Zero Rated) pamoja na viwanda vitakavyolindwa na Serikali kutokana na sera za kuongeza kodi kwenye bidhaa zinazotoka nje ya nchi. Hatua hii inalenga kuhakikisha malengo ya utoaji wa unafuu wa kodi husika yanafikiwa na hatimaye kuleta manufaa tarajiwa katika ukuaji wa uchumi wa nchi.

Hatua hizi kwa ujumla wake zinatarajiwa **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi **milioni 205,727.**

**20. Sheria ya Kudhibiti Uingizwaji wa Bidhaa Nchini, SURA 276**

**162**. ***Mheshimiwa Spika,*** Napendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Kudhibiti Uingizwaji wa Bidhaa Nchini, Sura 276 kwa kuanzisha Tozo ya Maendeleo ya Viwanda (industrial Development Levy) kwa baadhi ya bidhaa zinazoingizwa nchini kama ifuatavyo: kiwango cha asilimia 10 kwenye *wire rods* zinazotambulika kwa HS Code 7213.91.10 na 7213.91.90; asilimia 10 kwenye bia zinazotambulika kwa *heading* 22.03 pamoja na mvinyo (wine); asilimia 5 kwenye bia zisizo na kilevi (non-alcoholic beer) zinazotambulika kwa HS Code 2202.91.00; asilimia 5 kwenye vinywaji vya kuongeza nguvu (energy drinks) vinavyotambulika kwa HS Code 2202.99.00; asilimia 10 kwenye sabuni za unga (detergents) zinazotambulika kwa HS Code 3402.50.00 na sabuni za maji

zinazotambulika kwa HS Code 3402.90.00. Tozo hii haitatozwa kwenye bidhaa zinazozalishwa katika nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC Partners States) ambazo zinakidhi vigezo vya uasilia (Rules of Origins). Aidha, Serikali itaendelea kufanya tathmini na tafiti kwenye bidhaa nyingine zinazozalishwa kwa wingi nchini kwa lengo la kuzijumuisha katika wigo wa utozaji. Lengo la hatua hii ni kuvutia uwekezaji nchini, kuchochea mauzo nje ya nchi na kulinda uzalishaji wa ndani kwa kuwa bidhaa husika zinazalishwa kwa wingi nchini. Hatua hii inatarajiwa **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi **milioni 11,147.**

**21. Sheria ya Usafirishaji Bidhaa Nje ya Nchi, SURA 196**

**163**. ***Mheshimiwa Spika,*** Napendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Usafirishaji wa Bidhaa Nje ya Nchi, Sura 196 kama ifuatavyo:

a) Kutoza ushuru kwa kiwango cha asilimia 10 kwenye mafuta ghafi ya kula ya alizeti (Crude Sunflower Oil), mashudu yanayotokana na mbegu za alizeti (Sunflower Cake) pamoja na mbegu za alizeti (Sunflower Seeds) zinazosafirishwa kwenda nje ya nchi. Lengo la hatua hii ni kuwezesha upatikanaji wa bidhaa za mafuta kwa bei nafuu nchini pamoja na kulinda wazalishaji wa ndani kwa kuhakikisha wanapata mbegu za alizeti za kutosha ambazo zinatumika kama malighafi katika viwanda hivyo. Hatua hii inatarajiwa **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi **milioni 2,048;**

Hatua hizi kwa ujumla wake zinatarajiwa **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha **shilingi milioni 2,048**

**22. Maboresho ya Ada na Tozo mbalimbali za Taasisi za Serikali pamoja na Utekelezaji wa Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Kufanya Biashara (Blueprint).**

**164**. ***Mheshimiwa Spika,*** Napendekeza kufanya maboresho ya sheria na kanuni mbalimbali, kufuta au kupunguza ada na tozo mbalimbali

zinazotozwa na Wizara, Idara na Taasisi zinazojitegemea ili kuleta usimamizi bora wa sekta mbalimbali na kuboresha mazingira ya biashara nchini. Hatua hizi pia ni moja ya sehemu ya mwendelezo wa utekelezaji wa Mpango wa kuboresha Mfumo wa udhibiti wa Biashara (Blueprint for Regulatory Reforms to Improve the Business Environment). Marekebisho hayo ni kama ifuatavyo:

**i. Tume ya nguvu za mionzi Tanzania**

Kufanya marekebisho kwenye ada ya Utambuzi wa Mionzi kama ifuatavyo:

a) Kuweka takwa la kutoza kiwango cha asilimia 0.1 ya malipwani kwenye bidhaa za mifugo na chakula inayosafirishwa kwenda nje ya nchi pale ambapo nchi hizo zina sharti la uhitaji wa cheti cha utambuzi wa mionzi au msafirishaji ameomba cheti hicho. Pendekezo hili linaondoa takwa la ulazima wa msafirishaji kulipia tozo hiyo hata pale ambapo cheti cha utambuzi wa mionzi hakihitajiki na nchi zinapopelekwa bidhaa hizo; na

b) Kupunguza ada ya mionzi kutoka asilimia 0.4 ya Malipwani hadi asilimia 0.2 ya malipwani kwa bidhaa za mwisho zinazoingizwa nchini. Lengo la hatua hizi ni kupunguza tozo kero na gharama za biashara na hivyo kuchochea uzalishaji na kukuza uwekezaji nchini sambamba na kupunguza uingizaji wa bidhaa hizo nchini kwa njia ya magendo. Hatua hii inatarajia **kupunguza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi **milioni 42.**

**ii. Jeshi la Zimamoto na Uokoaji**

Kufanya marekebisho ya Sheria ya Jeshi ya Zimamoto na Uokoaji, SURA 427 kwa kupunguza tozo ya mafunzo ya kinga na tahadhari za moto kwa wasimamizi (wardens) kutoka Shilingi 500,000 hadi Shilingi 200,000. Marekebisho haya yanaenda sambamba na kuweka sharti la mafunzo hayo kufanyika kwa msimamizi mmoja na kuendelea kwa kila mwaka badala ya utaratibu wa sasa wa wasimamizi zaidi ya wawili. Lengo la hatua hii ni kupunguza gharama za ufanyaji biashara na uwekezaji nchini.

**iii. Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania**

Kutoza ada ya kuhuisha leseni za uendeshaji wa ndege za kiusalama (Air Operators Certificates - AOC) kwa kiwango cha dola za Marekani 600 kwa Kampuni kwa mwaka badala ya kiwango kinachotozwa sasa cha dola za Marekani 600 kwa kila ndege kwa mwaka. Lengo la hatua hii ni kupunguza gharama za ufanyaji wa biashara katika sekta hiyo na kuchochea ukuaji wa Sekta ya Anga.

**iv. Wizara ya Maliasili na Utalii**

Kufanya marekebisho kwenye Kanuni ya Ada na Tozo za Utalii ya mwaka 2015 kama ifuatavyo:

a) Kutoza ada ya Leseni za Biashara za Utalii Tanzania kwa Shilingi ya Tanzania badala ya dola za Marekani. Mapendekezo haya yanaenda sambamba na kuweka takwa la ada hizo kulipwa katika kipindi cha miezi 12 kuanzia siku ya malipo ya mwisho ya leseni ya biashara yalipofanyika; na

b) Kupunguza ada ya Leseni ya Biashara za Utalii Tanzania inayolipwa na wakala wa wapandisha watalii mlimani (mountain climbing) kutoka dola za Marekani 2,000 kwa mwaka hadi shilingi milioni 3 kwa mwaka. Aidha, ada hiyo italipwa kwa thamani ya shilingi ya Tanzania.

Lengo la hatua hizi ni kurahisisha mfumo wa ulipaji wa ada za utalii, kupunguza gharama za uendeshaji, kuvutia uwekezaji katika tasnia ya utalii na kuendana na matakwa ya Kifungu cha 26 cha Sheria ya Benki kuu ya Tanzania kinachoelekeza malipo yanayofanywa nchini kutumia shilingi ya Tanzania.

**v. Wizara ya Mifugo na Uvuvi a) Sekta ya Mifugo**

Kufanya marekebisho kwenye ada ya kibali cha kusafirisha mifugo katika minada kutoka shilingi 30,000 hadi shilingi 31,000 kwa kila ng' ombe; na shilingi 6,500 hadi shilingi 7,000 kwa kila mbuzi na kondoo.

Ongezeko hilo ada litapelekwa Halmashauri kwa lengo la kuongeza usimamizi katika minada husika.

**b) Sekta ya Uvuvi**

Kufanya marekebisho ya tozo mbalimbali kwenye Sekta ya Uvuvi kama ifuatavyo:

i. Kupunguza ada ya kibali cha kusafirisha samaki na mazao ya uvuvi (dagaa, furu) samaki wakavu,wabichi na waliogandishwa kutoka Shilingi 100 kwa kila kilo moja hadi shilingi 50 kwa kila kilo moja. Aidha, Samaki na mazao ya uvuvi yaliyokaushwa yenye uzito chini ya kilo 20 pamoja na yale mabichi au yaliyogandishwa yenye uzito chini ya kilo 30 hayatatozwa ada hiyo;

ii. Kupunguza ada ya kibali cha kusafirisha mazao ya mabondo kutoka shilingi 2,500 hadi shilingi 2,000 kwa kilo ya Mabondo mabichi na kutoka shilingi 3,500 hadi shilingi 2,800 kwa kilo ya Mabondo makavu; na

iii. Kuongeza ushuru wa kusafirisha mabondo nje ya nchi (export royalty) kutoka Dola za Marekani 2.7 hadi Dola za Marekani 3.0 kwa kilo kwa mabondo mabichi na Dola za Marekani 3.3 hadi Dola za Marekani 3.5 kwa kilo kwa mabondo makavu.

Hatua hizi kwa pamoja zinatarajia **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi **milioni 554.**

**165.** ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na maboresho ya sheria mbalimbali yaliyofanywa na Serikali ili kuboresha mazingira ya uwekezaji na biashara kwa kupunguza mwingiliano wa majukumu baina ya taasisi mbalimbali za udhibiti nchini na kufuta/kupunguza ada na tozo kero, bado kumekuwa na changamoto ya taasisi nyingi za udhibiti zinazosimamia sekta mbalimbali kuongeza kero za ufanyaji biashara na uwekezaji kutokana na ada, tozo na adhabu mbalimbali wanazotoza pamoja na kaguzi nyingi na zisizokuwa na tija. Ili kuondoa kero hizo, Serikali ipo katika hatua za kuanzisha

mfumo wa pamoja wa ukusanyaji wa ada, tozo na adhabu za taasisi za udhibiti (Single Window Payment System) na kuweka utaratibu kwa taasisi hizo kufanya kaguzi kwa namna ambayo haitaleta usumbufu na bila kuathiri majukumu ya msingi yanayofanywa na taasisi husika.

**23. Marekebisho madogo madogo katika baadhi ya Sheria za Kodi, Sheria nyingine na Kanuni mbalimbali.**

**166.** ***Mheshimiwa Spika,*** napendekeza kufanya marekebisho mengine madogo madogo yasiyo ya kisera katika sheria mbalimbali za kodi, sheria nyingine pamoja na Kanuni za Sheria mbalimbali ili ziwe sanjari na azma ya kurahisisha utekelezaji wake. Marekebisho hayo yataainishwa katika Muswada wa **Sheria ya Fedha ya mwaka 2024** na Matangazo ya Serikali *(Government Notices)*.

**Tarehe ya Kuanza Kutekeleza Hatua Mpya za Kodi.**

**167**. ***Mheshimiwa Spika,*** hatua hizi za kikodi zinazopendekezwa zitaanza kutekelezwa tarehe 1 Julai, 2024, isipokuwa pale itakapoelezwa vinginevyo.

**VII. SURA YA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA 2024/25**

**168**. **Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka 2024/25, Serikali inatarajia kukusanya na kutumia jumla ya shilingi trilioni 49.35, sawa na ongezeko la asilimia 11.2 ikilinganishwa na bajeti ya mwaka 2023/24. Ongezeko la bajeti kwa kiasi kikubwa limetokana na kugharamia: deni la Serikali ambalo limeongezeka kutokana na kushuka kwa thamani ya shilingi, kuongezeka kwa viwango vya riba na kuiva kwa mikopo ya zamani; ajira mpya; ulipaji wa hati za madai; Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa Mwaka 2024; maandalizi ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025; na maandalizi ya michuano ya mpira wa miguu ya mataifa ya Afrika (AFCON) ya mwaka 2027 ikiwemo ujenzi na ukarabati wa viwanja.

**Mapato**

**169. Mheshimiwa Spika**, mapato ya ndani yanakadiriwa kuwa jumla ya shilingi trilioni 34.61, sawa na asilimia 70.1 ya bajeti yote na asilimia 15.7 ya Pato la Taifa. Kati ya mapato hayo, mapato yatakayokusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania yanakadiriwa kuwa shilingi trilioni 29.41, mapato yasiyo ya kodi yatakayokusanywa na Wizara, Taasisi na Idara zinazojitegemea shilingi trilioni 3.84 na mapato yatakayokusanywa na Mamlaka za Serikali za Mitaa shilingi trilioni 1.36. Mikakati ya kufikia malengo haya ya mapato ni kama nilivyoeleza hapo awali.

**170. Mheshimiwa Spika**, misaada na mikopo nafuu kutoka kwa Washirika wa Maendeleo inakadiriwa kuwa shilingi trilioni 5.13. Naomba nizitambue nchi wahisani zilizoahidi kuchangia bajeti ya mwaka 2024/25 ambazo ni pamoja na: Australia, Austria, Canada, China, Denmark, Finland, India, Ireland, Italia, Japan, Korea ya Kusini, Marekani, Norway, Poland, Sweden, Ubelgiji, Ufaransa, Uhispania, Uholanzi, Uingereza, Ujerumani na Uswisi. Aidha, taasisi na Mashirika ya Kimataifa yaliyoahidi kuchangia ni pamoja na: Benki ya Dunia; Shirika la Fedha la Kimataifa; Benki ya Maendeleo ya Afrika; Benki ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Kiuchumi katika Afrika; Benki ya Uwekezaji ya Ulaya; Mfuko wa Abu Dhabi; Mfuko wa Kuwait; Mfuko wa Kimataifa wa Kusaidia Mapambano Dhidi ya Ukimwi, Kifua Kikuu na Malaria; Mfuko wa OPEC kwa Maendeleo ya Kimataifa; Mfuko wa Mazingira Duniani; Adaptation Fund; Mfuko wa GRMF; Umoja wa Mataifa na mashirika yote yaliyopo chini yake; Umoja wa Ulaya; na Shirikisho la GAVI.

**171. Mheshimiwa Spika**, kwa dhati kabisa, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru washirika wetu wa maendeleo kwa misaada na mikopo nafuu wanayoendelea kutupatia katika kutekeleza miradi na programu mbalimbali za maendeleo nchini. Ni matarajio yetu kuwa rasilimali zilizoahidiwa na marafiki zetu hawa zitatolewa kwa wakati na kwa kiasi kilichoahidiwa. Nasi, kwa upande wa Serikali tunaahidi kusimamia ipasavyo matumizi ya fedha hizo kama ilivyokusudiwa.

**172. Mheshimiwa Spika**, Serikali inakadiria kukopa shilingi trilioni 6.62 kutoka soko la ndani ambapo shilingi trilioni 4.02 ni kwa ajili ya kulipia hatifungani na dhamana za Serikali zinazoiva na shilingi trilioni 2.60 kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo. Aidha, Serikali inakadiria kukopa shilingi trilioni 2.99 kutoka soko la nje kwa masharti ya kibiashara kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo.

**173. Mheshimiwa spika**, katika kuhakikisha soko la mitaji la ndani linaendelea kuwa chanzo muhimu cha fedha, Serikali itaendelea kutoa hati fungani kizio (benchmark bonds) kwa lengo la kujenga viwango vya bei rejea na shindani katika soko la fedha na mitaji nchini. Aidha, Serikali itaendelea kufungua wigo kwa wawekezaji kutoka nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika.

**Matumizi**

**174. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2024/25, Serikali imepanga kutumia jumla ya shilingi trilioni 49.35. Kiasi hicho kinajumuisha: shilingi trilioni 15.74 kwa ajili ya ulipaji wa deni la Serikali na gharama nyingine za Mfuko Mkuu; shilingi trilioni 11.77 kwa ajili ya mishahara ikiwemo ajira mpya pamoja na upandishaji wa madaraja kwa watumishi; shilingi trilioni 2.17 kwa ajili ya mifuko ya reli, barabara, maji, REA na TARURA; na ruzuku ya maendeleo ya shilingi trilioni 1.19 kwa ajili ya kugharamia mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu na vyuo vya kati pamoja na Programu ya Elimumsingi na Sekondari bila Ada.

**175. Mheshimiwa Spika**, sura ya bajeti kwa mwaka 2024/25 ni kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 1.**

**Jedwali Na. 1: Sura ya Bajeti ya Mwaka 2024/25**

| | | Shilingi Milioni |
|---|---|---|
| **Mapato** | 2024/ | |
| **Mapato ya Ndani-Serikali Kuu** | | **33,254,306** |
| (i) Mapato ya Kodi (TRA) | 29,415,289 | |
| (ii) Mapato yasiyo ya kodi | 3,839,017 | |
| **Mapato ya Halmashauri** | | **1,356,341** |
| **Misaada na Mikopo nafuu kutoka Washirika wa Maendeleo** | | **5,130,613** |
| (i) Misaada na Mikopo nafuu - GBS | 1,489,775 | |
| (ii) Misaada na Mikopo nafuu ya Miradi | 3,461,946 | |
| (iii) Misaada na Mikopo nafuu ya Kisekta | 178,892 | |
| **Mikopo ya Kibiashara Ndani na Nje** | | **9,604,428** |
| (i) Mikopo ya Nje | 2,986,638 | |
| (ii) Mikopo ya Ndani | 2,595,417 | |
| (iii) Mikopo ya Ndani- Rollover | 4,022,373 | |
| **JUMLA YA MAPATO YOTE (A+B+C+D)** | | **49,345,688** |
| | | |
| **Matumizi** | | |
| **Matumizi ya Kawaida** | | **34,590,391** |
| (i) Mfuko Mkuu wa Serikali | | 15,736,279 |
| -Malipo ya Riba Ndani | 3,146,668 | |
| -Malipo ya Mtaji Ndani (Rollover) | 4,022,373 | |
| -Malipo ya Mtaji Nje | 3,517,120 | |
| -Malipo ya Riba Nje | 2,435,305 | |
| -Michango ya Serikali kwenye Mifuko ya Hifadhi za Jamii | 2,000,000 | |
| -Matumizi Mengine ya Mfuko Mkuu | 614,813 | |
| (ii) Mishahara | | 11,767,987 |
| (iii) Matumizi Mengineyo (OC) | | 7,086,125 |
| -Matumizi ya Halmashauri (own | | 815,065 |

| | | |
|---|---|---|
| source) | | |
| | | |
| **Matumizi ya Maendeleo** | | **14,755,296** |
| (i) Fedha za Ndani | | 11,114,458 |
| -Malipo ya Madeni yaliyohakikiwa | 400,000 | |
| -Mifuko ya Reli, Maji, Barabara, REA na TARURA | 2,167,623 | |
| -Matumizi ya Halmashauri | 541,276 | |
| -Miradi mingine | 8,005,559 | |
| (ii) Fedha za Nje | | 3,640,838 |
| **JUMLA YA MATUMIZI YOTE (E+F)** | | **49,345,688** |
| **NAKISI YA BAJETI (kama asilimia ya Pato la Taifa)** | | **2.9%** |

**Chanzo:** Wizara ya Fedha

**Vihatarishi vya Utekelezaji wa Bajeti**

**176. Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2024/25 unaweza kuathiriwa na vihatarishi mbalimbali vinavyohusisha mabadiliko ya sera za uchumi, fedha, bajeti, siasa na mahusiano ya kidiplomasia. Aidha, utekelezaji wa bajeti unaweza kuathiriwa na masuala mtambuka hususan mabadiliko ya tabianchi, majanga ya asili, magonjwa ya mlipuko na athari za vita baina ya mataifa. Vihatarishi katika bajeti ya mwaka 2024/25 ni pamoja na: kudorora kwa uchumi wa dunia; mabadiliko ya bei za bidhaa na huduma; mabadiliko ya riba katika masoko ya fedha ndani na nje ya nchi; mabadiliko ya viwango vya kubadilisha fedha; madeni sanjari; siasa na mahusiano ya kidiplomasia; na mabadiliko ya tabianchi, majanga ya asili na magonjwa ya mlipuko.

**177. Mheshimiwa Spika**, endapo vihatarishi hivyo vitatokea, athari zinazoweza kujitokeza ni pamoja na: kutokufikiwa kwa lengo la ukusanyaji wa mapato; kasi ndogo ya utekelezaji wa miradi; kuongezeka kwa gharama za bidhaa, malighafi, huduma na utekelezaji wa miradi; kuongezeka kwa gharama za kuhudumia deni la Serikali; na kuongezeka kwa gharama za mikopo ya kibiashara katika masoko ya fedha. Athari nyingine ni: kupungua kwa misaada

na mikopo nafuu kutoka kwa Washirika wa Maendeleo; kuongezeka kwa nakisi ya bajeti; kupungua kwa uzalishaji wa mazao ya kilimo; uharibifu wa miundombinu; na kuongezeka kwa madai na madeni ya wazabuni na watoa huduma.

**178. Mheshimiwa Spika**, Serikali itaendelea kuchukua hatua mbalimbali za kukabiliana na vihatarishi vinavyoweza kujitokeza ili kufikia malengo na shabaha za utekelezaji wa Bajeti ya mwaka 2024/25. Hatua hizo ni pamoja na: kuendelea kusimamia sera ya fedha na bajeti; kuimarisha mifumo ya kielektroniki ya ukusanyaji mapato; kuboresha mazingira ya uwekezaji wa ndani na nje; kuendelea kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Mikopo, Misaada na Dhamana, Sura 134; kuimarisha hifadhi ya chakula ya Taifa; kusimamia utekelezaji wa Mwongozo wa Taifa wa Kuandaa na Kusimamia Mfumo wa Usimamizi wa Vihatarishi katika Taasisi za Umma; kuendelea kuimarisha na kusimamia Mfuko wa Taifa wa Maafa; kuimarisha utawala bora na utawala wa sheria; na kutekeleza Mkakati wa Taifa wa Kuimarisha Upatikanaji wa Fedha za Kigeni.

## VIII. HITIMISHO

**179. Mheshimiwa Spika**, ni dhahiri kuwa, Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, imepata mafanikio makubwa kutokana na kuwepo kwa sera madhubuti za Serikali ya Chama Cha Mapinduzi zilizolenga kuimarisha uchumi. Katika kipindi cha miaka mitatu ya uongozi wake, Mheshimiwa Rais amedhihirisha kuwa ni kiongozi **mwadilifu, msikivu, makini, shupavu, mchapa kazi na aliye na dhamira thabiti** ya kuendelea kuiletea nchi yetu maendeleo makubwa kwa kutekeleza miradi mbalimbali ya kimkakati. ***Hakika MAMA Mitano Tena!*** Aidha, niwashukuru wananchi wote wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kudumisha amani na utulivu hapa nchini ambayo imetusaidia sana kuwatumikia vyema na kufanikisha mafanikio yaliyopatikana katika kipindi chote cha miaka mitatu ya MAMA.

**180. Mheshimiwa Spika**, pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha miaka mitatu ya MAMA, bado wananchi wana kiu ya kuona huduma za jamii kama vile barabara, maji, afya, elimu na umeme zinaendelea kuwa bora zaidi. Bajeti ya mwaka 2024/25 inalenga kuwawezesha watanzania kuwa na maisha bora kwa kuendeleza juhudi za kujenga msingi wa uchumi wa viwanda ili kupanua fursa za ajira na kuchochea ukuaji wa uchumi wa Taifa na ustawi endelevu wa jamii. Katika kufikia malengo hayo, Serikali itaendelea kuchukua hatua madhubuti ikiwemo: kuboresha miundombinu ya nishati, usafiri na usafirishaji; kuimarisha mazingira wezeshi ya biashara na uwekezaji kupitia sera madhubuti ili kuwezesha ushindani huria wa sekta binafsi; kuboresha mifumo ya elimu na mafunzo; na kuunganisha tafiti na maendeleo na shughuli za kiuchumi zenye tija.

**181. Mheshimiwa Spika**, ili kufikia matamanio haya, rai yangu kwa Watanzania wenzangu, na hasa sisi viongozi ni lazima tujitoe kuijenga Tanzania kwa kumuunga mkono Rais wetu kwa vitendo. Hivyo, ni lazima tufanye kazi kwa bidii tukijielekeza kutekeleza malengo tuliyojiwekea ya kujenga uchumi imara unaotengeneza ajira ili kila mtanzania anufaike na matunda ya jasho lake.

**182. Mheshimiwa Spika**, kama mnavyofahamu, nchi yetu ipo katika mchakato wa kidemokrasia wa kufanya uchaguzi wa serikali za mitaa mwaka 2024 na maandalizi ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2025. Nipende kulihakikishia Bunge lako Tukufu na wananchi kwa ujumla kuwa Serikali imejipanga kikamilifu kugharamia mchakato mzima wa chaguzi hizo. Nitoe rai kwa viongozi wa vyama vya siasa na wananchi kwa ujumla kuhakikisha kuwa tunatumia haki yetu ya kikatiba kuchagua au kuchaguliwa kwa amani, undugu na upendo. Aidha, tuhakikishe kuwa viongozi tunaowachagua wawe ni waadilifu, wasikivu, wazalendo, wachapa kazi na wanaotoka ndani ya chama cha siasa kinachotetea maslahi na haki za wanyonge na **chama hicho ni Chama Cha Mapinduzi!**

**183. Mheshimiwa Spika**, napenda kutoa pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kutimiza miaka mitatu tangu aingie

madarakani mwezi Machi 2021 na kuendelea kuliongoza vyema Taifa letu kwa umahiri mkubwa huku tukishuhudia mafanikio makubwa katika nyanja za kiuchumi, kisiasa na kijamii kama nitakavyoelezea hapo baadae.

**184. Mheshimiwa Spika**, tunapozungumzia mafanikio ya miaka mitatu ya Serikali ya Awamu ya Sita, hatuwezi kumsahau Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hivyo, naomba nitumie nafasi hii kumpongeza kwa kumsaidia vyema Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kuongoza shughuli za Serikali ambazo matokeo yake yanaonekana na tunajivunia.

**185. Mheshimiwa Spika**, nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa uongozi wake thabiti alioonesha tangu kuchaguliwa kwake. **Hakika Zanzibar ya Uchumi wa Buluu Inameremeta!** Aidha, nitoe pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mbunge wa Jimbo la Ruangwa, pamoja na Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko, Naibu Waziri Mkuu, Waziri wa Nishati na Mbunge wa Jimbo la Bukombe, kwa kuendelea kuratibu na kusimamia shughuli za Serikali kwa weledi na umahiri mkubwa. **Hakika Safu hii Imesheheni Viongozi Makini, Kazi Iendelee!**

**186. Mheshimiwa Spika**, nitumie tena fursa hii kukupongeza wewe binafsi Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson Mwansasu, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mbunge wa Jimbo la Mbeya Mjini, kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani. Kuchaguliwa kwako kumeliletea heshima kubwa Taifa letu kwa kuwa mwanamke wa kwanza kutoka Bara la Afrika kushika wadhifa huo. **Hongera sana!** Tunakutakia kila la kheri katika majukumu hayo na unapoendelea kuliheshimisha Taifa letu katika nyanja za siasa za kimataifa. Nikupongeze pia Mheshimiwa Spika pamoja na Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Naibu Spika na Mbunge wa Jimbo la Ilala, kwa kuendelea kutekeleza kikamilifu majukumu ya kuliongoza Bunge letu Tukufu. Hakika mmeendelea kuonesha

ukomavu, ustahimilivu na weledi wa hali ya juu katika kusimamia na kuendesha shughuli za Bunge.

**187. Mheshimiwa Spika**, nimpongeze Mheshimiwa Prof. Ibrahim Hamis Juma, Jaji Mkuu wa Tanzania; Mheshimiwa Mustapher Mohamed Siyani, Jaji Kiongozi – Mahakama kuu ya Tanzania; Prof. Elisante Ole Gabriel, Mtendaji Mkuu wa Mahakama na Katibu wa Tume ya Utumishi wa Mahakama; na Mheshimiwa Eva Kiaki Nkya, Msajili Mkuu wa Mahakama ya Tanzania, kwa kazi nzuri ya kuongoza mhimili wa Mahakama.

**188. Mheshimiwa Spika**, nawapongeza pia waheshimiwa wabunge waliopata heshima ya kuteuliwa kushika nafasi mbalimbali serikalini mwaka 2023/24. Wabunge hao ni: Mheshimiwa Doto Mashaka Biteko (Mb), Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati; Mheshimiwa Deogratius John Ndejembi (Mb), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu; Mheshimiwa Jerry William Silaa (Mb), Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi; Mheshimiwa Zainab Athuman Katimba (Mb), Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa; Mheshimiwa Stanslaus Haroon Nyongo (Mb), Naibu waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – Mipango na Uwekezaji; Mheshimiwa Daniel Baran Sillo (Mb), Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi; Mheshimiwa Judith Salvio Kapinga (Mb), Naibu Waziri wa Nishati; Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile (Mb), Naibu Waziri Uchukuzi; Mheshimiwa Alexander Pastory Mnyeti (Mb), Naibu waziri Kilimo; na Dunstan Luka Kitandula (Mb), Naibu Waziri Maliasili na Utalii.

**189. Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya pekee kabisa nimpongeze Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi kwa kuaminiwa na kuteuliwa kuwa Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi. Hakika, uzoefu na umahiri wake katika siasa na diplomasia ya kimataifa hauna shaka yoyote katika kusimamia kwa weledi na umahiri utekelezaji wa mipango ya Serikali na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020. **Kidumu Chama Cha Mapinduzi!**

**190. Mheshimiwa Spika**, niwapongeze Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika, Mbunge wa Jimbo la Njombe Mjini, na Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama, Mbunge wa Jimbo la Madaba, kwa kuchaguliwa na kuungana na Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, Mbunge wa Viti Maalumu, kuwa wenyeviti wa Bunge. Nawatakia utendaji mwema katika majukumu yao. Aidha, nimpongeze Mheshimiwa Oran Manase Njeza, Mbunge wa Jimbo la Mbeya Vijijini, kwa kuteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti pamoja na makamu wake Mheshimiwa Twaha Ally Mpembenwe, Mbunge wa Jimbo la Kibiti. Ni matumaini yangu wataendeleza ushirikiano na umakini mkubwa katika kupitia, kuchambua na kushauri wakati wote wa maandalizi ya Bajeti ya Serikali. Vilevile, ninawashukuru Wenyeviti, Makamu Wenyeviti na Wajumbe wa Kamati zote za Kudumu za Bunge kwa michango yao waliyoitoa kupitia vikao vya Kamati za Kisekta katika kuboresha makadirio ya mapato na matumizi ya wizara mbalimbali na Serikali kwa ujumla.

**191. Mheshimiwa Spika**, nitumie fursa hii kuwapongeza na kuwashukuru kwa dhati kabisa wakuu wote wa vyombo vya ulinzi na usalama kwa uzalendo na utumishi wao uliotukuka. Naomba niwatambue kwa majina: Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama, Jenerali Jacob John Mkunda; Inspekta Jenerali wa Polisi, Camillus Mongoso Wambura; Mkurugenzi wa Usalama wa Taifa, Balozi Ali Idi Siwa; Kamishna Jenerali wa Magereza, Mzee Ramadhani Nyamka; Kamishna Jenerali wa Uhamiaji, Dkt. Anna Peter Makakala; Kamishna Jenerali wa Zimamoto na Uokoaji, John William Masunga; Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, CP Salum Rashid Hamduni; na Kamishna Jenerali wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, Aretas James Lyimo. Aidha, niwapongeze Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Dkt. Eliezer Mbuki Feleshi na Wakili Mkuu wa Serikali Dkt. Boniphace Nalija Luhende kwa kazi zao nzuri za kuwatumikia wananchi.

**192. Mheshimiwa Spika**, nawapongeza Waheshimiwa Mawaziri wenzangu na Naibu Mawaziri kwa kumsaidia Mheshimiwa Rais katika kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi.

Aidha, namshukuru Katibu Mkuu Kiongozi, Makatibu Wakuu, Naibu Makatibu Wakuu, Wakuu wa Taasisi pamoja na wataalam wote wa Serikali na sekta binafsi kwa ushirikiano na michango waliyotoa katika kila hatua ili kukamilisha bajeti hii.

**193. Mheshimiwa Spika**, napenda kuwashukuru viongozi na watumishi wenzangu wa Wizara ya Fedha kwa ushirikiano mkubwa walionipa na kwa kujituma katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara hususani katika maandalizi ya bajeti hii. Kipekee ninamshukuru Mheshimiwa Hamad Hassan Chande (Mb), Naibu Waziri wa Fedha na Mbunge wa Jimbo la Kojani; Dkt. Natu El-maamry Mwamba, Katibu Mkuu HAZINA na Mlipaji Mkuu wa Serikali pamoja na Naibu Makatibu Wakuu, Amina Khamis Shaaban, Elijah Greenton Mwandumbya na Jenifa Christian Omolo. Aidha, namshukuru Ndugu Emmanuel Mpawe Tutuba, Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania, kwa kusimamia sekta ya fedha kwa ustadi. Pia nimshukuru Ndugu Alphayo Japan Kidata, Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania, kwa jitihada kubwa anazofanya za kuongeza ukusanyaji wa mapato ya Serikali. Vilevile, namshukuru CPA Charles Edward Kichere, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, kwa kazi nzuri ya kukagua hesabu za taasisi mbalimbali za Serikali. Nimshukuru pia Dkt. Albina Andrew Chuwa, Mtakwimu Mkuu wa Serikali, kwa kusimamia vizuri Ofisi ya Taifa ya Takwimu.

**194. Mheshimiwa Spika**, naomba nitumie fursa hii pia kuwashukuru kwa dhati wananchi wa Jimbo langu la Iramba Magharibi kwa kuendelea kuniunga mkono na kutambua wajibu wa kitaifa nilionao na dhamana niliyokabidhiwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, niwashukuru Watanzania wote kwa kuendelea kuiunga mkono Serikali ya Awamu ya Sita ambayo inaendelea kutekeleza kwa dhati dhamira ya kujenga uchumi wa nchi na kuboresha hali ya maisha ya kila mtanzania. Kwa namna ya pekee, nawashukuru viongozi na waumini wa dini zote kwa kuendelea kuliombea Taifa letu na kumuombea Rais wetu pamoja na viongozi wote wa Serikali katika utekelezaji wa majukumu yao. Niwaombe tuendelee kumuomba Mwenyezi Mungu bila kuchoka.

**195. Mheshimiwa Spika**, niipongeze timu ya Azam kwa kushika nafasi ya pili katika mashindano ya Ligi kuu ya NBC na kufuzu kushiriki mashindano ya Klabu Bingwa ya Afrika. Aidha, niipongeze timu ya Coastal Union kwa kufuzu kushiriki michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika baada ya muda mrefu. Kwenye mafanikio ya timu ya Coastal Union, nimpongeze kwa dhati Mheshimiwa Ummy Ally Mwalimu, Mbunge wa Tanga Mjini kwa kujitoa kwa hali na mali ikiwa ni pamoja na kuhudhuria katika uwanja wa Mkwakwani na viwanja vingine bila kukosa na kushirikiana na wadau wengine kuiwezesha timu hiyo kufuzu kushiriki mashindano ya Kombe la Shirikisho barani Afrika. **Mheshimiwa Spika**, ni vyema kuwakumbusha wanatanga walikotoka maana kiubinadamu nyumba ikipendeza kuna wakati sifa huwa zinakwenda kwa fundi rangi tu na kuwasahau aliyechora ramani, aliyejenga msingi imara, ukuta imara na aliyepaua na kumpa fursa anayepaka rangi akiwa kwenye kivuli.

**196. Mheshimiwa Spika**, kwa umaalum kabisa nimpongeze GSM kwa uwekezaji mzuri alioufanya ambao umebadilisha kabisa taswira na uwezo wa kiuchezaji wa timu ya Yanga. Mafanikio hayo yametokana na uwekezaji mzuri uliofanywa na GSM; GSM wewe ni mwamba, ujengewe Sanam/Mnara pale Makao Makuu ya Yanga. Napenda nitoe pongezi kwa Menejimenti Bora ya timu chini ya Eng. Hersi Saidi kwa kuiongoza vyema timu ya wananchi Yanga na kuipeperusha bendera ya nchi yetu katika medani za kimataifa. Kama tunavyofahamu, Tanzania iliingiza timu mbili katika hatua ya robo fainali ya Klabu Bingwa Afrika, ikiwa ni kwa mara ya kwanza katika historia ya soka nchini. Pamoja na kwamba wenzetu Simba walipigwa ndani nje katika hatua hiyo lakini ni sehemu ya kujifunza na kujipanga upya. Kipekee, niipongeze timu ya YANGA kwa kuitoa jasho timu ya Mamelodi Sundowns. Nina hakika siku ile ya mechi ya mwisho kule Afrika Kusini, wale wachezaji wa Mamelodi Sundowns walilala na viatu kufuatia kitu kizito walichokumbana nacho uwanjani.

**197. Mheshimiwa Spika**, mafanikio haya yamechangiwa kwa kiasi kikubwa na hamasa ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambapo amekuwa akitoa

shilingi milioni tano kwa kila goli linalofungwa katika hatua ya makundi na shilingi milioni kumi kuanzia hatua ya robo fainali. Hivyo, kwa namna ya pekee naomba nitoe pongezi kwa MAMA yetu kwa ubunifu huo ambao umeliletea Taifa letu sifa na heshima kubwa katika nyanja ya michezo. Ni rai yangu kuwa tuendelee kuhamasisha michezo mingine ili nchi yetu iweze kushiriki katika mashindano mbalimbali ya kimataifa na hatimaye kurudi na tuzo au makombe. Aidha, napenda kutumia fursa hii kuipongeza timu ya YANGA kwa kutwaa ubingwa wa ligi kuu ya kandanda nchini kwa mara ya tatu mfululizo na Kombe la Shirikisho la Benki ya CRDB. Yanga ni wafalme wa soka la Tanzania, natamani kumshauri Gavana wa Benki kuu kuweka nembo ya klabu ya Yanga kwenye noti ya shilingi 100 kuyaenzi mafanikio haya.

**198. Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya kipekee kabisa nitumie fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kunijalia afya njema katika utekelezaji wa majukumu yangu. Naomba pia kumshukuru mke wangu na rafiki yangu kipenzi Bi. Neema Mwigulu Nchemba pamoja na watoto wetu kwa maombi yao na kunipa faraja inayoniwezesha kutekeleza wajibu niliopewa wa kuwatumikia watanzania.

**199. Mheshimiwa Spika**, niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge, Viongozi na Wananchi wote kwa kunisikiliza.

**200. Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, naafiki

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri, Waheshimiwa Wabunge hoja imeungwa mkono, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Waziri wa Fedha amesoma hotuba hiyo ya makadirio ya mapato na matumizi kwa Serikali kwa mwaka wa fedha 2024/2025, na hatua zitaendelea kwa utaratibu ambao tumejiwekea.

Nitumie fursa hii kipekee kabisa kwa sababu utaratibu utaendelea lakini nimpongeze kwa kuwa amesimama muda wote huu akisoma hongera sana Mheshimiwa Waziri, sasa Waheshimiwa Wabunge watapata nafasi ya kuisoma hotuba hii ambayo umeitoa hapa pia na Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti na wananchi pia wataendelea kusoma na wao. Basi tutaendelea na utaratibu wetu lakini tunawapongeza kwa kuja na hotuba hii ambayo inatoa matumaini. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia nitumie fursa hii kipekee kabisa kumshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuungana nasi katika kusikiliza bajeti hii muhimu kabisa ya Serikali anayoingoza ambayo pia imetupa mwelekeo wa namna mwaka ujao tunayoyatarajia. Kwa hiyo tunamshukuru sana kwa kuungana nasi Wabunge wenzake. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo sasa nilete matangazo niliyonayo hapa mbele na tutaanza na tangazo la wageni.

Waheshimiwa Wabunge, kwanza tutaanza na wageni walioko Jukwaa la Spika, tutaanza na Mheshimiwa Balozi. Dkt. Moses Mpogole Kusiluka ambae ni Katibu Mkuu Kiongozi, karibu sana. *(Makofi)*

Pia yupo Dkt. Emmanuel John Nchimbi, Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo pia Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Waziri Mkuu Mstaafu na Mzee wa Dodoma, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo Mheshimiwa Anne Semamba Makinda, Spika Mstaafu, karibu sana. *(Makofi)*

Tunae Jenerali Jacob John Mkunda, Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi, karibu sana. *(Makofi)*

Tunae *CP* Liberatus Sabas ambaye ni Mwakilishi wa Mkuu wa Jeshi la Polisi Tanzania *(IGP)*, karibu sana. *(Makofi)*

Tunae pia Balozi Ali Idi Siwa, Mkurugenzi Mkuu wa Idara ya Usalama wa Taifa, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo Ndugu Jeremia Yoram Katungu, Mwakilishi wa Kamishna Jenerali wa Jeshi la Magereza, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo Ndugu John William Masunga, Kamishna Jenerali wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo Ndugu Amiru Sadik Salim ambaye ni Mwakilishi wa Kamishna Jenerali wa Uhamiaji, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo *CP*. Salum Hamduni ambaye ni Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge mnaozungumza bado nimesimama. Tunaye Ndugu Shaban Khatibu Baraza, Mwakilishi wa Kamishna Jenerali wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana Dawa za Kulevya, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo Brigedia Generali Andrew Vitalis Chakila ambaye ni Mratibu Mkuu Msaidizi wa Baraza la Usalama la Taifa, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo Mheshimiwa Jaji Mstaafu Kipenka Msemembo Mussa ambaye ni Katibu wa Bunge Mstaafu, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo Mheshimiwa George Francis Mlawa ambaye ni Katibu wa Bunge Mstaafu, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo Dkt. Thomas Kashililah, Katibu wa Bunge Mstaafu, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo Ndugu Ndele Jailos Mwaselela, Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Chama cha Mapinduzi Taifa akiwakilisha Mkoa wa Mbeya, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo Mheshimiwa Dor Mohamed, Meya wa Jiji la Mbeya, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo Ndugu. Emmanuel Mwalupindi, Mwenyekiti Wazazi Wilaya ya Mbeya Mjini. *(Makofi)*

Yupo Ndugu Suma Mwaikambo, Mwenyekiti Umoja wa Wanawake Tanzania Mbeya Mjini. *(Makofi)*

Yupo Ndugu Clement Mwandemba ambaye ni Mwenyekiti UVCCM Mbeya Mjini. *(Makofi)*

Yupo Mheshimiwa Lucas Mwampiki, Diwani Kata ya Mwakibete. Yupo Mheshimiwa Pitson Mtalibani, Diwani Kata ya Iduda, Mbeya Mjini. Yupo Mheshimiwa Mariam Kabuje, Diwani Viti Maalum, Mbeya Mjini. Yupo Ndugu Ruth Mwasubi ambaye ni Katibu wa Umoja wa Wanawake Tanzania, Mbeya Mjini. Yupo Ndugu Stephen Chambanenge, Katibu wa Mbunge wa Mbeya Mjini. Yupo Dkt. Salvatory Muhando, Mjumbe wa Kamati ya Siasa Mbeya Mjini. Yupo Ndugu Bakari Kimaya, Mjumbe wa Kamati ya Siasa Mbeya Mjini. Yupo Ndugu Lidia John Gunda, Mjumbe wa Kamati ya Siasa Mbeya Mjini. *(Makofi)*

Yupo Bwana Nehemiah Mchechu, Msajili wa Hazina. Yupo Ndugu Bernice Mwigulu Nchemba, Mtoto wa Mheshimiwa Waziri wa Fedha. Sasa hapa wacha nitafute jina la mkewe; naona wameweka mtoto, mtoto, mtoto, jamani! Mkewe si ndiyo itifaki hapa? Haya naona wametangulizwa watoto hapa lakini Mke wa Mheshimiwa Mwigulu Nchemba tuanze na huyo, karibu sana; ameambatana na watoto wa Mheshimiwa Waziri wa Fedha. Yupo Ndugu Bernice Mwigulu Nchemba, Ndugu Gracius Mwigulu Nchemba, Ndugu Isaac Mwigulu Nchemba na Veronica Yohana Jackson, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, yupo Dkt. Natu Mwamba, Katibu Mkuu Wizara ya Fedha. Yupo Mheshimiwa Rosemary Senyamule, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma. Yupo Mheshimiwa *Professor* Davis Mwamfupe Mstahiki Meya wa Jiji la Dodoma. Yupo Ndugu Alphayo Kidata, Kamishna wa Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)*. Yupo Ndugu Charles Kichere Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Yupo Jaji Sivangilwa Sikalakwa Mwangesi, Kamishna wa Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo Mheshimiwa Nurdin Babu, Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, karibu sana. Yupo Mheshimiwa Peter Serukamba, Mkuu wa Mkoa wa Iringa, karibu sana. Yupo Mheshimiwa Queen Sendiga, Mkuu wa Mkoa wa Manyara, karibu sana. Yupo Mheshimiwa Paul Matiko Chacha, Mkuu wa Mkoa wa Tabora, karibu sana. Yupo Ndugu Yohana Musa, Mwenyekiti wa Chama cha *ACT* Wazalendo Mkoa wa Dodoma, karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao Makatibu Wakuu wa Wizara mbalimbali. Tutaanza na Ndugu Majura Mahendeka, Katibu Mkuu Ikulu, karibu sana. Yupo Ndugu Xavier Mrope Daudi, Mwakilishi wa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, karibu sana. Yupo Dkt. Tausi Kida Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais Mipango na Uwekezaji, karibu sana. Yupo Ndugu Mary Makondo, Katibu Mkuu Wizara ya Katiba na Sheria, karibu sana. Yupo Ndugu Gerald Mweli, Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo, ahsante sana. *(Makofi)*

Yupo Ndugu Ally Gugu, Katibu Mkuu Wizara ya Mambo ya Ndani ya nchi, ahsante sana. Yupo *Professor* Riziki Shemdoe, Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi, karibu sana. Yupo Dkt. Hassan Abbas, Katibu Mkuu Wizara ya Maliasili na Utalii, ahsante sana. Yupo Mhandisi Felchesmi Mramba, Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, karibu sana. Yupo Ndugu Kheri Mahimbali, Katibu Mkuu Wizara ya Madini, karibu sana. Yupo Balozi Mhandisi Aisha Amour, Katibu Mkuu Wizara ya Ujenzi, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo Profesa Godius Kahyarara, Katibu Mkuu Wizara ya Uchukuzi, ahsante sana. Yupo Dkt. Hashil Abdallah, Katibu Mkuu wa Wizara ya Viwanda na Biashara, ahsante sana. Yupo Dkt. John Jingu, Katibu Mkuu Wizara ya Afya, karibu sana. Yupo *Professor* Frankling Rosemura, Mwakilishi wa Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, ahsante sana. Yupo Mhandisi Mwajuma Waziri, Katibu Mkuu Wizara ya Maji, ahsante sana. Yupo Ndugu Mohammed Abdullah, Katibu Mkuu Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo Ndugu Lawrence Mafuru, Katibu Mtendaji, Tume ya Mipango. Ndugu Jenifa Omolo, Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha - Huduma za Hazina, ahsante sana. Ndugu Elijah Mwandumbya, Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha - Usimamizi wa Uchumi, karibu sana. Yupo Ndugu Amina Shaaban, Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha - Usimamizi wa Fedha za Umma, karibu sana. Yupo Dkt. Seif Shekalaghe, Katibu Mkuu Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia wapo Mabalozi, wawakilishi wa Mashirika ya Kimataifa na washirika wa maendeleo. Yupo *His Excellency* Ricardo Ambrosio Sampaio Mtumbuida, Balozi wa Msumbiji, karibu sana. Pia, yupo *His Excellency* Isaack Njenga Gatitu, Balozi wa Kenya, karibu sana. Pia, yupo *His Excellency* Leontine Nzeyimana, Balozi wa Burundi, karibu sana. Pia, yupo *His Excellency* Mathew Jere, Balozi wa Zambia, karibu sana. Yupo *Ms.* Margaret Gaynar, Mkuu wa Utawala Ubalozi wa Ireland, karibu sana. *(Makofi)*

Pia, yupo *Ms.* Elke Wisch ambaye ni Mwakilishi wa Umoja wa Mataifa *(Children's Emergency),* karibu sana. Pia, yupo *Ms.* Clara Makenya, Mwakilishi wa Umoja wa Mataifa *(UNICEF* na *UNEP),* karibu sana. Yupo Dkt. Majaliwa Marwa, Mwakilishi Msaidizi Umoja wa Mataifa *(UNFPA)* karibu sana. Yupo *Ms.* Vivian Ngowi, *Programme Manager (EU),* ahsante sana. Yupo *Ms.* Alessandro Pissani, *Programme Manager (EU),* karibu sana. Yupo *Ms.* Stella Manda, Mratibu wa Ofisi ya Dodoma Umoja wa Mataifa Wanawake, karibu

sana. Yupo Dkt. Patricia Laverely ambaye ni Mwakilishi wa Nchi Benki ya Maendeleo ya Afrika, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo *Mr. Keni Williams,* Naibu Balozi wa Uingereza, ahsante sana. Yupo *Mr.* Sylvester Ernest, Afisa Siasa Mwandamizi Ubalozi wa Uingereza, ahsante sana. Yupo *Mr.* Sunday John, Mchumi Ubalozi wa Uingereza, ahsante sana. Yupo *Mr.* Francis Sampa, Meneja Progaramu Uchumi Shirikishi Ireland, ahsante sana. *(Makofi)*

Yupo *Mr.* Narender Kumar, Afisa Ubalozi Jamhuri ya India, karibu sana. Pia, yupo Heide Morten ambaye ni Mshauri wa Masuala ya Nishati, Norway, ahsante sana. Yupo Priva Clemence, Mshauri Mwandamizi Masuala ya Uchumi na Petroli, Norway, ahsante sana. Yupo Zakiya Kunaeva Afisa Ubalozi Jamhuri ya Russia, karibu sana. Yupo *Mr.* Nathan Belete, Mwakilishi Mkazi Benki ya Dunia, karibu sana. Yupo *Mr.* Sebastian Asevedo Mwakilishi Mkazi *IMF*, karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao viongozi wa dini wa Kitaifa na wa Mkoa wa Dodoma. Tutaanza na Sheikh Ahmed Said, Mwakilishi wa Sheikh Mkuu na Mufti wa Tanzania, karibu sana. Yupo Askofu Nelson Kisare, Askofu Mkuu Kanisa la Menonite na Mwenyekiti wa Kamati ya Viongozi wa Dini, karibu sana. Yupo Sheikh Yusuph Marengu, Mwenyekiti Mweza Kamati ya Viongozi wa Dini, karibu sana. Yupo Sheikh Hussein Kuzungu, Mwakilishi wa Katibu Mkuu Baraza Kuu la Waislamu Tanzania, karibu sana. *(Makofi)*

Pia, yupo Mchungaji Dkt. Canon Moses Matonya, Katibu Mkuu Jumuiya ya Kikristo Tanzania, karibu sana. Yupo Sheikh Othman Hariri, Sheikh wa Mkoa (BAKWATA – Dodoma), karibu sana. Yupo Mchungaji Timothe Holela, Mchungaji wa Kanisa la *ELCT* Dodoma, karibu sana. Yupo Askofu Yussuf Mtolela ambaye ni Mwenyekiti wa *CCT* Dodoma, ahsante sana. Yupo Kuhani Musa Richard Mwacha ambaye ni Mchungaji wa *Fresh Spring Fellowship,* karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao maafisa kutoka Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Tunaye Ndugu Benjamin Majura ambaye ni Naibu Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali za Mitaa, karibu sana. Yupo Ndugu Salhina Mkumba, Naibu Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali za Umma, ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia wapo Viongozi Waandamizi wa Mkoa wa Dodoma. Tutaanza na *SACP* Anania Amo, Mwakilishi wa Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Dodoma, karibu sana. Yupo Kanal Justas Mwilambeghe, *Base* Kamanda Jeshi la Wananchi Dodoma, karibu sana. Yupo Mheshimiwa Jabiri Shekimweri, Mkuu wa Wilaya ya Dodoma Mjini, karibu sana. Yupo Ndugu Christopher Mwaikambo, Mkuu wa Usalama wa Mkoa wa Dodoma, karibu sana. Yupo Ndugu George Wambura ambaye ni Mkuu wa Magereza Mkoa wa Dodoma, karibu sana. Yupo Ndugu Rehema Menda, Kamanda wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji wa Mkoa wa Dodoma, karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wapo Wakuu wa Mashirika ya Umma na Taasisi za Fedha. Tutaanza na Ndugu Gilead Teri ambaye ni Mtendaji Mkuu Kituo cha Uwekezaji cha Tanzania *(TIC),* karibu sana. Yupo Ndugu Mussa Makame Mkurugenzi Mtendaji Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania *(TPDC),* karibu sana. Yupo Mhandisi Asajile John, Mwakilishi wa Mkurugenzi Mkuu Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania *(TCRA),* karibu sana. Yupo Ndugu Daniel Malange, Mwakilishi wa Mkurugenzi Mkuu Mamlaka ya Usafiri wa Anga *(TCAA),* karibu sana. Yupo Ndugu Masanja Kadogosa, Mkurugenzi Mkuu Shirika la Reli Tanzania, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo Mhandisi Gissima Nyamo-Hanga ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji Shirika la Ugavi wa Umeme *(TANESCO),* karibu sana. Yupo Ndugu David Semeo, Mwakilishi wa Mkurugenzi Mtendaji Shirika la Madini la Taifa *(STAMICO),* karibu sana. Yupo Kamishna Mussa Juma Kuji, Mkurugenzi Mkuu Shirika la Hifadhi za Taifa *(TANAPA),* karibu sana. Yupo Ndugu Kaimu Mkeyenge ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji Shirika la Bima la Taifa *(NIC),* karibu sana. Yupo Ndugu Masha Mshomba ambaye ni Mkurugenzi Mkuu Mfuko wa Taifa wa

Hifadhi ya Jamii *(NSSF),* ahsante sana. Yupo Ndugu Neema Kuwite, Mwakilishi Mkurugenzi Mkuu Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma *(PSSSF)*. *(Makofi)*

Pia, yupo Ndugu Grace Tariba, Mwakilishi wa Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya *(NHIF)*. Yupo Ndugu Mwanahiba Mzee, Mkurugenzi Mkuu Mfuko wa Pembejeo za Kilimo, karibu sana. Yupo Dkt. Immakulate Sware Semesi, Mkurugenzi Mkuu Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira, karibu sana. Haya yupo Mhandisi Hassan Saidy, Mkurugenzi Mkuu wa Wakala wa Nishati vijijini *(REA),* karibu sana. *(Makofi)*

Pia, yupo Mhandisi Victor Seif, Mtendaji Mkuu Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini *(TARURA),* haya Waheshimiwa Wabunge ahsanteni sana. Mhandisi Victor Seif makofi hayo yanaashiria mambo mawili; kwanza, kukupongeza kwa kazi nzuri na pili, mategemeo ya Waheshimiwa Wabunge kwenye majimbo yao barabara zikatengenezwe, ahsante sana. *(Makofi/Vigelegele)*

Waheshimiwa Wabunge, pia, yupo *Professor* Presley Muro ambaye ni Mwakilishi wa Mtendaji Mkuu Wakala ya Huduma ya Ununuzi Serikalini *(GPSA),* ahsante sana. Yupo Ndugu Elihuruma Lema, Mwakilishi wa Mkurugenzi Mkuu Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu, karibu sana. Yupo Ndugu Ephraim Balozi Mafuru ambaye ni Mkurugenzi Mkuu Bodi ya Utalii *(TTB),* karibu sana. Yupo Dkt. Ally Laay ambaye ni Mwenyekiti wa Bodi ya *CRDB,* karibu sana. Yupo Ndugu Ruth Zaipuna, Afisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya *NMB,* karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, yupo Ndugu Theobald Sabi, Afisa Mtendaji Mkuu *National Bank of Commerce,* karibu sana. Yupo Ndugu Geofrey Mchangila, Afisa Mtendaji Mkuu *CITI Bank,* karibu sana. Yupo Ndugu Happy Usiri, Mwakilishi wa Afisa Mtendaji Mkuu *Azania Bank.* Yupo Ndugu Manzi Rwegasira, Afisa Mtendaji Mkuu *STANBIC BANK.* Pia, yupo Ndugu Frank Nyabudenge ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji Benki ya Maendeleo ya Kilimo *(TADB),* ahsante sana. *(Makofi)*

Pia yupo Ndugu Gbenga Makinde, Mkurugenzi Mtendaji wa *United Bank for Africa,* karibu sana. Yupo Ndugu Fanuel Philemon, Mwakilishi wa Afisa Mtendaji Mkuu wa *Diamond Trust Bank.* Yupo Ndugu Adam Mihayo Mkurugenzi Mtendaji wa *TCB Bank,* karibu sana. Yupo Ndugu Claver Serumaga, Mkurugenzi Mkuu Benki ya *NCBA PLC,* karibu sana. Yupo Ndugu Lilian Mbassy, Mkurugenzi Mkuu *Tanzania Investment Bank,* karibu sana. Yupo Ndugu Tusekelege Mwaikasu, Mkurugenzi Mtendaji *TAB,* karibu sana. Yupo Ndugu Mzilasi Mbena, Mwakilishi wa Afisa Mtendaji Mkuu *Standard Chartered Bank. (Makofi)*

Yupo Ndugu Silvest Uiso Arumasi ambaye ni Afisa Mtendaji Mkuu *Akiba Commercial Bank;* yupo pia Ndugu Takashi Araki, Mkurugenzi Mtendaji Kampuni ya Sigara *(TCC);* yupo Ndugu John Wanyancha ambaye ni mwakilishi wa Mkurugenzi Mtendaji wa *Serengeti Breweries;* yupo Ndugu Emma Kawawa ambaye ni mwakilishi Chama cha *Graca Machel Trust;* yupo Dkt. Fred Msemwa ambaye ni Mkurugenzi Mkuu *Watumishi Housing;* yupo Mheshimiwa Thomas Apson ambaye ni Mkuu wa Wilaya ya Ikungi; yupo Ndugu Salum Nassoro ambaye ni Mkurugenzi Mahusiano ya Jamii *Coca-Cola* na Ndugu Baraka Munisi ambaye ni Mtendaji Mkuu *Faidika Bank,* karibuni sana. *(Makofi)*

Vilevile wapo Wakuu wa Taasisi za Elimu Dodoma; yupo Profesa Tandi Lwoga ambaye ni Mkuu wa Chuo cha Biashara (*CBE);* yupo Profesa Hozen Mayaya ambaye ni Mkuu wa Chuo cha Mipango *(IRDP);* yupo Profesa Yohana Msanjila ambaye ni Mkuu wa Chuo cha *St. John's;* yupo Profesa Lughano Jeremy Kusiluka ambaye ni Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dodoma *(UDOM)* na pia yupo Ndugu Elvanus Kapira ambaye ni Mkuu wa Chuo cha Madini, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaye pia mwakilishi wa Shirikisho la Vyama vya Watu Wenye Ulemavu Dodoma, huyu ni Ndugu Maiko Salali Hosea ambaye ni Mwenyekiti wa Watu wenye Ulemavu Mkoa wa Dodoma, karibu sana. *(Makofi)*

Kwa upande wa vyombo vya habari wapo Dkt. Ayoub Rioba ambaye ni Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Utangazaji wa Taifa *(TBC);* yupo Ndugu Patrick Kahemele ambaye ni Afisa Mtendaji Mkuu wa *Azam Media;* yupo Ndugu Bakari Machumu ambaye ni Mhariri Mkuu wa *Mwananchi Communications;* yupo Ndugu Aisha Dachi ambaye ni Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni Magazeti ya Serikali *(TSN);* yupo Ndugu Shaban Kissu ambaye ni Mtendaji Mkuu wa Vyombo vya Habari vya Chama Cha Mapinduzi na Ndugu Dotto Bahemu ambaye ni mwakilishi wa Mtendaji Mkuu wa *Clouds Media,* karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wapo watendaji wa Wizara ya Fedha pamoja na taasisi zake. Sasa huyu mmoja alikuwa ameshatambulishwa, lakini ninaambiwa kuwa yupo Mhasibu Mkuu wa Serikali. Haya majina yamepishana.

Haya, yupo Katibu Mtendaji wa Tume ya Pamoja ya Fedha, yupo Kamishna wa Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu. Mniwie radhi majina yamepishana kwa hivyo wengine watatajwa kwa vyeo vyao, karibuni sana. *(Makofi)*

Yupo pia Dkt. Albina Chuwa, Mtakwimu Mkuu wa Serikali, karibu sana. Haya ahsanteni sana. *(Makofi/Vigelegele)*

Yupo pia Ndugu Eliakim Maswi ambaye ni Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Kudhibiti Ununuzi wa Umma *(PPRA); CPA* Nicodemus Mkama ambaye ni Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana *(CMSA)*, Ndugu Ephraim Mdee ambaye ni Meneja wa *TRA*; Ndugu Moshi Kabwengwe ambaye ni Mkurugenzi wa Idara ya Usimamizi na Rasilimali Watu; Ndugu James Mbalwe ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Bodi ya Michezo ya Kubahatisha; Ndugu Benjamin Maggai ambaye ni Mkaguzi wa Ndani Mkuu wa Serikali; Dkt. Baghayo Sagware ambaye ni Kamishna wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania; Ndugu Godfrey Malekano ambaye ni Mtendaji Mkuu Soko la Bidhaa Tanzania *(TMX)* na Ndugu James Sando ambaye ni Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Rufaa za Zabuni, karibuni sana. *(Makofi)*

Vilevile yupo Ndugu Mcha Hassan Mcha ambaye ni Naibu Kamishna Mkuu wa *TRA*; Ndugu Johnson Nyella ambaye ni Kamishna wa Uchambuzi wa Sera *(CPAD),* Ndugu Agaton Kitandula ambaye ni Mkurugenzi Huduma za Kibenki Wizara ya Fedha; Profesa William Pallangyo ambaye ni Mkuu wa Chuo Cha *TIA* na Dkt. Leonada Mwagike…

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tupunguze kelele kidogo, bado nimesimama.

Pia yupo Dkt. Leonada Mwagike ambaye ni Mwenyekiti wa Bodi *(PPRA);* yupo Ndugu Michael Muhoja ambaye ni Kamishna wa Walipa Kodi Wakubwa na Ndugu David Kafulila ambaye ni Kamishna wa Ubia wa Umma na Sekta Binafsi, karibuni sana. Haya ahsanteni sana. *(Makofi)*

Yupo Dkt. Charles Mwamaja ambaye ni Kamishna wa Maendeleo ya Sekta ya Fedha; yupo Ndugu Bashiru Hussein ambaye ni Kaimu Kamishna wa Ubia wa Sekta ya Umma na Binafsi; yupo Ndugu Bahati Mgongolwa ambaye ni Kamishna Msaidizi wa Bajeti Mishahara; yupo Ndugu Geofrey Mahemba ambaye ni Mhasibu wa Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu; yupo Ndugu Mbayani Saruni ambaye ni Kamishna Msaidizi Uchambuzi wa Sera; yupo Ndugu Mohamed Magati ambaye ni Mtendaji *TRAT* na yupo Ndugu Raymond Kwohelera ambaye ni Kamishna Msaidizi wa Bajeti Wizara, Idara ya Mawakala, karibuni sana. *(Makofi)*

Vilevile yupo Ndugu Fundi Makama ambaye ni Kamishna Msaidizi wa Bajeti – Mbinu; yupo Dkt. Kelvin Njunwa ambaye ni mwakilishi wa Mkuu wa Chuo cha *IAA* na yupo Ndugu Jonson Nyalu, Kamishna wa Fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Halima, tusikilizane.

Waheshimiwa Wabunge, pia yupo Ndugu Willium Mhoja ambaye ni Kamishna Msaidizi wa Fedha, ahsante sana na karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ninao wageni wengine; yupo Ndugu Mwalizi Mwanshinga ambaye ni Msaidizi wa Mbunge Ofisi ya Mbunge Mbeya Mjini, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo pia Ndugu Daud Shurbat kutoka Shirikisho la Walimu Chama Cha Mapinduzi – Mbeya; yupo Ndugu Suma Lwena kutoka Shirikisho la Walimu Chama Cha Mapinduzi – Mbeya; yupo Ndugu Pascal Obeid kutoka Chama cha Walimu Tanzania – Mbeya; yupo Ndugu Zaitun Rajabu kutoka Chama cha Walimu Tanzania – Mbeya; yupo Ndugu Itika Mwaijande ambaye ni Mweka Hazina kutoka Chama cha Walimu Tanzania – Mbeya na Ndugu Frida Balukege kutoka Chama cha Walimu Tanzania – Mbeya. *(Makofi)*

Vilevile yupo Ndugu Ibrahim Mbembela ambaye ni mfanyabiasha; yupo Ndugu Richard Mbwambo ambaye ni mfanyabiashara; yupo Ndugu Lumuli Kibona ambaye ni mfanyabiashara; yupo Ndugu Alphonce Maganga ambaye ni mfanyabiashara na yupo Ndugu Geofrey Mwansapeta ambaye ni mfanyabiashara, karibuni sana. *(Makofi)*

Yupo Ndugu John Mwankenja ambaye ni Mwenyekiti wa Umoja wa Madereva Mbetukye; yupo Ndugu Daniel Moses ambaye ni Katibu wa Umoja wa Madereva Mbetukye; yupo Ndugu Mussa Japhet Mkoma ambaye ni Katibu wa Bodaboda Mbeya Mjini; yupo Ndugu Lucas Mwakyusa ambaye ni Mwenyekiti wa Bajaji Jiji la Mbeya, ahsante sana. *(Makofi)*

Mwenyekiti wa Bajaji Jiji la Mbeya ameongozana na Ndugu Issa Mwanaluhemeja ambaye ni Makamu Mwenyekiti wa Bajaji Jiji la Mbeya na ameongozana na Ndugu Fanuel Sanga ambaye ni Katibu wa Bajaji Jiji la Mbeya. *(Makofi/Kicheko)*

Hapa naona wamechanganya kidogo majina, lakini yupo Mtunza Hazina wa Bajaji kutoka Jiji la Mbeya, ahsante sana na karibu sana. *(Makofi)*

Pia yupo Ndugu Joseph Mwaisango kutoka *Mbeya Yetu Tv* anatoka Mbeya huyu, yupo Ndugu Haroub Kabwe ambaye ni mwandishi wa *Haroub Tv,* yupo Ndugu Ally Abdallah ambaye ni mtafiti kutoka Mbeya, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wapo wageni wengine wa Mheshimiwa Waziri wa Fedha; yupo Ndugu Elizaberth Lyimo ambaye ni ndugu wa Mheshimiwa Waziri, yupo Ndugu Seif Hassan ambaye ni *CEO* wa *IIA Tanzania*; yupo Ndugu Christine Mbonya ambaye ni *Advocacy Committee Member wa IAA*; yupo Ndugu Jonathan Ngoma ambaye ni *Vice President* wa *IAA Tanzania*; yupo Ndugu Iq-lima Issa ambaye ni *Advocacy Committee Member* wa *IAA*; yupo Ndugu Veronica Amosi Masorwa ambaye ni ndugu wa Mheshimiwa Waziri, yupo Ndugu Frannie Leautier ambaye ni Makamu wa Rais Mstaafu wa Benki ya Maendeleo ya Afrika *AFDB*; yupo Ndugu Shaban Madelu ambaye ni mdogo wake Mheshimiwa Waziri; yupo Ndugu Japhet Richard Shani ambaye ni mjomba wa Mheshimiwa Waziri; yupo Ndugu Jesca Mbogo ambaye ni ndugu wa Mheshimiwa Waziri na yupo Ndugu Emmanuel Richard Shani ambaye ni ndugu wa Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wapo wageni wengine ambao tumeletewa orodha baadaye kwa hiyo hawakuweza kupangwa na nitawatangaza kama ifuatavyo: -

Yupo Ndugu Benoit Araman ambaye ni Mkuruugenzi Mkuu wa *Oryx Gas Tanzania;* yupo Bi. Khadija Omari ambaye anatoka Ofisi Binafsi ya Rais – Ikulu; yupo Bwana Salum Lupambe kutoka Ofisi Binafsi ya Rais – Ikulu; yupo Ndugu Sigfried Kuwite ambaye ni Mjumbe kutoka *TSEBA;* yupo Ndugu Geofrey Malauri ambaye ni Mwenyekiti wa *TSEBA*; yupo Ndugu Celicius Kizitto ambaye ni *Branch Manager* wa *Diamond Trust Bank Plc* kutoka Dodoma; yupo Ndugu Lawrence Mafuru ambaye ni Katibu Mtendaji wa Tume ya Mipango;

yupo Dkt. Mursali Milanzi ambaye ni Naibu Katibu Mtendaji wa Tume ya Mipango; yupo Dkt. Lorah Madete ambaye ni Naibu Katibu Mtendaji Ubunifu na Biashara na yupo Dkt. Linda Ezekiel ambaye ni Naibu Katibu Mtendaji Menejimenti ya Utendaji na Tathmini, karibuni sana. *(Makofi)*

Vilevile yupo Ndugu Juma Kimori ambaye ni *Chief Finance Officer* wa *NMB*; yupo Ndugu Vicky Bishuba ambaye ni *Head of Government Business* kutoka *NMB;* yupo Ndugu Raphael Maganga ambaye ni *CEO* wa *TPSF*; yupo Ndugu Theobald Sabi; naona ana cheo kingine mbaye ni Mwenyekiti wa *Bankers Association* na pia yupo Ndugu Godwin Sumunyu ambaye ni *Head of Corporate Affairs*, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Hawa wengine walikwishatangazwa.

Yupo Ndugu Dkt. Rhimo Nyansahao ambaye ni Mkurugenzi wa Biashara wa *Azania Bank*; yupo Ndugu Joseph Kusaga, sijui kama yupo lakini naona mwakilishi alikwishatangazwa. *(Makofi)*

Haya, yupo Dkt. Joseph Mayala Mitinje ambaye ni Mkurugenzi Mwandamizi wa *World Vision Tanzania*; yupo Ndugu Ibrahim Haji kutoka *CRDB HQ* Dar es Salaam; yupo Ndugu Fredrick Nshekanabo kutoka *CRDB HQ* Dar es Salaam; yupo Ndugu Mirage Msuya ambaye ni *Zonal Manager* wa *NBC Bank* Kanda ya Kati; yupo Ndugu Godfrey Nyaisa ambaye ni Afisa Mtendaji Mkuu wa *BRELA;* yupo Ndugu James Meitaron ambaye ni *Director of Corporate Banking* wa *NBC*; yupo Ndugu Emmanuel Mseti kutoka *Akiba Commercial Bank*; yupo Ndugu Zela Njeza ambaye ni Mwenyekiti wa Bodi *IIA Tanzania;* yupo Ndugu Kubelwa Mwakatundu ambaye ni Naibu Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali za Mitaa; huyu si alikwishatangazwa? Au huyu ni mwingine tena? *(Makofi)*

Haya, yupo Ndugu Hussein Mwaga ambaye ni mwakilishi wa Naibu Katibu Mkuu wa Zanzibar; yupo Ndugu Amos Makalla ambaye ni Katibu wa *NEC* – Itikadi na Uenezi wa Chama Cha Mapinduzi, pia yupo Ndugu Suzan Kamambi ambaye ni Katibu wa

Umoja wa Wanawake Tanzania wa Chama Cha Mapinduzi Taifa; yupo Ndugu Jokate Mwegelo ambaye ni Katibu wa UVCCM Taifa; yupo Ndugu Ally Salim Happi ambaye ni Katibu wa Jumuiya ya Wazazi wa Chama Cha Mapinduzi Taifa na yupo Dkt. Francis Daud ambaye ni mwakilishi wa Mjumbe wa *NEC Organization,* karibuni sana na ahsanteni sana. *(Makofi)*

Yupo Ndugu Grace Adam ambaye ni Meneja wa *CRDB* Tawi la Bunge. *(Makofi)*

Haya Mwenyekiti wa Bodi ya *CRDB* makofi hayo yanaashiria aongezewe mshahara, ahsanteni sana. *(Makofi/Vigelegele)*

Pia yupo Ndugu Grace Matemu ambaye ni Meneja wa *NMB* Tawi la Bunge, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mtendaji Mkuu wa Benki ya *NMB* makofi hayo pia yanaashiria Grace huyu naye aongezewe mshahara. *(Makofi/Vigelegele)*

Pia yupo Dkt. Charles Alex Prosperity ambaye ni Mchungaji Kiongozi wa Kanisa la *Covenant Place* na yupo Ndugu Nuru Kateti ambaye ni Mkuu wa Kitengo cha Biashara ya Serikali, ahsanteni sana. *(Makofi/Vigelegele)*

Vilevile yupo Ndugu Godwin Mafie ambaye ni ndugu wa Mheshimiwa Waziri; yupo Ndugu Baraka Wilfred Ngure ambaye ni shemeji wa Waziri na yupo Ndugu Lilian Lucas Kisasa ambaye ni ndugu wa Mheshimiwa Waziri wa Fedha, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, yapo majina mengine ya wageni ambao nimeletewa hapa mbele kwamba nao tuko nao hapa Bungeni. Wapo Makatibu Wakuu ambao hawakuwa wamewekwa kwenye orodha.

Yupo Mhandisi Cyprian Luhemeja ambaye ni Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Rais; yupo Dkt. Jim Yonazi ambaye ni Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu; yupo Katibu Mkuu Adolf

Ndunguru ambaye ni Katibu Mkuu-TAMISEMI; yupo Ndugu Antony Sanga ambaye ni Katibu Mkuu wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na pia yupo Ndugu Faraji Mnyepe ambaye ni Katibu Mkuu wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia nimeletewa jina la Dkt. Frannie Leautier, ambaye ni *Former Vice President* wa *World Bank* ambaye alikuwa anashughulikia miundombinu. Pia alikuwa *Vice President* wa *AFDB*, nadhani tulimtangaza cheo kimoja cha *Vice President* cha *AFDB*, karibu sana. *(Makofi)*

Wageni wetu mnakaribishwa sana Bungeni. Sasa kwa sababu majina mengine nimeletewa hapa mbele kwa maandishi ya wale waliokumbukwa na waalikaji humu ndani, mniwie radhi ikiwa yupo mgeni ambaye hakutangazwa. Hatuna jina hapa mbele pengine yamerukwa na wale waandishi huko ofisini. Kwa hiyo, mtuwie radhi. *(Makofi)*

Tunawashukuru sana kwa kuja kuungana nasi siku ya leo katika kusoma Bajeti Kuu ya Serikali ambayo ninyi mmekuja kuwakilisha umma wa Watanzania wote ili wasikilize bajeti hii na katika hizi siku ambazo tutakuwa tukiijadili basi waweze kutoa maoni yao juu ya haya ambayo yameletwa na Serikali. Kwa hiyo, wageni wetu tunawashukuru sana kwa kuja kuungana pamoja na sisi. *(Makofi)*

Haya, ahsanteni sana. *(Makofi)*

W aheshimiwa Wabunge, nina tangazo moja hapa kutoka kwa Katibu wa Bunge; anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kuwa siku ya Jumamosi tarehe 15 Juni, 2024 kutakuwa na semina kuhusu bajeti ya Serikali ya mwaka 2024 itakayoendeshwa na wataalamu mbalimbali wa masuala ya uchumi. *(Makofi)*

Semina hii inaratibiwa kupitia Mradi wa Kulijengea Bunge Uwezo *(LSP III)*. Semina itafanyika Ukumbi wa Msekwa kuanzia saa 4.00 asubuhi. Waheshimiwa Wabunge wote mnakaribishwa kwa ajili ya kazi hii.

Waheshimiwa Wabunge, kwa kawaida, kanuni ambazo tumejiwekea siku ya kesho huwa hakuna Bunge ili Waheshimiwa Wabunge mpate nafasi ya kutafakari hotuba hii ambayo imesomwa na Mheshimiwa Waziri wa Fedha.

Wakati huo huo tunazo taarifa kwamba *Eid* itakuwa siku ya Jumatatu au huenda ikawa siku ya Jumatatu. Kwa hiyo, baada ya kusema hayo ninaahirisha Shughuli za Bunge mpaka siku ya Jumanne, tarehe 18 Juni, 2024 saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 1.02 Usiku Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumanne, Tarehe 18 Juni, 2024 Saa Tatu Asubuhi)*